SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

# AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ZANZIBAR

## RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

## KUHUSU UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA KWA TAASISI ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2023



SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU
WA HESABU ZA SERIKALI ZANZIBAR

# RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

# KUHUSU UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA KWA TAASISI ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2023

**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**
**AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ZANZIBAR**
2 Mtaa wa Tume, S.L.P 258, 71125 Kilimani Zanzibar
Simu/Nukushi: +255 24 223 400, Barua Pepe: info@ocagz.go.tz
Tovuti: www.ocagz.go.tz

**MAREJEO NAM: CAC.132/385/01/4** **TAREHE: 26 MACHI, 2024**

**MHE. DKT HUSSEIN ALI MWINYI,**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI,**
**AFISI YA RAIS IKULU,**
**S.L.P. 437,**
**ZANZIBAR, TANZANIA.**

**KUH: KUWASILISHA RIPOTI YA MWAKA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023**

---

Ninayo furaha kuwasilisha kwako Ripoti ya Mwaka inayohusu Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kipindi cha mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023 kwa mujibu wa kifungu nambari 112(5) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 pamoja na kifungu nambari 46(1) cha Sheria nambari 7 ya Ukaguzi wa Umma ya 2023.

Naomba kuwasilisha.

Ahsante.

........................................

**DKT. OTHMAN ABBAS ALI**
**MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU**
**WA HESABU ZA SERIKALI**
**ZANZIBAR.**

# AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ZANZIBAR

## Mamlaka

Kwa mujibu wa kifungu nambari 112 cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 pamoja na kifungu nambari 46(1) cha Sheria nambari 7 ya Ukaguzi wa Umma ya 2023, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibika kikatiba kukagua hesabu za Taasisi za Serikali na baadae kutoa taarifa za ukaguzi huo angalau mara moja kila mwaka.

## Dira

Kuwa na Taasisi ya ukaguzi iliyo huru na inayoongoza katika kusimamia uwajibikaji na uwazi.

## Dhamira

Kusimamia uwajibikaji wa Taasisi za umma kwa kufanya ukaguzi wa hesabu wenye kuleta tija na kulihakikishia Taifa kwamba rasilimali za Umma zitatumika kama ilivyokusudiwa.

## MISINGI YA MAADILI YA UKAGUZI

1. **Uaminifu**
Kuhakikisha Afisi ina kiwango cha juu cha uaminifu na kuzingatia utawala bora unaozingatia Sheria.

2. **Uadilifu**
Kuwa ni Afisi inayozingatia misingi ya uadilifu kwa kutoa huduma bila ya upendeleo.

3. **Kuwa Huru**
Kuwa ni Afisi iliyo huru na inayotekeleza majukumu yake bila ya kuingiliwa kwa mujibu wa Sheria.

4. **Uwezo na Taaluma ya Ukaguzi**
Kuwa ni Afisi yenye kutoa huduma za ukaguzi zenye ubora wa kiwango cha juu.

5. **Kutunza Siri**
Kuwa ni Afisi yenye kutunza siri katika utekelezaji wa kazi zake.

6. **Uwazi na Uwajibikaji**
Kutoa taarifa sahihi na muhimu kwa wadau ili kuweza kupima uwajibikaji katika matumizi bora ya rasilimali za Umma

# YALIYOMO

YALIYOMO ........ V
ORODHA YA MAJADWELI ........ VIII
ORODHA YA PICHA ........ XII
VIFUPISHO NA TAFSIRI ........ XIV
SHUKURANI ........ XVII
DIBAJI ........ XIX
MUHTASARI ........ XXI
**SURA YA KWANZA** ........ 1
1.0 UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA KATIKA TAASISI ZA UMMA ........ 1
1.1 UTANGULIZI ........ 1
1.2 MAMLAKA YA KUFANYA UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA ........ 1
1.3 UPEO WA UKAGUZI ........ 1
1.4 MALENGO YA UKAGUZI ........ 2
1.5 SERA, VIWANGO NA MIONGOZO ILIYOTUMIKA ........ 3
1.6 NJIA NA MBINU ZA UKAGUZI ZILIZOTUMIKA ........ 3
**SURA YA PILI** ........ 6
2.0 MUHTASARI WA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA HOJA ZA UKAGUZI KWA MWAKA WA FEDHA ULIOPITA ........ 6
2.1 TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA HOJA ZA MWAKA ULIOPITA ........ 6
**SURA YA TATU** ........ 17
3.0 TATHMINI YA UKAGUZI NA DOSARI ZA UJUMLA ZILIZOBAINIKA KATIKA UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA ........ 17
3.1 KUNDI LA KWANZA LA MIFUMO YA TEHAMA ........ 17
3.2 KUNDI LA PILI LA MIFUMO YA TEHAMA ........ 18
3.3 MAENEO MAKUU YALIYOFANYIWA UKAGUZI ........ 18
3.4 MUHTASARI WA DOSARI ZILIZOBAINIKA KATIKA UKAGUZI ........ 19

3.4.1 DOSARI ZA UJUMLA ZILIZOBAINIKA KATIKA UKAGUZI ...........21

**SURA YA NNE**.........................................................................53

4.0 MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 ............................53

4.1 UFAFANUZI WA DOSARI ZILIZOBAINIKA...................................53

4.1.1 MAMLAKA YA UNUNUZI NA UONDOSHAJI WA MALI ZA UMMA (ZPPDA)..................................................................53

4.1.2 WAKALA WA SERIKALI MTANDAO ZANZIBAR (eGAZ) .............75

4.1.3 OFISI YA RAIS KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA (OR-KSUUB).......................................................96

4.1.4 MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU UCHUMI ZANZIBAR (ZAECA)................................................113

4.1.5 WIZARA YA UJENZI MAWASILIANO NA UCHUKUZI ................130

4.1.6 WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI................................133

4.1.7 MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE ZANZIBAR (ZAA) ............146

4.1.8 TAASISI YA VIWANGO ZANZIBAR (ZBS)...............................160

4.1.9 KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA..........................161

4.1.10 MAMLAKA YA MAPATO ZANZIBAR (ZRA).............................175

4.1.11 MFUKO WA HIFADHI YA JAMII (ZSSF) ...............................183

4.1.12 SHIRIKA LA UMEME ZANZIBAR (ZECO)..............................187

4.1.13 WAKALA WA MATUKIO YA KIJAMII ZANZIBAR (ZCSRA)........197

4.1.14 MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI ZANZIBAR (ZURA)...................................................199

4.1.15 BARAZA LA USIMAMIZI WA LESENI ZA BIASHARA (BRLC)...220

4.1.16 BARAZA LA MANISPAA YA MJINI ......................................222

4.1.17 SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA ZANZIBAR (ZSTC)............232

4.1.18 OFISI YA RAIS FEDHA NA MIPANGO (MOFP).....................248

4.1.19 SHIRIKA LA BANDARI ZANZIBAR (ZPC).............................251

4.1.20 MAMLAKA YA UWEKEZAJI WA VITEGA UCHUMI ZANZIBAR (ZIPA)....258

4.1.21 WAKALA WA CHAKULA DAWA NA VIPODOZI ZANZIBAR (ZFDA) )....261

4.1.22 KAMISHENI YA UTALII ZANZIBAR (ZTC) ....266

4.1.23 OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ )....271

4.1.24 OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI ....275

4.1.25 MAHAKAMA YA ZANZIBAR....279

4.1.26 MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI ZANZIBAR (ZMA) ....283

**5.0 HITIMISHO** ....287

**VIAMBATISHO** ....289

## ORODHA YA MAJADWELI


Jadweli Nambari 1: Hali ya Utekelezaji wa mapendekezo ya hoja za ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa mwaka wa fedha uliopita 2021/2022 ....................7

Jadweli Nambari 2: Mifumo Jumuishi ya TEHAMA inayosimamiwa na eGAZ ....................18

Jadweli Nambari 3: Taasisi zilizobainika kuwa na dosari katika Sera, Miongozo na Mipango Mikakati ya TEHAMA ....................22

Jadweli Nambari 4: Taasisi zilizokaguliwa ambazo hazina Kamati Tendaji ya TEHAMA ....................24

Jadweli Nambari 5:Taasisi zilizowasilisha Nyaraka pungufu ....................25

Jadweli Nambari 6: Taasisi zenye mapungufu katika mgawanyo wa majukumu (SoD) ya TEHAMA ....................27

Jadweli Nambari 7: Taasisi zilizobainika kuwa na dosari katika "ICT Asset Register na "ICT risk register" za TEHAMA ....................29

Jadweli Nambari 8: Taasisi zilizobainika kuwa na udhaifu katika kudhibiti na kusimamia akaunti za watumiaji wa Mifumo (User Access Management) ....................31

Jadweli Nambari 9: Taasisi zilizobainika kuwa na dosari katika Mpango wa Kusimamia Mabadiliko yanayofanyika katika Mifumo (System Change Management Plan) ....................32

Jadweli Nambari 10: Taasisi zilizobainika kuwa na dosari katika tovuti zake ....................34

Jadweli Nambari 11: Taasisi ambazo hazina Active Directory ....................35

Jadweli Nambari 12: Taasisi ambazo hazina BCP, DRP na vile vile DRS ....36

Jadweli Nambari 13: Taasisi zenye dosari ya ufanyaji ya nakala za taarifa pamoja na kufanya majaribio ya nakala hizo ....................38

Jadweli Nambari 14: Taasisi zilizobainika kuwa na mapungufu kwenye Vitengo vya Habari ....................39

Jadweli Nambari 15: Taasisi zilizobainika kuwa na dosari katika udhibiti wa taarifa za mahudhurio kwa kutumia mfumo wa Biotime Attendance System ....................40

Jadweli Nambari 16: Taasisi zilizobainika kuwa na mapungufu katika Mpango wa Kusimamia, kudhibiti na kudumisha Mifumo .......42
Jadweli Nambari 17: Taasisi zilizokuwa hazijaunganisha mifumo yao na mifumo mengine husika kwa mujibu wa shughuli zao........................................................43
Jadweli Nambari 18: Taasisi ambazo hazijafanya tathmini ya kuchunguza na Majaribio ya Kupenya katika mifumo ..................44
Jadweli Nambari 19: Taasisi ambazo zina dosari katika kifaa cha kusimamia ulinzi na usalama wa Mtandao wa Afisi “Firewall”.....46
Jadweli Nambari 20: Taasisi ambazo zina dosari katika vifaa vyake vya kudhibti ulinzi na usalama wa mtandao “SOPHOS FIREWALL”..........................................................47
Jadweli Nambari 21: Taasisi zilizobainika kuwa na mapungufu katika kudhibiti na kusimamia usalama wa taarifa ndani ya kompyuta za Afisi ...........................................50
Jadweli Nambari 22: Taasisi ambazo hazina Mpango wa Usimamizi wa matukio (Incident Management Plan).....................51
Jadweli Nambari 23: Malipo ya huduma ya matumizi ya Mfumo wa e-Proz yanayolipwa kwa OZONE International LLC..............61
Jadweli Nambari 24: Malipo ya Huduma za Mfumo wa e-Proz kuanzia Novemba 2022 hadi Juni 2023...............................64
Jadweli Nambari 25: Mchanganuo wa malipo yaliyofanywa kwa Ozone International Limited...........................................79
Jadweli Nambari 26: Fofauti ya fedha zinazolipwa kwa kila mwezi............81
Jadweli Nambari 27: Mchanganuo wa malipo kwa Kampuni ya UBX, yanayotokana na mikato ya asilimia ya thamani ya miamala ya malipo..............................................84
Jadweli Nambari 28: Mfumo kushindwa kuzuwia wasambazaji walio na vyeti vya usajili vilvyomaliza muda wa kushiriki mashindano ya zabuni .........................................................87
Jadweli Nambari 29: Tofauti ya mapato yanayokusanywa baina ya mfumo wa ZanMalipo na mifumo mwengine. ...........................89

Jadweli Nambari 30: Hali halisi ya utekelezaji wa mahitaji ya ripoti ya watumiaji wa mfumo wa BAMAS ............................94

Jadweli Nambari 31: Idadi ya Kamera zilizofungwa na Afisi....................112

Jadweli Nambari 32: Zabuni zilizotolewa kwa watoa huduma ambao bei zao ni kubwa ukilinganisha na watoa huduma waliochaguliwa na mfumo wenye bei nafuu. ...........122

Jadweli Nambari 33: Kukosekana kwa vigezo vilivyotumika kumpata mzabuni wa 16 na kuwaacha wazabuni wa nafasi za awali wenye bei nafuu. .......................................123

Jadweli Nambari 34: Malipo yaliyolipwa kinyume na makubaliano ya Mkataba wa Mfumo wa Madini zaidi ya shilingi 877,174,447 ....................................................137

Jadweli Nambari 35: Idadi ya ankara zilizozalishwa kwa kujirejea na hali zake ...................................................................144

Jadweli Nambari 36: Uchambuzi wa bei na Kiwango cha huduma za "Internet" kwa Kampuni za Ndege kwa kipindi cha zaidi ya miezi 12.........................................157

Jadweli Nambari 37: Viwango vya gharama za uhifadhi wa vifaa vya kielekroniki (Charges for Coolocation Services) kutoka ZICTIA...................................................159

Jadweli Nambari 38: Huduma za kuhifadhi vifaa vya kielekroniki zinazotolewa na ZAA kwa makampuni binafsi pamoja na makadirio ya gharama kwa kipindi cha miezi 15.......................................................159

Jadweli Nambari 39: Tofauti ya takwimu za Taarifa kati ya Mfumo wa CRVS na Vitabu .....................................................198

Jadweli Nambari 40: Utofauti baina ya ripoti zinazopatikana kutoka kwenye mfumo wa Malalamiko (CMS) na Taarifa zinazopatikana kutoka kwenye ripoti za Utekelezaji wa Kitengo cha Uhusiano wa Umma ZURA...................................214

Jadweli Nambari 41: Tofauti ya Mapato yaliyokusanywa baina ya ECONEX na MUTM kwa mwaka wa fedha 2022/2023...........225

Jadweli Nambari 42: Miamala iliyofanyika kwa kupitia Ankara zenye mapungufu ....................................................226
Jadweli Nambari 43: Idadi ya kamera zilizofungwa katika Baraza la Manispaa Mjini ................................................231
Jadweli Nambari 44: Hali ya kupita muda wa matumizi wa mitungi ya kuzimia moto katika afisi mbali mbali za ZSTC Unguja na Pemba .........................................................232
Jadweli Nambari 45: Miamala ambayo haijatumia nambari ya udhibiti .....244
Jadweli Nambari 46 :Akaunti zisizotambulika ndani ya mfumo wa MUTM.........................................................274
Jadweli Nambari 47: Mashine za POS zinazofanyakazi ambazo hazijathibitishwa kupitia mfumo wa MUTM ............275
Jadweli Nambari 48: Orodha ya watumiaji wa ndani (internal users) ambao wamepewa haki ya kuwa wasimamizi wa mfumo.........................................................281

# ORODHA YA PICHA

Picha Nambari 1: Kanzidata ya toleo la majaribio ambayo inamaliza muda Januari 2024 ........................................................ 107

Picha Nambari 2: Kanzidata ya Mfumo wa HR-Payroll Information System haijasanidiwa kwa ajili ya kunasa Audit Logs ............... 108

Picha Nambari 3 : Mapunfugu ya usalama katika Seva ya Mfumo wa HR – Payroll Information System haiko salama ........... 110

Picha Nambari 4: Mfumo wa Usambazaji wa Kesi ukionesha Afisa wa Kitengo cha IC (Information Center) kufikia katika Moduli zote za Mfumo ..................................................... 119

Picha Nambari 5: Wazabuni ambazo wamekosa tuzo ya zabuni na hawakupewa taarifa ya sababu ya kukosa kupitia mfumo kwenye zabuni ya RFQ_2637.................................... 124

Picha Nambari 6: Mpangilio wa bei za huduma ya Mtandao (Internet) kutoka ZICTIA........................................................ 157

Picha Nambari 7: Muongozo kutoka katika mfumo wa ZAMIS namna ya kufanya malipo....................................................... 166

Picha Nambari 8: Ujumbe wa "An error has occured" unaojitokeza wakati wa utumiaji wa mfumo ................................................ 170

Picha Nambari 9: Ukurasa ambao utamuwezesha mtumiaji kuanza kujisajili ndani ya mfumo. .................................................. 171

Picha Nambari 10: Majina ya warithi waliojitokeza wakati wa usajili wa mfumo............................................................ 172

Picha Nambari 11: Neno siri la kuingia ndani ya mfumo wa ZAMIS ambalo ni namba kuanzia moja mpaka nne (1234).................... 173

Picha Nambari 12: Leseni ambayo haijamaliza taratibu za malipo katika mfumo wa ZIRS ambapo Afisa wa ZURA ana uwezo wa kuipakua kabla ya kufanyiwa malipo ......................... 210

Picha Nambari 13: Hali ya takwa la mfumo la kuingiza taarifa kuhusiana na kituo cha Mafuta wakati wa ukaguzi ingawa taarifa hizo zilishaingizwa katika mfumo wakati Kituo husika kinasajiliwa. ....................................................... 210

Picha Nambari 14: Eneo la kijiografia kinapopatikana Kituo cha Mafuta cha Bavuai ambapo mfumo unaonesha K "Chwaka Police Station" tofauti na uhalisia ambao ni kwamba Kituo husika kinapatikana eneo la "Mombasa Unguja" umbali wa zaidi ya kilomita 34.5 kutoka eneo linalosomeka katika mfumo. .................................... 212

Picha Nambari 15: Upatikanaji wa Mfumo wa usimamizi wa Malalamiko (Complaint Managent system) kupitia mtandao (WAN) bila ya kua na "SSL certificate" iliokua hai: ...... 218

## VIFUPISHO NA TAFSIRI

| | |
|---|---|
| AD | Active Directory |
| ADDENDUM | Mkataba wa Nyongeza. |
| AFROSAI-E | Jumuiya ya Taasisi Kuu za Ukaguzi kwa nchi za Kiafrika zinazozungumza lugha ya kiingereza. |
| BANKS | Mfumo Mkuu wa Usimamizi wa Biashara za Benki ya PBZ |
| BCP | Mpango wa Kuendeleza Huduma za Biashara |
| BOT | Benki Kuu ya Tanzania |
| CAG | Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali |
| CCTV | Mfumo wa Ulinzi unaotumia Kamera kurikodi matukio kwa picha |
| CD | Compact Disc |
| CIA | Confidentiality, Integrity and Availability |
| CIMIS | Mfumo Mkuu wa Usimamizi wa Biashara za Bima |
| CMS | Bohari Kuu ya Dawa |
| COBIT-5 | Control Objectives for Information and Related Technology. |
| DRP | Mpango wa Kukabiliana na Maafa |
| DRS | Disaster Recovery Site |
| DVD | Digital Video Disc |
| eGA | Mamlaka ya Serikali Mtandao Tanzania |
| eGAZ | Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar |
| eOffice | Mfumo wa Taarifa za Kiofisi za Serikali |
| e-Proz | Mfumo wa Manunuzi wa Serikali |
| EY | Ernst & Young |
| FuMIS | Mfumo Mkuu wa Usimamizi wa Mafao ya ZSSF |
| GOV | Governance |
| ICT | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| IFMIS | Mfumo Mkuu wa Usimamizi wa Fedha wa Serikali |
| INTOSAI | Shirika la Kimataifa la Taasisi Kuu za Ukaguzi |

| | |
|---|---|
| ISACA | Information Systems Audit and Control Association |
| ISO | International Organization for Standardization |
| ISP | Internet Service Providers |
| ISSAI | International Standards of Supreme Audit Institutions |
| IT | Information Technology |
| ITAC | Information Technology Application Control |
| ITAF | Information System Assurance Framework |
| ITGC | Information Technology General Control |
| ITGOV | Information Technology Governance |
| ITIL | Information Technology Infrastructure Library |
| ITPRJ | Information Technology Project |
| ITSEC | Information Technology Security |
| LAN | Local Area Network |
| MDAs | Wizara, Idara na Wakala wa Serikali |
| MoU | Mkataba wa Makubaliano (Memorandum of Understanding) |
| NAOT | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi Tanzania |
| NIDA | Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa Tanzania |
| OCAGZ | Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar |
| PAC | Picture archiving and Communication system. |
| PAM | Privileged Access Management |
| PBZ | Benki ya Watu wa Zanzibar |
| PDLC | Project Development Life Cycle |
| POS | Point Of Sales |
| PWC | PriceWaterhouse Coopers |
| RgoZ | Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar |
| SaaS | Mfumo Kama Huduma |
| SDLC | System Development Life Cycle |
| SHIPCO | Shirika la Meli Zanzibar. |

| | |
|---|---|
| SLA | Mkataba wa Kiwango cha Huduma |
| SMZ | Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar za Umeme |
| SUPRIMA | Mfumo Mkuu wa Usimamizi wa Biashara |
| SUZA | Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar |
| TAC | Tanzania Audit Corporation |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TOR | Hadidu Rejea |
| TRA | Mamlaka ya Usimamizi wa Mapato Tanzania |
| UPS | Kifaa cha Kuimarisha Mwenendo wa Umeme. |
| USD | Dola ya Kimarekani |
| VAPT | Vulnerability Assessment and Penetration Test |
| VAT | Kodi ya Ongezeko la Thamani |
| www | World Wide Web |
| ZANID | Kitambulisho cha Mzanzibar |
| ZBPRA | Wakala wa Kusajili Biashara Zanzibar |
| ZECO | Shirika la Umeme Zanzibar |
| ZIC | Shirika la Bima Zanzibar |
| ZICTIA | Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA Zanzibar |
| ZPC | Tume ya Mipango Zanzibar |
| ZPPDA | Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Zanzibar. |
| ZRA | Mamlaka ya Mapato Zanzibar. |
| ZSSF | Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar |

# SHUKURANI

Napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa jitihada zake za mara kwa mara anazoendelea kuzichukuwa ikiwa ni pamoja na kuweka msisitizo na kutoa maelekezo katika kufanya maboresho juu ya dosari mbali mbali zinazobainishwa katika Ripoti za Ukaguzi wa Hesabu za Serikali pamoja na hatua anazoendelea kuzichukua kutokana na hoja za ukaguzi zinazoibuliwa kuhusu matumizi ya fedha pamoja na usimamizi wa rasilimali za Umma.

Vile vile napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Viongozi Wakuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar akiwemo Makamu wa Kwanza wa Rais Mhe. Othman Masoud Othman, Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Hemed Suleiman Abdulla, pamoja na watendaji mbali mbali wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mashirikiano yao wanayokupatia katika utekelezaji wa majukumu yako ya kuwatumikia wananchi wa Zanzibar kwa lengo la kuwaletea maendeleo endelevu ya nchi yao.

Shukurani zangu za dhati ziende kwa Spika wa Baraza la Wawakilishi Mhe. Zubeir Ali Maulid, Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati zote za kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa kujitolea kwa dhati kujadili na kutoa mapendekezo pamoja na kufuatilia hatua zinazochukuliwa na Serikali kutokana na dosari zilizojitokeza na kuibuliwa katika Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika kusimamia uwajibikaji na utekelezaji wa majukumu ya watendaji katika sekta mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Aidha, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba Sheria, Utumishi na Utawala Bora Mhe. Mwalimu Haroun Ali Suleiman kwa kuniunga mkono na kunipa nguvu katika utekelezaji wa majukumu yangu ya kikatiba, pamoja na jitihada zake anazozichukuwa katika kusimamia misingi ya utawala bora na kupelekea kuimarika kwa nidhamu na uwajibikaji.

Vile vile nitoe shukurani zangu za dhati kwa Bodi ya Utumishi ya Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kusimamia maadili na nidhamu ya wafanyakazi wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kupelekea kuimarika kwa nidhamu na uwajibikaji katika utekelezaji wa majukumu ya kazi za ukaguzi.

Kwa namna ya kipekee niwashukuru wafanyakazi wote wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Afisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT), Tanzania Audit Corporation (TAC Associates), PriceWaterhouse Coopers (PWC), pamoja na Ernst & Young (EY) kwa kufanya kazi za ukaguzi kwa mashirikiano na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na juhudi zao mbali mbali walizozichukuwa hadi kukamilika kwa ripoti hii.

Mwisho, niwashukuru wale wote waliochangia kwa namna moja au nyengine kuanzia kazi za ukaguzi, ufuatiliaji wa maeneo mbali mbali yaliyokaguliwa hadi kukamilika kwa ripoti hii ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Aidha, nitakuwa mchache wa shukurani kama sitatambua jukumu la Vyombo mbali mbali vya Habari kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuutambulisha Umma juu ya kazi zinazofanywa na Afisi ya Mdhibiti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambapo matokeo na mapendekezo ya kazi hizo huwasilishwa kwa jamii kupitia kazi za ukaguzi zilizofanywa na Afisi hii.

Natumia fursa hii, kuwasihi wafanyakazi wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuendelea kuwa na moyo wa dhati katika kufanya kazi kwa bidii na kuongeza mashirikiano kwa ajili ya siku zijazo ili kuendelea kudumisha nidhamu ya Afisi ya Mdhibiti katika kutoa huduma za ukaguzi zenye ubora.

# DIBAJI



Ninafuraha kubwa ya kuwasilisha Ripoti ya Ukaguzi inayohusu Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa Mawizara, Taasisi na Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023. Wasilisho hilo ni kwa mujibu wa kifungu nambari 112(5) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 pamoja na kifungu nambari 46(1) cha Sheria Nambari 7 ya Ukaguzi wa Umma ya 2023, ambapo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibika kikatiba kukagua hesabu za Taasisi za Serikali na baadae kutoa taarifa zake za ukaguzi huo angalau mara moja kwa kila mwaka.

Taarifa hizo zitaelezea hali halisi ya mifumo ya TEHAMA katika Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inavyofanya kazi, inavyosimamiwa, dosari na changamoto zinazojitokeza pamoja na mapendekezo yanayotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika kuimarisha utendaji kazi wa mifumo hiyo pamoja na usalama wa taarifa za Serikali na kwa lengo la kupatikana kuongezeka kwa tija, ufanisi na huduma bora kwa wakati.

Kwa Mujibu wa Mamlaka niliyonayo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ni jukumu langu kutoa taarifa huru, zilizosahihi na zilizojitosheleza kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuhusiana na usimamizi wa fedha na matumizi sahihi ya rasilimali za Umma ambapo taarifa hizo baadae huwasilishwa Baraza la Wawakilishi kwa hatua za utekelezaji.

Nilifanya ukaguzi huu kwa kuzingatia Viwango kubalifu vya Kitaifa na Kimataifa vya Taasisi za Juu za Hesabu za Serikali (ISSAIs) vinavyotolewa na Shirika la Kimataifa la Taasisi za Juu za Ukaguzi (INTOSAI) ambazo zinahusu ukaguzi wa Sekta za Umma.

Ripoti hii imejumuisha Mifumo Sitini (60) niliyoikaguliwa katika Taasisi Ishirini na sita (26) nimebainisha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambapo mambo mbali mbali yamebainika katika maeneo yaliyokaguliwa kwa kuzingatia udhibiti na usalama wa mifumo ya TEHAMA uliopo kwenye Taasisi za Umma.

Baadhi ya maeneo niliyokagua yamebainika kuwa na mapungufu na baadhi yameonekana kuwa madhubuti kwa kuekewa usimamizi mzuri. Nashauri kudumisha maeneo yote yaliyo mazuri na kurekebisha dosari kwa viongozi wa taasisi za Umma kuendelea katika ripoti hii.

Maeneo Makuu kwa mwaka wa fedha 2022/2023 niliyofanya ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA ni matano (5) ikiwemo eneo la Utawala wa TEHAMA (IT Governance), Usimamizi wa Miradi ya TEHAMA (IT Project Management), Udhibiti wa Jumla wa TEHAMA (IT General Controls), Udhibiti wa Programu na Mifumo ya TEHAMA (IT Application Controls) pamoja na Usimamizi wa Usalama wa TEHAMA (IT Security Management).

Nilifanya ukaguzi huu kwa mujibu wa miongozo na Viwango vya Kitaifa (eGAZ, eGA) pamoja na viwango vya Kikanda na Kimataifa vya Ukaguzi (INTOSAI, ISSAI, ISA, ITAF, AFROSAI-E, ISACA, COBIT, ISO, ITL).

Aidha, nilitoa barua za ukaguzi "Management Letters" zinazoonesha dosari zilizobainika kwa kila taasisi niliyoikagua na kuainisha mapendekezo ya kutekeleza ili kuondoa dosari hizo kwa lengo la kuboresha na kutorejea kwa mara nyengine dosari hizo.

Nichukue fursa hii kwa dhati kumshukuru na kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dk. Hussein Ali. Mwinyi kwa jitihada zake anazoendelea kuzichukua katika kufuatilia Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa lengo la kusimamia na kuimarisha uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za Umma hali inayopelekea kuimarika kwa utawala bora.

.......................................................

**DKT. OTHMAN ABBAS ALI**

**MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI**

**ZANZIBAR**

## MUHTASARI

Katika awamu ya nane ya uongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayosimamiwa na Mhe. Dk. Hussein Ali Mwinyi, kumekuwa na mabadiliko makubwa ya kidijitali (Digital Transformation) ambapo Serikali imendelea kuwekeza katika masuala ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.

Aidha, kupitia awamu hiyo Mkakati wa Kidijitali (Digital Government Strategy) umeanzishwa na Serikali na kupelekea Taasisi mbali mbali za Umma kuimarika kiutendaji kwa kutoa huduma zilizo bora, zenye ufanisi na kwa wakati kwa wananchi wa Zanzibar kupitia Mifumo ya TEHAMA pamoja na Miundombinu mbali mbali ya kidijitali.

Katika kwenda sambamba na kasi ya mabadiliko hayo, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali nayo imefanya mabadiliko makubwa katika misingi ya utendaji kazi ili kuimarisha kazi za ukaguzi pamoja na kuunga mkono jitihada za Serikali, hali hii imepelelekea Afisi kufanya mabadiliko makubwa katika sheria yake na hatimae kuanzishwa kwa Sheria nambari 7 ya Ukaguzi wa Umma ya 2023.

Sheria hiyo imezingatia maswala yote ya kidijitali yanayohusiana na mabadiliko ya TEHAMA yaliyofanyika na yanayoendelea kufanyika katika Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuweka misingi imara ya kufanya kazi za ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA katika Taasisi za Umma kwa lengo la kuhakikisha kunakuwepo na usalama wa kutosha, usiri, uadilifu na upatikanaji wa taarifa sahihi zinazohifadhiwa ndani ya mifumo pamoja na miundombinu ya TEHAMA kwenye taasisi hizo.

Vile vile Afisi imehakikisha Taasisi za Umma zinakuwa na utaratibu mzuri wa kusimamia na kudumisha mifumo ya TEHAMA pamoja na kurahisisha utendaji kazi kupitia mifumo jambo ambalo litaweza kufanikisha kwa urahisi na kufikia kwa wakati malengo, dira, mikakati inayopangwa na hatimae kupelekea kuimarika kwa uchumi, kuongezeka kwa huduma bora katika jamii na kupatikana kwa maendeleo endelevu nchini.

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ukaguzi wa mifumo ya TEHAMA uliofanyika ulitathmini zaidi udhibiti na usalama wa taarifa uliopo kutokana na matumizi ya mifumo pamoja na rasilimali za TEHAMA, vile vile uliangalia hali halisi ya upatikanaji wa taarifa kwenye mifumo, usafirishaji wa taarifa kupitia mifumo na miundombinu mbali mbali ya TEHAMA pamoja na usimamizi wa miradi ya TEHAMA inayoanzishwa na Taasisi za Umma na miradi inayoanzishwa na Wakala wa Serikali Mtandao (eGAZ) kwa lengo la kutoa wa huduma bora kwa jamii.

Zaidi ya hivyo, ukaguzi ulifanya tathmini ya hali halisi ya kiwango cha ongezeko la makusanyo ya mapato kwa Serikali kupitia mifumo ya TEHAMA pamoja na udhibiti wa uvujaji wa mapato unaotokana na makusanyo yanayokusanywa nje ya mifumo au kuchezewa kwa mifumo na wasiohusika.

Ukaguzi huo ulifanyika kwa mujibu wa miongozo ya Kitaifa na Kimataifa ya ukaguzi wa mifumo ya TEHAMA ikiwemo Sera za TEHAMA za Taasisi husika, sera na miongozo ya Wakala wa Serikali Mtandao, Viwango Kubalifu pamoja na viwango vya kimataifa ambavyo ni ISSAI, AFROSAI-E, ISACA, ITAF, ISO, COBIT, ISA n.k. na vile vile ulizingatia athari za majanga " Risk Based Audit". Dosari zilizobainika zimewasilishwa kwa Maafisa Masuuli wa Taasisi za Umma kupitia barua za ukaguzi "Management Letters" kwa mujibu wa kiwango ambacho kumbukumbu, nyaraka, na baadhi ya taarifa zilizoombwa kwa madhumuni ya ukaguzi ziliwasilishwa kwa usahihi na kwa wakati kwa lengo la kuweza kufanyiwa kazi na wakaguzi wa mifumo.

Hivyo, ukaguzi uliweza kubaini uwepo wa mapungufu yanayotokana na usimamizi duni katika matumizi ya rasilimali za TEHAMA kwa baadhi ya taasisi za Umma, ambapo kwa kiasi kikubwa udhaifu huo umetokana na mapungufu katika udhibiti wa ndani wa TEHAMA (Poor IT Internal Controls) pamoja na kutofuatwa kikamilifu kwa Sera, Miongozo na Viwango viliyowekwa vya Matumizi sahihi ya TEHAMA vilivyowekwa kitaifa na kimataifa (Non compliance of Policies, guidelines, standards and frameworks).

Vile vile imebainika kuwepo uelewa mdogo kwa watumishi wa Umma kuhusiana na Vihatarishi vinavyotokana na mashambulizi ya mitandao (cyber attacks).

Uwepo wa dosari mbali mbali za kiusalama na dosari za kiutendaji kwenye Mifumo Jumuishi ya Serikali ambayo inasimamiwa na kuendeshwa na Wakala wa Serikali Mtandao, baadhi ya mifumo hiyo ni pamoja na Mfumo wa Manunuzi (e-Proz), Mfumo wa Afisi Mtandao (e-Office), Mfumo wa ZANMALIPO, Mfumo wa IFMIS/BAMAS na Mfumo wa Barua Pepe (GMS).

Aidha, imebainika uwepo wa dosari katika michakato ya Utengenezwaji, ununuzi au uanzishwaji wa Mifumo ya TEHAMA ambapo Taasisi nyingi zimekuwa hazifuati matakwa, taratibu na miongozo ya utengenezwaji wa Mifumo ya TEHAMA "System Development Life Cycle" au "Project Development Life Cycle". Miongoni mwa dosari kuu zilizobainika katika miradi ya TEHAMA ni kukosekana kwa nyaraka za mifumo ya TEHAMA kwa kila hatua utengenezwaji wake mfumo (system development phases) pamoja na kukosekana kwa mipango ya Usimamizi, uendeshaji na udumishaji wa mfumo baada ya kukamilika hatua za miradi hiyo.

Kushindwa kuzingatia vyema matakwa (mahitaji) ya watumiaji wa mifumo ili kuhakikisha kunapatikana mifumo iliyobora yenye tija na ufanisi na kufanya kazi kama iliyohitajiwa kisheria.

Aidha, imebainika taasisi nyingi kuwa na udhaifu katika kudhibiti kuimarisha usalama wa taarifa kutokana na kwenda kinyume na matakwa ya viwango vya Kimataifa vya ulinzi na usalama wa taarifa (data) katika Taasisi (ISO/IEC 27001).

Kukosekana kwa muunganiko wa moja kwa moja wa mifumo ya TEHAMA baina ya vyanzo vya mapato na taasisi zinazokusanya mapato ili kuongeza ufanisi wa makusanyo na kuimarisha udhibiti wa mapato dhidi ya upotevu na uvujaji wa mapato unaotokana na kukusanywa mapato nje ya mifumo kwa njia ya kawaida.

## MAPENDEKEO KWA TAASISI ZA UMMA (MDAs)

**Ninapendekeza kwa Wizara, Idara na Mawakala wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (MDAs) kufanya yafuatayo:**

(a) Kuzingatia na kufuata kikamilifu Sheria, kanuni, sera, miongozo, taratibu pamoja na viwango kubalifu vya kitaifa na kimataifa vya TEHAMA vinavyopaswa kutumika katika Taasisi za Umma kwenye utekelezaji wa Miradi ya TEHAMA kama vile kwenye ununuzi, utengenezwaji, usimamizi, uboreshaji, udhibiti, uendeshaji na udumishaji wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA. Vile vile kuishirikisha kikamilifu Wakala wa Serikali Mtandao (eGAZ) kwenye hatua za michakato hiyo ili kuweza kupatikana ushauri uliobora wa kiufundi, usimamizi mzuri wa miradi hiyo na hatimae kuweza kuwa na mifumo iliyo salama, yenye tija na inayolingana na thamani halisi ya fedha ambayo itarahisisha kufikia malengo yaliyokusudiwa na Taasisi husika.

(b) Kuandaa mpango imara wa ufuatiliaji na utekelezaji wa mapendekezo ya hoja za ukaguzi zilizobainishwa katika Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili kuimarisha shughuli za Taasisi na kufikia malengo kwa wakati na kwa ufanisi.

(c) Kutoa kipaombele kwenye matumizi ya TEHAMA kwa kuandaa bajeti za kutosha za utekelezaji wa shughuli za TEHAMA katika Taasisi pamoja na kuwajengea uwezo Maafisa wa TEHAMA kuhusiana na usimamizi bora, uendeshaji, uboreshaji na udumishaji wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA jambo ambalo litasaidia kupatikana huduma bora kwa wananchi wa Zanzibar kupitia mabadiliko ya TEHAMA.

(d) Kuandaa mpango maalum wa mafunzo ya usalama wa matumizi ya mtandao (cyber security awareness programme) kwa wafanyakazi wote wa Taasisi angalau mara moja kwa mwaka ili kupata uelewa juu ya vihatarishi vinavyotokana na mitandao, jambo ambalo litaweza kusaidia kuongeza udhibiti kwenye matumizi ya vifaa vya TEHAMA vya Taasisi pamoja na kuimarisha usalama wa taarifa za afisi na taarifa binafsi za watumishi dhidi ya mashambulizi yanayotolewa na vihambatishi vya mitandao kama vile malwares, virusi phishing, hacking n.k. kimtandao (cyber attacks) ambayo ni malwares, viruses, phishing, hacking n.k.

(e) Taasisi za umma zinazohusika na makusanyo ya mapato kuendelea na jitihada za kuimarisha usalama na utendaji kazi wa mifumo ya mapato kwa kufanya maboresho kwenye mifumo yao ili kuendana na wakati, kuongeza ufanisi wa makusanyo na kuziba mianya ya upotevu (uvujaji) wa mapato dhidi ya watumiaji wasiohusika, wasiokuwa na maadili, wasiojuulikana pamoja na wanaokusanya mapato nje ya mifumo.

(f) Kuchukua jitihada za kutumia mifumo jumuishi inayoanzishwa na Wakala wa Serikali Mtandao ili kuweza kurahisisha mawasiliano, kuongeza usalama wa taarifa za Taasisi pamoja na kuongeza ufanisi katika usimamizi na udhibiti wa mapato na matumizi ya fedha.

## MAPENDEKEZO KWA WAKALA WA SERIKALI MTANDAO ZANZIBAR (EGAZ)

**Ninapendekeza kwa Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar (eGAZ) kufanya yafuatayo:**

a) Kuendelea na jitihada za kufanya mafunzo ya uelewa (Awareness Programme) kwenye Taasisi za Umma kuanzia ngazi ya Maafisa Masuuli, viongozi wa Taasisi za Umma hadi watendaji juu ya umuhimu wa matumizi bora, sahihi na salama ya rasilimali za TEHAMA ikiwemo vifaa, miundombinu na mifumo ya TEHAMA, pamoja na kutoa elimu kuhusiana na athari zinazotokana na matumizi yasiofaa kwenye rasilimali hizo pamoja na athari zinazotokana na mashambulizi ya mitandao (cyber attacks).

b) Kuongeza kasi ya kutoa miongozo, sera, viwango, taratibu, majukwaa ya kidigitali (platforms) na matoleo mbali mbali yatakayotumika kwenye Taasisi za Umma katika kuhakikisha kunakuwa na uwajibikaji wa utekelezaji wa shughuli za TEHAMA ili kufikia lengo la kuimarisha ulinzi wa taarifa, usimamizi wa miradi, uboreshaji na udumishaji wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA kwa mujibu wa sera, viwango na miongozo iliyopo.

c) Kuanzisha Mifumo Jumuishi itakayokuwa na umiliki kamili (Full Ownership & Source Codes) kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambapo mifumo hiyo itatengenezwa na kutumika kwa mujibu wa mahitaji ya watumiaji wa Zanzibar na kwa kuzingatia mazingira halisi ya utendaji wa kazi kwenye Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Aidha, mifumo hiyo pamoja na miundombinu yake ihifadhiwe katika Kituo Kikuu cha Taarifa cha Serikali (Zanzibar National Data Center) kinachosimamiwa na ZICTIA ambapo eGAZ kwa kushirikiana na ZICTIA zitasimamia, zitahifadhi na kudumisha mifumo hiyo ikiwemo kutengeneza nyaraka zote zinazohitajika kwa ajili ya uanzishaji, usimamizi, uendeshaji na udumishaji wa mifumo hiyo (system documents). Baadhi ya Mifumo Jumuishi iliyokusudiwa ni pamoja na Mfumo wa Manunuzi wa Umma (e-Proz), Mfumo wa baruapepe wa Serikali (GMS), Mfumo wa Afisi Mtandao (e-Office), Mfumo wa Usimamizi wa Mapato na Matumizi wa Serikali (BAMAS), Mfumo wa Serikali wa Usimamizi wa Taarifa za Afya (e-Heath), Mfumo wa kusimamia na kudhibiti malipo ya Serikali (ZanMalipo) n.k.

d) Kwa kuzingatia usiri, usalama, unyeti na umuhimu wa taarifa za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, si utaratibu mzuri kwa Wakala wa Serikali Mtandao kukodi au kuazima Mifumo ya TEHAMA kutoka Kampuni binafsi au Serikali nyengine na kuitumia mifumo hiyo kwa kutoa huduma kwenye Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwani kufanya hivyo kunaweza kuondoa usiri na usalama wa taarifa za Serikali ambazo zinaingizwa, zinachakatwa na kuhifadhiwa ndani ya mifumo hiyo zikiwemo taarifa za siri kama vile taarifa za matumizi ya fedha za nchi, taarifa za mapato ya nchi, taarifa za mawasiliano ya nchi, barua pamoja na nyaraka mbali mbali za taasisi, hasa ikizingatiwa kwamba mifumo hiyo inamilikiwa, kuhifadhiwa na kusimamiwa na wenyewe kwenye nchi zao ambapo ni nje ya mipaka ya Zanzibar.

e) Kuunganisha Mifumo ya Makusanyo ya Mapato na kutumia vifaa vya kisasa vya makusanyo kwenye vyanzo vikuu vya mapato kama vile Uwanja wa Ndege, Bandarini, Mahotelini, Madukani n.k ili kudhibiti upotevu wa mapato na kuepuka kukusanya nje ya mifumo. Vile vile kuunganisha mifumo inayofanana kwenye utendaji kazi ili kurahisisha mawasiliano ya taarifa, kuongeza kasi ya utoaji wa huduma bora kwa wakati kwenye jamii pamoja na kuongeza udhibiti wa usalama wa taarifa dhidi ya kuchezewa au kubadilishwa na wasiohusika.

f) Kuwajengea uwezo watendaji wa Wakala wa Serikali Mtandao kwenye taaluma mbali mbali za TEHAMA (Professional Certifications) pamoja na kuongeza ajira mpya za wataalamu wa TEHAMA kwenye Taasisi hiyo ili kuongeza idadi ya wataalamu itakayopelekea eGAZ kufanya kazi zake za kutoa huduma, ushauri wa kitaalamu na mafunzo kwa ufanisi, weledi na kwa wakati na hatimae kupatikana tija iliyokusudiwa pamoja na kuondoa changamoto iliyopo ya upatikanaji wa miongozo hafifu, kiwango kidogo cha ushauri na uhaba wa kutoa mafunzo kuhusiana na Uendeshaji na Utawala wa TEHAMA (IT Governance and Frameworks) kwenye Taasisi za Umma.

g) Kuishirikisha kikamilifu Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa lengo kupatikana ushauri pamoja na maoni ya kisheria kwenye rasimu za Mikataba ya Utengenezwaji wa Mifumo ya TEHAMA ambayo Wakala wa Serikali Mtandao huingia na Kampuni mbali mbali zinazotoa huduma ya Mifumo kwa Serikali kama vile Kampuni ya UBX, OZONE international n.k. Vile vile kuzingatia matakwa ya Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 pamoja na Kanuni zake za 2021.

Kufanya hivyo kutaweza kusaidia Wakala kuingia mikataba yenye maslahi mapana kwa Serikali na Wananchi kwa ujumla na hatimae kuepusha Serikali kuingia hasara ya kulipa fedha nyingi kwa Watoa huduma kulingana na tija na thamani ya huduma inayotolewa.

Hivyo, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inatarajia kwamba dosari zilizobainishwa zitafanyiwa kazi kwa mujibu wa sheria, miongozo ya Taasisi na Serikali pamoja na viwango vya kimataifa ili kuongeza udhibiti na usalama katika usimamizi wa taarifa zilizomo ndani ya Mifumo ya TEHAMA na hatimae kupatikana kwa ufanisi na tija katika matumizi ya TEHAMA kwa Serikali.




# SURA YA KWANZA



# 1.0 UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA KATIKA TAASISI ZA UMMA

## 1.1 Utangulizi

Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023 umefanyika katika Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambazo ni Mawizara, Maidara, Mashirika na Taasisi zinazojitegemea. Ukaguzi umefanyika kwa mujibu wa kifungu nambari 112 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, Sheria nambari 7 ya Ukaguzi wa Umma ya 2023 pamoja na kuzingatia miongozo, vigezo na viwango kubalifu vya Kitaifa na Kimataifa vya Taasisi za Juu za Hesabu za Serikali (ISSAIs) vinavyotolewa na Shirika la Kimataifa la Taasisi za Juu za Ukaguzi (INTOSAI) ambazo zinahusu ukaguzi wa Sekta za Umma.

## 1.2 Mamlaka ya kufanya Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amepewa Mamlaka ya kufanya ukaguzi kwa mujibu wa kifungu nambari 112 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, Sheria Nambari 7 ya Ukaguzi wa Umma ya 2023, Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 na kama ilivyoainishwa katika aya ya A2.2 na A4 ya muongozo wa Kimataifa wa Ukaguzi wa TEHAMA-ISSAI 5300.

## 1.3 Upeo wa Ukaguzi

Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA umefanyika kwa kuzingatia athari zinazoweza kujitokeza katika maeneo hatarishi ya mifumo na miundombinu ya TEHAMA "risk based audit" ambapo kiwango cha athari kimebainika kwa mujibu wa uchambuzi wa nyaraka na taarifa zilizoombwa na kuwasilishwa kwa ukaguzi, vile vile kutokana na kufanyika majadiliano na wahusika pamoja na kufanya mapitio ya mifumo na miundombinu mbalimbali ya TEHAMA ili kuangalia udhibiti na usalama wa taarifa zinazochakatwa na kuhifadhiwa ndani yake.

Ukaguzi huu umejumuisha taarifa za Mifumo Sitini (60) iliyokaguliwa katika Taasisi Ishirini na Sita (26) za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambapo hoja zake zimebainishwa katika ripoti hii pamoja na kutolewa ufafanuzi wa athari na mapendekezo kwa Taasisi zilizokaguliwa.

Kwa ujumla ukaguzi uliangalia maeneo tofauti ikiwemo Utawala wa TEHAMA (ICT Governance), Udhibiti wa Ujumla wa TEHAMA (IT General Controls), Udhibiti wa Programu (Application Controls), Usimamizi wa Vihatarishi vya TEHAMA (ICT Risk Management), Usimamizi wa Usalama wa Mifumo na Miundombinu ya TEHAMA (ICT Security Management), Usimamizi wa Matukio (Incident Management), Usimamizi wa Mabadiliko ya Programu (Program Change Management), Utaratibu wa Mananunuzi ,Utengenezaji na Udumishaji wa Mifumo, (System Acquisition, Development and Management), pamoja na uzingatiaji wa Sheria, Sera, Kanuni na Miongozo iliyopo kitaifa na kimataifa (Compliance with Standards, Policies & Guidelines).

## 1.4 Malengo ya Ukaguzi

Lengo kuu la kufanya ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa Taasisi za Umma ni kutoa uhakika iwapo Mifumo ya Habari pamoja na Miundombinu ya TEHAMA iliyopo kwenye Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kiasi gani ina uwezo wa kulinda taarifa, kutunza usiri na kudumisha uadilifu wa taarifa zinazohifadhiwa ndani yake na vile vile kutoa taarifa wakati zinapohitajika pamoja na kusaidia kufikia malengo ya Taasisi kwa uweledi na ufanisi na hatimae kupatikana huduma bora pamoja na kukua kwa maendeleo ya kiuchumi nchini.

Aidha, ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA ulikuwa na malengo mengine maalum ikiwemo kufanya mambo yafuatayo: -

- Kufanya tathmini ya usimamizi, uendeshaji na utunzaji wa mifumo ya TEHAMA pamoja na kupima udhibiti uliopo kwenye mifumo na miundombinu ya TEHAMA inayochakata, kusafirisha na kuhifadhi taarifa katika Taasisi.
- Kufanya tathmini ya kuhakikisha uwepo wa usiri na uadilifu katika matumizi ya mifumo ya TEHAMA na kuangalia kwa kiwango gani TEHAMA inavyosaidia Taasisi za Umma katika kufikia malengo waliyojipangia pamoja na kuongeza tija, ufanisi na uchumi kwenye utendaji wa shughuli za Taasisi hizo.
- Kuhakikisha kunafuatwa kwa Sheria, kanuni, sera, miongozo, taratibu na viwango vya Kitaifa na kimataifa vya TEHAMA.

- Kufanya tathmini ya mifumo ya TEHAMA kwa kupima jinsi gani mifumo inavyosaidia Taasisi katika kudhibiti, kuimarisha na kuongeza tija kwenye michakato ya makusanyo ya mapato kwa Serikali.
- Kupima thamani halisi ya kiwango cha fedha kinachotumika katika kutengeneza au kuanzisha mifumo ya TEHAMA kwa kulinganisha na huduma zinazotolewa kupitia mifumo hiyo (Value for Money).

## 1.5 Sera, Viwango na Miongozo iliyotumika

Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni mwanachama wa Shirikisho la Kimataifa la Taasisi Kuu za Ukaguzi Duniani (INTOSAI) na Shirikisho la Taasisi Kuu za Ukaguzi Barani Afrika zinazozungumza Lugha ya Kingereza (AFROSAI-E). Ushiriki huo unapatikana kupitia nafasi ya Afisi ya Taifa ya Ukaguzi Tanzania (NAOT) kwa niaba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Ukaguzi uliofanyika umezingatia matakwa ya kimaadili katika kupanga na kufanya ukaguzi ili kupata uhakika wa kutosha juu ya udhibiti na ufanisi wa utendaji wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA.

Ukaguzi wa TEHAMA ulifanyika kwa kufuata na kuzingatia Sheria, miongozo, sera na viwango vya ukaguzi vya kitaifa na kimataifa ikiwemo Sera za Taasisi husika, miongozo ya Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar (eGAZ), Sheria ya Usimamizi wa Fedha na Kanuni zake za Zanzibar, miongozo ya Mamlaka ya Serikali Mtandao Tanzania (eGA) ikiwa ni kama taratibu zinazokubalika kitaifa (best practises), miongozo na Viwango vya Kimataifa ikiwemo COBIT, ITIL, ISACA, ITAF, AFROSAI-E, INTOSAI, ISA, ISO n.k.

## 1.6 Njia na Mbinu za Ukaguzi Zilizotumika

Katika kukagua mifumo na miundombinu ya TEHAMA kwa Taasisi za Umma ukaguzi ulitumia njia pamoja na mbinu mbali mbali kama zilivyoainishwa hapo chini:-

a) Kufanya mapitio (review) ya nyaraka mbali mbali za Taasisi ikiwemo Sheria, Kanuni, Sera, Miongozo, Mpango Mkakati pamoja na nyaraka zinazohusiana na mifumo ya TEHAMA ya Taasisi husika.

b) Kufanya Tathmini ya vihatarishi (risk assessment) katika Mifumo na Miundombinu ya Taasisi.

c) Kufanya mapitio ya miundombinu ya TEHAMA iliyopo kwa lengo la kupima utendaji kazi na udhibiti wa ndani (Internal Controls) uliowekwa.

d) Kufanya uhakiki wa utendaji kazi wa miundombinu ya TEHAMA inayotumika kwa ajili ya kuhifadhia taarifa kwa lengo la kujiridhisha usahihi na usalama wake.

e) Kufanya mahojiano na majadiliano na watendaji katika Idara, divisheni na vitengo mbali mbali vya Taasisi.

f) Kufanya uchambuzi wa Taarifa na miamala mbalimbali ya Taasisi (Data analytics).

# SURA YA PILI



# 2.0 MUHTASARI WA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA HOJA ZA UKAGUZI KWA MWAKA WA FEDHA ULIOPITA

Sura hii inaainisha kwa muhtasari mapendekezo ya Ripoti ya Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa mwaka uliopita na hatua zake za utekelezaji zilizopo. Uwajibikaji na utawala bora hautafikiwa kama hapatakuwa na jitihada binafsi kutoka kwa maafisa masuuli husika kutekeleza mapendekezo ambayo niliyatoa.

Aidha, ningependa kuifahamisha Serikali kwamba mapendekezo ninayoyatoa mara kwa mara yana lengo la kuhakikisha kwamba kunakuwa na hatua madhubuti na makini katika kuimarisha mifumo ya TEHAMA kwa lengo la kurahisisha ukusanyaji na utumiaji wa mapato ya rasilimali za umma. Mapendekezo hayo pia yanalenga kuhakikisha matumizi bora ya mifumo ya TEHAMA yanaidhinishwa na kusimamiwa na wenye mamlaka na hatimae hutumika kwa malengo yaliyokusudiwa. Kwa hali hiyo na kwa kuzingatia sheria na kanuni katika utumiaji wa mifumo ya TEHAMA thamani ya fedha, tija na ufanisi vinaweza kufikiwa.

Hivyo, nimeona ni vyema kuyarudia tena mapendekezo niliyoyatoa katika ripoti zilizopita ambayo yametekelezwa, hayajatekelezwa au yametekelezwa kwa kiwango kidogo na taasisi husika.

## 2.1 Tathmini ya utekelezaji wa mapendekezo ya hoja za mwaka uliopita

Tathmini niliyoifanya kwenye hali ya utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi ya Mwaka Uliopita nimebaini jumla ya mapendekezo 473 yalitolewa kwa Taasisi 16 za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambazo zimekaguliwa na kutolewa maoni katika ripoti za ukaguzi. Kati ya mapendekezo hayo jumla ya mapendekezo 302 yaliweza kutekelezwa kikamilifu na kuondolewa ambayo ni sawa na asilimia 63.85, mapendekezo 93 yapo katika hatua ya utekelezaji sawa na asilimia 19.66, hata hivyo, mapendekezo 34 bado hayajatekelezwa ambayo ni sawa na asilimia 7.19 na mapendekezo 27 yamejirudia sawa na asilimia 5.71, vile vile mapendekezo 17 yamepitwa na wakati sawa na asilimia 3.59.

Ukaguzi umebaini uwepo wa baadhi ya dosari zilizojirejea katika ripoti ya ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ambazo dosari hizo zilibainishwa katika ripoti ya ukaguzi ya mwaka wa fedha 2021/2022. Hali hii inaonesha kuwepo kwa udhaifu katika kufanyiwa kazi kwa baadhi ya mapendekezo yanayotolewa kwenye ripoti za ukaguzi ambapo lengo na madhumuni ya mapendekezo hayo ni kufanya maboresho na kurekebisha dosari zilizobainishwa kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utekelezaji na usimamizi wa Mifumo na miundombinu ya TEHAMA katika Taasisi za Umma.

Baadhi ya Mapendekezo ambayo hayakutekelezwa na yanayoendelea na hatua za utekelezaji ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 1: Hali ya Utekelezaji wa mapendekezo ya hoja za ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa mwaka wa fedha uliopita 2021/2022**

| Namba | Hoja Namba | Hoja ya Ukaguzi | Hali Halisi ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi |
|---|---|---|---|
| **TAASISI YA SAYANSI NA TEKNOLOJIA YA KARUME (KIST)** | | | |
| 1. | 10.9.1.1 | Kukosekana kwa mpango wa matumizi endelevu ya TEHAMA | Haijatekelezwa |
| 2. | 10.9.1.2 | Uhaba wa vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya kuhifadhia taarifa za Mifumo ya TEHAMA | Hoja ipo kwenye utekelezaji |
| **BENKI YA WATU WA ZANZIBAR (PBZ)** | | | |
| 3. | 14.2.1.5 | Kuendelea kuwepo kwa dosari katika Utawala wa TEHAMA (IT Governance) | Ipo katika hatua za utekelezaji. |
| **SHIRIKA LA MELI ZANZIBAR** | | | |
| 4. | 18.10.1.1 | Udhaifu uliobainika kwenye mfumo wa Voucher System | Ipo katika hatua ya utekelezaji |
| 5. | 18.10.1.2 | Mapungufu yaliyopo kwenye mfumo wa Quick Book | Ipo katika hatua ya utekelezaji |
| 6. | 18.10.1.3 | Matumizi hafifu ya mfumo wa mishahara | Haijatekelezwa |
| 7. | 18.10.1.4 | Mapungufu kwenye mfumo wa Container Management System (CMS). | Ipo katika hatua ya utekelezaji |

| Namba | Hoja Namba | Hoja ya Ukaguzi | Hali Halisi ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi |
|---|---|---|---|
| 8. | 18.10.1.10 | Udhaifu wa ulinzi na kutumika kwa programu za bure kwenye vifaa vya TEHAMA | Ipo katika hatua ya utekelezaji |
| 9. | 3.1.1.1 | Dosari katika Muendelezo wa Huduma za Biashara na Usimamizi wa Uokoaji wa Maafa (Business Continuity and Disaster Recovery Management) | Hazijatekelezwa |
| 10. | 3.1.1.2 | Kutokuwepo kwa Sera na Miongozo ya TEHAMA, Mipango Mikakati, Mipango ya Uwezeshaji ya TEHAMA kuhusiana na Utawala wa TEHAMA (ICT Governance) | Ipo katika hatua ya utekelezaji |
| 11. | 3.1.1.4 | Kukosekana kwa daftari la kusajili Rasilimali za TEHAMA, Vihatarishi pamoja na Hitilafu zinazotokea kwenye TEHAMA (ICT Asset, Risk and Issue Register) | Ipo katika utekelezaji |
| 12. | 3.1.1.7 | Kukosekana kwa baadhi ya nyaraka zilizoombwa kwa ajili ya ukaguzi | Haijatekelezwa |
| 13. | 3.1.1.8 | Kutofanyika kwa tathmini ya mahitaji ya mafunzo na mpango wa mafunzo ya TEHAMA kwa watumishi | Haijatekelezwa |
| 14. | 3.1.1.9 | Kukosekana kwa mgawanyo wa majukumu (Segregation of Duties) | Haijatekelezwa |
| 15. | 3.1.1.10 | Kukosekana kwa mafunzo ya usalama katika matumizi ya TEHAMA (Lack of IT Security Awareness Program) | Ipo katika utekelezaji |

| Namba | Hoja Namba | Hoja ya Ukaguzi | Hali Halisi ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi |
|---|---|---|---|
| **CHUO KIKUU CHA TAIFA ZANZIBAR (SUZA)** | | | |
| 16. | 9.4.1.1 | Matumizi hafifu ya Mfumo wa SAGE kwenye kufanya Malipo. | Ipo katika hatua ya utekelezaji |
| 17. | 9.4.1.3 | Kutokuwepo kwa mikataba ya utengenezaji na utoaji wa msaada wa kitaalamu kwenye Mfumo wa OSIM na SAGE. | Ipo katika hatua ya utekelezaji |
| 18. | 9.4.1.4 | Mazingira yasiyoridhisha katika Vyumba vya kuhifadhia Mifumo ya Tehama. | Ipo katika hatua ya utekelezaji |
| 19. | 9.4.1.5 | Mapungufu yaliyobainika kwenye Kamera za ulinzi (CCTV) | Ipo katika hatua ya utekelezaji. Manunuzi yapo kwenye mfumo wa eProz. |
| 20. | 9.4.1.6 | Uhaba na uchakavu wa Kompyuta za kufundishia wanafunzi pamoja na Kompyuta za wafanyakazi wanaotumia mifumo na shughuli nyengine za kiutendaji katika Vyuo vya SUZA | Ipo katika hatua ya utekelezaji. Manunuzi yapo kwenye mfumo wa eProz. |
| 21. | 9.4.1.10 | Udhaifu wa ulinzi na Kutumia programu za bure kwenye vifaa vya TEHAMA | Ipo katika hatua ya utekelezaji. |
| 22. | 9.4.1.11 | Mapungufu yaliyobainika katika mfumo wa OSIM | Ipo katika hatua ya utekelezaji. |
| 23. | 9.4.1.11 | Tovuti ya SUZA kutofanyiwa uboreshwaji kwa wakati | Ipo katika hatua ya utekelezaji. |
| **WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII JINSIA WAZEE NA WATOTO** | | | |
| 24. | 10.10.1.3 | Mfumo kutohifadhiwa kwenye chumba maalum cha Seva. | Haijatekelezwa |
| 25. | 10.10.1.4 | Kuendelea kutumika kwa Mfumo wa Microsoft Access Datadase Wazee | Haijatekelezwa |
| 26. | 10.10.1.5 | Kukosekana kwa udhibiti wa uthibitishaji/ uidhinishaji wa taarifa zinazoingizwa kwenye Mfumo. | Haijatekelezwa |

| Namba | Hoja Namba | Hoja ya Ukaguzi | Hali Halisi ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi |
|---|---|---|---|
| 27. | 10.10.1.6 | Uwepo wa nakala za taarifa (dublicate data). | Haijatekelezwa |
| 28. | 10.10.1.8 | Udhaifu wa udhibiti wa Mfumo kwenye kuufikia (System access control) | Haijatekelezwa |
| 29. | 10.11.1.1 | Kutotumika kwa Mfumo wa ZUPS MIS kufanya malipo ya kielektroniki | Haijatekelezwa |
| 30. | 10.11.1.2 | Kukosekana kwa udhibiti wa uthibitishaji/ uidhinishaji wa taarifa zinazoingizwa kwenye Mfumo | Haijatekelezwa |
| 31. | 10.11.1.4 | Usajili wa taarifa za Wazee kutofanyika kwenye Seva moja kwa moja kupitia mtandao. | Haijatekelezwa |
| 32. | 10.11.1.5 | Kukosekana kwa mpango wa matuumizi endelevu ya Mfumo ikiwa ni pamoja na mafunzo ya Mfumo wa ZUPS MIS. | Haijatekelezwa |
| 33. | 10.11.1.7 | Mfumo kuruhusu usajili wa baadhi ya Wazee wasiokidhi matakwa ya Kisheria (Validation). | Haijatekelezwa |
| 34. | 10.11.1.8 | Kutozingatiwa mgawanyo wa majukumu kwenye Mfumo (Segregation of Duties) | Haijatekelezwa |
| 35. | 10.11.1.9 | Kukosekana kwa ripoti mbalimbali za taarifa za Wazee kwenye Mfumo. | Haijatekelezwa |
| 36. | 10.11.1.10 | Kukosekana kwa mawasiliano baina ya taarifa za Unguja na zile za Pemba ndani ya Mfumo wa ZUPS MIS | Haijatekelezwa |
| 37. | 10.11.1.12 | Kutozingatiwa kwa usahihi wa taarifa zinazoingizwa katika Mfumo. | Ipo katika hatua za utekelezaji |

| Namba | Hoja Namba | Hoja ya Ukaguzi | Hali Halisi ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi |
|---|---|---|---|
| 38. | 10.11.1.13 | Kutotumika kwa alama za vidole katika kufanya malipo kwa Wazee. | Haijatekelezwa |
| 39. | 10.11.1.14 | Kutosajiliwa kwa POS kwenye Mfumo wa ZUP MIS | Haijatekelezwa |
| 40. | 10.11.1.15 | Uwezo mdogo wa POS katika kuhifadhi taarifa za usajili wa Wazee. | Haijatekelezwa |
| 41. | 10.11.2.1 | Kukosekana kwa "ICT Streering Committee Charter" na "ICT Steering Committee". | Ipo katika hatua za utekelezaji |
| 42. | 10.11.2.4 | kukosekana kwa mpango wa kuchukua nakala za taarifa za mifumo (Backup Plan). | Haijatekelezwa |
| 43. | 10.11.2.5 | Kutopatikana kwa ripoti za majaribio nakala za taarifa za mifumo (Backup testing report). | Haijatekelezwa |
| 44. | 10.11.2.7 | Kutokuwepo kwa mpango wa kuendelea Biashara (business Continuity Plan). | Haijatekelezwa |
| 45. | 10.11.2.8 | Kukosekana kwa mpango wa kukabiliana na maafa (Disaster Recovery Plan). | Haijatekelezwa |
| 46. | 10.11.2.9 | Kutokuwepo kwa makubaliano ya msaada wa ufundi wa Mfumo wa ZIPS MIS (Service level Agreement). | Haijatekelezwa |
| 47. | 10.11.2.10 | Kukosekana kwa Sera za TEHAMA (ICT Policy). | Ipo katika hatua za utekelezaji |
| 48. | 10.11.2.11 | Kukosekana kwa eneo la kuendeleza Mfumo baada ya maafa (Disaster Recovery Site). | Haijatekelezwa |
| 49. | 10.11.2.12 | Udhaifu katika utekelezaji wa mkataba wa kutengeneza Mfumo wa ZUPS-MIS | Haijatekelezwa |

| Namba | Hoja Namba | Hoja ya Ukaguzi | Hali Halisi ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi |
|---|---|---|---|
| **MANISPAA YA MAGHARIBI A** | | | |
| 50. | 11.2.6 | Kukosekana kwa tovuti ya Taasisi kwaajili ya kutoa taarifa mbalimbali | Ipo katika hatua za utekelezaji |
| **OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM** | | | |
| 51. | 11.5.1.1 | Kukosekana kwa kumbukumbu za gharama zilizotumika kutengeneza mfumo wa MUTM | Haijatekelezwa |
| 52. | 11.5.1.5 | Kukosekana kwa muongozo rasmi wa vigezo vya POS | Ipo katika hatua za utekelezaji |
| 53. | 11.5.1.11 | Kukosekana kwa Sera za TEHAMA | Ipo katika hatua za utekelezaji |
| 54. | 11.5.1.12 | Kutokuepo kwa Mpango Mkakati ya TEHAMA | Ipo katika hatua za utekelezaji |
| 55. | 11.5.1.14 | Kukosekana kwa Mpango wa kuendeleza biashara (Business Continuity Plan) | Ipo katika hatua za utekelezaji |
| 56. | 11.5.1.15 | Kukosekana kwa mpango wa kukabiliana na Maafa (Disaster Recovery Plan). | Ipo katika hatua za utekelezaji |
| 57. | 11.5.1.16 | Mpango wa kufanya mabadiliko kwenye mfumo (System Change Management Plan). | Ipo katika hatua za utekelezaji |
| 58. | 11.5.1.17 | Mpango wa kutengeneza nakala za taarifa za mfumo (Backup plan) | Ipo katika hatua za utekelezaji |
| 59. | 11.5.1.19 | Eneo la kuendeleza mfumo baada ya maafa (Disaster Recovery Site) | Ipo katika hatua za utekelezaji |

| Namba | Hoja Namba | Hoja ya Ukaguzi | Hali Halisi ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi |
|---|---|---|---|
| **MAMLAKA YA MAJI (ZAWA)** | | | |
| 60. | 11.12.1.1 | Kukosekana kwa mita za kusoma kiwango cha maji yanayozalishwa, kusambazwa na kuuzwa Unguja na Pemba. | Ipo katika hatua ya utekelezaji |
| 61. | 11.12.1.2 | Kutokuingizwa kwenye mfumo taarifa za uzalishaji na ubora wa maji Unguja na Pemba kwa mtiririko. | Ipo katika hatua ya utekelezaji |
| 62. | 11.12.1.3 | Kukosekana kwa muongozo rasmi wa kufuta madeni ya maji, na kukata huduma ya maji kwa wananchi. | Ipo katika hatua ya utekelezaji |
| 63. | 11.12.1.4 | Kutofautiana kwa taarifa za mapato zilizomo kwenye Mfumo wa Sage Pastel na Mapato halisi yaliyokusanywa Benki ya PBZ. | Haijatekelezwa |
| 64. | 11.12.1.6 | Kutokuwepo kwa mkataba wa kupatiwa huduma za kiufundi (Service Level Agreement) baina ya ZAWA na Kampuni zilizowauzia ZAWA mifumo ya Smart Billing Management, Sage Pastel, Aruti, DeoGin, na Unit Billing System. | Ipo katika hali ya utekelezaji |
| 65. | 11.12.1.7 | Kukosekana kwa "audit logs/ trails" kwenye mifumo na Kanzidata za mifumo yote 5, Smart Billing Management, Sage Pastel, Aruti, DeoGin, na Unit Billing System. | Ipo katika hatua ya utekelezaji |
| 66. | 11.12.1.9 | Kukosekana kwa mpango wa kufanya mabadiliko kwenye mifumo ya TEHAMA. | Ipo katika hatua ya utekelezaji |
| 67. | 11.12.1.10 | Kutopatikana kwa Mikataba ya Sage Pastel na Unify Billing. | Haijatekelezwa |

| Namba | Hoja Namba | Hoja ya Ukaguzi | Hali Halisi ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi |
|---|---|---|---|
| 68. | 11.12.1.13 | Udhaifu wa udhibiti na mazingira duni kwenye chumba cha Seva (Server Room). | Ipo katika hatua ya utekelezaji |
| 69. | 11.12.1.15 | Kukosekana kwa muunganiko (integration) wa mfumo wa Sage Pastel na Unify Billing System. | Ipo katika hatua ya utekelezaji |
| 70. | 11.12.1.16 | Uchakavu wa vitendea kazi kama vile Kompyuta. | Ipo katika hatua ya utekelezaji |
| **SHIRIKA LA UMEME (ZECO)** | | | |
| 71. | 16.7.1.2 | Udhaifu katika kutoa Nambari za "Tempered" kwa ajili ya Mita za Umeme zilizoshindwa kupitisha umeme. | Utekelezaji hakukamilika |
| 72. | 1 6.7.1.4 | Udhaifu wa mfumo wa SAP kwenye kudhibiti maombi ya vifaa na kutambua nambari za mita za umeme. | Utekelezaji haukukamilika |
| 73. | 16.8.0 | Udhaifu wa udhibiti kwenye matumizi ya Mfumo wa SAP | Utekelezaji haukukamilika |
| 74. | 16.8.1.2 | Udhaifu uliobainika kwenye Mkataba wa huduma za kiufundi za mfumo wa Suprima (Service Level Agreement). | Utekelezaji haukukamilika |
| **ZANZIBAR HIGH EDUCATION LOAN BOARD** | | | |
| 75. | 7.11.1.3 | Mfumo wa ZOLAS unaruhusu kuomba mkopo wa pili bila ya kuhakiki asilimia 25 ya marejesho ya mkopo wa awali | Ipo katika hatua za utekelezaji |
| 76. | 7.11.1.5 | Kuwepo kwa ziada ya jumla ya shilingi 157,531,346.80 zilizokatwa kwa wadaiwa wa mikopo kimakosa | Ipo katika hatua za utekelezaji. |
| 77. | 7.11.1.6 | Wanufaika wa mikopo ambao hawajalipa madeni ya muda mrefu | Ipo katika hatua za utekelezaji. |

| Namba | Hoja Namba | Hoja ya Ukaguzi | Hali Halisi ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi |
|---|---|---|---|
| 78. | 7.11.1.7 | Kufanya upembuzi wa uteuzi wa wanufaika nje ya mfumo wa ZOLAS | Haijatekelezwa. |
| 79. | 7.11.1.12 | Mapungufu yaliyobainika katika Mpango wa Kukabiliana na Maafa (DR Plan) | Ipo katika hatua za utekelezaji |
| 80. | 7.11.1.13 | Kutokuwa na ushahidi wa kufanya zoezi la Uchambuzi wa Athari za Biashara (Business Impact Analysis, BIA) | Ipo katika hatua za utekelezaji |
| **ZANZIBAR SOCIAL SECURITY FUND (ZSSF)** | | | |
| 81. | 17.2.2.6 | Mapitio ya Mpango wa Mafunzo wa Utumishi kuhusu Mafunzo ya TEHAMA | Haijatekelezwa |
| **TUME YA MIPANGO** | | | |
| 82. | 5.12.1.8 | Kukosekana kwa mpango wa usimamizi wa matukio (Incidence Management Plan) | Haijatekelezwa |
| **HOSPITALI YA MNAZI MMOJA** | | | |
| 83. | 6.5.1.1 | Mikataba kutopitiwa na Mwanasheria Mkuu | Imetekelezwa kwa Sehemu |
| 84. | 6.5.1.3 | Usimamizi Usioridhisha wa Miradi ya Mifumo ya TEHAMA | Imetekelezwa kwa sehemu |
| 85. | 6.5.1.5 | Mifumo kutotumika kikamilifu | Imetekelezwa kwa sehemu |


RISK
AVOID
CONTROL
ACCEPT
TRANSFER
FINANCIAL INFORMATION SYSTEM
Total Revenue
Cash Flow
Revenue & Backlog
Bookings & Billings
Revenue
OCAGZ

# SURA YA TATU

# 3.0 TATHMINI YA UKAGUZI NA DOSARI ZA UJUMLA ZILIZOBAINIKA KATIKA UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA

Katika ukaguzi uliofanyika wa Mifumo ya TEHAMA kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imebainika kwamba kwa utaratibu wa kutumia Teknolojia ya Habari kwa kufanya shughuli za utekelezaji wa majukumu pamoja na kutoa huduma kwa jamii umeimarika kwa kiasi kikubwa katika sekta za umma ambapo Taasisi nyingi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimekuwa zikipata huduma mbali mbali kutoka nje ya Taasisi zao kupitia Mifumo ya TEHAMA na vile vile zimekuwa zikitoa baadhi ya huduma zao kwa kutumia mifumo ya TEHAMA. Aidha, ukaguzi umebaini kwamba mifumo ya TEHAMA inayotumiwa na Taasisi za Umma imegawika katika makundi makuu mawili.

## 3.1 Kundi la kwanza la Mifumo ya TEHAMA

Kundi hili limejumuisha mifumo ya TEHAMA ambayo imeanzishwa, inasimamiwa, inaendeshwa, na kudhibitiwa na Wakala wa Serikali Mtandao (eGAZ). Taasisi za umma zimekuwa hazina mamlaka ya udhibiti na utengenezaji wa mifumo na nyaraka zinazohusiana na mifumo hiyo isipokuwa zimepewa ruhusa ya matumizi tu katika mifumo hiyo kwenye moduli maalum zilizotengenezwa ambazo hutumiwa na Idara au kitengo husika ndani ya Taasisi za Umma.

Kwa ujumla mifumo hiyo ni Jumuishi na hutumiwa na Taasisi za Umma kwa shughuli mbali mbali kama vile shughuli za matumizi ya fedha kupitia bajeti zilizoidhinishwa na Serikali, manunuzi ya bidhaa na huduma mbalimbali, utoaji wa nambari za udhibiti kwa ajili ya malipo, shughuli za mawasiliano pamoja na usambazaji wa taarifa (nyaraka) mbali mbali katikaTaasisi. Orodha ya Mifumo iliyo katika kundi hilo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 2: Mifumo Jumuishi ya TEHAMA inayosimamiwa na eGAZ**

| Namba | Jina la Mfumo | Huduma Inayotoa | Msimamizi Mkuu |
|---|---|---|---|
| 1. | IFMIS/BAMAS | Kusimamia Mapato na Matumizi ya Bajeti | eGAZ |
| 2. | e-Office | Huduma za Afisi Mtandao | |
| 3. | GMS | Huduma za mawasiliano ya baruapape | |
| 4. | ZanMalipo | Kusimamia nambari za Udhibiti wa malipo (Control Numbers) | |
| 5. | e-Proz | Kusimamia Manunuzi ya Umma | eGAZ/ZPPDA |
| 6. | HR – Payroll Information System | Kushuhudia Utumishi, Rasilimali watu na Mishahara | eGAZ/OR-KSUUB |

## 3.2 Kundi la Pili la Mifumo ya TEHAMA


Kundi hili limejumuisha mifumo ya TEHAMA ambayo hutengenezwa au kununuliwa, husimamiwa, huendeshwa, hudhibitiwa na kumilikiwa na Taasisi husika ndani ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mifumo, miundombinu pamoja na nyaraka halisi zinazohusiana na mifumo hiyo huwa ni mali ya Taasisi husika kwa mujibu wa sheria, taratibu na miongozo iliyopo. Orodha ya Mifumo hiyo ambayo imebainika kwa taasisi zilizokaguliwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Nambari 1.**

## 3.3 Maeneo Makuu Yaliyofanyiwa Ukaguzi

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ukaguzi wa mifumo ya TEHAMA ulifanyika katika maeneo makuu matano (5). Maeneo hayo yamebainishwa kupitia maelezo na mchoro hapo chini kama ifuatavyo: -

a) Utawala wa TEHAMA (IT Governance) - ITGOV
b) Usimamizi wa Miradi ya TEHAMA (IT Projects Management) - ITPRJ
c) Udhibiti wa Jumla wa TEHAMA (IT General Control) - ITGC
d) Udhibiti wa Programu na Mifumo ya TEHAMA (IT Application Control) - ITAC
e) Usimamizi na Usalama wa TEHAMA (ICT Security Management) – ITSEC

### Mchoro Nambari 1: Maeneo Makuu yaliyokaguliwa kwenye TEHAMA




## 3.4 Muhtasari wa Dosari zilizobainika katika Ukaguzi


Katika ukaguzi uliofanyika wa Mifumo ya TEHAMA kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imebainika uwepo wa dosari mbali mbali zinazotokana na makosa ya kiutendaji, udhaifu katika usimamizi wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA, upungufu wa taaluma katika TEHAMA pamoja na ukiukwaji wa sheria na miongozo mbali mbali ambapo imepelekea dosari hizo kujitokeza kwa taasisi zaidi ya moja katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kuwepo kwa dosari hizo kunaweza kupelekea kupungua kwa ufanisi na kukosekana kwa tija katika matumizi ya mifumo na miundombinu ya TEHAMA kwa taasisi za Serikali na hatimae kupungua kwa utendaji kazi wa Taasisi katika matumizi ya Mifumo ya TEHAMA.

Jumla ya hoja Mia saba Aroubaini na Moja (741) zimeibuliwa kutoka kwenye maeneo makuu matano (5) yaliyokaguliwa kwenye Taasisi Ishirini na Saba (27) za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mwaka wa fedha 2022/2023 ambapo hoja hizo zimebainika kupitia ukaguzi uliofanyika kwenye Mifumo Sitini (60) ya TEHAMA ya Taasisi hizo. Aidha, kwa kila eneo hoja zake zimeelezwa kwa kina katika Ripoti za awali za Uongozi (Management Letters) zilizowasilishwa kwenye Taasisi za Umma wakati wa kipindi cha ukaguzi. Hata hivyo, Sura ya Nne ya Ripoti hii imeeleza dosari kuu (key findings) zilizobainika katika ukaguzi huo ambapo athari na mapendekezo yamebainishwa pia.

Kwa ujumla kiwango cha mapungufu yaliyobainika katika kila eneo lililokaguliwa kwenye Taasisi za Umma yamewasilishwa kwa njia ya mchoro kama inavyoonekana hapo chini:-

**Mchoro Nambari 2: Kiwangocha Mapungufu ya TEHAMA kilichobainika kwenye Taasisi za Umma**




Mchoro hapo juu unaonesha kwamba mapungufu mengi yamebainika kwenye eneo la Udhibiti wa Programu na Mifumo ya TEHAMA (IT Application Controls - ITAC). Hali hii inamaanisha kwamba Taasisi za Umma zimekuwa na udhaifu mkubwa katika kusimamia na kudhibiti programu pamoja na Mifumo ya TEHAMA jambo ambalo linaweza kusababisha hatari kubwa (High Risk) ya kupata mashambulizi ya mifumo, kuchezewa, kuharibiwa au kubadilishwa kwa taarifa na watu wasiohusika kutokana na kukosekana kwa udhibiti imara kwenye pogramu na mifumo ya TEHAMA katika Taasisi za Umma.

Hivyo, ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi za Umma kuweka kipaombele katika kufanyia kazi eneo hili kwa lengo la kuimarisha dosari zote zilizobainika na kupunguza hatari (Risk) zinazoweza kujitokeza kwenye programu na Mifumo ya TEHAMA inayotumika katika shughuli mbali mbali kwenye Taasisi zenye mifumo.

### 3.4.1 DOSARI ZA UJUMLA ZILIZOBAINIKA KATIKA UKAGUZI

Ukaguzi umebaini uwepo wa dosari mbali mbali kwenye Taasisi za Umma zilizokaguliwa ambapo dosari hizo zimepelekea kujitokeza kwa athari na changamoto za utendaji kazi na ukamilishaji wa malengo ya Taasisi hizo kwa ufanisi, weledi na kwa wakati. Dosari za ujumla zilizobainika ni kama zifuatazo:

#### 3.4.1.1 Dosari katika Sera, Miongozo na Mipango Mikakati ya TEHAMA

Sera za TEHAMA, Sera za Usalama, Mipango Mikakati ya TEHAMA pamoja na Miongozo ya utawala wa TEHAMA kwa ujumla wake ni nyaraka ambazo ndani yake zimekusanya miongozo na taratibu mbali mbali zinazoelekeza matumizi sahihi ya vifaa, miundombinu na mifumo ya TEHAMA kwa lengo la kudumisha, kulinda, kuongeza ufanisi na kuimarisha utendaji kazi na usalama wa rasilimali hizo.

Aidha, nyaraka hizo hueleza njia bora za kusimamia na kutumia rasilimali za TEHAMA katika Afisi na vie vile husaidia katika kutoa maamuzi kutokana na ukiukwaji wa taratibu za matumizi sahihi ya mifumo na rasilimali za TEHAMA.

Wakati zinapoandaliwa huzingatia vihatarishi vyote vinavyoweza kujitokeza katika Taasisi kwa watumiaji wa rasilimali za TEHAMA na huzingatia viwango vya Kitaifa na Kimataifa.

Nyaraka hizo husainiwa na uongozi wa Afisi husika kabla ya kuanza kutumika ili kupata idhini ya matumizi na hutolewa nakala mbali mbali na kufanyiwa mafunzo kwa watumiaji wa rasilimali za TEHAMA kwa lengo la kupatikana uelewa wa matumizi, ufanisi, usalama, tija na weledi juu ya matumizi sahihi na ya rasilimali za TEHAMA.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa baadhi ya Taasisi za Umma ambazo zinatumia rasilimali mbali mbali za TEHAMA ikiwemo kompyuta, mifumo ya TEHAMA, printa, mashine za photokopi, Servers, UPS pamoja na vifaa mbali mbali vya Mtandao, dosari iliyobainika kwa Taasisi hizo ni kutokuwa na Sera, Miongozo na Mipango Mikakati ya TEHAMA inayotumika katika matumizi, usimamizi, utunzaji na usalama wa rasilimali zao za TEHAMA. Vile vile imebainika kuwa baadhi ya Taasisi zinatumia sera za TEHAMA bila ya kuidhinishwa na Uongozi wa Taasisi hizo.

Aidha, ukaguzi ulifanya mahojiano na baadhi ya watumishi pamoja na watendaji katika Idara na vitengo mbali mbali vya Taasisi hizo kuhusiana na kupatiwa mafunzo ya matumizi ya Kompyuta, usalama wa Taarifa na Mitandao, usalama wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA na kubaini kwamba baadhi ya Taasisi kwa muda mrefu hazijatoa mafunzo hayo kwa watumishi wake na baadhi yao kutotoa kabisa.

Kukosekana kwa Sera, Miongozo na Mipango Mikakati ya TEHAMA ni kwenda kinyume na kifungu nambari 1.3, 2.3 na 4.3 cha Muongozo wa Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar, toleo la nambari 1.0 la mwaka 2022.

Aidha, kukosekana kwa nyaraka hizo pamoja na kutofanyika kwa mafunzo ya matumizi na usalama wa TEHAMA kwa watendaji kunapelekea kuwepo kwa usimamizi mbaya wa rasilimali za TEHAMA na hatimae kunaweza kujitokeza kwa vitendo vya uhujumu wa rasilimali hizo kama vile uharibifu, wizi, upotevu, utunzaji mbovu jambo linaloweza kusababisha hasara kwa Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi hizo kuandaa Sera, Miongozo, Mipango Mikakati na nyaraka zote zinazohusiana na matumizi ya rasilimali za TEHAMA kwa kushirikiana na Wakala wa Serikali Mtandao, nyaraka hizo zitasainiwa kwa ajili ya kutumika rasmi katika Taasisi husika na kufanyiwa mafunzo kwa watendaji ili kupatikana ufanisi wa utendaji. Miongoni mwa Taasisi zilizobainika kuwa na dosari hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

### Jadweli Nambari 3: Taasisi zilizobainika kuwa na dosari katika Sera, Miongozo na Mipango Mikakati ya TEHAMA

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Zanzibar |
| 2. | Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora |
| 3. | Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi |
| 4. | Wizara ya Maji, Nishati na Madini |
| 5. | Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar |
| 6. | Kamisheni ya Wakf na Mali ya Amana |
| 7. | Mamlaka ya Mapato Zanzibar |
| 8. | Baraza la Usimamizi wa Leseni za Biashara Zanzibar |
| 9. | Baraza la Manispaa ya Mjini |
| 10. | Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar |

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 11. | Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Zanzibar |
| 12. | Shirika la Bandari Zanzibar |
| 13. | Mamlaka ya Uwekezaji wa Vitega Uchumi Zanzibar |
| 14. | Kamisheni ya Utalii Zanzibar |
| 15. | Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ |
| 16. | Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar |

### 3.4.1.2 Kukosekana kwa Kamati Tendaji ya TEHAMA (IT Steering Committee)

Taratibu zinazokubalika (Best Practises) zinaelekeza Viongozi wa Taasisi kuanzisha Kamati Tendaji (ICT Steering Committee) ambayo itakuwa na lengo la kushughulikia masuala yote ya maendeleo ya TEHAMA, utoaji wa huduma kwa njia ya TEHAMA pamoja na kuhakikisha sera, mipango na mikakati ya TEHAMA inasimamiwa na kutekelezwa kwa ufanisi na kwa wakati.

Aidha, Muongozo nambari eGAZ/EXT/IGG/001 wa eGAZ unaohusiana na utendaji kazi wa Kamati Tendaji ya TEHAMA unaelekeza kwamba Mwenyekiti wa Kamati atakuwa ni Afisa Masuuli na Kamati Tendaji ya TEHAMA itakuwa na idadi ya watu saba (7) ambapo watatakiwa kupewa Hadidu Rejea na kuwekwa kumbukumbu za uendeshaji wa vikao vya TEHAMA.

Vile vile Mwenyekiti wa Kamati anaweza kuwaalika wajumbe kutoka taasisi za nje zinazosimamia utawala wa TEHAMA katika Serikali kwa lengo la kutoa ushauri na kuimarisha mipango mikakati ya TEHAMA kwa Ofisi.

Ukaguzi uliofanyika umebaini kwamba baadhi ya Taasisi za Umma hazina Kamati Tendaji ya TEHAMA ili kuweza kusaidia utekelezaji wa malengo na mikakati ya TEHAMA katika taasisi hiyo.

Kukosekana kwa Kamati Tendaji ya TEHAMA kunaweza kusababisha mipango kazi na maendeleo ya TEHAMA kuchelewa kutekelezwa kwa wakati na hatimae kutofikia malengo yaliyopangwa kwa ufanisi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi hizo kuanzisha Kamati Tendaji ya TEHAMA ili kuweza kuandaa mipango kazi mizuri itakayorahisisha utoaji wa huduma kwa wakati.

Aidha, kuwepo kwa Kamati Tendaji ya TEHAMA kutaweza kuhakikisha sera, miongozo na mikakati yote ya TEHAMA katika Taasisi inasimamiwa na kutekelezwa kwa ufanisi. Miongoni mwa Taasisi zilizokuwa hazina Kamati Tendaji ya TEHAMA (IT Steering Committee) ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 4: Taasisi zilizokaguliwa ambazo hazina Kamati Tendaji ya TEHAMA**

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Zanzibar |
| 2. | Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora |
| 3. | Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar |
| 4. | Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi |
| 5. | Wizara ya Maji, Nishati na Madini |
| 6. | Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar |
| 7. | Taasisi ya Viwango Zanzibar |
| 8. | Kamisheni ya Wakf na Mali ya Amana |
| 9. | Wakala wa Matukio ya Kijamii Zanzibar |
| 10. | Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar |
| 11. | Baraza la Usimamizi wa Leseni za Biashara |
| 12. | Bohari Kuu ya Dawa |
| 13. | Baraza la Manispaa ya Mjini |
| 14. | Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar |
| 15. | Mamlaka ya Uwekezaji wa Vitega Uchumi Zanzibar |
| 16. | Kamisheni ya Utalii Zanzibar |

#### 3.4.1.3 Kukosekana kwa nyaraka zilizoombwa kwa ajili ya ukaguzi

Ukaguzi uliomba nyaraka mbalimbali muhimu kuhusiana na maeneo makuu matano (5) yaliyokaguliwa kwenye Taasisi za Umma ikiwemo Eneo la Utawala wa TEHAMA, Udhibiti wa Ujumla wa TEHAMA, Udhibiti wa Programu na Mifumo ya TEHAMA, Usalama wa TEHAMA, pamoja na Usimamizi wa Miradi ya TEHAMA. Lengo ni kufanya uhakiki na uchambuzi wa taarifa zilizomo ndani yake pamoja na kupima hali halisi ya utelekezaji na uzingatiaji wa matakwa na mahitaji yaliyomo kwenye nyaraka hizo.

Hata hivyo ukaguzi umebaini Taasisi nyingi ziliwasilisha nyaraka kwa kiwango pungufu (hafifu) ikilinganishwa na orodha ya nyaraka zilizoombwa kwenye Taasisi hizo kupitia "Evidence Tracking Sheet" zilizoambatanishwa na "Engagement Letter" wakati wa kuanza kazi za ukaguzi.

Kukosekana kwa nyaraka hizo kunaweza kupelekea Taasisi za umma kukosa fursa za kushauriwa katika maeneo mbalimbali yakiwemo mapungufu yaliyopo yanayoweza kuathiri usimamizi na utendaji kazi wa rasilimali za TEHAMA za Taasisi na kupelekea kuongezeka kwa changamoto mbalimbali kama vile upotevu wa rasilimali za TEHAMA, uharibifu, utumiaji usioridhisha wa rasilimali hizo, matokeo yasiyotarajiwa katika mifumo, kukosekana kwa usalama wa taarifa jambo ambalo litapelekea kutopatikana kwa tija na ufanisi uliokusudiwa na hatimae kuingiza hasara Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi zilizokuwa na dosari hizo kuweka mpango imara wa kuandaa nyaraka zote ambazo hazikupatikana kwa ajili ya ukaguzi na kushirikisha Wakala wa Serikali Mtandao ili kupata msaada wa utengenezwaji wa nyaraka hizo kwa mujibu wa miongozo ya kitaifa na kimataifa. Baadhi ya Taasisi zilizobainika kuwa na kiwango pungufu cha nyaraka za TEHAMA ni kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

### Jadweli Nambari 5: Taasisi zilizowasilisha nyaraka pungufu

| Namba | Jina la Taasisi | Nyaraka zilizowasilishwa kwa ukaguzi (%) |
|---|---|---|
| 1. | Ofisi ya Rais Katiba, Sheria Utumishi na Utawala Bora | 25 |
| 2. | Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi | 29 |
| 3. | Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar | 22 |
| 4. | Wizara ya Maji, Nishati na Madini | 30 |
| 5. | Baraza la Usimamizi wa Leseni za Biashara | 13.3 |
| 6. | Bohari Kuu ya Dawa | 18 |
| 7. | Baraza la Manispaa ya Mjini | 19 |
| 8. | Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar | 35 |
| 9. | Mamlaka ya Uwekezaji wa Vitega Uchumi Zanzibar | 36 |
| 10. | Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali | 20 |

#### 3.4.1.4 Kukosekana kwa Mgawanyo wa Majukumu (Segregation of Duties)

Kwa mujibu wa kifungu (control) 5.3 cha ISO 27002:2022 kinahitaji Taasisi kuweka sera na taratibu zitakazoweza kusimamia utendaji kazi Taasisi ambapo sera hizo zitapaswa kuwa wazi na kufahamishwa watendaji mgawanyiko wa majukumu ili kuepuka kujitokeza mgongano wa majukumu.

Aidha, kwa mujibu wa viwango kubalifu vya TEHAMA (Best Practices) kwenye mgawanyo wa majukumu vinataka majukumu ya usimamizi wa mifumo, kanzidata, miundombinu pamoja na usalama wa mitandao yagawanywe kwa watu tofauti ambao ni "System Administrator", "Database Administrator", "Network Administrator" "Security Administrator - Security Personnel" n.k.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika uwepo wa baadhi ya Taasisi za Umma kutozingatia mgawanyo wa majukumu ya TEHAMA kutokana na Afisi hizo kuwa na uhaba wa Maafisa TEHAMA na baadhi yao kutoweka kipaombele shughuli za TEHAMA jambo ambalo linasababisha Afisa TEHAMA mmoja kufanya majukumu yote ya TEHAMA katika Idara, Divisheni na Vitengo vyote vilivyo ndani ya Afisi hiyo kama vile kusimamia Mtandao wa Afisi (Network administration), kusimamia kompyuta za Afisi (IT Personnel), kusimamia mifumo ya TEHAMA na kanzidata zinazotumika katika Afisi (System and Database Administration), kutoa mafunzo kwa watumiaji wa rasilimali za TEHAMA (Trainer) na kutoa msaada kwa watumiaji wa mifumo katika Afisi pamoja na kufanya matengenezo ya vifaa na miundombinu ya TEHAMA (Technical Support), kulinda taarifa za mifumo (Security Administration) n.k.

Hali hii husababisha kuwepo kwa changamoto nyingi na ugumu katika kutekeleza majukumu ya kazi na hatimae kujitokeza kwa uchelewaji wa upatikanaji wa huduma kwa wakati.

Aidha, kutokuwepo kwa mgawanyo wa majukumu kunaongeza hatari (risk) kwenye uadilifu, usiri, usalama pamoja na upatikanaji wa taarifa zinazohifadhiwa kwenye mifumo ya TEHAMA.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi hizo kuhakikisha unazingatia mgawanyo wa majukumu ya TEHAMA kwa kuongeza ajira za maafisa TEHAMA ili kupatikana idadi yenye usawa kwa watendaji kulingana na majukumu yao na kwa mujibu wa Sheria, kanuni na miongozo ya Utumishi jambo ambalo litapelekeka kuimarika kwa utendaji kazi, ufanisi na kuongezeka kwa uadilifu, udhibiti na usiri wa taarifa. Orodha ya Taasisi zilizobainika kuwa na dosari ya mgawanyo wa majukumu ya TEHAMA ni kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

### Jadweli Nambari 6: Taasisi zenye mapungufu katika mgawanyo wa majukumu (SoD) ya TEHAMA

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Zanzibar |
| 2. | Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora |
| 3. | Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar |
| 4. | Wizara ya Maji, Nishati na Madini |
| 5. | Taasisi ya Viwango Zanzibar |
| 6. | Kamisheni ya Wakf na Mali ya Amana |
| 7. | Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar |
| 8. | Baraza la Usimamizi wa Leseni za Biashara |
| 9. | Bohari Kuu ya Dawa |
| 10. | Baraza la Manispaa ya Mjini |
| 11. | Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar |
| 12. | Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Zanzibar |
| 13. | Wakala wa Chakula Dawa na Vipodozi Zanzibar |
| 14. | Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali |
| 15. | Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar |

#### 3.4.1.5 Kukosekana kwa daftari la kusajili Rasilimali za TEHAMA (ICT Asset Register) pamoja na kuweka kumbukumbu za Vihatarishi vinavyohusiana na TEHAMA (ICT Risk Register)

Kwa mujibu wa Muongozo wa kimataifa ISO 31000:2018 pamoja na kifungu nambari 4.3.1 cha Muongozo wa Wakala wa Serikali Mtandao toleo nambari 1 la mwaka 2022, kinaitaka Taasisi ya Umma kufanya tathmini ya Vihatarishi (risk assessment) ili kuweza kubaini udhaifu na athari zinazoweza kujitokeza katika shughuli, rasilimali au biashara za Taasisi na kuchukuwa hatua mapema za kuweza kusimamia na kujikinga na athari kabla ya kutokea.

Ukaguzi umebaini kwamba baadhi ya Taasisi za Umma hazina daftari/ Rejista maalum kwa ajili ya kuweka kumbukumbu za hatari, mapungufu na changamoto zote zinazobainika kwenye miundombinu, mifumo na miradi ya TEHAMA ya Afisi (ICT Risk Register) na vile vile kusajili na kusimamia rasilimali za TEHAMA (ICT Asset Register)

Daftari hili linaweza kuwekwa kwa njia ya kidijitali ambapo watumiaji wa mfumo na miundombinu ya TEHAMA hurikodi vifaa, miundombinu na mifumo yote ya TEHAMA iliyopo kwenye Taasisi pamoja na kuweka kumbukumbu za changamoto na hatari zote zinazoweza kujitokeza na kuathiri usalama wa taarifa katika rasilimali hizo.

Baada ya kurikodiwa kwa hatari hizo hufanyiwa uchambuzi, tathmini na kutafutiwa ufumbuzi pamoja na kuwekewa udhibiti wa haraka ili kuepusha kuleta athari kwa taarifa zilizomo ndani ya mifumo, miundombinu au miradi ya TEHAMA ya Taasisi.

Kutokuwepo kwa daftari la kurikodia na kusajili rasilimali za TEHAMA (ICT Asset Register) kunaweza kusababisha wasimamizi kushindwa kudhibiti na kusimamia rasilimali hizo na kupelekea urahisi wa upotevu na matumizi mabaya ya rasilimali za TEHAMA za Taasisi.

Aidha, kukosekana kwa daftari hilo kunaweza kusababisha kuongezeka kwa hatari zilizopo kwenye mazingira ya TEHAMA ya Mamlaka kutokana na kutofanyiwa huduma za maboresho kwa wakati kwa sababu ya kusahauliwa, kutopewa vipaombele au kutojuulikana na hatimae kupelekea rasilimali hizo kufanya kazi chini ya kiwango.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi za Umma kuanzisha daftari maalum kwa njia ya mfumo au vyenginevyo litakaloweza kusajili na kusimamia rasilimali zote za TEHAMA ambapo pia litatumika kuwekea kumbukumbu zote kuhusiana na hatari (risks) , changamoto, dosari pamoja na mapungufu yanayobainika kwenye utendaji kazi wa rasilimali za TEHAMA ili kuweza kutambulika mapema na kutafutiwa ufumbuzi wa haraka kabla ya kuleta athari.

Orodha ya Taasisi zilizobainika kutofanya tathmini ya vihatarishi vya TEHAMA ni kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 7: Taasisi zilizobainika kuwa na dosari katika "ICT Asset Register" na "ICT risk register" za TEHAMA**

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Zanzibar |
| 2. | Ofisi ya Rais Katiba Sheria Utumishi na Utawala Bora |
| 3. | Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi |
| 4. | Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar |
| 5. | Wizara ya Maji, Nishati na Madini |
| 6. | Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar |
| 7. | Taasisi ya Viwango Zanzibar |
| 8. | Kamisheni ya Wakf na Mali ya Amana |
| 9. | Wakala wa Matukio ya Kijamii Zanzibar |
| 10. | Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar |
| 11. | Bohari Kuu ya Dawa |
| 12. | Baraza la Manispaa ya Mjini |
| 13. | Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar |
| 14. | Ofisi ya Rais Fedha na Mipango |
| 15. | Mamlaka ya Uwekezaji wa Vitega Uchumi Zanzibar |
| 16. | Wakala wa Chakula Dawa na Vipodozi Zanzibar |
| 17. | Shirika la Umeme Zanzibar |
| 18. | Kamisheni ya Utalii Zanzibar |
| 19. | Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali |

### 3.4.1.6 Udhaifu katika kudhibiti na kusimamia akaunti za watumiaji wa Mifumo (User Access Management)

Kwa mujibu wa viwango vinavyokubalika kwenye udhibiti na usimamizi wa akaunti za watumiaji wa mifumo vinaelekeza kufanyika kwa mapitio ya mara kwa mara kwenye akaunti za watumiaji wa mifumo (Periodic Access Reviews) ili kuhakikisha kwamba watumiaji wa mifumo wanapata haki na ruhusa zilizo sahihi za kuingia katika mifumo na kuzifikia taarifa kwa mujibu wa majukumu yao na si vyenginevyo.

Aidha, mapitio hayo husaidia kubaini orodha ya watumiaji wasiohusika, watumiaji waliopewa ruhusa kinyume na majukumu yao, watumiaji wasiotambulika na vile vile watumiaji waliokuwa hai ambao hawapo kazini, na Afisi kufanya utaratibu wa kuwadhibiti ili kuepusha hatari zinazoweza kutokezea katika mifumo kupitia akaunti hizo.

Ukaguzi umebaini kwamba baadhi ya Taasisi za Umma mifumo yake haifanyiwi mapitio ya mara kwa mara kwa lengo la kuhakikiwa usalama na kudhibitiwa akaunti za watumiaji wa mifumo hiyo, hali hii imebainika kwenye mifumo mbali mbali ya Taasisi za Umma kutokana na kuwepo kwa akaunti nyingi za watengenezaji wa mfumo "System Vendors" kutoka kampuni ambazo akaunti hizo si za watumishi wa umma lakini zinaonekana zipo hai "Active" licha ya kua hazitumiki kwa muda mrefu, vile vile akaunti za watumishi wengine kuwa zipo hai lakini wenyewe wameshahama katika Taasisi husika.

Mbali na hayo ukaguzi umebaini kuwepo kwa akaunti za watumiaji wa mifumo ambazo zimepewa uwezo mkubwa wa kutumia mfumo "Administrative Rights" bila ya kuzingatia majukumu yao pamoja na matakwa ya usalama wa taarifa ndani ya mifumo hiyo.

Aidha, imebainika kwamba baadhi ya watumiaji wa mifumo kwenye Taasisi za umma hutumia akaunti za asili "default Accounts" zilizomo kwenye mifumo na kanzidata, baadhi ya akaunti hizo pamoja na "System Administrator, manager, root, Admin, user, n.k." ambapo akaunti hizo hutumiwa kwa kufanya shughuli mbali mbali ndani ya mifumo na kanzidata zake bila ya udhibiti wa aina yoyote.

Kwa ujumla dosari za udhibiti wa akaunti zilizotajwa hapo juu zinaweza kuwa ni chanzo cha kufanyika kwa mashambulizi katika mifumo ya Taasisi, kusababisha matumizi yasiyofaa ndani ya mifumo kama vile kuingiza taarifa zisizo sahihi kwa makusudi, kubadilisha au kufuta taarifa muhimu kinyume na utaratibu, kuharibu mfumo n.k.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi hizo kuhakikisha unaandaa utaratibu maalum wa kufanya mapitio ya mara kwa mara ya kuhakiki akaunti za watumiaji katika mifumo yote ya Taasisi na kuweka usimamizi mzuri wa akaunti zenye uwezo mkubwa wa kufikia taarifa "Privileged Access Management – (PAM)" pamoja na kudhibiti watumiaji wasiohusika na wasiotambulika (unauthorized/ unidentified users) kuweza kuingia ndani ya mfumo na kuzifikia taarifa zilizomo.

Kwa upande wa akaunti asili na zenye majina ya ujumla "Default / Generic Accounts" Ukaguzi unashauri akaunti hizo zisajiliwe na kutambulika rasmi umiliki wake ikiwa zitatumika kuendesha huduma katika mifumo "service accounts", vyenginevyo zisitishwe na zitengenezwe akaunti nyengine mbadala zitakazopewa haki "Rights" sawa na akaunti za asili zilizositishwa, na kutumiwa kwa malengo yaliyokusudiwa.

Baadhi ya Taasisi zilizobainika kuwa na dosari hiyo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 8: Taasisi zilizobainika kuwa na udhaifu katika kudhibiti na kusimamia akaunti za watumiaji wa Mifumo (User Access Management)**

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Zanzibar |
| 2. | Ofisi ya Rais Katiba Sheria Utumishi na Utawala Bora |
| 3. | Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar |
| 4. | Ofisi ya Rais Fedha na Mipango |

### 3.4.1.7 Kukosekana kwa Mpango wa Kusimamia Mabadiliko yanayofanyika katika Mifumo ya Afisi (System Change Management Plan)

Mpango wa kusimamia mabadiliko katika mfumo ni moja kati ya taratibu na njia bora zinazotumika katika uendeshaji, usimamizi, udumishaji na utoaji wa huduma bora kupitia mifumo ya TEHAMA katika Taasisi. Lengo la kufanya usimamizi wa mabadiliko ni kuhakikisha kiwango cha utendaji kazi katika mfumo kinaimarika na kuendelea kudumu, kupunguza changamoto zinazojitokeza kuhusiana na mabadiliko ya Teknolojia na shughuli za biashara, kudhibiti hatari na athari zinazoweza kutokezea wakati wa mabadiliko pamoja na kuimarisha usalama wa taarifa zilizo ndani ya mfumo.

Ukaguzi umebaini kwamba baadhi ya Taasisi za Umma hazina mpango wa kusimamia mabadiliko yanayofanyika katika mifumo yao ambapo mpango huo ungeonesha utaratibu gani unaotumika katika kuwasilisha maombi ya mabadiliko kutoka kwa watumiaji wa mifumo, watu watakaohusika kuidhinisha kufanyika kwa maombi hayo, njia zitakazotumika kuwasilisha mabadiliko kwa mtengenezaji wa mfumo "Vendor", mazingira yatakayotumika kufanyia na kujaribu mabadiliko, aina ya timu itakayohusika kushuhudia matokeo ya mabadiliko na kuhakikisha yanafanyika kwa ufanisi, sehemu zitakazohifadhiwa kumbukumbu za matokeo na namna ya kuhifadhi, baada ya kufanyika mabadiliko watu watakaosimamia na kuangalia mwenendo wa mabadiliko hayo katika mfumo, n.k.

Kutokuwepo na mpango wa kusimamia mabadiliko yanayofanyika katika mifumo kunaweza kusababisha kujitokeza kwa changamoto nyingi za kiutendaji zitakazopelekea mifumo ya Afisi kutofanya kazi kwa ufanisi kama ilivyokusudiwa jambo ambalo linaweza kusababisha kukosekana usalama wa taarifa, upotevu wa taarifa, kuharibika kwa mifumo na hatimae kuingiza hasara Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi hizo kuanzisha mpango wa kusimamia mabadiliko kwenye mifumo ya TEHAMA kwa kuzingatia miongozo ya kitaifa na kimataifa, vile vile kuhakikisha mpango huo unatumika kwenye mabadiliko yanayofanyika kwa mifumo yote ya Taasisi ili kupatikana ufanisi katika uimarishaji wa utendaji kazi "perfomance" na uimarishaji wa usalama "security". Orodha ya Taasisi zilizobainika kuwa na dosari hiyo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 9: Taasisi zilizobainika kuwa na dosari katika Mpango wa Kusimamia Mabadiliko yanayofanyika katika Mifumo (System Change Management Plan)**

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Zanzibar |
| 2. | Ofisi ya Rais Katiba Sheria Utumishi na Utawala Bora |
| 3. | Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar |
| 4. | Wizara ya Maji, Nishati na Madini |
| 5. | Taasisi ya Viwango Zanzibar |
| 6. | Kamisheni ya Wakf na Mali ya Amana |
| 7. | Wakala wa Matukio ya Kijamii Zanzibar |
| 8. | Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar |
| 9. | Bohari Kuu ya Dawa |
| 10. | Ofisi ya Rais Fedha na Mipango |
| 11. | Mamlaka ya Uwekezaji wa Vitega Uchumi Zanzibar |
| 12. | Wakala wa Chakula Dawa na Vipodozi Zanzibar |

### 3.4.1.8 Dosari katika Utengenezaji, Usimamizi, Uendeshaji na Utunzaji wa Tovuti za Serikali

Katika kipindi cha awamu ya nane, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefanya jitihada kubwa za kuimarisha maendeleo katika sekta ya TEHAMA kwa taasisi za Serikali ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi, kuongeza udhibiti wa ukusanyaji mapato na matumizi, kuimarisha ulinzi na usalama wa taarifa na nyaraka mbali mbali za Serikali pamoja na kuboresha miundombinu na mifumo ya mawasiliano kwa lengo la kupatikana tija na ufanisi wa kazi na huduma bora kwa Jamii.

Taasisi za Serikali hutumia tovuti "Website" kama ni zana kuu ya utoaji wa habari kwa umma na wadau mbali mbali kuhusiana na huduma zinazotolewa na Taasisi kwa lengo la kutambulika haraka, kwa ufanisi na kwa wakati.

Ukaguzi ulifanya mapitio ya Tovuti za Taasisi za Umma kwa lengo la kuangalia taarifa zilizomo, utendaji kazi wa tovuti hizo pamoja na kuangalia usalama na kubaini baadhi ya Taasisi za Umma kuwa na dosari zifuatazo:-

a) Lugha zinazotumika katika tovuti ya baadhi ya Taasisi ni Kiingereza pekee na sio lugha mbili ambazo ni Kiswahili na Kiingereza kama inavyohitajika kwa mujibu wa kifungu nambari 5.2 cha Muongozo nambari 1 wa mwaka 2022 wa Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar wa Utengenezaji, Uendeshaji na Usimamizi wa Tovuti za Serikali.

b) Kutokuwepo kwa sehemu ya kuhesabu na kuonesha idadi ya wageni waliotembelea tovuti hiyo ili kuweza kubaini kwa kiasi gani tovuti hiyo inatizamwa na kuweza kushajihisha utoaji wa taarifa kwa jamii pamoja na kuboresha tovuti, hali hii ni kwenda kinyume na kifungu nambari 5.3 cha Muongozo huo.

c) Kukosekana kwa taarifa muhimu za Taasisi ikiwemo eneo la Afisi kwa upande wa Unguja na Pemba na nambari ya simu kwa ajili ya mawasiliano pamoja na Mpango Mkakati wa Taasisi (Strategic Plan) jambo ambalo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 4.1.1 (iii) na (vii) cha Muongozo huo.

d) Baadhi ya Taasisi kushindwa kuweka tovuti zao katika Vituo Vikuu vya Serikali vya Kuhifadhi na Kusimamia Mifumo na badala yake husimamiwa na kuhifadhiwa na kampuni binafsi za nje jambo ambalo ni kinyume na kifungu nambari 7.1 cha muongozo wa eGaz wa Kutayarisha na Kusimamia tovuti ya Serikali.

Kwa ujumla uwepo kwa dosari hizo unaweza kusababisha tovuti za Afisi kutofanya kazi kwa ufanisi na hatimae kukosekana kwa tija iliyokusudiwa ya kuanzishwa kwa tovuti hizo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi hizo kuweka utaratibu wa lugha mbili au zaidi, taarifa za sasa (current information), kuimarisha usalama wa tovuti na taarifa zake (information security) pamoja na kuweka taarifa kamili za mawasiliano ili kwenda sambamba na Muongozo nambari 1 wa mwaka 2022 wa Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar kuhusiana na Utengenezaji, Uendeshaji na Usimamizi wa Tovuti za Serikali. Baadhi ya Taasisi zilizobainika kuwa na dosari katika Tovuti zake ni kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 10: Taasisi zilizobainika kuwa na dosari katika tovuti zake

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Zanzibar |
| 2. | Ofisi ya Rais Katiba Sheria Utumishi na Utawala Bora |
| 3. | Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi |
| 4. | Wakala wa Matukio ya Kijamii Zanzibar |
| 5. | Baraza la Manispaa ya Mjini |
| 6. | Ofisi ya Rais Fedha na Mipango |
| 7. | Kamisheni ya Utalii Zanzibar |
| 8. | Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar |
| 9. | Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar |

### 3.4.1.9 Kutokuwepo kwa "Active Directory – AD " katika Afisi

Active Directory ni moja ya kanzidata muhimu zinazotolewa kwenye huduma za Microsoft kwa ajili ya kuwaunganisha watumiaji wa kompyuta na vifaa vyengine vya TEHAMA kupitia mtandao, aidha AD hutumika kwa ajili ya kudhibiti na kusimamia matumizi ya vifaa vya TEHAMA katika Afisi, watumiaji wa mifumo pamoja na programu mbalimbali kupitia sera maalum za usalama zinazosanidiwa kwa lengo la kuimarisha usalama wa taarifa za Afisi pamoja na kudhibiti matumizi mabaya ya mifumo ya TEHAMA.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba baadhi ya Taasisi za Umma hazina "Active Directory" ambayo ingeunganisha kompyuta, printa na vifaa vyengine vya TEHAMA vinavyotumika na Afisi ili kuweza kusimamia na kuviendesha kwa lengo la kuongeza udhibiti, usalama, ufanisi na tija katika matumizi ya vifaa hivyo.

Kutokuwepo kwa Active Directory kunaweza kupelekea kompyuta na vifaa vengine vya TEHAMA vya Taasisi kukosa usalama, usimamizi na udhibiti na hatimae kusababisha vifaa kushambuliwa na virusi pamoja na programu hatarishi kwa urahisi na kupoteza taarifa za Afisi.

Aidha, kutokuwepo kwa AD kunaweza kupelekea kukosekana kwa udhibiti mzuri wa taarifa dhidi ya wasiohusika kuweza kuzifikia, kuona, na kuzitumia taarifa zilizomo ndani ya kompyuta na mifumo kwa maslahi yao binafsi na hatimae kuharibu taswira ya Taasisi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi hizo kuanzisha kanzidata ya Active Directory ili kurahisisha matumizi ya kompyuta na vifaa vyengine vya TEHAMA pamoja na kuimarisha usalama wa taarifa na vifaa kwa watumiaji wa mifumo na kompyuta.

Orodha ya Taasisi zilizobainika kuwa na dosari hiyo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 11: Taasisi ambazo hazina Active Directory**

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Ofisi ya Rais Katiba Sheria Utumishi na Utawala Bora |
| 2. | Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar |
| 3. | Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi |
| 4. | Wizara ya Maji, Nishati na Madini |
| 5. | Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar |
| 6. | Kamisheni ya Wakf na Mali ya Amana |
| 7. | Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar |
| 8. | Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar |
| 9. | Kamisheni ya Utalii Zanzibar |

### 3.4.1.10 Kutokuwepo kwa Mpango wa Muendelezo wa Biashara (BCP), Mpango wa Kukabiliana na Maafa (DRP) pamoja na Eneo la Kujikinga na Maafa (DRS)

Kwa mujibu wa kifungu nambari 4.3.3 cha Muongozo wa Serikali Mtandao toleo nambari 1 la Mwaka 2022 pamoja na viwango vya kimataifa vya usalama vya Taasisi (ISO 27031) vinahitaji Taasisi zenye kutoa huduma kupitia mifumo na miundombinu ya TEHAMA kuwa na Mpango maalum wa kuweza kuendeleza Biashara, kurejesha huduma pamoja na kukabiliana na maafa wakati janga likitokea katika taasisi husika (BCP & DRP).

Mpango huo hueleza utaratibu utakaotumika katika kuendeleza utoaji wa huduma wakati janga au dharura itakapotokezea katika taasisi, na hatua zitakazochukuliwa kabla na baada ya janga kutokezea ili kuweza kudhibiti na kupunguza athari zinazoweza kutokezea pamoja na kurudisha huduma zinazotolewa na taasisi kwa wakati.

Aidha, taasisi inatakiwa kutenga eneo mbadala *(Disaster Recovery Site - DRS)* kwa mujibu wa vigezo na umbali unaokubalika wa angalau maili 62 kutoka katika eneo la kituo kikuu cha taarifa na kuweka miundombinu madhubuti ya mawasiliano itakayoweza kusafirisha, kuhifadhi na kuokoa taarifa pamoja na kuendeleza utoaji wa huduma za biashara endapo janga likitokea.

Ukaguzi umebaini kwamba baadhi ya Taasisi za Umma hazina Mpango wa Muendelezo wa Biashara, Mpango wa Kukabiliana na Maafa na vile vile hazina eneo jengine mbadala (DRS) lililotengwa na kutumika kwa ajili ya kuokoa taarifa na kuendeleza utoaji wa huduma mbali mbali kupitia mifumo yake endapo janga au maafa yakitokezea katika taasisi hizo.

Kutokuwepo kwa Mipango ya Muendelezo wa Biashara na Kukabiliana na Maafa na kutokuwepo kwa eneo mbadala la kujikinga na kuokoa taarifa wakati janga litakapotokea kunaweza kusababisha upotevu mkubwa wa taarifa na kupelekea kukosekana kwa huduma katika kipindi cha muda mrefu kupitia mifumo ya Taasisi jambo ambalo linaweza kukosa tija ya uwepo wa mifumo hiyo na kusababisha hasara kwa Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi hizo kuchukuwa hatua za kuanzisha Mpango wa Kuendeleza Biashara, Mpango wa Kupona Maafa pamoja na kutenga eneo mbadala la kuhifadhi na kuokoa taarifa kwa mujibu wa vigezo vinavyokubalika ili kuendeleza huduma zake za kiutumishi kupitia mifumo endapo janga likitokea katika Makao makuu ya Ofisi hiyo. Orodha ya Taasisi zilizobainika kuwa na dosari hiyo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 12: Taasisi ambazo hazina BCP, DRP na vile vile DRS**

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Zanzibar |
| 2. | Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar |
| 3. | Ofisi ya Rais Katiba Sheria Utumishi na Utawala Bora |
| 4. | Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar |
| 5. | Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi |
| 6. | Wizara ya Maji, Nishati na Madini |
| 7. | Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar |
| 8. | Taasisi ya Viwango Zanzibar |
| 9. | Kamisheni ya Wakf na Mali ya Amana |
| 10. | Wakala wa Matukio ya Kijamii Zanzibar |
| 11. | Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar |
| 12. | Baraza la Usimamizi wa Leseni za Biashara |
| 13. | Bohari Kuu ya Dawa |
| 14. | Baraza la Manispaa ya Mjini |

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 15. | Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar |
| 16. | Ofisi ya Rais Fedha na Mipango |
| 17. | Mamlaka ya Uwekezaji wa Vitega Uchumi Zanzibar |
| 18. | Wakala wa Chakula Dawa na Vipodozi Zanzibar |
| 19. | Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali |
| 20. | Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar |

### 3.4.1.11 Kutofanyika kwa mchakato wa kuhifadhi nakala za taarifa na kuzifanyia majaribio kwenye mifumo (backup and restoration process)

Kwa mujibu wa sera za usalama za kimataifa (ISO 27001) zinahitaji Taasisi kuwa na sera au miongozo itakayofafanua namna ya kuweka nakala za taarifa za Taasisi (backup policy) na vile vile kuwa na utaratibu maalum wa kufanya mchakato wa kuhifadhi nakala hizo kupitia njia mbalimbali (backup process) ambapo mchakato huu husaidia kuokoa taarifa wakati janga au uharibifu unapotokea kwenye taarifa za asili.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa baadhi ya Taasisi za Umma hazina sera na utaratibu mzuri wa kuhifadhi nakala za taarifa zilizo ndani ya mifumo yao (backup policy & backup process), Aidha imebainika kwa zile Taasisi zinazofanya backup, zinashindwa kufanya majaribio ya nakala zinazohifadhiwa kwa mujibu wa masharti na miongozo iliyopo ili kubaini ikiwa taarifa hizo zinaweza kufanya kazi na kutegemewa wakati janga au uharibifu wowote ukitokea katika mifumo na miundombinu ya Afisi.

Kutokuwepo kwa sera, kutofanyika kwa mchakato wa kuhifadhi nakala za taarifa na kutofanyika majaribio ya utendaji kazi wa nakala hizo kunaweza kusababisha upotevu mkubwa wa taarifa na kuingiza hasara Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi hizo kutengeneza sera zitakazotoa muongozo wa namna ya kufanya mchakato wa kuhifadhi nakala za taarifa pamoja na kuzijaaribu nakala hizo ili kuhakikisha zinafanya kazi ipasavyo na kuweza kutumika endapo janga au uharibifu ukitokea kwenye mifumo au miundombinu ya TEHAMA ya Afisi. Orodha ya Taasisi zilizobainika kuwa na dosari ya kufanya mchakato wa nakala na majaribio (backup and restoration process) ya taarifa ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 13: Taasisi zenye dosari ya ufanyaji ya nakala za taarifa pamoja na kufanya majaribio ya nakala hizo

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Zanzibar |
| 2. | Ofisi ya Rais Katiba Sheria Utumishi na Utawala Bora |
| 3. | Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar |
| 4. | Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi |
| 5. | Kamisheni ya Wakf na Mali ya Amana |
| 6. | Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar |
| 7. | Bohari Kuu ya Dawa |
| 8. | Mamlaka ya Uwekezaji wa Vitega Uchumi Zanzibar |

### 3.4.1.12 Mapungufu katika Vitengo vya Habari

Kwa mujibu wa majukumu ya Kitengo cha Habari katika Taasisi za Umma ni kuratibu shughuli zote za habari ikiwemo kutoa taarifa katika vyombo vya habari, mitandao ya Afisi na Kijamii, kuandika makala, kuandaa vipindi vya habari (documentary) kuandaa taarifa za majarida, vipeperushi, kuandaa mikutano mbali mbali ya Afisi n.k.

Ukaguzi umebaini kwamba Vitengo vya Habari katika baadhi ya Taasisi za Umma kwa Unguja na Pemba vina uhaba wa kupatiwa mafunzo kuhusiana na matumizi ya vifaa vya habari pamoja na programu za kufanyia kazi, vile vile vimebainika kuwa na uhaba wa watendaji na vitendea kazi, ambapo vingi vilivyopo vinatumia teknolojia ya zamani jambo ambalo linapelekea kazi kushindwa kufanyika kwa urahisi na ufanisi, vile vile kuwepo kwa changamoto za usafiri unaotumika katika kufanya shughuli za kufuatilia habari.

Hali hii imesababisha kuibuka kwa changamoto nyingi katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku kwa watumishi wa vitengo hivyo na kupelekea kuchelewa kukamilika kazi zao kwa wakati.

Aidha, kuwepo kwa dosari hizo kunaweza kusababisha athari ya kupungua kwa ufanisi katika utoaji wa habari kwa jamii kuhusiana na mambo mbali mbali ya Taasisi husika na hatimae kupelekea kukosekana kwa tija iliyokusudiwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi hizo kufanya jitihada za kuimarisha vitengo vya Habari vya Afisi Unguja na Pemba kwa kuongeza watendaji, kuwapatia zana za kisasa za kufanyia kazi zinazokwenda na wakati, kuwapatia mafunzo ya mara kwa mara ya matumizi ya programu na zana hizo za kisasa pamoja na kuwapatia usafiri utakaosaidia kufanya kazi za ufuatiliaji wa habari kwa ufanisi. Taasisi zilizobainika kuwa na dosari hiyo ni kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 14: Taasisi zilizobainika kuwa na mapungufu kwenye Vitengo vya Habari**

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Ofisi ya Rais Katiba Sheria Utumishi na Utawala Bora |
| 2. | Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi |

### 3.4.1.13 Kukosekana kwa udhibiti wa taarifa za mahudhurio kutoka kwenye mfumo wa Biotime Attendance System

Kanuni nambari 45(1) na 45(8) za Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014 zinaeleza uwekaji wa utaratibu wa kuchukua mahudhurio ya wafanyakazi kwa njia ya kielekroniki (Biometric System).

Aidha, kwa mujibu wa toleo nambari **CAB.78/388/01** la tarehe 12/10/2022 kutoka Afisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora limesisitiza juu ya kuweka utaratibu wa kuchukua mahudhurio ya watumishi kwa njia ya kielektroniki kwa Taasisi zote za Umma.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika baadhi ya Taasisi za Umma hazitumii Mfumo wa kielektroniki wa Usimamizi wa Mahudhurio ya wafanyakazi (Biometric Attendance System) ambapo imebainika kuwa bado kuna baadhi ya Taasisi zinaendelea kutumia utaratibu wa njia ya kawaida (manually) kuweka kumbukumbu za mahudhurio kwenye madaftari.

Mbali na hayo imebainika kwamba baadhi ya Taasisi utaratibu uliopo ni kwamba taarifa za mahudhurio ya watumishi hutolewa na kitengo cha TEHAMA cha Taasisi husika kutoka kwenye mfumo wa mahudhurio na kuwasilishwa Idara ya Utumishi ya Taasisi kufanyiwa uhakiki wa mahudhurio ya kazini jambo ambalo sio sahihi kwa mujibu wa utaratibu unaokubalika, hali hii inaweza kupelekea kubadilishwa (tampered) taarifa hizo kwa makusudi wakati wa mchakato wa utoaji katika mfumo na hatimae idara ya Utumishi kupatiwa taarifa zisizokuwa sahihi na halisi.

Aidha, kutotumika vifaa vya kielektroniki pamoja na mifumo katika kusimamia na kuweka kumbukumbu za mahudhurio ya wafanyakazi kunaweza kusababisha Taasisi kushindwa kupata taarifa sahihi za mahudhurio kwa wafanyakazi wake, kwa mfano kutambua muda sahihi wa kuingia na kutoka kazini kwa wafanyakazi, idadi ya siku za mahudhurio ya wafanyakazi kwa kila wiki, mwezi hadi mwaka jambo ambalo linaweza kusababisha kuongezeka kwa utoro kazini, uchelewaji na uondokaji mapema kazini, na hatimae kupungua kwa ufanisi wa utendaji kazi wa Taasisi.

Vile vile kunaweza kupelekea taasisi kushindwa kutoa maamuzi sahihi kutokana na kutopatikana kwa takwimu halisi za kufanyia tathmini ya utendaji wa wafanyakazi, tathmini ya malipo, na idadi ya siku za likizo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi hizo kuhamisha jukumu la utoaji wa taarifa za mahudhurio moja kwa moja kufanywa na watendaji wa Idara ya Utumishi na sio kitengo chengine chochote. Ikiwa Idara ina upungufu wa taaluma katika mchakato wa kuzitoa taarifa kwenye mfumo ni vyema kitengo cha TEHAMA kutoa mafunzo kwa watendaji wa Idara ya Utumishi na kutoa msaada wa kiufundi pale itakapohitajika. Hali hii itasaidia katika kuongeza udhibiti wa kupata taarifa sahihi za mahudhurio ya watumishi.

Vile vile kwa Taasisi zilizokuwa hazijachukuwa hatua za utekelezaji wa agizo lililonakiliwa hapo juu ni vyema kufanya jitihada za makusudi za kuandaa mpango wa dharura wa ununuzi wa vifaa na mfumo wa kielektroniki wa kusimamia mahudhurio ili kwenda sambamba na maagizo ya Serikali kupitia Wizara ya Utumishi na hatimae kupatikana kwa ufanisi na tija iliyokusudiwa. Taasisi zilizobainika kuwa na dosari hiyo ni kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 15: Taasisi zilizobainika kuwa na dosari katika udhibiti wa taarifa za mahudhurio kwa kutumia mfumo wa Biotime Attendance System**

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Ofisi ya Rais Katiba Sheria Utumishi na Utawala Bora |
| 2. | Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar |
| 3. | Wakala wa Matukio ya Kijamii Zanzibar |
| 4. | Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar |
| 5. | Shirika la Bandari Zanzibar |
| 6. | Mamlaka ya Uwekezaji wa Vitega Uchumi Zanzibar |
| 7. | Kamisheni ya Utalii Zanzibar |

### 3.4.1.14 Kukosekana kwa Mpango wa Kusimamia, kudhibiti na Kudumisha Mfumo (System Sustainability Plan)

Ukaguzi uliomba mkataba wa Makubaliano ya Utoaji wa Huduma (Service Level Agreement – SLA) baina ya Taasisi husika na Washauri Elekezi (Vendors) wanaohusika katika utengenezaji wa mifumo na upatikanaji wa huduma za msaada wa kiufundi kwenye Mifumo ya Taasisi inayotengenezwa.

Lengo ni kupima kwa kiasi gani Taasisi za Serikali zimejipanga katika kusimamia, kudhibiti na kuendeleza huduma zinazotolewa kupitia mifumo yao. Hadi ukaguzi unakamilika baadhi ya Taasisi zimeshindwa kuwasilisha mikataba ya utoaji wa huduma ili kuweza kubaini na kupima kiwango gani cha huduma kinapatikana kupitia mikataba hiyo na hali halisi ya thamani ya fedha zinazotumika kwa kulipia huduma hizo.

Aidha, baadhi ya Taasisi zimewasilisha mikataba, hata hivyo imebainika mikataba hiyo ni dhaifu katika kusimamia, kudumisha na kuendeleza huduma za mfumo baada ya kukamilika utengenezwaji wake kutokana na kukosekana kwa baadhi ya vipengele muhimu vya usimamizi na uendelezaji wa mifumo kwenye mkataba. Vile vile imebainika baadhi ya Kampuni zinazotengeneza Mifumo kushindwa kutekeleza masharti ya kuendeleza kutoa huduma na maboresho ya mifumo kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba.

Dosari zilizobainishwa hapo juu zinaweza kusababisha Taasisi kushindwa kufuatilia na kupima uwajibikaji wa Mshauri Elekezi /Kampuni zinazotengeneza mifumo (Vendors) katika utekelezaji wa mkataba kwa taasisi zitakazohusika na makubaliano hayo.

Aidha, taasisi inaweza kushindwa kusimamia mifumo yake ipasavyo hususan katika matumizi sahihi, matengenezo na maboresho ya mfumo jambo ambalo litapelekea mfumo kukosa ufanisi wa utendaji kazi na hatimae kuharibika kabla ya muda wa makubaliano ya matumizi  na kuingiza hasara Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi hizo kuandaa mpango wa kusimamia, kudhibiti na kudumisha Mfumo (System Sustainability Plan) pamoja na kufunga mkataba wa kuendeleza huduma za msaada wa kiufundi (SLA) baina yao na watengenezaji wa mifumo utakaofafanua kwa uwazi makubaliano yote ya huduma za kiufundi yatakayotolewa, muda wa mkataba, njia zitakazotumika kutoa msaada pamoja na gharama zitakohitajika kufanikisha huduma hizo ili mfumo uweze kudumu na kupata msaada wa kiufundi pamoja na huduma za sasisho kwa wakati.

Vile vile kuweka vifungu vya masharti ya kuwabana na kutoa adhabu kwa zile Kampuni zinazoshindwa kutekeleza au zinazokiuka masharti ya makubaliano ya mkataba.

Taasisi zilizobainika kuwa na dosari hiyo ni kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 16: Taasisi zilizobainika kuwa na mapungufu katika Mpango wa Kusimamia, kudhibiti na kudumisha Mifumo**

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Zanzibar |
| 2. | Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar |
| 3. | Ofisi ya Rais Katiba Sheria Utumishi na Utawala Bora |
| 4. | Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar |
| 5. | Wakala wa Matukio ya Kijamii Zanzibar |
| 6. | Mamlaka ya Uwekezaji wa Vitega Uchumi Zanzibar |

### 3.4.1.15 Kutounganishwa kwa Mfumo ya Taasisi (System Integration)

Ukaguzi umebaini kwamba baadhi ya Taasisi za Umma mifumo yao huingizwa taarifa kutoka katika mifumo mengine tofauti ya Taasisi nyengine ambapo taarifa hizo huingizwa kwa njia ya kawaida bila ya kuunganisha mifumo hiyo. Kwa mfano mifumo ya kukusanyia mapato na matumizi kutounganishwa na mifumo ya kibenki pamoja na mifumo ya ZanMalipo ili kupatikana nambari za udhibiti wa malipo na taarifa sahihi za makusanyo na matumizi ya fedha.

Vile vile imebainika kuwepo kwa mifumo katika baadhi ya Taasisi ambayo haijaunganishwa na mifumo mikuu ya Taarifa kama vile mfumo ya ZSSF, NIDA, ZANID, mifumo ya Utumishi n.k. jambo ambalo linapelekea kujitokeza kwa changamoto nyingi za usahihi wa taarifa kutokana na kutokuunganishwa mifumo hiyo ili kuhamisha taarifa kwa njia ya kiotomatiki na sio kwa njia ya mkono (manually).

Kutounganishwa kwa mifumo hiyo kunaweza kusababisha kujitokeza kwa makosa katika uingizaji wa nambari za NIDA, ZSSF na hesabu za Benki, nambari za udhibiti na hatimae kusababisha mfumo kuwa na taarifa zisizo sahihi "gabbages" na kupelekea kutopatikana kwa uadilifu wa taarifa (integrity) jambo ambalo linaweza kuingiza hasara Serikali.

Aidha, kutounganishwa kwa mifumo kunaweza kupelekea kuongezeka kwa vitengo vya uvujaji wa mapato ya Serikali kutokana na mapato hayo kukusanywa kwa njia za kawaida (manually) kwenye vyanzo vya mapato.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi hizo kufanya jitihada za kuunganisha mifumo hiyo ili kuimarisha utendaji kazi na kupatikana kwa usahihi wa taarifa mbali mbali pamoja na kudhibiti uvujaji wa mapato ya Serikali. Orodha ya Taasisi zilizobainika kuwa na dosari hiyo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 17: Taasisi zilizokuwa hazijaunganisha mifumo yao na mifumo mengine husika kwa mujibu wa shughuli zao**

| Namba | Jina la Taasisi | Mfumo wa Taasisi | Mifumo inayopaswa kuunganishwa nayo |
|---|---|---|---|
| 1. | Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Zanzibar | eProz | ZanMalipo,ZANID, ZBPRA, Leseni, Mifumo ya Benki |
| 2. | Ofisi ya Rais Katiba Sheria Utumishi na Utawala Bora | HR-Payroll System | NIDA, Mifumo ya Benki, ZSSF |
| 3. | Wizara ya Maji Nishati na Madini | Madini Management System | ZanMalipo, ZBPRA, ZRA |
| 4. | Mamlaka ya Viwanja vya Ndege | ZAAID, Car Sticker | ZanMalipo |
| 5. | Kamisheni ya Wakf na Mali ya Amana | Mfumo wa Mirathi (ZAMIS) | ZBPRA, Mifumo ya Benki, Kamisheni ya Ardhi, ZSSF |
| 6. | Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar | ZIRS | Petroman (Fuel Marking System), ZIDRAS, Tax Payer (TIN Number System) |
| 7. | Shirika la Umeme Zanzibar | Suprima | ZanMalipo |

### 3.4.1.16 Kutofanyika kwa Tathmini ya Kuchunguza na Kufanya Jaribio la Kupenya (Vulnerability Assesment and Penetration Test - VAPT)

Tathmini ya kuchunguza (Vulnerability Assessment) ni mchakato wa kufanya uchunguzi na uchambuzi wa kitaalamu katika mazingira ya TEHAMA kwa lengo la kubaini udhaifu au mwanya uliopo na hatari (Risk) zilizopo zinazoweza kusababisha madhara kwa rasilimali za TEHAMA kama vile mifumo, taarifa na miundombinu ya TEHAMA katika Taasisi na kuchukuwa hatua za kuziondoa na kuziba mianya inayoweza kusababisha hatari hizo kutokea.

Aidha, Jaribio la Kupenya (Penetration Test) ni mchakato unaofanyika wa kuingia ndani ya mazingira ya TEHAMA ikiwa ni mifumo au miundombinu ya TEHAMA kinyume na taratibu za kawaida (hacking) ili kuweza kuzifikia taarifa zilizomo ndani yake (gain access). Lengo la kufanya jaribio la kupenya ni kupima usalama wa mfumo na miundombinu iliyopo.

Ukaguzi umebaini kwamba, baadhi ya Taasisi za Umma hazifanyi zoezi la kupima tathmini ya Vihatarishi na kufanya jaribio la kupenya kwenye Mifumo na Miundombinu yao ya TEHAMA "Vulnerability Assessment and Penetration Test" ili kubaini maeneo dhaifu (hatarishi) katika mifumo na miundombinu ambayo inaweza kutumiwa na wasiohusika kupenya na kufanya mashambulizi ndani ya Mifumo.

Kutofanyika kwa zoezi hilo kunaweza kusababisha kutojuulikana kwa maeneo hatarishi yanayoweza kushambuliwa kirahisi katika mfumo kupitia udukuzi "cyber attack" au njia nyenginezo na kusababisha hatari kubwa ya kuvuja kwa taarifa za Taasisi au kuharibiwa kwa mfumo na kuingia hasara Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa taasisi hizo kuhakikisha unachukuwa hatua za kufanya mchakato wa Tathmini ya Kuchunguza na Majaribio ya Kupenya katika mifumo yake mikuu na miundombinu ya TEHAMA ili kubaini dosari zilizopo na kuziba mianya inayoweza kusababisha hatari za mashambulizi. Aidha zoezi hili linatakiwa kufanywa kwa kushirikiana na Wakala wa Serikali Mtandao ili kupatikana usimamizi bora, ufanisi na tija inayokusudiwa. Orodha ya Taasisi zilizokuwa hazijafanya mchakato huo ni kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 18: Taasisi ambazo hazijafanya tathmini ya kuchunguza na Majaribio ya Kupenya katika mifumo**

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Zanzibar |
| 2. | Ofisi ya Rais Katiba Sheria Utumishi na Utawala Bora |
| 3. | Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar |
| 4. | Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi |
| 5. | Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar |
| 6. | Kamisheni ya Wakf na Mali ya Amana |
| 7. | Wakala wa Matukio ya Kijamii Zanzibar |

### 3.4.1.17 Dosari katika Usimamizi, Uendeshaji na Udumishaji wa Kifaa cha Kudhibiti Mawasiliano katika Mtandao "SOPHOS XG FIREWALL"

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika uwepo wa dosari mbalimbali kwa baadhi ya Taasisi za Umma ambapo dosari hizo ni pamoja na kutokuwepo kwa kifaa cha "SOPHOS XG Firewall" kwa ajili ya kudhibiti mawasiliano na kulinda mtandao wa Afisi, vile vile imebainika baadhi ya Taasisi kutumia vifaa vya Taasisi nyengine jambo ambalo linapelekea usimamizi dhaifu wa kifaa hicho na hatimae kushindwa kupatikana kwa usalama wa kutosha wa mtandao wa Afisi.

Aidha, ukaguzi umebaini baadhi ya Taasisi zinatumia vifaa hivyo bila ya kuwa na leseni katika program zake za kuimarisha ulinzi na usalama wa rasilimali za TEHAMA jambo ambalo linapelekea vifaa hivyo kushindwa kufanya kazi vizuri katika kuimarisha ulinzi na kuongeza usalama wa mtandao na mifumo ya Taasisi.

Vile vile imebainika baadhi ya Taasisi za Umma zinazotumia vifaa hivyo kushindwa kufanya usanidi wa sera za kiusalama (security policy configuration) kwenye "Firewall" hizo ili kudhibiti baadhi ya tovuti zilizokuwa na asili ya vihatarishi vya kiusalama wa mitandao (Risky Websites) kama vile tovuti za kupakua "download sites/Torrent sites", tovuti za kubeti "gambling sites", tovuti zisizo za kimaadili "porn sites", tovuti za kuangalia michezo "netflix" pamoja na tovuti nyenginezo ambazo zimekatazwa kutumika kwa mujibu wa miongozo, kanuni, Sheria na Utamaduni wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kukosekana kwa usimamizi wa kifaa cha kudhibiti mawasiliano "Sophos XG Firewall" kunaweza kusababisha Taasisi kutopata huduma za mawasiliano au kuchelewa kupata huduma hizo kwa wakati endapo ikitokea changamoto katika mtandao wa Afisi.

Vile vile kukosekana kwa leseni ya kufanyia kazi katika vifaa hivyo kunaweza kupelekea vifaa kushindwa kufanya kazi zake za kuimarisha ulinzi na usalama wa mifumo na miuondombinu ya TEHAMA kwa weledi na ufanisi na hatimae kusababisha upotevu wa taarifa, uharibifu, kuongezeka kwa mashambulizi na kuingiza hasara Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi hizo kufanya marekebisho ya dosari zilizobainishwa hapo juu katika vifaa vya kudhibiti mawasiliano "Sophos XG Firewall" ikiwemo kununua vifaa vya kisasa, imara na vyenye leseni kamili za matumizi ili kuondosha usumbufu na vile vile kuweza kufanya usimamizi na udhibiti mzuri wa mtandao wa Taasisi pamoja na miundombinu yao kwa ujumla. Orodha ya Taasisi zilizobainika kuwa na dosari katika kifaa cha kusimamia ulinzi na usalama wa Mtandao "Firewall" ni kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 19: Taasisi ambazo zina dosari katika kifaa cha kusimamia ulinzi na usalama wa Mtandao wa Afisi "Firewall"**

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Ofisi ya Rais Katiba Sheria Utumishi na Utawala Bora |
| 2. | Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar |
| 3. | Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi |
| 4. | Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar |
| 5. | Taasisi ya Viwango Zanzibar |
| 6. | Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar |
| 7. | Shirika la Bandari Zanzibar |
| 8. | Mamlaka ya Uwekezaji wa Vitega Uchumi Zanzibar |
| 9. | Wakala wa Chakula Dawa na Vipodozi Zanzibar |
| 10. | Kamisheni ya Utalii Zanzibar |
| 11. | Mamalaka ya Usafiri Baharini. |

### 3.4.1.18 Mapungufu ya kiusalama yaliyobainika katika Udhibiti wa Mtandao wa ndani (LAN) kwa Taasisi za Umma

Kwa mujibu wa ISA 315 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2019 inahitaji kwamba rasilimali pamoja na miundombinu yote ya TEHAMA kulindwa kwa kuekewa usalama kutokana na kuingiliwa (kufikiwa) na wasiohusika au wasioidhinishwa kwenye Mazingira ya TEHAMA.

Ukaguzi ulifanya tathmini ya usalama wa Mitandao ya Ndani (Local Area Network - LAN) pamoja na miundombinu ya mtandao (network infrastructures) inayotumiwa na taasisi mbali mbali za Umma kwa kuangalia hali ya udhibiti wa kiusalama (security controls) uliopo kwenye Mitandao hiyo na kubaini kwamba hakuna udhibiti imara wa kiusalama uliowekwa katika mitandao ya ndani ya Afisi (LAN) dhidi ya wasiohusika au wasioidhinishwa kutumia mitandao hiyo.

Kifaa chochote cha TEHAMA kwa mfano kompyuta mara tu kinapoungwa kwenye Mtandao wa Afisi (LAN) kwa kutumia 'network cable' au 'wireless connection' kinaweza kupata huduma ya 'Internet', lakini pia kinaweza kuona na kufikia vifaa vyote muhimu vilivyoungwa ndani ya Mtandao huo (network devices) bila ya kuwepo kwa udhibiti wowote wa kiusalama (authentication) kutoka kwenye 'SOPHOS Firewall' ambao ungeweza kuzuwia kompyuta hiyo kuona au kufikia vifaa vyengine mara tu baada ya kuunganishwa na LAN.

Kutokuwepo kwa udhibiti imara wa kiusalama kwenye mitandao ya LAN kwa Afisi kunaweza kusababisha hatari ya kuvuja kwa taarifa (data breaches) zilizo ndani ya kompyuta za afisi, vile vile kuweza kupata mashambulizi (cyber attacks) kwenye server za mifumo jambo ambalo litapelekea Afisi kupoteza taarifa muhimu na kuingiza hasara Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi hizo kununua vifaa hivyo na kuhakikisha unaimarisha udhibiti na usalama katika mtandao wa ndani (LAN) pamoja na mazingira yake ya TEHAMA kwa kufanya usanidi wa kiusalama kwenye kifaa cha ulinzi kinachotumika na Afisi 'SOPHOS Firewall' ili kuweza kudhibiti, kuimarisha ulinzi na usalama wa Mtandao dhidi ya watumiaji wasiohusika, wasioidhinishwa au wasiojuulikana, baadhi ya maeneo kwenye firewall yanayopaswa kufanyiwa usanidi ni kama vile Captive Portal, AD SSO, NTLM n.k.

Vile vile ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi kuweka mtandao zaidi ya mmoja (Multiple LAN/ DMZ) kwa lengo la kutenganisha huduma zinazotolewa kupitia mitandao baina ya wafanyakazi wa ndani na wageni, wasiohusika, wasioidhinishwa au wasiojulikana katika Afisi. Orodha ya Taasisi zilizobainika kuwa na dosari hizo ni kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 20: Taasisi ambazo zina dosari katika vifaa vyake vya kudhibti ulinzi na usalama wa mtandao "SOPHOS FIREWALL"

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Zanzibar |
| 2. | Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora |
| 3. | Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi |
| 4. | Kamisheni ya Wakf na Mali ya Amana |
| 5. | Mamlaka ya Mapato Zanzibar |
| 6. | Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar |
| 7. | Ofisi ya Rais Fedha na Mipango |

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 8. | Shirika la Bandari Zanzibar |
| 9. | Mamlaka ya Uwekezaji wa Vitega Uchumi Zanzibar |
| 10. | Wakala wa Chakula Dawa na Vipodozi Zanzibar |
| 11. | Kamisheni ya Utalii Zanzibar |
| 12. | Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali |

### 3.4.1.19 Kukosekana kwa udhibiti na usalama wa taarifa zilizomo ndani ya komyputa za Afisi

Mabadiliko ya Sera na Miongozo inayotolewa na Wakala wa Serikali Mtandao yamekuwa yakizingatia sera ya kisasa ya Mkakati wa Kidigitali wa Serikali *(Digital Government Strategy)* ambapo Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zinashajihishwa kutekeleza majukumu yao kupitia mifumo ya TEHAMA kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utendaji kazi, urahisi, usalama wa taarifa pamoja na kupatikana kwa tija.

Moja ya mambo muhimu yaliyozingatiwa katika Sera hizo ni kuhakikisha kwamba Taasisi za Serikali zinatumia miundombinu iliyo salama na imara kwa lengo la kutunza taarifa za Serikali katika hali ya usalama, vile vile taasisi kufanya huduma za matengenezo na maboresho ya rasilimali za TEHAMA kwa wakati kwa lengo la kuzidumisha na kuziendeleza ili zeweze kufanya kazi kwa ufanisi.

Ukaguzi ulifanya uhakiki wa kompyuta zinazotumika katika Taasisi za Umma kwa lengo la kuangalia hali ya udhibiti na usalama wa taarifa zilizopo ndani yake pamoja na kuangalia utaratibu wa kufanya matengenezo na maboresho "service and maintanance" kwa rasilmali za TEHAMA ambazo ni vifaa, mifumo na miundombinu ya TEHAMA ili kuweza kudumisha na kufanya kazi kwa ufanisi.

Ukaguzi umefanya tathmini na kubaini kompyuta nyingi zinazotumika kwenye Taasisi za Umma Unguja na Pemba zipo katika hatari ya kuungua, kushambuliwa na virusi na programu hatarishi (malicious software), hatari ya kuharibika au kupotea kutokana na kukosekana kwa udhibiti mzuri na usimamizi bora unaopaswa kuwepo kwenye rasilimali hizo za TEHAMA. Aidha, ukaguzi umebaini uwepo wa dosari mbali mbali kama zifuatazo;

- Kukosekana kwa Mashine za UPS Backup Power Supply zinazoungwa na kompyuta za Afisi kwa ajili ya kuziendeleza kompyuta kuwaka wakati umeme unapozimwa, vile vile imebainika baadhi ya mashine za UPS zimeharibika, hivyo umeme ukizimwa na kompyuta huzima papo hapo.
- Baadhi ya kompyuta kukosa "Antivirus" na baadhi yao zimeisha muda wa matumizi kwa kipindi cha muda mrefu (expired).
- Baadhi ya kompyuta hazina leseni za matumizi katika Mfumo wa Uendeshaji wa kompyuta "The Copy of Windows Operating System are not Genuine".
- Kutowekwa udhibiti kwenye kompyuta katika sehemu za kuingiza flash disk, wire za kuchaji simu, pamoja na milango ya CD/DVD.
- Kuchelewa au kutofanyiwa kabisa huduma za matengenezo ya rasilimali za TEHAMA "services & maintanance".
- Baadhi ya kompyuta kotowekwa udhibiti wa nenosiri.

Kuwepo kwa hali hii kunaweza kusababisha hatari ya kuungua kwa kompyuta za Afisi, upotevu wa taarifa pamoja na uharibifu wa mifumo inayotumika na Taasisi na kupelekea kuingiza hasara Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi hizo kufanya jitihada za kuongeza udhibiti katika kompyuta ili kulinda taarifa zilizomo ndani yake, aidha baadhi ya njia zinazoshauriwa kutumika katika Taasisi ili kudhibiti upotevu wa taarifa ni pamoja na kuandaa mpango na kufanya matengenezo ya maboresho "services and maintanance" mara kwa mara kwa vifaa na miundombinu ya TEHAMA kwa kutumia mpango maalum utakaondaliwa na Afisi kwa kushirikisha kitengo cha TEHAMA, kuweka mfumo imara wa umeme (power backup system) utakoweza kudhibiti kompyuta kutozima mara tu umeme unapokatika, kusimamia utekelezaji wa sera za matumizi ya kompyuta katika ofisi ikiwemo kuweka sera imara za kudhibiti matumizi ya media kwenye kompyuta kama vile matumizi ya flash disk, CD/DVD na uunganishwaji wa simu katika kompyuta, kutumia mfumo wa network za ndani (Files and Folders Sharing - LAN) kwa ajili ya kuhamisha taarifa kutoka kompyuta moja kwenda nyengine ndani ya ofisi na vile vile kununua programu halisi (Genuine and licensed Software) zenye ubora na za kisasa ili kuweza kupata usalama "Security Updates" katika matumizi ya kompyuta.

Orodha ya Taasisi zilizobainika kuwa na dosari hiyo ni kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 21: Taasisi zilizobainika kuwa na mapungufu katika kudhibiti na kusimamia usalama wa taarifa ndani ya kompyuta za Afisi**

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Zanzibar |
| 2. | Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora |
| 3. | Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar |
| 4. | Wizara ya Ujenzi,Mawasiliano na Uchukuzi |
| 5. | Wizara ya Maji, Nishati na Madini |
| 6. | Kamisheni ya Wakf na Mali ya Amana |
| 7. | Wakala wa Matukio ya Kijamii Zanzibar |
| 8. | Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar |
| 9. | Baraza la Usimamizi wa Leseni za Biashara |
| 10. | Baraza la Manispaa ya Mjini |
| 11. | Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar |
| 12. | Ofisi ya Rais Fedha na Mipango |
| 13. | Mamlaka ya Uwekezaji wa Vitega Uchumi Zanzibar |
| 14. | Wakala wa Chakula Dawa na Vipodozi Zanzibar |
| 15. | Kamisheni ya Utalii Zanzibar |
| 16. | Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali |
| 17. | Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar |

### 3.4.1.20 Kukosekana kwa Mpango wa kusimamia Matukio ya TEHAMA (ICT Incident Management Plan)

Usimamizi wa matukio ya TEHAMA (Incidence Management Plan) ni mpango unaojumuisha utunzaji wa kumbukumbu za matukio ya TEHAMA katika nyaraka maalumu na kuelekeza hatua kwa hatua nini kifanyike mpaka suluhisho linapopatikana na kufungwa kwa changamoto husika. Aidha, mpango huo hufafanua namna ya kuripoti na hatua za kuchukuliwa kwa tukio (changamoto) tangu inapoanza kujitokeza katika utendaji kazi wa mifumo na rasilimali za TEHAMA hadi inapokamilika kuchukuliwa hatua na wahusika wa kitengo cha TEHAMA.

Ukaguzi haukupatiwa nyaraka inayoonesha Mpango na utaratibu wa Kusimamia matukio ya TEHAMA kwa baadhi ya Taasisi ambazo ukaguzi umefanyika.

Aidha, ukaguzi ulishindwa kupata ripoti ya Matukio ya TEHAMA yaliyogunduliwa na kufanyiwa kazi katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na matakwa ya Viwango bora kubalifu (Best Practice) ISO/IEC 27001 kifungu nambari 10.2 kinachotoa utaratibu wa uwepo wa "ICT incident managent procedures" na utekelezaji wake ili kuboresha ufanisi katika utowaji huduma za TEHAMA

Aidha, kutochukua njia za kutosha katika kupambana na Matukio ya TEHAMA pamoja na kutokua na muongozo rasmi unaotumika kuripoti na kutatua matatizo kunaweza kusababisha kuchelewa kutatuliwa matukio hayo na kupelekea kutopatikana huduma kwa muda mrefu bila ya sababu za msingi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa taasisi hizo kutengeneza mpango na kuweka utaratibu wa kuhifadhi na kushughulikia matukio mbalimbali yanayohusiana na TEHAMA katika Taasisi hiyo. Miongoni mwa Taasisi zilizobainika kuwa na dosari hiyo ni kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 22: Taasisi ambazo hazina Mpango wa Usimamizi wa matukio (Incident Management Plan)**

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi |
| 2. | Baraza la Usimamizi wa Leseni za Biashara |
| 3. | Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar |
| 4. | Ofisi ya Rais Fedha na Mipango |
| 5. | Wakala wa Chakula Dawa na Vipodozi Zanzibar |




# SURA YA NNE



# 4.0 MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

## 4.1 UFAFANUZI WA DOSARI ZILIZOBAINIKA

Sehemu hii imeeleza kwa kina dosari zilizobainika katika ukaguzi wa Mifumo na Miundombinu ya TEHAMA kwa Taasisi za Umma ambapo dosari hizo zimefafanuliwa na kupangwa kwa kuzingatia maeneo (domain) tofauti kulingana na uhalisia (nature) wa dosari hizo.

Kwa ujumla katika ukaguzi uliofanyika wa Mifumo ya TEHAMA kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imebainika kwamba Taasisi nyingi zimeimarika katika kuhakikisha kunafuatwa miongozo, taratibu, viwango, uanzishwaji, usimamizi imara, uendeshaji na udumishaji bora wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA ya Taasisi.

Hata hivyo ukaguzi umebaini kuendelea kujitokeza kwa dosari za kiutendaji kwa baadhi ya Taasisi za Serikali ambapo baadhi ya dosari ziliweza kurekebishwa na kupatiwa ufafanuzi wakati wa ukaguzi na baadhi ya dosari hazikuweza kupatiwa ufafanuzi hadi ukaguzi unakamilika na kupelekea kujitokeza kwa hoja za ukaguzi. Matokeo ya ukaguzi huo ni kama ifuatavyo:-

### 4.1.1 MAMLAKA YA UNUNUZI NA UONDOSHAJI WA MALI ZA UMMA (ZPPDA)

Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma (ZPPDA) kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 4.1.1.1 Kukosekana kwa Nyaraka muhimu za Utengenzwaji wa Mfumo

Kwa mujibu wa utaratibu unaokubalika (best practises) na Muongozo wa eGA nambari **eGAZ/EXT/IGG /001** wa Utekelezwaji wa Miradi ya TEHAMA, wa mwaka 2020 ya Utekelezwaj inahitaji Mifumo ya TEHAMA inapoanzishwa lazima ifuate taratibu na mbinu "Methodology" bora za utengenezwaji wa Mifumo hiyo (System Development Life Cycle -SDLC) pamoja na Project Development life Cycle – PDLC. Mbinu hizo zimekusanya hatua tofauti za mchakato wa utengenezwaji wa mfumo.

Aidha, unahitaji mradi wa TEHAMA unapotekelezwa lazima ufuate taratibu na mbinu "Methodology" ya Project Development life Cycle – PDLC . Mbinu hiyo imekusanya hatua tofauti za mchakato wa utengenezwaji wa mfumo.

Aidha kifungu nambari 2.3 cha muongozo huo kimefafanua kwamba kwa kila hatua kutakuwa na matayarisho ya nyaraka ambazo zitasaidia katika utengenezwaji, uendeshaji, usimamizi na udumishaji wa mfumo.

Aidha, Miongozo hiyo imefafanua kwamba kwa kila hatua kutakuwa na matayarisho ya nyaraka ambazo zitasaidia katika utengenezwaji, uendeshaji, usimamizi na udumishaji wa mfumo. Baada ya kukamilika kwa mradi kutakuwa na mpango wa kusimamia na kudumisha mradi ili kuweza kufanya kazi kwa ufanisi na kuendelea kutoa huduma bora kama ilivyokusudiwa.

Ukaguzi ulifanya mapitio ya Mradi wa TEHAMA wa Uanzishwaji wa Mfumo wa **e-Proz** unaosimamiwa na Wakala wa Serikali Mtandao na Mfumo wa **Vendor Registration System** unaosimamiwa na watendaji wa Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma pamoja na kuomba nyaraka mbalimbali za utengenezwaji wa Mifumo hiyo, lakini hadi ukaguzi unakamilika baadhi ya nyaraka muhimu hazikuweza kupatikana kwa mifumo yote miwili, nyaraka zilizokosekana ni kama zifuatazo: -

- Ripoti ya Pendekezo la Mradi na Ripoti ya Upembuzi Yakinifu (Project Proporsal Report / Business Case/Feasibility Study Report) kuhusiana na uanzishwaji wa Mfumo wa e-Proz na Mfumo wa Vendor Registration System inayoeleza kwa ufupi hatua mbalimbali za utengenezwaji wa mfumo pamoja na kuchambua kwa kina gharama zote za fedha zitakazotumika kwenye kila kipengele cha mradi huo (Project Breakdown Cost).
- Ripoti ya kufanyika kwa Tathmini ya Vihatarishi vya Mradi (Risk Assessment Report).
- Nyaraka za mahitaji ya Mtumiaji zilizoidhinishwa (User Requirements document).
- Nyaraka za mahitaji ya Mfumo (System Requirements Specifications).
- Hati ya uendeshaji wa Mfumo (Business Process Document).
- Nyaraka za usanifu wa Mfumo (System Design Documents).

- Mpango wa kusimamia, kuzikabili na kuziepuka hatari zinazoweza kujitokeza kwenye utekelezaji wa Mradi (Risk Management Plan).
- Ripoti ya hali ya Mradi iliyofikia (Progress Project Report) pamoja na gharama zilizokuwa zimetumika kabla ya kumalizika kwa mradi huo wa utengenezwaji wa Mfumo.
- Ripoti ya uthibitisho wa kukubalika kwa utendaji kazi katika majaribio ya mifumo (UAT Report).
- Ripoti ya Kuhakiki Ubora wa Mfumo (Quality Assurance Report) kwa mujibu wa Mpango wa kusimamia Ubora (Quality Management Plan) uliopo.
- Kodi za kutengenezea Mifumo "Source Codes".
- Barua ya kukubalika Mfumo (Acceptance Letter).
- Miongozo ya usanidi wa Mfumo (System Configuration Manuals).
- Miongozo ya watumiaji wa Mfumo (Application User Manuals).
- Nyaraka za Taarifa za Mfumo na Haki walizopewa watumiaji kwenye Mfumo (User Matrix documents).

Kukosekana kwa nyaraka hizo kunatoa ishara kwamba kuna udhaifu katika mchakato wa utengenezwaji wa mfumo wa manunuzi wa e-Proz pamoja na Mfumo wa Vendor Registration System kutokana na kutokuzingatiwa kwa Miongozo wa utekelezaji wa miradi ya TEHAMA (SDLC).

Aidha, kukosekana kwa nyaraka hizo kunaweza kusababisha hatari (risk) ya kutengenezwa mifumo isiyokuwa na tija na ufanisi wa utendaji kazi na kupelekea kushindwa kufikia malengo yaliyokusudiwa jambo ambalo linaweza kusababisha Afisi kuingia gharama za ziada za marekebisho ya mfumo na hatimae kuingiza hasara Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kuhakikisha unazingatia na kufuata kikamilifu miongozo na viwango vinavyokubalika kitaifa na kimataifa katika utekelezaji wa miradi ya TEHAMA. Vile vile, Mamlaka kuhakikisha nyaraka zote zinazohusika kwenye mfumo zinatengenezwa na kuwekewa kumbukumbu kwa kila hatua ili kupatikana ufanisi katika usimamizi na udumishaji na mifumo ya TEHAMA ya Afisi.

#### 4.1.1.2 Kukosekana kwa Mpango wa Kusimamia, kudhibiti na Kudumisha Mfumo (System Sustainability Plan)

Ukaguzi uliomba mkataba wa Makubaliano ya Utoaji na Uendelezaji wa Huduma za Mfumo wa e-Proz (Service Level Agreement – SLA) ulioingia baina ya Mshauri elekezi wa Mfumo (Ozone International LLC) na Wakala wa Serikali Mtandao (eGAZ) kupitia ZPPDA kuhusiana na upatikanaji wa huduma za msaada wa kiufundi kwenye Mfumo wa e-Proz. Lengo la kuomba mkataba ni kupima kwa kiasi gani ZPPDA imejipanga katika kusimamia, kudhibiti na kuendeleza huduma zinazotolewa kupitia mfumo huo. Hadi ukaguzi unakamilika mkataba huo haukupatikana kwa ukaguzi.

Kutopatikana kwa mkataba wa makubaliano ya utoaji wa huduma na muongozo wa mtumiaji (SLA) kunaweza kusababisha mfumo kushindwa kusimamiwa ipasavyo hususan katika matumizi sahihi, matengenezo na maboresho ya mfumo jambo ambalo litapelekea kukosekana ufanisi wa utendaji kazi na hatimae kuingiza hasara Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZPPDA kufanya jitihada za upatikanaji wa mkataba wa makubaliano ya kuendeleza huduma za msaada wa kiufundi (SLA) utakaofafanua kwa uwazi makubaliano yote ya huduma za kiufundi yatakayotolewa, muda wa mkataba, njia zitakazotumika kutoa msaada pamoja na gharama vile vile gharama zitakohitajika kufanikisha huduma izo ili mfumo uweze kudumu na kupata huduma za msaada wa kiufundi na pamoja na huduma za sasisho kwa wakati.

#### 4.1.1.3 Uhifadhi wa Taarifa za manunuzi ya Serikali nje ya Mipaka ya Zanzibar

Kwa mujibu wa kifungu nambari 4.3.3 cha Muongozo wa Serikali Mtandao toleo nambari 1 la Mwaka 2022 pamoja na viwango vya kimataifa vya usalama vya Taasisi (ISO 27031) vinahitaji Taasisi zenye kutoa huduma kupitia mifumo na miundombinu ya TEHAMA kuwa na Mpango maalum wa kuweza kuendeleza Biashara, kurejesha huduma pamoja na kukabiliana na maafa wakati janga likitokea katika taasisi husika (Business Continuity Plan & Disaster Recovery Plan).

Aidha kutokana na kuimarisha ulinzi na usalama wa taarifa, kwa mujibu wa utaratibu bora unaokubalika (best practise) Taasisi za Umma zinatakiwa kuhifadhi taarifa zake za msingi kwenye Kituo Kikuu cha Mawasiliano (Primary Data Center) kilichopo kwenye Taasisi hiyo au Kituo Kikuu cha Taifa cha Kuhifadhi Taarifa kilichopo ndani ya Mamlaka ya Serikali kwa mujibu wa Sheria (National Data Center). Vile vile nakala za taarifa (backup data) zinatakiwa kuhifadhiwa katika Kituo Mbadala cha Taarifa (Disaster Recovery Site) kilichopo maeneo yenye umbali wa angalau maili 62 kutoka kwenye Kituo Kikuu cha Kuhifadhi Taarifa (Primary Data Center) ambacho Taasisi husika itakuwa na mamlaka nacho kamili katika kusimamia, kuendesha na kuhakikisha kuna usalama wa taarifa zake. Lengo ni kwamba pindipo janga likitokea katika kituo kikuu, taarifa zitaweza kupatikana na huduma kuendelezwa kupitia kituo Mbadala cha Taarifa.

Ukaguzi umebaini kwamba Mfumo wa e-Proz pamoja na Taarifa zake za manunuzi zinazotumiwa na Serikali zinahifadhiwa nje ya mipaka ya Zanzibar. Hali hii imebainika kutokana na kuthibitika kuwa Kituo Kikuu cha Kuhifadhi Taarifa za Mfumo wa e-Proz kipo katika mji wa Muscat nchini OMAN ambacho kinajuulikana kama ni OMAN DATA PARK. Aidha, kituo hicho kinamilikiwa na kampuni hiyo binafsi ambapo taarifa zote za manunuzi ya Serikali zinahifadhiwa humo, ikizingatia kwamba taarifa za manunuzi ni siri na ni Mali ya Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kuhifadhiwa kwa taarifa za Serikali nje ya Mipaka ya Zanzibar kunaweza kusababisha kukosekana kwa usiri kwenye taarifa na vile vile kunaweza kupelekea hatari ya kuvuja, kushambuliwa, kuchezewa au kuharibiwa kwa taarifa za manunuzi ya Serikali kutokana na kutojulikana usalama wa kituo na miundombinu inayotumika katika kuhifadhi taarifa, kusafirisha taarifa, kusimamia na kuendesha mfumo wa e-Proz.

Aidha, kutotumika kituo kikuu cha Taifa cha Kuhifadhia Taarifa na mifumo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 7(1)(b) cha Sheria ya Uanzishwaji wa Shirika la Mawasiliano Zanzibar (ZICTIA) kinachoeleza kwamba Shirika la Mawasiliano Zanzibar litakuwa na kazi ya kusimamia na kuendeleza Kituo Kikuu cha Taifa cha Kuhifadhia Taarifa Zanzibar.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZPPDA kuchukuwa hatua muafaka za kufahamu na kujiridhisha kwa eneo ambalo mfumo wa e-Proz umehifadhiwa na kufanya kazi na  vile vile kuhakikisha kunakuwa na usiri na usalama wa taarifa dhidi ya kuchezewa, kudukuliwa, kushambuliwa au taarifa hizo kutumika kwengine kusikohusika, na vile vile kuhakikisha kunafuatwa kwa miongozo na sheria za ulinzi wa taarifa za kitaifa na kimataifa katika kutoa huduma bora kwa Umma.

#### 4.1.1.4 Ukiukwaji wa Sheria nambari 11 ya Mamlaka ya Manunuzi katika Mchakato wa Uanzishwaji, Usimamizi na Uendeshaji wa Mfumo wa e-Proz

Kwa mujibu wa kifungu nambari 5(1)(i) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Nambari 11 ya 2016 kinaitaka Mamlaka ya Manunuzi (ZPPDA) kuanzisha na kusimamia Mfumo wa Manunuzi kwa njia ya Kielektroniki.

Ukaguzi umebaini kwamba mfumo wa e-Proz husimamiwa na kuendeshwa kibiashara (business process) katika manunuzi na Wakala wa Serikali Mtandao (eGAZ) badala ya ZPPDA licha ya kwamba Wakala haina taaluma ya kutosha kuhusiana na kuendesha kibiashara kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma.

Aidha, ukaguzi umebaini mapungufu mbali mbali katika mchakato wa utengenezwaji wa  wa mfumo wa e-Proz ambapo mapungufu yenyewe ni kama yafuatayo:

- Kutoshirikishwa kwa Mamlaka ya Manunuzi (ZPPDA) katika mchakato wa utengenezwaji wa mfumo kuanzia hatua za awali hadi hatua ya kukamilika kwa mfumo huo wa e-Proz *(Planning Phase, Requirement and Analysis Phase, Design Phase, Implementation and Coding Phase, Testing Phase, Maintanance Phase)* licha ya kwamba utaratibu wa manunuzi kwa Taasisi za Serikali unasimamiwa na Mamlaka ya ZPPDA kwa mujibu wa Sheria.
- Mfumo kusimamiwa na kuendeshwa kibiashara na Wakala wa Serikali Mtandao (eGAZ) licha ya kwamba Wakala haina taaluma juu ya masuala ya Manunuzi na biashara kwa mujibu wa upeo wa majukumu yake.
- Kwa upande wa ZPPDA ukaguzi umebaini hakuna Afisa wa TEHAMA aliyepewa akaunti ya usimamizi (admin account) katika Mfumo wa e-Proz kwa ajili ya kutengeneza akaunti za watumiaji wa mfumo kwa upande wa ZPPDA badala yake akaunti hizo hutengenezwa na Maafisa wa eGAZ na wao kupewa ruhusa ya kutumia tu mfumo.

- Kutofanyika kwa kazi za ukaguzi na ufuatiliaji wa manunuzi ndani ya mfumo kwa zaidi ya kipindi cha mwaka kutokana na watendaji wa eGAZ kutowapa ruhusa watendaji wa Mamlaka ya Manunuzi kuingia katika mfumo na kufanya kazi zao ufuatiliaji kwa mujibu wa sheria.

Kutoshirikishwa kikamilifu kwa ZPPDA katika hatua za uanzishwaji, usimamizi na udumishaji wa Mfumo wa e-Proz ni kwenda kinyume na kifungu nambari 5(1)(h) na (i) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 jambo ambalo linaweza kusababisha Mamlaka ya Manunuzi kushindwa kusimamia majukumu yao ipasavyo kwa mujibu wa sheria na kupelekea majukumu hayo kufanyika nje ya mfumo.

Vile vile kunaweza kuingiza hasara kwa Serikali kutokana na kutopatikana kwa tija iliyokusudiwa na hatimae kujitokeza malalamiko mengi kwa watumiaji wa mfumo huo.

Katika kuimarisha hatua za kuendeleza mfumo wa e-Proz Ukaguzi unaushauri Mamlaka ya Ununuzi na Uendeshaji wa Mali za Umma kuishauri Serikali kwamba kwa vile mfumo tayari ulishaanzishwa na unaendelea kufanya kazi hivyo jukumu la Usimamizi na uendeshaji mfumo huo kibiashara (business process) libakie kwa Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma.

Kwa upande wa Wakala wa Serikali Mtandao (eGAZ) jukumu lao liwe ni kusimamia mfumo kiufundi kwa kutoa huduma bora za msaada wa kiufundi (Technical Support) pindipo mfumo ukipata changamoto za kifundi, kwa mfano ikitokezea baadhi ya moduli zilizomo kutofanya kazi au kutoa matokeo tofauti na ilivyotarajiwa, vile vile kuhakikisha mfumo upo salama dhidi ya vihatarishi na mashambulizi ya mtandao (cyber attack) na kuwa mfumo unapatikana muda wote hewani kwa kasi nzuri na ufanisi uliobora (secure, reliable and good performance).

## MAPITIO YA MFUMO WA e-PROZ

Ukaguzi ulifanya mapitio ya Mfumo wa Manunuzi ya Umma (e-Proz) kwa lengo la kuhakikisha kwamba mfumo umekidhi mahitaji yaliyokusudiwa, unazingatia Sheria na Kanuni za Manunuzi ya Umma katika utekekezaji wake pamoja na kuhakiki uhalali wa malipo ya tozo yanayofanyika kwa Mtoa Huduma (OZONE International) kulingana na makubaliano ya Mkataba.

Katika ukaguzi huo imebainika kwamba mfumo bado una mapungufu mengi katika utendaji kazi wake pamoja na usalama wa taarifa ambapo mapungufu hayo yasipofanyiwa kazi yataendelea kuathiri ufanisi, weledi na utendaji kazi wa mfumo huo na hatimae kushindwa kufikia tija iliyokusudiwa. Baadhi ya mapungufu yaliyobainika ni kama ifuatavyo:-

#### 4.1.1.5 Kukosekana kwa Usiri wa Taarifa za Manunuzi katika Mfumo

Ukaguzi umebaini Mfumo wa e-Proz hauna usiri katika kutunza taarifa zake za manunuzi kutokana na kubainika kwamba fomu za mualiko wa Zabuni (Request for Quote - RFQ) zinazotolewa na Taasisi husika kwenda kwa wasambazaji (bidders) kwa ajili ya kuomba zabuni, zinaweza kuonekana, kuchukuliwa na kubadilishwa na Taasisi nyengine yenye mahitaji ya kutoa mialiko ya zabuni inayofanana na Taasisi hiyo.

Mfumo wa e-Proz kushindwa kutunza usiri wa taarifa za Taasisi jambo ambalo linaweza kusababisha hasara ya kufanyika kwa manunuzi ya bidhaa kinyume na vigezo vilivyokusudiwa kutokana na Taasisi inayofanya manunuzi kuchukuwa na kukopia fomu ya Taasisi nyengine iliyomo kwenye mfumo bila ya kuifanyia kazi, na vile vile kupelekea kufanyika kwa udanganyifu katika michakato ya zabuni.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZPPDA kufanya jitihada za makusudi za kurekebisha mapungufu ya mfumo wa e-Proz ili kuongeza usiri, ulinzi na usalama wa taarifa zinazoingizwa kwa kila moduli kwenye mfumo na hatimae kupatikana tija na ufanisi uliokusudiwa.

#### 4.1.1.6 Mfumo wa e-Proz kukosa udhibiti wa kiusalama kwa Wasiohusika " Hackers /Intruders "

Kwa mujibu wa Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 ni kwamba Taasisi inaweza kutangaza zabuni kwa njia ya chanzo kimoja (Single Source/ Direct Suppliers) kwa mzabuni maalum kulingana na vigezo, uwezo,muda, mahitaji husika n.k. Vile vile inaweza kutangaza zabuni kwa njia ya ushindani wa wazi (Open Competitive Bidding) ili kila mzabuni kuweza kuona na kushiriki katika ushindani wa zabuni hiyo.

Ukaguzi umebaini kwamba katika mfumo wa e-Proz zabuni zinazotolewa na Taasisi kwenda kwa wazabuni maalum (Direct Suppliers), watu wasiohusika (intruders) huweza kuingia kwenye mfumo na kuangalia bei za wazabuni waliopewa zabuni husika na hatimae kuweza kujitumia na kujialika wenyewe zabuni hizo (Invitation Tenders) bila ya hata kualikwa na Taasisi husika.

Aidha, imebainika kwamba katika mfumo wa e-Proz watu wasiohusika wanaweza kuingia ndani ya mfumo na kuona taarifa za kila mzabuni aliyeomba zabuni iliyotangazwa pamoja na bei zao na hatimae kuweza kushusha bei yake ili kuweza kushinda zabuni hiyo au kutoa taarifa za bei kwa wazabuni wengine walioomba pamoja zabuni hiyo.

Kutokuwepo kwa usiri na usalama kwenye mfumo huo kunaweza kusababisha taarifa za manunuzi kuweza kupotea, kuvuja, kuchezewa au kuharibiwa na hatimae kusababisha hasara kwa Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZPPDA kwa kushirikiana na Wakala wa Serikali Mtandao (eGAZ) pamoja na Mshauri elekezi wa Mfumo wa e-Proz kuweza kutatua changamoto hizo ili kuongeza usalama wa taarifa, ufanisi na weledi wa utendaji kazi katika mfumo wa e-Proz.

#### 4.1.1.7 Kutojulikana kwa Kiwango halisi cha gharama za Malipo ya Mfumo wa e-Proz

Kwa mujibu wa mkataba wa makubaliano uliofungwa baina ya Wakala wa Serikali Mtandao na M/S OZONE International kwa kushirikiana na kampuni ya Oman Data Park utaratibu unaotumika katika kumlipa Mshauri Elekezi wa Mfumo wa e-Proz (Ozone International) ni kwa kutumia njia ya Malipo ya Huduma za Mfumo (service charges). Gharama za malipo zilizobainishwa kwenye mkataba ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 23: Malipo ya huduma ya matumizi ya Mfumo wa e-Proz yanayolipwa kwa OZONE International LLC**

| Namba | Kiasi cha Malipo ya zabuni (USD) | Asilimia ya fedha inayolipwa kwa OZONE baada ya kutozwa Kodi (%) |
|---|---|---|
| 1. | 41,000,000 na zaidi | 1 |
| 2. | 21,000,000 – 40,000,000 | 1.25 |
| 3. | 11,000,000 – 20,000,000 | 2 |
| 4. | Chini ya 10,000,000 | 3 |

Jadweli hapo juu linaonesha kwamba utaratibu wa malipo uliopangwa kufanyika kwa mujibu wa mkataba ni wa tozo ya asilimia kulingana na aina ya zabuni iliyoshinda na sio utaratibu wa kufanya malipo kwa pamoja (fixed price).

Kulipa malipo ya fedha kwa njia ya tozo ya asilimia bila ya kujulikana wazi jumla ya gharama zote za malipo hayo kunaweza kupelekea malipo hayo kulipwa kwa gharama kubwa na hatimae kusababisha hasara kwa Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZPPDA pamoja na eGAZ kuwa makini katika uingiaji wa mikataba kwa kuweza kutambua mapema jumla ya gharama zote za utengenezwaji wa mfumo zinazohitajika kulipwa kwa kila hatua (lump sum contract) na sio kwa tozo za asilimia ya huduma.

#### 4.1.1.8 Kuongezeka kwa gharama za bidhaa kwenye Mfumo wa e-Proz (Over Price)

Ukaguzi ulifanya tathmini ya gharama za bidhaa zinazouzwa kwenye maduka ya wasambazaji kwa kulinganisha na gharama za bidhaa za aina hiyo zinazouzwa ndani ya Mfumo wa e-Proz na kubaini kwamba gharama za bidhaa kwenye mfumo wa e-Proz ni kubwa kulinganisha na gharama za madukani.

Aidha, ukaguzi uliweza kubaini moja kati ya sababu kuu zilizopelekea kuongezeka kwa gharama za bidhaa kwenye mfumo wa e-Proz ni kutokana na kukatwa tozo ya asilimia tatu (3%) kwa kila bidhaa inayotangazwa kwenye zabuni ambayo msambazaji atapaswa kuilipa baada ya kushinda zabuni na kusambaza bidhaa.

Kuongezeka kwa gharama za bei za bidhaa katika mfumo wa e-Proz kunaweza kusababisha wasambazaji (wazabuni) kushindwa kuomba zabuni zinazotangazwa na Taasisi kwenye mfumo huo kutokana na hasara wanayoweza kuipata kwa kukatwa tozo ya asilimia (3%) ya huduma za matumizi ya mfumo inayotozwa baada ya kukatwa kwa kodi ya zuio (VAT).

Aidha, hali hii inaweza kupunguza mwenendo wa makusanyo ya kodi kwa Serikali kutokana na wasambazaji kuweza kufanya kazi nje ya mfumo na hatimae kuingiza hasara Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZPPDA kwa kushirikiana na uongozi wa eGAZ kufanya utaratibu wa kupunguza au kuondoa kabisa tozo hiyo ya asilimia tatu (3%) ili kupungua gharama za bidhaa katika Mfumo wa e-Proz na kuwezesha kupatikana tija ya matumizi ya mfumo huo.

### 4.1.1.9 Gharama kubwa za Ukodishwaji wa Mfumo wa e-Proz kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar shilingi 4,503,873,948.53

Kwa mujibu wa kifungu nambari 5(1)(i) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 kinaitaka Mamlaka ya Ununuzi (ZPPDA) kusimamia Mfumo wa Manunuzi kwa njia ya Kielektroniki. Kifungu hiki kina maana ya kwamba Mfumo wa Manunuzi utakaoanzishwa na ZPPDA ndio utakuwa Mfumo Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambapo Taasisi zote za Umma zitafanya utaratibu wa manunuzi kupitia Mfumo huo.

Ukaguzi umebaini kwamba ZPPDA haina Mfumo wa kieleketroniki wa Manunuzi kwa mujibu wa Sheria ambapo Mfumo huo ungekuwa ndio mali ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na ndio Mfumo Mkuu wa Manunuzi kwa Taasisi zote za SMZ.

Aidha, ukaguzi umebaini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatumia Mfumo wa kukodi ambao ni Mfumo wa **e-Proz** kwa ajili ya kufanya manunuzi ya bidhaa na huduma mbalimbali kwa njia ya Kielektroniki (e-procurement) ambapo mfumo huo umekodiwa kutoa huduma kwa muda wa **Miaka Mitano na Miezi Mitatu** kuanzia tarehe 8 Aprili, 2022 hadi Julai, 2027 kwa mujibu wa kifungu nambari 14.1 cha Masharti Maalum ya Mkataba (SCC) wa mfumo huo.

Mfumo wa e-Proz ni Mali ya Kampuni binafsi ya **OMAN DATA PARK** iliyopo mjini Muscat OMAN ambapo SMZ imekuwa ikitozwa fedha kutokana na kufanya huduma za manunuzi kwenye mfumo (Software as a Service), lakini haina umiliki (Ownership) katika mfumo huo kama vile kumiliki kodi asili za kutengenezea mfumo "source codes" n.k. Aidha mfumo huo kwa upande wa Zanzibar unasimamiwa na Kampuni ya OZONE International LLC ambae ndio Mshauri Ekelezi na ndio Wakala wa OMAN DATA PARK kwa Zanzibar.

Hivyo, katika kipindi cha kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imebainika jumla ya shilingi **4,503,873,948.53** zimelipwa na Wizara ya Fedha na Mipango kutoka kwenye hesabu ya Mfuko Mkuu wa Hazina kwenda kwenye hesabu ya PBZ nambari 0828583001 ya Kampuni ya OZONE International LLC ikiwa ni malipo ya tozo (ukodishwaji) kwa ajili ya kupatiwa huduma za manunuzi kupitia Mfumo wa e-Proz kwa kipindi cha miezi **Tisa (9)** kuanzia mwezi wa oktoba 2022 hadi mwezi wa Juni 2023.

Mchanganuo wa gharama hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

## Jadweli Nambari 24: Malipo ya Huduma za Mfumo wa e-Proz kuanzia Novemba 2022 hadi Juni 2023

| Namba | Hati Namba | Ankara Namba | Tarehe ya Malipo | Kiasi kilicholipwa (Tsh) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | 13/12 | OZN/2022/003 | 8/12/2022 | 92,452,158.90 | Malipo ya Huduma ya Mfumo wa e-Proz kwa mwezi wa Novemba 2022. |
| 2. | 57/12 | OZN/2022/002 | 13/12/2022 | 27,978,385.40 | Malipo ya Huduma ya Mfumo wa e-Proz kwa mwezi wa Oktoba 2022. |
| 3. | 92/01 | OZN/2022/004 | 17/01/2023 | 144,110,705.28 | Malipo ya Huduma ya Mfumo wa e-Proz kwa mwezi wa Disemba 2022. |
| 4. | 89/02 | OZN/2023/001 | 21/02/2023 | 111,066,832.30 | Malipo ya Huduma ya Mfumo wa e-Proz kwa mwezi wa Januari 2023. |
| 5. | 212/03 | OZN/2023/002 | 22/03/2023 | 191,177,953.50 | Malipo ya Huduma ya Mfumo wa e-Proz kwa mwezi wa Febuari 2023. |
| 6. | 219/04 | OZN/2023/003 | 18/04/2023 | 1,294,290,852.80 | Malipo ya Huduma ya Mfumo wa e-Proz kwa mwezi wa Machi 2023. |
| 7. | 61/05 | OZN/2023/004 | 11/05/2023 | 507,209,116.35 | Malipo ya Huduma ya Mfumo wa e-Proz kwa mwezi wa Aprili 2023. |

| Namba | Hati Namba | Ankara Namba | Tarehe ya Malipo | Kiasi kilicholipwa (Tsh) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 8. | 37/06 | OZN/2023/005 | 9/6/2023 | 673,025,830.00 | Malipo ya Huduma ya Mfumo wa e-Proz kwa mwezi wa Mei 2023. |
| 9. | 203/06 | OZN/2023/006 | 30/06/2023 | 1,459,562,114.00 | Malipo ya Huduma ya Mfumo wa e-Proz kwa mwezi wa Juni 2023. (Kuanzia tarehe 1 hadi tarehe 15 Juni 2023). |
| **Jumla ya Malipo** | | | | **4,500,873,948.53** | |

Hadi ukaguzi unakamilika Januari 2024 zaidi ya **shilingi Bilioni 4.5** zimeshalipwa kwa Mshauri elekezi (OZONE International LLC) kwa ajili ya Mfumo huo. Hivyo kuendelea kulipwa fedha hizo hadi mwaka 2027 kwa ajili ya kupata huduma za manunuzi ya Mfumo wa e-Proz ni kuingiza hasara Serikali kutokana na kuwa Serikali inalipa fedha nyingi kwa ajili ya kukodi huduma na sio kuumiliki ambapo fedha hizo zingetosha kuanzisha Mfumo wa Manunuzi wa Serikali na kuumiliki wenyewe (Ownership) kupitia Kituo Kikuu cha Taifa cha Serikali cha Kuhifadhi Taarifa (ZICTIA) ambapo mfumo huo ungehifadhiwa na kuendeshwa kama mifumo mengine ya Taasisi za Serikali iliyopo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZPPDA kwa kushirikiana na Wakala wa Serikali Mtandao (eGAZ) pamoja na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Zanzibar kufanya taratibu za kusitisha Mkataba wa Mfumo wa e-Proz ili kunusuru Serikali kuendelea kupata hasara ya kulipa fedha nyingi kwa ajili ya huduma za mfumo wa e-Proz, ikizingatiwa Mfumo umebainika na dosari nyingi za kiutendaji kutokana na kwamba haujakidhi mahitaji na matakwa ya Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 pamoja na mazingira halisi ya biashara kwa Taasisi za Umma na wafanya biashara wa Zanzibar.

#### 4.1.1.10 Mfumo wa e-Proz kukwazana na Matakwa ya Sheria ya Manunuzi

Kwa mujibu wa kifungu nambari 74(2) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 kinaeleza kwamba utaratibu wa kutoa dondoo utatumika kupata ushindani na ubora wa huduma kulingana na thamani yake kwa kadri itakavyowezekana, ambapo thamani ya mali au mazingira maalum hayahalalishi au kuruhusu uwazi au taratibu za zabuni zilizowekewa vikwazo.

Aidha, kifungu nambari 76(2) cha Sheria hiyo kinaeleza kwamba ununuzi au uondoshaji wa thamani ndogo utatumika kupata ununuzi na uondoshaji unaozingatia ufanisi na wakati endapo thamani ya mali hairuhusu kutumia njia ya ushindani.

Ukaguzi umebaini Mfumo wa e-Proz unakwazana na matakwa ya Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 kutokana na Mfumo kuzingatia kigezo kimoja cha gharama ndogo pekee (lowest Price) katika kumpata msambazaji atakaeshinda bila ya kuzingatia vigezo vyengine kama ubora, uwezo na ufanisi wa kiwango cha huduma atakachotoa mzabuni husika aliyeteuliwa (economy, efficiency and effectiveness of the bidder = best price).

Uzingatiaji wa kigezo kimoja cha bei ndogo pekee kwenye zabuni kinaweza kusababisha Taasisi kununua bidhaa zisizokuwa na ubora na viwango kwa mujibu wa vigezo vilivyohitajika kutokana na kuwa baadhi ya wazabuni hushusha bei zao makusudi ili kushinda zabuni husika, lakini wakati wa uwasilishaji wa bidhaa zinakuwa hazina kiwango na ubora na vigezo vilivyohitajika kwa mujibu wa tangazo la zabuni na hatimae kupoteza muda na kuingiza hasara Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZPPDA kwa kushirikiana na eGAZ kuandaa vigezo imara vya kutumika kwenye Mfumo wa e-Proz kwa kuzingatia sheria na kanuni za Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kwenye masuala yote ya manunuzi.

#### 4.1.1.11 Dosari katika Moduli ya Utoaji wa Ripoti za Mfumo wa e-Proz

Katika mapitio ya mfumo wa e-Proz ukaguzi umebaini kwamba Afisa Msajili hana uwezo wa kutoa ripoti yoyote katika mfumo huo ambapo ukaguzi umeshindwa kupata ripoti kamili kuhusiana na mambo mbali mbali yakiwemo yafuatayo:-

- Idadi kamili ya kampuni zote zilizosajiliwa ndani ya mfumo wa e-Proz.
- Idadi kamili ya kampuni ambazo zimekwisha muda wake na zinahitaji kusajiliwa tena (Renewal).
- Idadi kamili ya kampuni zilizopewa zabuni na Serikali baada ya kushinda.
- Usajili wa kampuni zilizosajiliwa kutoka nje ya nchi pamoja na idadi ya kampuni hizo kulingana na nchi husika.

Vile vile ukaguzi umebaini kwamba sampuli (templates) za Ripoti ya Tathmini pamoja muundo wa Mikataba inayotolewa kwenye mfumo haziko sahihi na hazifahamiki "unclear" jambo ambalo linapelekea ripoti za Tathmini pamoja na mikataba kuandaliwa nje ya Mfumo kwa taasisi inayofanya manunuzi.

Kutofanya kazi ipasavyo kwa Moduli ya Utoaji wa Ripoti za Mfumo wa e-Proz kunapelekea kukosekana kwa ripoti muhimu za manunuzi na zabuni zinazohitajika kwa kumbukumbu pamoja na rejea za manunuzi mbali mbali ya Taasisi na hatimae kushindwa kufikia lengo na tija iliyokusudiwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZPPDA, Wakala wa Serikali Mtandao pamoja na Mshauri Elekezi kufanya jitihada za pamoja za kuimarisha utendaji kazi wa mfumo huo kwa kufanya marekebisho ya moduli ya ripoti ili kupatikana aina zote za ripoti za manunuzi kwa mujibu wa mahitaji ya Taasisi husika.

#### 4.1.1.12 Kukosekana ruhusa (access) kwa Mwanasheria Mkuu ya kutoa ushauri kwenye Mikataba ya Serikali kwa kutumia Mfumo wa e-Proz

Ukaguzi umebaini mfumo wa e-Proz haujazingatia mahitaji ya Mwanasheria Mkuu kuweza kuona na kutoa ushauri kwenye taarifa za mikataba ya Serikali ambayo inapita kwake kwa ajili ya kupatiwa ushauri kwa mujibu wa sheria.

Hali hii imepelekea mikataba hiyo kupelekwa kwa Mwanasheria Mkuu kwa njia ya kawaida "manually" na kupatiwa ushauri nje ya Mfumo jambo ambalo linaweza kupelekea kuchelewesha zoezi la manunuzi kwa Taasisi kutokana na kuchelewa kupatikana ushauri wa kisheria kwenye mikataba hiyo na hatimae kupungua kwa ufanisi kwenye michakato ya manunuzi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZPPDA kwa kushirikiana na eGAZ kufanya marekebisho ya Mfumo kwa kuimarisha dosari zote zinazojitokeza pamoja na kuingiza kipengele cha Ukaguzi wa Mikataba kwa Mwanasheria ili kuweza kupitiwa na kutolewa ushauri wa kisheria.

### 4.1.1.13 Kukosekana kwa Mafunzo endelevu ya Mfumo wa e-Proz kwa Watendaji wa Serikali

Malengo makuu ya Mfumo wa manunuzi wa e-Proz ni kuhakikisha kwamba manunuzi yote ya Serikali yanafanyika kwa njia ya mfumo ambapo itawalazimu watendaji wote wa Serikali kufanya shughuli za manunuzi kupitia mfumo.

Ukaguzi umebaini kwamba Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma pamoja na Wakala wa Serikali Mtandao (eGAZ) hawana utaratibu mzuri wa kufanya mafunzo ya mara kwa mara kwa taasisi za Serikali, wajumbe wa Bodi pamoja na wadau wengine juu ya namna bora ya kutumia mfumo wa Manunuzi jambo ambalo limepelekea kwa baadhi ya taasisi kuomba kupatiwa mafunzo na wengine kushindwa kutumia mfumo huo hadi sasa.

Kukosekana kwa mafunzo ya Mfumo wa manunuzi wa e-Proz kwa watendaji wa Taasisi za Serikali kumepelekea athari mbalimbali ikiwemo kushindwa kutambua namna bora ya matumizi ya mfumo ambapo watendaji wanaweza kusababisha kufanyika makosa ya manunuzi kwa taasisi hizo wakati wa kutekeleza majukumu yao na Taasisi nyengine kushindwa kutumia mfumo huo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao (eGAZ) pamoja na Mamlaka ya Manunuzi Zanzibar (ZPPDA) wahakikishe kwamba mafunzo ya Mfumo wa e-Proz yanafanyika kwa taasisi zote za Serikali.

#### 4.1.1.14 Mfumo kushindwa kutuma taarifa ya ukumbusho (Notification) kwa njia ya ujumbe mfupi "sms".

Ukaguzi umebaini Mfumo wa e-Proz hautoi taarifa ya ukumbusho (notification) kwa njia mbili ambazo ni njia ya baruapepe (email) na njia ya ujumbe mfupi "sms" kupitia simu za mkononi kwa wazabuni walioomba zabuni kwa lengo la kuwapa taarifa mbali mbali kuhusiana na matokeo yao ya zabuni walizoomba ikiwa wameshinda au kukosa, matangazo mbalimbali ya zabuni n.k., badala yake taarifa hizo hutumwa kwa njia moja pekee ya baruapepe (email) jambo ambalo husababisha wazabuni wengi kushindwa kuziona taarifa kwa wakati kutokana na changamoto mbalimbali za mtandao wa Internet zinazoweza kujitokeza katika mazingira yao wanayofanyia kazi.

Wazabuni kutopatiwa taarifa za ukumbusho (notification) kwa njia ya "sms" kunaweza kupelekea baadhi yao kushindwa kuwasilisha au kuomba zabuni kwa wakati kutokana na kuchelewa kuona au kupata taarifa za zabuni hizo kupitia mtandao wa internet.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZPPDA kwa kushirikiana na eGAZ kufanya jitihada za kuimarisha Mfumo wa e-Proz kwa maeneo yote yenye mupungufu kwa mujibu wa mahitaji ya watumiaji wa mfumo hususan kwa mazingira ya Zanzibar ambapo Taasisi za Serikali ndio wadau wakuu wa Mfumo wa e-Proz ambao hufanya manunuzi.

Aidha, wasambazaji wengi waliojisajili ni kampuni zenye asili ya Zanzibar pamoja na Tanzania kwa ujumla, hivyo ni vyema kupatiwa taarifa kwa njia zote mbili kupitia baruapepe na ujumbe mfupi "sms" ili taarifa hizo ziweze kuonekana kwa wakati na kupatikana kwa tija iliyokusudiwa.

#### 4.1.1.15 Kukosekana kwa udhibiti, uhakiki na uthibitishwaji wa taarifa zinazoingizwa ndani ya mfumo wa e-Proz

Katika mapitio ya mfumo wa e-Proz ukaguzi umebaini kwamba mfumo wa e-Proz unashindwa kuthibitisha uhalali wa taarifa zinazoingizwa ndani yake ambapo wazabuni kutoka nchi za nje **(Overseas)** wana uwezo wa kufanya usajili kwa kuingiza taarifa zao za kampuni, taarifa za vyeti vya kufanya biashara pamoja na taarifa nyengine zinazohitajika kwenye mfumo bila ya kuhakikiwa na kuthibitishwa uhalali wake (verification and authentication of certificates).

Ukaguzi unatia shaka juu ya uhalali wa baadhi ya nyaraka za usajili wa kampuni za nchi za nje zilizoingizwa ndani ya mfumo huo ambapo nyaraka hizo zimepelekea kampuni hizo kupewa usajili na kuweza kuomba zabuni kwa Serikali.

Kukosekana kwa udhibiti, uhakiki na uthibitisho wa uhalali wa nyaraka zinazoingizwa kwenye mfumo wa e-Proz kunaweza kusababisha mfumo kuingizwa nyaraka zisizokuwa halisi, nyaraka zenye lugha za kigeni zisizotambulika na kupelekea kampuni zisizokuwa na vigezo kupata zabuni zisizolingana na uwezo wao na hatimae kuingiza hasara Serikali.

Aidha, kunaweza kupelekea kuingizwa taarifa za usajili wa aina moja kwa zaidi ya mara moja (duplication of data) na kupelekea kupunguza ufanisi, kasi na utendaji kazi wa mfumo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZPPDA, Wakala wa Serikali Mtandao pamoja na Mshauri Elekezi kuimarisha utendaji kazi wa mfumo wa e-Proz kwa kuweka utaratibu wa kuchunguza na kuhakiki uhalali wa nyaraka zinazoingizwa kwenye mfumo wa e-Proz kwa kutumia zana maalum za kiuchunguzi wa kidijitali wa nyaraka (digital Tracking software) ili kuthibithisha uhalali wa nyaraka hizo kabla ya kuchagua mzabuni kutoka nje.

#### 4.1.1.16 Kutofanyika kwa ukaguzi wa manunuzi katika Mfumo wa e-Proz

Kwa mujibu wa kifungu nambari 5(1)(j) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 kinaitaka Mamlaka ya Manunuzi (ZPPDA) kuanzisha ukaguzi wa ununuzi na uondoshaji wa Mali za Umma, ukaguzi wa mikataba ya zabuni wakati wa utekelezaji wa zabuni na baada ya kukamilika mkataba wa ununuzi.

Ukaguzi uliofanyika umebaini kwamba kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ZPPDA imeshindwa kufanya jukumu lao la kisheria la kukagua manunuzi ya Taasisi za Umma ndani ya Mfumo wa e-Proz.

Hali hii ilisababishwa na watendaji wa ZPPDA kutopatiwa akaunti za ukaguzi katika Mfumo wa e-Proz ili kuweza kuingia kama wakaguzi na kukagua manunuzi ya Taasisi zote za SMZ.

Kutokagua manunuzi yanayofanywa na Taasisi za Ununuzi kunapunguza udhibiti katika masuala ya manunuzi kwa Taasisi za Umma na vile vile kunaweza kusababisha ongezeko la makosa ya ukiukwaji wa taratibu, miongozo, Kanuni na Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 katika michakato ya manunuzi ya bidhaa na huduma jambo ambalo linaweza kuingiza hasara Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZPPDA kufanya jitihada na utaratibu wa kupatiwa akaunti za ukaguzi wa manunuzi kutoka eGAZ ili kuendelea na jukumu lao la ukaguzi wa Manunuzi ya Umma kwa mujibu wa Sheria kwenye mfumo wa e-Proz kwa lengo la kuhakikisha tija na ufanisi uliokusudiwa unapatikana.

#### 4.1.1.17 Kukosekana kwa mazingira ya kufanya Majaribio (Test Environment) kwa Mfumo wa e-Proz

Kwa mujibu wa viwango vinavyokubalika **(Best Practice)** vinaelekeza kwamba kuwepo na mazingira ya kufanya majaribio ya mfumo kabla ya kuanza kutumika kwa lengo la kutambua na kurekebisha hitilafu zozote zinazoweza kuathiri utendaji kazi mzuri wa mfumo au kuathiri matumizi ya mtumiaji. Vile vile ikitokezea mabadiliko katika mfumo, kwanza hutakiwa kufanyiwa majaribio katika mazingira ya majaribio (Test environment) ambapo mfumo wa majaribio unakuwepo pamoja na miundombinu yake, vile vile majaribio yote yanayofanyika huwekewa kumbukumbu za matokeo yake kwa ajili ya kuboresha mfumo katika utendaji wake.

Ukaguzi umeshindwa kupata ushahidi wa uwepo wa mfumo wa mazingira ya majaribio.

Kukosekana kwa mazingira ya kufanyia majaribio (Test environment) kwa Mfumo wa Manunuzi wa e-Proz ni kwenda kinyume na miongozo inayokubalika (Best Practice) na vile vile kunaweza kusababisha kuchelewa kufanyiwa maboresho ya hitilafu zinazojitokeza kwenye Mfumo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZPPDA pamoja na eGAZ kuhakikisha kwamba mfumo wa e-Proz unakuwa na mazingira ya Majaribio (Test Enviroment) ambayo yatatoa fursa ya kuona changamoto mbali mbali zitakazojitokeza ndani ya mfumo ili ziweze kutatuliwa na kurahisisha matumizi bora ya mfumo huo.

#### 4.1.1.18 Kutothibitika kwa usalama na uwezo wa utendaji kazi wa Seva inayoendesha Mfumo wa e-Proz (Application Server)

Ukaguzi umebaini kwamba Seva ambayo inayoendesha Mfumo wa e-Proz haijathibitika usalama wake kiutendaji kutokana na kushindwa kukaguliwa, kufanyiwa tathmini ya mazingira hatarishi "Vulnerability Assessment", kushindwa kutambulika programu gani zinazotumika kuweza kuzuwia virusi na vihatarishi vinavyotokana na mashambulizi ya Mtandao na hali halisi ya leseni za programu hizo. Vile vile ukaguzi umeshindwa kuthibitisha uwezo na vigezo vya seva hizo pamoja na taarifa za wanaoweza kuingia katika seva hiyo na mfumo wa e-Proz (application logs).

Kutothibitika kwa usalama na uwezo wa Seva inayoendesha Mfumo wa e-Proz kunaweza kusababisha hatari kubwa ya mfumo kupata mashambulizi ya virusi, udukuzi, utendaji mdogo wa kazi na hatari nyengine zisizojulikana pindipo usalama ukiwa mdogo katika mazingira yanayoizunguka seva ya Mfumo jambo ambalo litapelekea mfumo kuharibika na hatimae kuingiza hasara Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZPPDA kwa kushirikiana na eGAZ kufanya jitihada za kuhakikisha Seva hiyo ipo salama, ina leseni halisi "Original license" katika mfumo wa uendeshaji "Operating System" na vile vile inaingizwa programu ya kusaidia kuzuwia mashambulizi na hatari mbali mbali za mitandao dhidi ya virusi, udukuzi n.k. na pia kuongeza uwezo ili iweze kufanya kazi kwa ufanisi.

### MAPITIO YA MFUMO WA VENDOR REGISTRATION SYSTEM

Ukaguzi ulifanya mapitio ya Mfumo wa Vendor Registration System na kubaini mapungufu mbali mbali ya kiutendaji kwa watumiaji wa mfumo huo, miongoni mwa mapungufu yaliyobainika ni kama ifuatavyo:-

#### 4.1.1.19 Udhaifu katika utengenezaji wa Nenosiri (Password) kwenye Mfumo wa Vendor Registration System

Katika ukaguzi uliofanyika wa mfumo wa Vendor Registration System unaoutumika kwa ajili ya utoaji wa vyeti vya usajili (Certificate of Registration) imebainika kuwa mfumo huo una udhaifu katika mipangilio yake ya utengenezaji wa neno siri (User Password) kwa watumiaji wa mfumo (Password configuration Settings).

Hali hii imebainika kwa kuonekana mfumo kuweza kuruhusu kutengenezwa neno siri la aina yoyote bila ya kuzingatia vigezo, sifa na mahitaji ya kiusalama yanayotakiwa kuwepo katika utengenezwaji wa neno siri (password security requirements settings).

Kuwepo kwa udhaifu huo kunahatarisha usiri wa taarifa zilizomo ndani ya mfumo, pia inaweza kusababisha kufanyika kwa matukio yasiyo ya kihalali kwa maslahi ya watu binafsi na hatimae kuingiza hasara Serikali. Vile vile kunaweza kutokezea uharibifu au kuvuja kwa taarifa za wasajiliwa au kutolewa kwa vyeti visivyo vya uhalali vya Usajili wa Kampuni.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZPPDA kufanya maboresho ya Mfumo wa Vendor Registration System ili kuhakikisha watumiaji wanakuwa na nenosiri madhubuti kwa ajili ya kulinda akaunti zao kutokana na uhalifu wa mitandaoni pamoja na uhalifu kwa watumishi wasio na maadili (intruders) katika Afisi.

### 4.1.1.20 Udhaifu katika utoaji wa vyeti vya wazabuni kwenye Mfumo wa Vendor Registration System

Ukaguzi umebaini kwamba vyeti vya usajili wa wazabuni vinavyotolewa na Mfumo wa Vendor Registration System havina utambulisho utakoweza kuonesha udhibiti wa pekee kwamba vyeti hivyo ni halisi kutoka Mamlaka ya Manunuzi ili kuepusha uwezekano wa kughushiwa na kutumika kwa vyeti feki, kwa mfano utambulisho wa kutumia QR Code, Bar Code n.k.

Kutokuwepo kwa udhibiti imara wa vyeti vya Usajili wa Wazabuni kunaweza kusababisha hatari ya kutengenezwa vyeti feki na kutumika katika kujisajili jambo ambalo linaweza kusabisha hasara kwa Serikali na kupunguza usalama wa mfumo wa e-Proz.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZPPDA kufanya utaratibu wa kuweka alama za utambuzi zitakazokuwa imara katika kudhibiti na kuzuwia hatari ya kughushiwa kwa vyeti hivyo na vile vile kutambua vyeti halisi kutoka Mamlaka ya Manunuzi ili kuepusha uwezekano wa kughushiwa na kutumika kwa vyeti feki, kwa mfano kutumia utambuzi wa QR Code, Bar Code n.k.

### 4.1.1.21 Kutofanyika kwa usanidi katika sehemu zinazoweka kumbukumbu za shughuli za watumiaji wa kanzidata ya Mfumo "database Audit logs"

Moja kati ya sehemu muhimu zinazopewa kipaombele cha udhibiti kwenye kanzidata ni sehemu ya kuhifadhi kumbukumbu za shughuli za watumiaji "database audit logs".

Sehemu hii hurikodi shughuli "activities" zote zinazofanywa na watumiaji wa kanzidata "database administrators and database users" ambapo hutumika kwa kuangalia ushahidi endapo tukio la kihalifu likifanywa kupitia kanzidata ya mfumo.

Ukaguzi ulifanya uhakiki wa kanzidata "database" ya mfumo wa **Vendor Registration System** na kubaini kwamba sehemu ya kuhifadhi "Audit logs" haijasanidiwa (not configured) kwa ajili ya kuchunguza na kuweka kumbu kumbu za matukio yanayofanyika ndani ya kanzidata.

Kutofanyika kwa usanidi wa kuweka kumbukumbu za uchunguzi kwa shughuli zinazofanyika katika kanzidata kunaweza kusababisha kukosekana kwa ushahidi wa kumtambua aliyehusika endapo ikitokezea kufanyika vitendo visivyokuwa na uadilifu moja kwa moja ndani ya kanzidata kama vile wizi, udukuzi, ufutaji wa taarifa bila ya idhini, ubadilishwaji wa data n.k.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZPPDA kuhakikisha kanzidata ya mfumo wa Vendor Registration System inasanidiwa ili kuweza kuchunguza, kubaini matumizi halisi na kuweka kumbukumbu za shughuli zote zinazofanyika ndani yake na akaunti yoyote inayohusika kufanya shughuli hizo. Hali hii itasaidia kupatikana kwa ushahidi wa kubaini tarehe, muda na akaunti iliyotumika kufanya kitendo kisichokuwa na uadilifu ndani ya kanzidata hiyo.

Aidha, katika kuongeza usiri, uadilifu na usalama wa kulinda taarifa za manunuzi ukaguzi unaushauri uongozi wa ZPPDA kuhakikisha unamuandaa mtu pekee atakaetunza, kusimamia na kuzifikia taarifa za uchunguzi zilizo ndani ya kanzidata za mifumo "database audit logs" ili kuepusha kuchezewa, kufutwa au kuharibiwa na wasiokuwa waadilifu.

### 4.1.2 WAKALA WA SERIKALI MTANDAO ZANZIBAR (eGAZ)

Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar (eGAZ) kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 4.1.2.1 Kukosekana kwa umiliki wa Mifumo ya Wakala wa Serikali Mtandao kuwa ni Mali ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

Kifungu nambari 62 na 64 cha Sheria nambari 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 vinaeleza kwamba Taasisi za Umma kutumia mbinu sahihi za kupata mali za umma na kutunza nyaraka zinazothibitisha kuwa mali zinamilikiwa kisheria. Aidha, mali hizo zinapaswa kuwekwa katika daftari la Mali za Kudumu.

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imebainika kuwa Wakala wa Serikali Mtandao inamiliki kwa njia ya usimamizi mifumo mbali mbali ambapo mifumo hiyo hutumika kwa Taasisi zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kufanya shughuli zao kuu ikiwemo shughuli za kukusanya mapato, kufanya manunuzi na matumizi, kupanga bajeti ya kuidhinisha fedha za matumizi kwa Taasisi za Umma, kutoa nambari za udhibiti wa malipo, kufanya mawasiliano ya ndani na nje ya Taasisi, kutuma barua na nyaraka mbali mbali kwa Taasisi ambapo nyaraka hizo baadhi yao ni siri za Serikali.

Baadhi ya mifumo hiyo ndiyo inayotekeleza dhana ya Serikali Mtandao kama vile Mfumo wa Afisi Mtandao kwa Serikali (e-Office), Mfumo wa Barua pepe za Serikali (GMS), Mfumo wa manunuzi ya Serikali (e-Proz), Mfumo wa Bajeti na Mapato wa Serikali (BAMAS), Mfumo wa Kutoa nambari za Udhibiti wa malipo ya Serikali (ZanMalipo) n.k.

Hata hivyo, ukaguzi umebaini baadhi ya mifumo hiyo ni mali ya Kampuni binafsi za Nje na mengineyo ni Mali ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo SMZ inatumia kwa mujibu wa makubaliano ya Ushirikiano (MoU) na sio mali ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa maana ya kuwa SMZ haina umiliki halisi (source codes) kwa mifumo hiyo, licha ya kuwa shughuli zote kuu za Taasisi za SMZ zinafanyika kupitia mifumo hiyo ikiwemo shughuli za kukusanya mapato, matumizi, manunuzi, barua na nyaraka za siri, mawasiliano ya Viongozi wa Umma n.k.

Kutumika mifumo hiyo bila ya kuwa na umiliki kamili kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kunaweza kupelekea kukosekana kwa usiri na usalama wa taarifa muhimu za Serikali jambo ambalo linaweza kusababisha kuvuja kwa Taarifa za Serikali na kusababisha kukosekana kwa usalama wa Nchi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar kwa kuzingatia kwamba Makubaliano ya Ushirikiano (MoU) hayafungamani na sheria, hivyo uongozi wa Wakala unapaswa kuanzisha mchakato wa kuwa na mifumo yake au kupata umiliki halisi kutoka kwa washirika waliowapatia na kuitambua mifumo hiyo kama Mali ya Umma ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kama ilivyoagizwa kupitia vifungu nilivyovinakili hapo juu.

#### 4.1.2.2 Seva za uzalishaji wa data za Mifumo ya Serikali Mtandao zipo katika Kituo cha Data kilichopo Dar-es-Salaam

Serikali Mtandao imebainika seva za uzalishaji wa data za mifumo ya Serikali mtandao (ZANMALIPO, e-Office na GMS) zimewekwa katika kituo cha data kinachosimamiwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao ya Tanzania (eGA) kilichopo Jijini Dar-es-Salaam.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na malengo ya Uanzishwaji wa Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA Zanzibar (ZICTIA) ambapo imepewa jukumu la kusimamia Kituo cha Data cha Serikali ya Zanzibar kinachotoa huduma za miundombinu ya seva za mifumo kwa taasisi za Umma.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao kutumia kituo cha Data cha Serikali ya Zanzibar kama ilivyoelekezwa katika kifungu nambari 4 cha Sheria ya Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA Zanzibar ya 2020 ili kwenda sambamba na malengo ya uanzishwaji wa Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA Zanzibar (ZICTIA) pamoja na kuongeza usiri na uadilifu wa matumizi ya taarifa za Serikali.

#### 4.1.2.3 Kushindwa kuwasilisha Mfumo wa Manunuzi uliohitajika kulingana na hadidu za rejea za mkataba

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa Kampuni ya Ozone International imeshindwa kutengeneza mfumo uliohitajika na badala yake imeleta na kuweka mfumo wa manunuzi ukiwa katika muundo wa huduma (System-as-a-Service).

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 2 cha makubaliano ya mkataba, ambapo kwa mujibu wa Hadidu za Rejea (ToR), Mamlaka ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma (User department) ilihitaji kutengenezewa mfumo kupitia njia bora za utengenezaji wa mifumo ya kielektroniki na sio kununua huduma ya mfumo.

Kwa vile mshauri elekezi ameshindwa kutekeleza makubaliano ya msingi wa mkataba, ukaguzi unaishauri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kupitia Wakala wa Serikali Mtandao kuchukua hatua stahiki, ikiwemo kusitisha utekelezaji wa mkataba kwa mujibu wa kifungu nambari 19.1 cha mkataba huo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar kusimamia vyema utekelezaji wa mikataba ili kuhakikisha kwamba mifumo inayonunuliwa au kutengenezwa inazingatia mahitaji ya watumiaji wa mifumo hiyo.

### 4.1.2.4 Mifumo wa e-Proz unatekelezwa na kufanya kazi kwa njia ya Mfumo kama Huduma (System-as-a-Service)

Ukaguzi uliofanyika kwa eGAZ umebaini kwamba Mfumo wa e-PROZ uliowekwa na Ozone International unafanyakazi kwa njia ya huduma (System-as-a-Service), hii ina maana kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inauziwa huduma ya mfumo badala ya kuwekewa mfumo wenyewe (On-premises System).

Matumizi ya mfumo wa e-Proz kwa njia ya huduma, yanahatarisha usiri wa taarifa za manunuzi ya Serikali kwa vile seva za mfumo huo zipo nje ya Mipaka ya Jamhuri ya Tanzania ambapo kuna utofauti katika utekelezaji wa sheria, kanuni na sera za ulinzi wa taarifa.

Aidha, Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Muongozo wa Utengenezaji, Uendeshaji na Usimamizi wa Tovuti za Serikali, toleo la 1.0 mwaka 2022, ambapo aya ya 7.1 inaelekeza kuwa tovuti zote zihifadhiwe kwenye kituo kikuu cha kuhifadhi taarifa cha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao kuandaa utaratibu wa kusitisha mkataba wa Ozone International Limited bila ya kuathiri shughuli za kiutendaji za Serikali kutokana na hoja zifuatazo:-

a) Mahitajio ya Mfumo wa e-Proz kupitia njia ya Huduma (System-as-a-Service) hayakutajwa wala kujadiliwa katika Majadiliano ya Mkataba yaliyofanyika baina ya Ozone International, Wakala wa Serikali Mtandao na Mamlaka ya Manunuzi (Kiambatisho nambari A cha Mkataba).

b) Mahitajio ya Mfumo wa e-Proz kupitia njia ya Huduma (System-as-a-Service) hayakubainishwa katika Hadidu za Rejea zilizobainisha msingi wa mahitaji ya mfumo, upeo na matokeo ya kazi (Kiambatisho nambari B cha Mkataba).

c) Hakuna ushahidi wa kuidhinishwa kwa manunuzi ya Mfumo wa e-Proz kupitia njia ya Huduma kutoka kwa Wakala wa Serikali Mtandao kama ilivyoelekezwa kupitia Viwango vya Utengenezaji, Upatikanaji, Uendeshaji na Utunzaji wa Mifumo ya Serikali Mtandao (Hati Namba. eGAZ/EXT/ESG/003, sehemu ya 2.2.2.1.2).

#### 4.1.2.5 Ukiukwaji wa Taratibu za malipo uliosababisha gharama kubwa za malipo ya tozo ya huduma ya Mfumo wa e-Proz shilingi 4,500,873,948.53

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2022/2023, imebainika jumla ya shilingi 4,500,873,948.53 zimelipwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Kampuni ya Ozone International kupitia Hesabu nambari 0828583001 ya PBZ kutoka Huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali, ikiwa ni malipo ya tozo za huduma ya matumizi ya mfumo wa e-Proz kuanzia mwezi wa Oktoba 2022 hadi Juni 2023.

Baada ya kufanyika tathmini ya fedha zilizolipwa kwa kulinganisha na thamani ya huduma ya mfumo inayotolewa (Value for Money) ukaguzi umebaini kwamba gharama zenye jumla ya shilingi 4,500,873,948.53 zilizolipwa kwa kipindi cha muda wa miezi tisa (9) kuanzia Oktoba 2022 hadi Juni 2023 ni kubwa kulinganisha na huduma yenyewe iliyokuwa ikipatikana kwa kipindi hicho.

Hivyo, ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao pamoja na Uongozi wa Afisi ya Rais Fedha na Mipango kusitisha malipo ya huduma ya mfumo wa e-Proz ili kuokoa kiasi kikubwa cha fedha zinazolipwa kwa kipindi cha miaka mitano (5) ya utekelezaji wa Mkataba, na badala yake fedha hizo ziwekezwe kwenye kutengeneza Mfumo wa manunuzi mwengine unaohitajika kwa mujibu wa Hadidu za Rejea za Mkataba.

Hali halisi ya malipo yanayolipwa kwa Mshauri elekezi (OZONE International Limited) kutokana na huduma za mfumo wa eProz anazotoa kwa kila mwezi ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

## Jadweli Nambari 25: Mchanganuo wa malipo yaliyofanywa kwa Ozone International Limited

| Namba | Hati ya Malipo | Nambari ya Ankara | Maelezo | Tarehe ya Malipo | Kiasi kilicholipwa (Tshs) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | 13/12 | OZN/2022/003 | Malipo ya e-Proz kwa mwezi wa Novemba 2022. | 8/12/2022 | 92,452,158.90 |
| 2. | 57/12 | OZN/2022/002 | Malipo ya e-Proz kwa mwezi wa Okto-ba 2022. | 13/12/2022 | 27,978,385.40 |
| 3. | 92/01 | OZN/2022/004 | Malipo ya e-Proz kwa mwezi wa Disemba 2022. | 17/01/2023 | 144,110,705.28 |
| 4. | 89/02 | OZN/2023/001 | Malipo ya e-Proz kwa mwezi wa Janu-ari 2023. | 21/02/2023 | 111,066,832.30 |
| 5. | 212/03 | OZN/2023/002 | Malipo ya e-Proz kwa mwezi wa Febuari 2023. | 22/03/2023 | 191,177,953.50 |
| 6. | 219/04 | OZN/2023/003 | Malipo ya e-Proz kwa mwezi wa Ma-chi 2023. | 18/04/2023 | 1,294,290,852.80 |
| 7. | 61/05 | OZN/2023/004 | Malipo ya e-Proz kwa mwezi wa Aprili 2023. | 11/05/2023 | 507,209,116.35 |
| 8. | 37/06 | OZN/2023/005 | Malipo ya e-Proz kwa mwezi wa Mei 2023. | 9/6/2023 | 673,025,830.00 |
| 9. | 203/06 | OZN/2023/006 | Malipo ya e-Proz Kuanzia 1 hadi 15 Juni) | 30/06/2023 | 1,459,562,114.00 |
| **Jumla** | | | | | **4,500,873,948.53** |

### 4.1.2.6 Malipo ya tozo ya huduma yaliyofanywa kabla ya muda wa malipo shilingi 1,459,562,114

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imebainika kuwa jumla ya shilingi 1,459,562,114 zimelipwa kwa Ozone International kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina kupitia hati namba 203/06 ya tarehe 30/06/2023 ikiwa ni malipo kwa ajili ya huduma ya mfumo wa e-Proz kuanzia tarehe 1 hadi 15 Juni, 2023.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na utaratibu wa malipo jambo ambalo linaashiria kuwa huduma ya mfumo wa e-Proz ina muelekeo zaidi wa kibiashara badala ya kuwa suluhisho la kazi za manunuzi ya Umma kama ilivyoanishwa kwenye dhamira ya utengenezaji wa mfumo ndani ya Mkataba.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao kusimamia utekelezaji wa makubaliono ya mikataba kwa kuhakikisha Serikali inapatiwa Mfumo wa manunuzi uliohitajika, ili kuepusha usumbufu wa upatikanaji wa huduma endapo Serikali itachelewa kulipia huduma hiyo.

#### 4.1.2.7 Kuwepo kwa tofauti baina ya fedha zinazodaiwa na Ozone International pamoja na kiwango halisi kinachotakiwa kulipwa na Serikali

Katika ukaguzi uliofanyika umebaini uwepo wa tofauti ya fedha zinazotozwa na Ozone International na kiasi halisi cha tozo kinachopaswa kulipwa kwa Ozone kutokana na matumizi ya mfumo kwa mujibu wa makubaliano.

Tofauti hiyo, imetokana na kwamba mfumo hautoi ankara za malipo kiotomatiki na badala yake huandaliwa baada ya uchakachuaji wa ripoti za tenda zilizoidhinishwa ndani ya mfumo huo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao, kupitia na kuthibitisha kiwango cha fedha za tozo zinazowasilishwa kwenye ankara ya Ozone International kabla ya kupelekwa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kwa ajili ya malipo. Aidha, katika kupitia ankara hizo, ukaguzi unashauri mambo yafuatayo kuzingatiwa:-

- Idadi ya zabuni halisi zilizoidhinishwa ndani ya mfumo katika mwezi husika, kwa sababu tumebaini umebaini uwepo wa nakala za zabuni (dublicate tenders).
- Kiasi halisi cha thamani ya zabuni alicholipwa msambazaji wa huduma, kwa sababu tumebaini uwepo wa zabuni zisizo na thamani (ZERO & NULL values).
- Kuthibitisha utekelezaji wa tenda zilizoidhinishwa ndani ya mfumo katika mwezi husika, kwa sababu tumebaini baadhi ya zabuni zilizoidhinishwa hazikutekelezwa kwa malipo.
- Kiwango cha ubadilishaji fedha, kinachotumika kwa ajili ya kubadili fedha za thamani ya zabuni zilizolipwa kwa shilingi kwenda kwenye dola za kimarekani, sababu makubaliano ya malipo yapo kwa dola za kimarekani. Mchanganuo wa tofauti hiyo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

## Jadweli Nambari 26: Fofauti ya fedha zinazolipwa kwa kila mwezi

| Namba | Nambari ya Ankara ya Ozone | Mwezi wa malipo ya huduma | Tozo ya Huduma iliyoombwa | Tozo halisi ya huduma inayopaswa Kudaiwa kwa kuzingatia Thamani za Zabuni. (TZS) | Tofauti ya fedha (TZS) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | OZN/2022/003 | November 2022 | 97,318,062.00 | 101,194,574.43 | (3,876,512.43) |
| 2. | OZN/2022/002 | October 2022 | 29,450,932.00 | 31,167,664.59 | (1,716,732.59) |
| 3. | OZN/2022/004 | December 2022 | 144,110,705.28 | 157,941,043.78 | (13,830,338.50) |
| 4. | OZN/2023/001 | January 2023 | 116,912,455.00 | 117,734,049.91 | (821,594.91) |
| 5. | OZN/2023/002 | February 2023 | 201,239,951.00 | 64,204,539.78 | 137,035,411.22 |
| 6. | OZN/2023/003 | March 2023 | 1,362,411,424.00 | 1,592,469,472.12 | (230,058,048.12) |
| 7. | OZN/2023/004 | April 2023 | 533,904,333.00 | 425,041,956.94 | 108,862,376.06 |
| 8. | OZN/2023/005 | May 2023 | 708,448,242.00 | 1,122,995,496.23 | (414,547,254.23) |
| 9. | OZN/2023/006 | June 2023, (from 1st to 15th) | 1,536,381,173.00 | 1,256,318,645.41 | 280,062,527.59 |
| **Total Amount** | | | | **4,869,067,443.18** | **(138,890,165.90)** |

#### 4.1.2.8 Kutokukatwa tozo ya huduma ya Mfumo wa e-Proz kwa Wasambazaji waliotunukiwa zabuni

Katika ukaguzi uliofanyika, imebainika kwamba wasambazaji wa huduma hawakukatwa kiwango cha fedha kubalifu kwa mujibu wa zabuni walizotunukiwa, ili kuzuia fedha zinazopaswa kulipwa Ozone International kwa ajili ya tozo ya huduma ya matumizi ya mfumo wa e-Proz.

Kushindwa kukata na kuzuia tozo ya huduma ya mfumo wa e-Proz kwa wasambazaji, ni kukiuka makubaliano ya mkataba na kunapelekea Serikali kubeba mzigo wa gharama za matumizi ya mfumo huo na hatimae kuingiza hasara Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar kusimamia utekelezaji wa makubaliano ya mikataba kwa kuhakikisha wasambazaji waliotunukiwa zabuni zilizopitia kwenye mfumo wa e-Proz wanawasilisha fedha za matumizi ya huduma hiyo kama ilivyokubalika kupitia mkataba wa utekelezaji wa mfumo huo.

#### 4.1.2.9 Kuwepo kwa zabuni ambazo hazikutekelezwa kwenye orodha ya malipo ya matumizi ya mfumo wa e-Proz

Baada ya kupitia orodha ya zabuni zilizowasilishwa na Ozone International kwa ajili ya malipo, ukaguzi umebaini uwepo wa zabuni zilizopo katika hatua za uanzishwaji, utangazwaji, zilizositishwa na zilizopitwa na wakati.

Hii inamaana kuwa kiasi cha tozo ya huduma kinachowasilishwa na Ozone hakina uhalisia wa thamani ya zabuni zilizoidhinishwa na kutekelezwa kwa mwezi husika, na kupelekea kulipwa malipo yasiyostahiki jambo ambalo ni kinyume na kifungu nambari 41.2 cha mkataba.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Serikali Mtandao kusimamia utekelezaji wa makubaliano ya mikataba kwa kuhakikisha tozo ya huduma inakatwa kwa zabuni ambayo imeidhinishwa katika mfumo na kutekelezwa kwa malipo ya zabuni hiyo.

#### 4.1.2.10 Kutokubainishwa kwa uwazi wa Hakimiliki ya kodi asili za utengenezwaji wa Mifumo (Software source codes)

Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar imeingia mkataba na Kampuni ya UBX (Tanzania) Limited kwa ajili ya kazi ya utengenezaji na uwekaji wa mifumo inayohusisha malipo ya huduma mbali mbali zinazotolewa na taasisi za Umma, Zanzibar.

Kifungu nambari 3 cha mkataba huo, kinaelekeza kwa kila taasisi ya Serikali inapohitaji mfumo unaohusisha malipo italazimika kuwasilisha mahitaji yao kwa Wakala wa Serikali Mtandao ili kuyatengenezea nyongeza ya mkataba (addendum) kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hiyo.

Katika ukaguzi uliofanyika umebaini kifungu nambari 28 cha mkataba Mkuu wa UBX hakijatosheleza katika kueleza Hakimiliki ya kodi za utengenezwaji wa Mifumo (Source Codes) ya Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kutokubainisha umiliki wa kodi hizo za utengenezwaji wa mifumo, kunatoa fursa kwa mtengenezaji (UBX) kuendelea kuwa na udhibiti wa mifumo hiyo hadi baada ya kumalizika kwa utekelezaji wa mkataba, jambo ambalo ni kwenda kinyume na Viwango vya Utengezaji, Upatikanaji, Uendeshaji na Utunzaji wa Mifumo ya Serikali Mtandao (Hati Na. eGAZ/EXT/ESG/003), aya nambari 2.2.2.1.3 ambapo inaelekeza mkataba lazima uwe na kifungu kinachotoa umiliki wa viasili vya programu (source codes).

Ukaguzi unaushauri Uongozi wa eGAZ kuzingatia ulinzi wa hakimiliki ya kodi asili za utengnezwaji wa mifumo ya TEHAMA katika kila mkataba unaohusisha utengenezaji wa mifumo kama ilivyoelekezwa katika kifungu nambari 3(1)(b) cha Sheria ya Hakimiliki ya Zanzibar, 2003 pamoja na muongozo wa viwango wenye kumbukumbu nambari eGAZ/EXT/ESG/003.

Vile vile katika Mktaba wa UBX, Wakala inapaswa kuhakikisha kwa kila nyongeza ya mkataba itakayofanywa izingatie kuboresha kipengele cha Umiliki (Kifungu cha 28) ili kulinda umiliki wa viasili vya kodi za mifumo kwa taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

### 4.1.2.11 Kutokuwepo kwa Kifungu cha uanzishwaji wa makubaliano ya Escrow

Ukaguzi umebaini kwamba Mkataba Mkuu wa UBX haujajumuisha kipengele cha Uanzishwaji wa Makubaliano ya Escrow, ambapo ni makubaliano ya kulinda na kutunza "source codes" kwenye Taasisi ya Tatu (third party) hadi kukamilika kwa utekelezaji wa mkataba wa utengenezaji wa mifumo hiyo.

Kushindwa kusimamia ulinzi na usalama wa viasili (source codes) vya mifumo ya Serikali, kunatoa fursa kwa mtengenezaji wa mifumo (UBX) kuendelea kuvitumia (re-uses) viasili hivyo kwa kuviboresha (customization) kwa ajili ya manufaa ya kibiashara.

Ili kudumisha uendelevu wa mifumo ya Serikali Mtandao, ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala kufanya maboresho ya Mkataba Mkuu wa UBX kwa kuweka nyongeza ya kifungu cha uanzishwaji wa Makubaliano ya Escrow kwa mifumo yote itakayotekelezwa kupitia mkataba huo.

### 4.1.2.12 Aina ya Mkataba na njia za malipo kutoendana na asili ya kazi zinazotekelezwa na mkataba (nature of assignment)

Kanuni ya 181 ya Kanuni za Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2021 inaelekeza kwamba kazi za utengenezaji wa programu (mifumo) zitumie Mkataba wa Mkupuo (Lump sum contract) na malipo yake yatokane na bei isiyobadilika (fixed price) itakayokubalika.

Ukaguzi umebaini Mkataba Mkuu wa UBX ni wa aina ya kubakiza (Retainer contract) ambapo malipo yake yanatokana na mikato ya asilimia ya thamani ya miamala ya malipo itakayopitishwa kwenye mifumo itakayo tengenezwa kwa muda wa miaka minne (4) ya utekelezaji wa mkataba huo. Kufanya hivyo, ni kwenda kinyume na kifungu cha kanuni nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar kuzingatia sheria, na kanuni za Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma katika kuingiza mikataba ya utengenezwaji wa mifumo kwa kampuni ya UBX. Aidha rasimu za mikataba hiyo ni vyema kuwasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu kabla kwa ajili ya kupatikana ushauri na maoni ya kisheria kabla ya kuanza kusainiwa na kutumika rasmi kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Mifumo.

Jadweli lifuatalo linaonyesha mchanganuo wa malipo kwa Kampuni ya UBX, yanayotokana na mikato ya asilimia ya thamani ya miamala ya malipo.

**Jadweli Nambari 27: Mchanganuo wa malipo kwa Kampuni ya UBX, yanayotokana na mikato ya asilimia ya thamani ya miamala ya malipo.**

| Kuanzia Shilingi (Tsh.) | Hadi Shilingi (Tshs) | Asilimia Itakayolipwa kwa UBX (%) | Asilimia atakayochukuwa eGAZ (%) | Jumla ya Asilimia zitazokatwa (%) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 100,000 | 2.0 | 0.5 | 2.5 |
| 100,001 | 500,000 | 1.6 | 0.4 | 2.0 |
| 500,001 | 1,000,000 | 1.0 | 0.3 | 1.3 |
| 1,000,001 | 5,000,000 | 0.2 | 0.1 | 0.3 |
| 5,000,001 | 10,000,000 | 0.1 | 0.05 | 0.15 |

### 4.1.2.13 Gharama za malipo ya Mkataba wa UBX zitabebwa na walipaji wa huduma

Katika ukaguzi uliofanyika, imebainika kuwa kifungu nambari 10.4 cha mkataba mkuu wa UBX kinaelekeza malipo ya utekelezaji wa mkataba yatatozwa kwa walipaji wa huduma.

Kufanya hivyo, kunapelekea kuongezeka kwa ada, tozo au bei ya huduma zitakazotolewa kwa wananchi kutoka Serikalini ambapo malipo yake yatapitishwa kwenye mifumo itakayotengenezwa na UBX.

Ukaguzi unaushauri uongozi Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar kufanya maboresho ya Mkataba Mkuu wa UBX kupitia nyongeza iliyotajwa katika kifungu nambari 3 ili kubatilisha kifungu nambari 10.4, na hivyo Kampuni ya UBX ilipwe kiasi cha mkupuo kulingana na asili ya kazi inayokwenda kutekelezwa.

### 4.1.2.14 Kutokuzingatiwa kwa Mpango wa Manunuzi ndani ya Mfumo wa e-Proz

Ukaguzi umebaini kuwa, mfumo wa e-Proz haujazingatia kuwepo kwa Mpango wa Manunuzi unaoandaliwa na kuidhinishwa na taasisi inayofanya manunuzi (PDEs) kwa kila mwaka kulingana na bajeti husika.

Kuwepo kwa dosari hiyo, kunawezesha mfumo kuruhusu manunuzi ya bidhaa au huduma ambazo hazikuainishwa katika mpango wa manunuzi na kupelekea kuathiri utekelezaji wa bajeti iliyopangwa kwa mwaka husika, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na sheria, kanuni na miongozo ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar kusimamia uboreshwaji wa mfumo kwa kujumuisha Mipango ya Manunuzi inayoandaliwa na taasisi za Umma ili kuweka udhibiti wa kiotomatiki kwa kuzuia zabuni zilizo nje ya mpango wa manunuzi uliowasilishwa katika Mamlaka ya Manunuzi ya Umma kama ilivyoelekezwa kupitia Kanuni ya 64(1) ya kanuni za Manunuzi ya Umma. Vile vile utaratibu huu utaweza kurahisisha jukumu la kufanya ukaguzi wa Manunuzi ya Umma linalotekelezwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Zanzibar.

#### 4.1.2.15 Kuwepo kwa zabuni zisizokuwa na thamani ya fedha alizolipwa msambazaji kupitia Mfumo wa eProz

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa zabuni ambazo hazina thamani ya fedha alizolipwa msambazaji, hii maana yake ni kwamba mfumo wa e-Proz hauna udhibiti wa kuzuia uingizaji wa zabuni isiyo na thamani ya fedha atakazolipwa msambazaji.

Kuwepo kwa dosari hii, kunatilia mashaka uhalisia wa malipo ya tozo ya huduma yanayofanywa kila mwisho wa mwezi, kwa vile ukokotoaji wa kiasi cha fedha hizo hutegemea thamani ya zabuni zilizoidhinishwa na kulipwa ndani mwezi husika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao kusimamia maboresho ya huduma za mfumo wa e-Proz, ili kuweza kujengewa udhibiti wa kulazimisha uingizwaji wa taarifa ya thamani ya zabuni wakati wa uandaaji wa zabuni hizo ndani ya mfumo. Mchanganuo wa zabuni zisizokuwa na thamani ya fedha ndani ya mfumo ni kama unavyoonekana katika **Kiambatisho Nambari 2.**

#### 4.1.2.16 Kuwepo kwa zabuni zisizo na uhalisia wa thamani ya fedha katika Mfumo wa eProz

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa zabuni zisizo na uhalisia wa thamani ya fedha (Tender values) alizolipwa msambazaji aliyetunukiwa zabuni, ukilinganisha na kiasi cha fedha kilichotangazwa (RFQ values).

Kuwepo kwa dosari hii, kunatilia mashaka uhalisia wa malipo ya tozo ya huduma yanayofanywa kila mwisho wa mwezi, kwa vile ukokotoaji wa kiasi cha fedha hizo hutegemea thamani ya zabuni zilizoidhinishwa na kulipwa ndani mwezi husika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar kusimamia maboresho ya mfumo kwa kuweka udhibiti wa kuthibitisha na kuzuia uingizwaji wa thamani ya zabuni iliyo nje ya kiwango cha bajeti ya manunuzi ya zabuni hiyo. Mchanganuo wa zabuni pamoja na thamani zisizokuwa halisi ni kama unavyoonekana katika **Kiambatisho Nambari 3.**

### 4.1.2.17 Mfumo wa e-Proz kushindwa kubaini vyeti vilivyomaliza muda

Ukaguzi umebaini kwamba mfumo wa e-Proz unashindwa kuwazuia wasambazaji walio na vyeti vya usajili vilivyopitwa na wakati kuingia katika mashindano na kutunukiwa zabuni, kufanya hivyo ni kinyume na Kanuni nambari 87 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma.

Ukaguzi umebaini msambazaji "OSAJU COMPANY LIMITED" mwenye nambari ya usajili G000394 ulioishia tarehe 19 /01/2023, alishiriki na kutunukiwa zabuni mbali mbali bila ya kuzingatia umalizikaji muda wa vyeti vyake vya usajili.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar kusimamia maboresho ya mfumo kwa kuweka udhibiti wa kiotomatiki wa kumzuia msambazaji mwenye nambari ya usajili iliyopitwa na wakati ashindwe kushiriki na kutunukiwa zabuni kama ilivyoelekezwa kwenye Kanuni za Manunuzi ya Umma. Mchanganuo wa Taarifa za cheti cha Msambazaji ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 28: Mfumo kushindwa kuzuwia wasambazaji walio na vyeti vya usajili vilvyomaliza muda wa kushiriki mashindano ya zabuni**

| S/N | RFX Code | RFX Tiltle | Division | RFX Publish RFx Date | RFX Award Date | Supplier Awarded |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | rfq_ 14781 | UNUNUZI WA NGUO ZA WATOTO MAZIZINI WAMJJWW | MINISTRY OF COMMUNITY DEVELOPMENT | 3/16/2023 | 01/04/2023 16:38 | 15,730,000. |
| 2. | rfq_ 13753 | UNUNUZI WA KARATASI ZA KUANDIKIA (A4 PAPER) | PUBLIC PROCUREMENT AND DISPOSAL OF PUBLIC ASSETS | 3/8/2023 | 13/03/2023 12:16 | 800,000. |
| 3. | rfq_ 14853 | UNUNUZI WA KOMPYUTA | PUBLIC PROCUREMENT AND DISPOSAL OF PUBLIC ASSETS | 3/20/2023 | 09/05/2023 11:09 | 6000,000. |

| S/N | RFX Code | RFX Tiltle | Division | RFX Publish RF x Date | RFX Award Date | Supplier Awarded |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 4. | rfq_ 14863 | UNUNUZI WA KOMPYUTA (DESKTOP) | PUBLIC PROCUREMENT AND DISPOSAL OF PUBLIC ASSETS | 3/20/2023 | 09/05/2023 12:27 | 6000,000. |
| 5. | rfq_ 18021 | TUNAOMBA KUSAMBAZIWA KOMPUTA ZA MEDANI DESKTOP COMPUTER KWA MATUMIZI YA | ZANZIBAR HIGHER EDUCATION LOAN BOARD (ZHELB) | 4/28/2023 | 04/05/2023 21:10 | 19,000,000. |
| 6. | rfq_1896 | SBD FOR SUPPLY OF XONSTRUCTION AND BUILDING MATERIAL FOR JKU SECURITY | NATIONAL SERVICES BRIGADE (JKU) | 1/19/2023 | 30/03/2023 10:14 | 2,632,042,250. |
| 7. | rfq_ 8696 | ZABUNI KWA AJILI YA KUJENGA VIBANDA PUMPING HOUSE PAMOJA NA FENSI JUMLA | ZANZIBAR WATER AUTHORITY (ZAWA) | 1/16/2023 | 12/05/2023 11:27 | 1,279,576,434. |

#### 4.1.2.18 Kuwepo kwa vyanzo vya mapato ambapo makusanyo yake hayapiti kwenye mfumo wa ZanMalipo

Kifungu nambari 55(a) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kinaelezea kwamba "Fedha zote za Umma zitakusanywa kupitia mfumo wa malipo wa kielektroniki uliowekwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali". Katika kutekeleza agizo hilo Serikali ilianzisha rasmi mfumo wa 'ZanMalipo' ili kuweza kukusanya fedha zote za Serikali kwa lengo la kuongeza ufanisi katika usimamizi wa mapato ya Serikali.

Ukaguzi umebaini uwepo wa vyanzo vya mapato ambapo makusanyo yake hayapiti kwenye mfumo wa Zanmalipo na badala yake yanakusanywa kwa kutumia mifumo mingine inayo simamiwa na kampuni binafsi. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na matakwa ya kifungu nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali mtandao kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma kwa kuunganisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato ili kuhakikisha fedha zote zinakusanywa kupitia mfumo wa malipo wa kielektroniki kwa lengo la kuongeza ufanisi katika usimamizi wa mapato ya Serikali.

**Jadweli Nambari 29: Tofauti ya mapato yanayokusanywa baina ya mfumo wa ZanMalipo na mifumo mwengine.**

| Namba | Taasisi ya Umma | mapato katika Taarifa za Hesabu. | Mapato yalikusanywa ZANMALIPO | Mapato yaliyokusanywa kwa mifumo mwengine | Mifumo iliyohusika kukusaya mapato |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Wizara ya Afya | 2,814,099,739.68 | 861,065,009.00 | 1,953,034,730.68 | Mfumo wa Usimamizi wa Vipimo na Chanjo ya Uviko-19 Zanzibar. |
| 2. | Wizara ya Maji, Nishati na Madini. | 12,574,306,012.00 | 768,321,103.00 | 11,805,984,909.00 | Mfumo wa Usimamizi wa Vibali (RAHISI SOLUTION). |

## MAPITIO YA MFUMO WA BAMAS

Mfumo wa BAMAS ni mfumo unaotarajiwa kuanza kutumika Serikalini kwa Mawizara, Idara na Wakala za Serikali (MDA) ambazo zinategemea ruzuku ya Serikali kuendesha shughuli zao. Mfumo huu unatarajiwa kusimamia Bajeti, Mapato na Matumizi yote ya Serikali pamoja na madeni na mali. Mfumo wa BAMAS ulitengenezwa na eGAZ kwa kushirikiana na Wataalamu kutoka Wizara ya Fedha Tanzania Bara na unasimamiwa na Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar.

Mapitio ya mfumo huu katika hatua ya utengenezaji yalikuwa na lengo la kupima uzingatiwaji wa Miongozo, Viwango na Sera mbali mbali za TEHAMA wakati wa utengenezaji, aidha ukaguzi ulikuwa na malengo ya kufanya tathmini ukamilifu na utayari wa mfumo kuanza kutumika katika maandalizi ya bajeti ya Serikali ya Mwaka wa fedha 2024/2025 ambapo tulibaini mapungufu mbali mbali yakiwemo: -

#### 4.1.2.19 Kukosekana kwa kipengele cha "Bajeti Reallocation" kwenye Moduli ya Bajeti

Ukaguzi ulibaini kwamba mfumo wa BAMAS haujawekewa kipengele (functionality) cha "Budget Reallocation" ambacho ni muhimu katika hatua ya kufanya mabadiliko ya mgawanyo wa bajeti kwenye mfumo ambapo bila ya kipengele hicho watumiaji wa mfumo hawawezi kubadilisha mgawanyo (reallocation) kutoka fungu moja la bajeti kwenda fungu jengine kulingana na mabadiliko yanayohitajika.

Kukosekana kwa Kipengele cha "budget reallocation" katika mfumo wa BAMAS kunaweza kupelekea kushindikana kutekelezwa kwa mabadiliko yanayopendekezwa kwa Serikali na Baraza la Wawakilishi wakati wa vikao vya Bajeti za Mapato na Matumizi Barazani. Aidha, utekelezaji wa "budget reallocation" unatakiwa kufanyika ndani ya "Vote" kutokana na makosa ya kibinadamu (human errors) katika kuweka bajeti kwenye mafungu tofauti na mpango.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao kutengeneza na kuweka kipengele cha "Budget Reallocation" katika Mfumo wa BAMAS ili kuwezesha watumiaji wa mfumo katika Idara ya Bajeti kutekeleza majukumu yao kulingana na taratibu za kazi.

#### 4.1.2.20 Kukosekana kwa kipengele cha "Supplementary Budget" kwenye Moduli ya Bajeti

Ukaguzi ulibaini kwamba mfumo wa BAMAS hauna kipengele cha Bajeti ya Nyongeza (Supplimentary Budget) ambacho ni maalumu kwa ajili ya kuwezesha uingizaji wa bajeti ya nyongeza ambayo inaidhinishwa na Baraza la Wawakilishi kwa sababu maalumu tofauti na bajeti kuu inayopitishwa kila mwaka.

Kukosekana kwa kipengele cha "Supplementary Budget" katika mfumo wa BAMAS kunaweza kupelekea Serikali kushindwa kuingiza bajeti iliyoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya kutekeleza kazi maalumu au dharura iliyosababishwa na majanga kama vile Mafuriko, Tetemeko la Ardhi, ugonjwa wa mlipuko n.k na kulazimu bajeti pamoja na matumizi hayo kufanyika nje ya mfumo jambo litakalo ondoa udhibiti wa bajeti na matumizi unaopatikana kupitia mfumo na kuhatarisha ufanyaji wa matumizi yasiyozingatia idhini na udhibiti uliopo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao kukamilisha vipengele vyote muhimu kulingana na "business processes" za Idara ya Bajeti ikiwa ni pamoja na uundaji wa kipengele cha "Supplementary Budget" kwa kizingatia miongozo ya Kitaifa.

Aidha, ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao kuhakikisha unafanya ushirikishaji wa karibu wa watumiaji wa mfumo wa BAMAS katika Idara ya Bajeti kwa hatua zote kuanzia kukusanya na kuandika mahitaji ya watumiaji (user requirements), kuthibitisha mahitaji (validation of documented user requirements), kufanya mafunzo ya watumiaji, kutoa nafasi kwa watumiaji wa mfumo kufanya majaribio ya mfumo na kutoa ruhusa au kuzuia mfumo kuanza kutumika ikiwa haujakidhi mahitaji (User Acceptance and Testing).

#### 4.1.2.21 Kukosekana kwa kipengele cha "Version Carryover" kwenye Moduli ya Bajeti

Ukaguzi ulibaini kwamba mfumo wa BAMAS hauna kipengele cha "Version Carryover" ambacho ni muhimu katika kufanikisha mchakato wa utayarishaji wa bajeti kwa kurahisisha kupeleka mbele katika mwaka mpya wa bajeti usanidi uliofanyika katika mwaka uliotangulia au kutoka "version" moja kwenda "version" nyengine ndani ya  mwaka mmoja.

Kukosekana kwa kipengele hiki kunaongeza ugumu wa kazi ya maandalizi ya bajeti na kupelekea kutumia muda mrefu katika uandaaji wa bajeti hali inayoweza kusababisha ucheleweshaji wa mchakato wa bajeti na kufanya utekelezaji wa bajeti husika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao kuhakikisha kwamba unatatua mapungufu hayo kwa kuzingatia umuhimu wake katika kukamilisha mchakato wa kuandaa bajeti ya Serikali ili mfumo wa BAMAS usaidie kupatikana kwa ufanisi kwa watumiaji wake na sio kuwa  kikwazo cha ufanisi.

#### 4.1.2.22 Mfumo kutofanyiwa majaribio na watumiaji (User Acceptance Testing) wakuu (Core Team Users) wa Moduli ya Bajeti

Ukaguzi ulibaini kwamba utengenezaji wa mfumo wa BAMAS haukuzingatia Miongozo ya Viwango Bora Kubalifu (best practice) katika utengenezaji wa mifumo ya TEHAMA kama vile "Software Development Life Cycle (SDLC)".

Hali hii ilibainika kupitia mahojiano na majadiliano yaliyofanywa na ukaguzi kwa watumishi wa Idara ya Bajeti ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango ambapo ilifahamika kwamba miongoni mwa hatua muhimu katika utengenezaji wa mifumo ya TEHAMA ni hatua ya kufanya majaribio ya mfumo (UAT) ili kubaini kama mfumo umekidhi mahitaji ya watumiaji, hali hii haikuzingatiwa ipasavyo na kwamba eGAZ iliunda mfumo kwa kushirikisha watumishi wachache katika Idara ya Bajeti na kupelekea watumishi waliobaki kukosa uelewa wa kutosha wa utendaji wa mfumo wa BAMAS katika eneo la kusimamia Bajeti ya Serikali (Budget Management).

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao kuzingatia Miongozo ya Viwango Bora kubalifu vya TEHAMA katika utengenezaji wa mifumo kama vile "SDLC" ambayo inahakikisha kwamba mifumo inayotengenezwa inatumia gharama ndogo na kukamilika kwa wakati pamoja na kuzingatia hatua zote muhimu kwa uzito unaostahili na kuepusha kufanya kazi moja zaidi ya mara moja (double works) zitakazoigharimu taasisi muda mrefu na fedha nyingi bila sababu.

### 4.1.2.23 Kukosekana kwa nyaraka muhimu za utengenezwaji wa Mfumo wa BAMAS

Ukaguzi uliomba nyaraka mbalimbali zilizotumika kutengeneza Mfumo wa BAMAS, hadi ukaguzi unakamilika Uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao haukuweza kuupatia ukaguzi nyaraka zilizoombwa ikiwemo Nyaraka ya Usanidi wa Mfumo, nyaraka zinazoonesha mahitaji ya watumiaji wa mfumo, nyaraka za kufanya majaribio ya mfumo, pamoja na nyaraka mbali mbali za usanifu wa mfumo wa BAMAS kwa ajili ya kufanya mapitio ya namna mfumo ulivyosanidiwa ili kupima utekelezaji wa miongozo ya viwango bora kubalifu vya TEHAMA (best practices) katika hatua ambayo mfumo ulikuwa umefika.

Kukosekana kwa Nyaraka hizi muhimu kumepelekea kutofanyika kwa mapitio ya usanifu na usanidi wa mfumo wa BAMAS, aidha hali hii imekwamisha ufanyaji wa tathmini za majaribio yaliyofanyika wakati wa utengenezaji wa Mfumo huo ili kuthibitisha ushiriki wa makundi mbalimbali ya watumiaji wa mfumo katika hatua za utengenezaji wa mfumo jambo ambalo linapelekea kuinyima Serikali fursa ya kushauriwa kuhusiana na Usalama, Usiri, Uadilifu na upatikanaji wa taarifa za kibajeti, mapato na matumizi pamoja na madeni ya Serikali katika mfumo wa BAMAS.

Aidha, Serikali imekosa fursa ya kupata ushauri sahihi kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusiana na matumizi endelevu ya mfumo huu yatakayohakikisha kwamba Serikali inanufaika na uwekezaji uliofanyika katika mfumo wa BAMAS kwa kutumia fedha za Umma.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao kuhakikisha kwamba unaandaa Nyaraka zote ambazo ni muhimu sana katika kuendeleza mfumo wa BAMAS na kuhakikisha kwamba Serikali inaweka mikakati ya matumizi endelevu ya Mfumo ambayo yanazingatia usalama, usiri, uadilifu na upatikanaji wa taarifa za kibajeti, mapato na matumizi pamoja na madeni ya Serikali.

### 4.1.2.24 Kukosekana kwa sehemu kubwa ya Ripoti za Bajeti katika Mfumo wa BAMAS


Ukaguzi ulibaini kwamba sehemu kubwa ya Ripoti mbali mbali za Bajeti hazikuwa tayari katika mfumo wa BAMAS kwa ajili ya matumizi ambapo tuligundua kwamba kati ya Ripoti 122 zinazohitajika na watumiaji wa mfumo ni ripoti 15 pekee ndizo zilizokuwepo katika mfumo wa BAMAS sawa na asilimia 12 ya ripoti zote.

Kukosekana kwa ripoti hizo kunapelekea mfumo wa BAMAS kutokuwa tayari kwa ajili ya kuanza kutumika kwa kuingiza bajeti za Serikali kwasababu hautaweza kutoa ripoti zinazotakiwa kupelekwa katika Baraza la Wawakilishi kujadiliwa na hatimaye kuidhinishwa kabla ya kuanza kutumika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar kufanya tathmini ya mahitaji ya watumiaji wa mfumo katika maeneo yote kuanzia Bajeti, Mapato, Matumizi na Ripoti mbalimbali zinazohitajika ikiwa ni pamoja na ripoti za Bajeti kama zilivyofanyiwa uchambuzi hapo juu na kuchukuwa hatua stahiki za kutekeleza mapungufu yote yaliyomo katika mfumo huo kwa kuwashirikisha watumiaji wa mfumo katika kila kitengo/ seksheni hatua kwa hatua na kuhakikisha kwamba inaandaa taarifa za utekelezaji ambazo zitapatikana kwa ajili ya ukaguzi.

Hali halisi iliyopo ya upatikanaji wa ripoti dhidi ya mahitaji ya ripoti za Mfumo wa BAMAS ni kama inavyoonekana katika Mchoro hapo chini:-

## Jadweli Nambari 30: Hali halisi ya utekelezaji wa mahitaji ya ripoti ya watumiaji wa mfumo wa BAMAS




### 4.1.2.25 Kutokamilika kwa Moduli ya Mapato katika mfumo wa BAMAS

Ukaguzi ulibaini kwamba Moduli ya kuratibu masuala ya Mapato (Revenue Management Module) haijakamilika katika mfumo wa BAMAS, aidha, ilibainika pia kwamba watumiaji wa mfumo katika eneo hili hawana uelewa wa kutosha kuhusiana na utendaji kazi wa mfumo wa BAMAS jambo linalotilia shaka mpango wa Wakala wa Serikali Mtandao katika kuhakikisha kwamba watumiaji wote wa mfumo huu wanashirikishwa ipasavyo na kwamba wanapata uelewa kamili wa namna mfumo unavyofanya kazi katika vitengo/ seksheni zao kulingana na mahitaji yao.

Kutokamilika kwa Moduli ya kusimamia mapato ni kikwazo kikubwa katika uratibu, udhibiti na usimamizi wa mapato unaofanywa na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kupitia Idara ya Muhasibu Mkuu wa Serikali jambo linaloweza kuathiri kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa taarifa sahihi za mapato ya nchi ambazo huwasilishwa kupitia ripoti za mwisho wa mwaka zinazoandaliwa na Muhasibu Mkuu wa Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao kuyafanyia kazi mapungufu hayo kwa kuzingatia umuhimu wa usimamizi wa ukusanyaji wa mapato pamoja na upatikanji wa taarifa sahihi zilizokamilika kwa wakati muafaka.

### 4.1.2.26 Kukosekana kwa ufahamu wa kutosha wa namna mfumo unavyofanya kazi kwa watumishi wa Idara ya Bajeti na Muhasibu Mkuu wa Serikali

Ukaguzi ulifanya mapitio kwa watumiaji wa mfumo wa BAMAS katika Idara ya Bajeti na Mhasibu Mkuu wa Serikali na kubaini kwamba wafanyakazi wa Idara hizo bado hawana uwelewa mzuri wa matumizi ya mfumo huo pamoja na kuwa wao ndio wanaotakiwa kuendesha na kutoa elimu kwa wengine kwa upande wa Bajeti, Mapato na Matumizi pamoja na Hesabu za mwisho wa mwaka (final accounts). Aidha, Idara ya bajeti na Idara ya Muhasibu Mkuu wa Serikali imedai kutokupatiwa mafunzo ya kutosha juu ya matumizi ya mfumo huo.

Kutokuwa na ufahamu wa kutosha wa mfumo wa BAMAS kwa Idara hizo ambazo ndizo watumiaji wakuu wa mfumo wa BAMAS kunaweza kupelekea Serikali kupata hasara kubwa kwa kuingia gharama nyingi za kutengeneza mfumo wa BAMAS ambao unaweza kutotumika ipasavyo na kutoongeza tija na ufanisi uliokusudiwa Serikalini. Aidha, hali hii inaweza kuwa chanzo kikuu cha kukosekana kwa matumizi endelevu ya mfumo huu wa BAMAS Serikalini.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao, kufanya tathmini ya uhitaji wa mafunzo ya mfumo wa BAMAS kwa wafanyakazi wa Idara ya Bajeti, Idara ya Muhasibu Mkuu wa Serikali na kuwapatia mafunzo ili kuhakikisha kuwa mfumo huo utakapoanza kutumika hakuna mapungufu ya uelewa wa mfumo kwa watumiaji.

### 4.1.2.27 Kukosekana kwa Ripoti za Kihasibu (final accounts) katika mfumo wa BAMAS zinazoendana na mahitaji ya sasa ya Serikali

Ukaguzi ulibaini kuwa mfumo wa BAMAS haujawekewa ripoti za "final accounts" ambazo zinaendana na matakwa ya sasa ya utendaji yaani" Cash Basis Final Accounts".

Kukosekana kwa ripoti hizo ambazo ni za lazima katika uhasibu zinazotolewa kila mwisho wa mwaka kunarudisha nyuma utendaji wa Idara ya Muhasibu Mkuu wa Serikali na kupelekea mfumo utakapoanza kutumika watumishi waandae Ripoti hizo kwa mikono (manually).

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao kujipanga vyema kwa kuandaa mpango kazi utakaozingatia mapungufu yote yaliyomo katika mfumo wa BAMAS na kuonesha muda utakaotumika kutatua mapungufu hayo kwa kila eneo la watumiaji wa mfumo na kuyatatua kwa haraka iwezekanavyo Kabla mfumo haujaanza kutumika (Live Operations).

### 4.1.3 OFISI YA RAIS KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA (OR-KSUUB)

Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa Ofisi ya Rais Katiba Sheria Utumishi na Utawala Bora (OR-KSUUB) kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 4.1.3.1 Kukosekana kwa nyaraka muhimu za Utengenzwaji wa Mfumo

Kwa mujibu wa Muongozo wa eGA nambari **eGA/EXT/BSA/008** wa Utekelezwaji wa Miradi ya TEHAMA, wa mwaka 2020 unahitaji mradi wa TEHAMA unapotekelezwa lazima ufuate taratibu na mbinu "Methodology" ya Project Development life Cycle – PDLC . Mbinu hiyo imekusanya hatua tofauti za mchakato wa utengenezwaji wa mfumo.

Aidha, kifungu nambari 2.3 cha muongozo huo kimefafanua kwamba kwa kila hatua kutakuwa na matayarisho ya nyaraka ambazo zitasaidia katika utengenezwaji, uendeshaji, usimamizi na udumishaji wa mfumo.

Baada ya kukamilika kwa mradi kutakuwa na mpango wa kusimamia na kudumisha mradi ili kuweza kufanya kazi kwa ufanisi na kuendelea kutoa huduma bora kama ilivyokusudiwa.

Ukaguzi ulifanya mapitio ya Mradi wa TEHAMA wa Uanzishwaji wa Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Mishahara na Rasilimali Watu (HR and Payroll Information Management System) uliotengenezwa na kampuni ya ENGO kupitia Mradi wa PFMRP mwaka 2021 kwa gharama za **shilingi 59,000,000.**

Mfumo huo unatumika katika Wizara na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na unasimamiwa na OR-KSUUB kwa kushirikiana na eGAZ.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika uwepo wa dosari mbali mbali kwenye mchakato wa utengenezaji, uendeshaji, usimamizi na udumishaji wa mfumo wa HR-Payroll Information System, baadhi ya dosari zilizobainika ni kama zifuatazo:-

Ukaguzi uliomba nyaraka mbali mbali za utengenezwaji wa mfumo wa HR-Payroll Information System, lakini hadi ukaguzi unakamilika baadhi ya nyaraka hazikuweza kupatikana. Miongoni mwa nyaraka zilizokosekana ni kama zifuatazo:-

- Ripoti ya Pendekezo la Mradi (Project Proporsal Report / Business Case) kuhusiana na uanzishwaji wa Mfumo inayoeleza kwa ufupi hatua mbali mbali za utengenezwaji wa mfumo pamoja na kuchambua kwa kina gharama zote za fedha zitakazotumika kwenye kila kipengele cha mradi huo (Project Breakdown Cost).
- Ripoti ya kufanyika kwa Tathmini ya Vihatarishi vya Mradi (Risk Assessment Report).
- Mpango wa kusimamia, kuzikabili na kuziepuka hatari zinazoweza kujitokeza kwenye utekelezaji wa Mradi (Risk Management Plan).
- Ripoti ya hali ya Mradi iliyofikia (Progress Project Report) pamoja na gharama zilizokuwa zimetumika kabla ya kumalizika kwa mradi huo wa utengenezwaji wa mfumo kwa mujibu wa kifungu cha 6.4(a) cha Masharti Maalum ya Mkataba (SCC).
- Ripoti ya uthibitisho wa kukubalika kwa utendaji kazi katika majaribio ya mifumo (UAT Report).
- Ripoti ya Kuhakiki Ubora wa Mfumo (Quality Assurance Report) kwa mujibu wa Mpango wa kusimamia Ubora (Quality Management Plan) uliopo.
- Kodi za kutengenezea Mfumo "Source Codes".
- Barua ya kukubalika Mfumo (Acceptance Letter).
- Muongozo wa mtumiaji wa Mfumo (Application User Manual).

Kukosekana kwa nyaraka hizo kunatoa ishara kwamba kuna udhaifu katika mchakato wa utengenezwaji wa mfumo wa TEHAMA kutokana na kutokuzingatiwa kwa Muongozo wa utekelezaji wa miradi ya TEHAMA wa eGA nambari **eGA/EXT/BSA/008** pamoja na miongozo ya kimataifa ya utengenezwaji wa Mifumo ya TEHAMA (SDLC).

Aidha, kukosekana kwa nyaraka hizo kunaweza kusababisha hatari (risk) ya kutengenezwa mifumo isiyokuwa na tija na ufanisi wa utendaji kazi na kupelekea kushindwa kufikia malengo yaliyokusudiwa jambo ambalo linaweza kusababisha Afisi kuingia gharama za ziada za marekebisho ya mfumo na hatimae kuingiza hasara Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa OR-KSUUB kuhakikisha unazingatia na kufuata kikamilifu miongozo na viwango vinavyokubalika kitaifa na kimataifa katika utekelezaji wa miradi ya TEHAMA. Vile vile, Afisi kuhakikisha nyaraka zote zinazohusika kwenye mfumo zinatengenezwa na kuwekewa kumbukumbu kwa kila hatua ili kupatikana ufanisi katika usimamizi na udumishaji na mifumo ya TEHAMA ya Afisi.

#### 4.1.3.2 Kuchelewa kukamilika kwa Mradi wa Utengenezwaji wa Mfumo

Kwa mujibu wa kifungu nambari 2.2 cha Masharti Maalum ya Mkataba (SCC) wa Uboreshaji wa Mfumo wa Mishahara wa Serikali (GPS), muda wa maboresho ya mfumo ulikuwa ni miezi minne (4) kuanzia tarehe 20 Mei 2021 hadi kumalizika mwezi wa Septemba, 2021.

Aidha Jadweli la Mpango Kazi wa Mradi limethibitisha kuwa kazi hiyo itafanyika kwa kipindi cha miezi minne (4) tu kuanzia mwezi wa Mei, 2021 hadi mwezi wa Septemba, 2021.

Moja kati ya maboresho makuu yaliyopangwa kufanyika ni kuingizwa taarifa kamili za rasilimali watu katika Mfumo wa zamani wa Mishahara (GPS) ili kwenda sambamba na mahitaji na kuweza kupatikana taarifa zote za watumishi pamoja na maslahi yao kwa ufanisi na kwa wakati.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba mradi huo umechelewa kumalizika kwa kipindi kirefu cha zaidi ya miezi 22 (mwaka mmoja na miezi kumi) na kuanza rasmi kutumika baada ya kumalizika kwa mafunzo ya mfumo mnamo mwezi wa Julai, 2023 badala ya mwezi wa Septemba, 2021.

Hali hii imesababishwa na kuwepo kwa udhaifu katika kukusanya mahitaji na kushirikisha ipasavyo watumiaji wa mfumo (user requirements) ili kuweza kupata taarifa sahihi na kwa wakati katika kipindi cha utengenezwaji wa mfumo.

Kuchelewa kukamilika kwa mradi huo kumepelekea Taasisi za Umma kuchelewa kupata huduma za rasilimali watu kwa ufanisi kupitia mfumo wa HR-Payroll Information System na hatimae kudhoofisha utendaji kazi wa Taasisi hizo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa OR-KSUUB katika miradi ijayo kuhakikisha unakuwa makini katika kuanzisha miradi ya TEHAMA kwa kufuata kikamilifu miongozo na taratibu zote za utengenezwaji wa mifumo pamoja na nyaraka husika.

#### 4.1.3.3 Dosari katika Mfumo wa HR-Payroll Information System

Ukaguzi ulifanya mapitio ya Mifumo ya OR-KSUUB kwa kuangalia udhibiti wa taarifa uliopo ndani na nje ya mifumo hiyo. Baadhi ya mifumo mikuu iliyopitiwa kwa mwaka wa fedha 2022-2023 ni pamoja na Mfumo wa HR-Payroll Information System, Mfumo wa LADS, Mfumo wa elibrary na Tovuti ya Afisi. Katika ukaguzi huo dosari mbali mbali zimebainika na kutolewa na matokeo ya mapitio hayo ni kama ifuatavyo:-

Katika ukaguzi uliofanyika wa mfumo wa HR-Payroll Information System imebainika kwamba mfumo bado una mapungufu mengi katika utendaji kazi wake ambapo mapungufu hayo yasipofanyiwa kazi kuwepo yanawea kuathiri ufanisi wa mfumo na kusababisha kusababisha kukosekana kwa tija iliyokusudiwa. Baadhi ya mapungufu yaliyobainika ni kama ifuatavyo:-

**a) Kutokafanya kazi kwa baadhi ya moduli za mfumo wa HR-Payroll System**

Mfumo wa HR-Payroll Information Management System umekusanya jumla ya moduli kumi na sita (16) ambazo hutumika kwa shughuli zote za taarifa za rasilimali watu na mishahara kwa Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuna baadhi ya moduli hazifanyi kazi licha ya kwamba mfumo unaendelea kutumika, moduli hizo ni kama zifuatazo:-

- ***Moduli ya kutoa Ripoti "Reporting Module"***

Moduli hii ilitarajiwa kutoa ripoti za aina zote zinazohusiana na taarifa za kiutumishi kama vile taarifa binafsi za mtumishi, mishahara, maposho, mikato, nyongeza, kupandishwa cheo, kushushwa cheo, masomo, adhabu, uhamisho, likizo, safari za kikazi n.k.

Aidha moduli hii ilitarajiwa kuweza kutoa ripoti hizo kwa vipindi tofauti vinavyohitajika kama vile kwa mwezi, miezi mitatu, miezi sita, kwa mwaka n.k ambapo ripoti hizo zilitarajiwa kupatikana katika mifumo tofauti kama vile mfumo wa pdf, spreadsheet, text file, JSON file, html file, Word file n.k.

Hivyo kutokana na kutofanya kazi kwa moduli hii kunapelekea Taasisi za Serikali kutoweza kupata ripoti za aina tofauti kama zilivyotajwa hapo juu.

- ***Moduli ya Kusimamia Bajeti "Budgeting Management Module"***

Moduli hii ilitarajiwa kusimamia taarifa zote zinazohusiana na bajeti ya mishahara zinazotolewa kutoka katika Mfumo wa BAMAS ambapo taarifa hizo zingeonesha kiasi gani cha fedha kinachoombwa na Taasisi husika kwa ajili ya malipo ya mishahara ya wafanyakazi kwa kila mwezi, kiasi gani kilichopo sasa na kiasi gani kinahitajika kwa ajili ya malipo ya area, maposho, nyongeza n.k. ambapo taarifa hizo zingesaidia taasisi kupanga mikakati ya ajira kwa watumishi wanaostaafu na wanaohitajika.

- ***Moduli ndogo ya likizo***

Sehemu hii ilitarajiwa kuonesha taarifa za likizo za mtumishi kama vile idadi ya siku za likizo alizonazo, tarehe ya kuanza likizo, tarehe ya kumaliza likizo n.k. ambapo taarifa hizo zingesaidia kuweka kumbukumbu nzuri ya likizo za wafanyakazi katika Taasisi za Umma.

Kutofanya kazi kwa moduli hizo kunasababisha kukosekana kwa baadhi ya Taarifa muhimu kama zilivyobainishwa hapo juu jambo ambalo linaweza kupelekea mfumo kuonekana hauna tija kama ilivyokusudiwa licha ya fedha nyingi kutumika katika utengenezwaji wake.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa OR-KSUUB kufanya jitihada za makusudi ili kuweza kuukamilisha mfumo huo na katika moduli zote kwa lengo la kuweka taarifa za kiutumishi na bajeti kama ilivyokusudiwa na hatimae kupatikana kwa tija na ufanisi wa utendaji kazi wa mfumo.

**b) Kutokuwepo kwa Rejista la Mishahara "Salary Register" ndani ya Mfumo wa HR-Payroll Information System**

Ukaguzi umebaini kwamba Mfumo wa HR-Payroll Information Management System hauna Rejista la Mshahara "Salary Register" ambapo lingeweza kuhifadhi taarifa zote za mishahara ya mfanyakazi kuanzia alipoajiriwa hadi atakapostaafu ili kuweza kusaidia kutoa taarifa za mishahara kwa usahihi wakati mfanyakazi anapostaafu.

Kutokuwepo kwa Rejista la Mishahara ndani ya mfumo kumepelekea kazi ya ujazaji wa taarifa za mishahara ya watumishi kwa kila mwezi kuendelea kufanyika nje ya mfumo kwenye makaratasi "manually" jambo ambalo husababisha ugumu na changamoto katika ujazaji na uwekaji wa kumbukumbu za taarifa hizo kwa Taasisi za Umma na kuonekana mfumo bado haujasaidia katika eneo hilo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa OR-KSUUB kufanya jitihada za kurekebisha dosari zinazobainika katika mfumo huo ili kuweza kupatikana ufanisi na tija iliyokusudiwa katika utendaji kazi wa mfumo.

### c) Mfumo kushindwa kutoa "Notification" kwa mtumishi anaekaribia kustaafu

Sheria na taratibu za kiutumishi zinamtaka Mtumishi wa umma kupewa barua ya notisi ya kustaafu kazi miezi sita kabla, aidha inapofika siku chache kabla ya kustaafu mtumishi hukumbushwa tena na kutakiwa kurejesha rasilimali zilizochini ya umiliki wa Afisi pamoja na kuzuiliwa mshahara wake "block" ili kutoendelea kulipwa mshahara baada ya kustaafu kazi, kwa sasa mchakato wa kutoa taarifa za kustaafu kazi hufanyika kwa njia ya kawaida "manually".

Kwa mujibu wa mahitaji ya watumiaji, Mfumo wa HR-Payroll Information Management System ulitakiwa kuweza kutoa taarifa ya ukumbusho "Notification information" kwa mtumishi wa umma anaekaribia kustaafu kazi ambapo taarifa hiyo ingetumwa kwa njia ya ujumbe mfupi "sms" kwenye simu ya mkononi au kwa njia ya barua pepe "email" ili kumkumbusha mtumishi husika siku zake chache alizobakisha kustaafu kazi. Aidha, kupitia taarifa hiyo uongozi wa Taasisi husika ungeweza kufanya maandalizi ya kustaafu kwa wakati bila ya kuchelewesha.

Ukaguzi umebaini kwamba Mfumo wa HR-Payroll Information System bado haujaweza kutoa taarifa ya ukumbusho wa kustaafu kazi (Notification Information) kwa njia ya "sms" au "email" kwa mtumishi wa umma anaemaliza muda wake wa utumishi ili kupata ukumbusho mapema na kufanya taratibu zote za kustaafu zinazotakiwa kwa wakati.

Mfumo kushindwa kutoa taarifa ya ukumbusho (Notification) kwa mtumishi anaekaribia kustaafu kunaweza kujitokeza ucheleweshwaji wa utengenezwaji wa maslahi ya mtumishi endapo wahusika, ya mtumishi akichelewa kupata taarifa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa OR-KSUUB kufanya marekebisho hayo mapema ili mfumo uweze kufanya kazi kama ilivyokusudiwa kwa kuweza kumjuulisha mtumishi kwa njia ya sms au baruapepe kabla ya kustaafu kazi ili kufanya maandalizi yanayohitajika kwa wakati bila ya kuchelewa.

#### 4.1.3.4 Dosari katika Mfumo wa Legal Aid Database System (LADS)

Mfumo wa LADS ni mfumo ulioanzishwa na Wizara ya Katiba na Sheria mwaka 2020 na unasimamiwa na OR-KSUUB. Mfumo huo umetengenezwa na mtaalamu kutoka Dar es Salaam kwa gharama za **shilingi 18,000,000** ukiwa na malengo ya kusajili na kuweka kumbukumbu za watoa huduma za msaada wa kisheria (legal service providers) kama vile Taasisi na Jumuiya za Kisheria, Wanasheria, Mawakili, Mavakili, Wasaidizi wa Kisheria n.k. ambapo taarifa zao za usajili, biashara, aina za huduma wanazotoa hupatikana kidijitali kupitia mfumo huo.

Ukaguzi ulifanya uhakiki wa mfumo na kubaini uwepo wa mapungufu mbali mbali, baadhi ya mapungufu hayo ni kama ifuatavyo:-

a) Kukosekana kwa msaada wa kiufundi "Technical Support" kutoka kwa mtengenezaji wa mifumo wakati zinapojitokeza changamoto kwenye mfumo, vile vile kutokuwepo kwa msimamizi wa mfumo "System Administrator " kwa upande wa Afisi jambo ambalo limepelekea umiliki wa mfumo wote (ownership) kubakia kwa mtengenezaji wa mfumo licha ya kwamba OR-KSUUB ina wataalamu katika kitengo cha TEHAMA wanaoweza kusimamia mfumo huo na fedha nyingi zimelipwa kwa ajili ya utengenezaji wa mfumo.

b) Mfumo kukosa sehemu ya kusajili na kuingiza viambatisho (attachment) vya taarifa za Vituo vya Msaada wa Kisheria jambo ambalo limesababisha baadhi ya vituo kuendelea kutoa huduma za msaada wa kisheria bila ya kusajiliwa, kwa mfano kituo cha Msaada wa Kisheria cha M/Kwerekwe kinachosimamiwa na Zanzibar University pamoja na kituo cha Msaada wa Kisheria kinachosimamiwa na Mkurugenzi wa Mashtaka.

c) Kutokuwepo kwa taarifa muhimu (mandatory *) zinazohitajika wakati wa usajili ambazo taarifa hizo hujazwa kwa njia ya kuchaguliwa kutoka kwenye sehemu ya orodha na sio kuingizwa kwa mkono, kwa mfano taarifa za Shehia ambapo baadhi yao hazimo kama vile Tumbatu, Kiembe Samaki, Donge Mchangani n.k. Hali hii husababisha kujitokeza kwa ugumu kwa wanaosajili kutoka maeneo hayo.

d) Mfumo kukosa sehemu ya kuingiza tarehe, mwezi na mwaka wa usajili kwa Taasisi/Jumuiya. Aidha mfumo hauna taarifa za jinsia kwa Wanasheria, Mawakili na Mavakili ambazo zitaonesha utambuzi wao kwa vile kuna baadhi ya majina hutumika katika jinsia zote mbili, hivyo ripoti zinazotoka kwenye Mfumo hazioneshi jinsia ya mtoa huduma na wala tarehe kamili ya kusajiliwa jambo ambalo linasababisha ugumu kwa watendaji wa Afisi katika kuwafahamu na kuweka kumbukumbu za kiutendaji.

e) Cheti cha usajili kinachotolewa na OR-KSUUB kwa ajili ya kupewa watoa huduma baada ya kukamilika usajili hakina udhibiti wa utambulisho kama vile QR Code, Barcode n.k. ambapo udhibiti huo utasaidia kubainisha cheti feki na halisi.

f) Mfumo wa LADS haujaunganishwa na Mfumo mkuu wa malipo (ZANMALIPO) kwa ajili ya kutoa nambari za udhibiti wa malipo "Control Numbers", vile vile wahasibu wa Afisi hawafanyi ulinganisho wa kibenki (Bank Reconcilliation) ili kuweza kulinganisha baina ya taarifa za kifedha kutoka katika akaunti na taarifa za kwenye mfumo.

g) Baadhi ya malipo hufanyika kwa Wakala, lakini mfumo hautambui uwepo wa Wakala katika orodha yake ya njia za malipo kutokana na kutoingizwa taarifa hizo, hivyo watoa huduma wanaolipia usajili kupitia wakala hupata ugumu wa kufanya usajili kwenye mfumo kutokana na risiti zao kushindwa kutambulika kwenye mfumo.

h) Kukosekana kwa udhibiti mzuri katika kufanya uhakiki "Verification" na utambuzi "Validation" wa uhalali wa vyeti na risiti za malipo zinazowasilishwa na watoa huduma wakati wa usajili. Mchakato huo hufanyika kwa njia ya kawaida "manually" bila ya kutumia Control Numbers. Vile vile wakati wa (re-registration) mfumo unashindwa kutambua ikiwa kiambatisho cha risiti za malipo kishawahi kutumika nyuma kabla.

i) Watoa huduma wanaoendelea kufanya usajili kwa mwaka unaofuata (re-registration) mfumo huwalazimisha kuingiza baruapepe mpya na sio ya awali ambayo ilitumika wakati wa usajili wa mwanzo, hivyo watoa huduma hulazimika kutengeneza baruapepe mpya kila wanapofanya re-registration kwa mwaka mwengine jambo ambalo husababisha changamoto za mawasiliano kwa wateja wao kutokana na kubadilisha taarifa hizo kila muda.

j) Watoa huduma za msaada wa kisheria kila mwaka hutakiwa kuwasilisha ripoti za utendaji kazi katika Idara ya Msaada wa Kisheria iliyopo OR-KSUUB ambapo ripoti hizo huwasilishwa kwa njia ya kielektroniki kwa kufanyiwa "attachment" kupitia mfumo wa LADS, dosari iliyobainika ni kwamba mfumo huo hauna sehemu ya kufanya "attachment" kwa ajili ya kuwasilisha ripoti za utekelezaji, kwa hivyo kunakuwa na changamoto kubwa katika kuwasilisha ripoti hizo kupitia mfumo ambapo watoa huduma hulazimika kutumia njia ya kudanganya kufanya usajili mpya ili kupatikana sehemu ya "attachment" ya vyeti na risiti za malipo na ndio hutumika kwa kuwasilisha ripoti zao.

k) Mfumo haujazingatia mahitaji na vigezo vya kiusalama vya utengenezwaji wa nenosiri "password requirement" kutokana na kubainika mfumo kuweza kutengeneza nenosiri kwa kutumia nambari pekee.

l) Baadhi ya Ripoti zinazotolewa katika mfumo hazioneshi uhalisia na usahihi wa taarifa zake, hadi ukaguzi unakamilika ripoti za waliosajiliwa zilikuwa zinaonesha kwamba jumla ya taasisi na watoa huduma wote waliosajiliwa katika mfumo ni **318** ambapo idadi hiyo sio sahihi na usahihi ni kwamba idadi iliyopo ni **272**, Changamoto hiyo imejitokeza kutokana na mfumo kuchanganya taarifa za watoa huduma wapya wanaojisajili na wanaoendelea kujisajili katika sehemu moja na kuwahesabu kama wasajiliwa wapya bila ya kuwatenganisha jambo ambalo watendaji wa Wizara wanaohusika na kazi hii hupata tabu ya kuwahesabu katika mfumo njia wanayotumia kuwahesabu ya mkono "manually" kwa kutumia vidole.

m) Baadhi ya nyaraka zinazohusiana na utengenezwaji wa mfumo wa LADS zimekosekana kwa ukaguzi jambo ambalo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 2.3 cha Muongozo wa eGA nambari eGA/EXT/BSA/008 wa Utekelezwaji wa Miradi ya TEHAMA, wa mwaka 2020. Nyaraka zilizokosekana ni kama zifuatazo:-

- Inception Report.
- User Requirement Document.
- System Requirement Specification
- System Design Document.
- System Quality Assurance Report.
- User Acceptance Test Report.
- Training Report.

Kwa ujumla uwepo wa changamoto zilizotajwa hapo juu umesababishwa na ukosefu wa usimamizi, udhibiti na msaada wa kiufundi wa mfumo na vile vile kutokuwepo kwa mashirikiano baina ya Afisi na mtengenezaji wa mfumo ambapo dosari zake ni kwamba mfumo huo unaweza kupoteza taarifa au kuharibika na kusababisha hasara kwa Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa OR-KSUUB kuandaa mkakati imara wa kufanya marekebisho ya dosari zote zilizobainika katika mfumo huo kwa kushirikiana na mtengenezaji wa mfumo ili kuweza kuimarisha ufanisi na utendaji kazi wa mfumo na vile vile kuongeza usalama wa taarifa zilizomo.

#### 4.1.3.5 Dosari katika Mfumo wa e-Library System

Mfumo wa Elibrary ni mfumo ambao umeanzishwa na OR-KSUUB kwa lengo la kuweka taarifa za kisheria katika sehemu moja ikiwa kama ni kitovu cha kitaifa cha taarifa za kisheria (One Stop Centre).

Aidha, mfumo huo husaidia kuweka mazingira ya maktaba katika hali ya kidijitali ili kuwawezesha majaji na maofisa wa sheria kupata taarifa kwa njia ya kielektroniki na kufanya tathmini kuhusiana na rasilimali mbalimbali za kisheria pamoja na ripoti za sheria, uamuzi wa mahakama, sera za Serikali n.k.

Mfumo huo umetengenezwa na mshauri elekezi (consultant) kutoka Zanzibar kwa gharama za **shilingi 9,300,000 sawa na USD 4,026.** Hata hivyo, mkataba wa makubaliano haukupatikana kwa ukaguzi. Ukaguzi ulifanya jitihada za kupitia mfumo huo na kubaini uwepo wa dosari kama ifuatavyo:-

**a) Kutofanya kazi kwa Mfumo wa e-library System**

Mfumo wa e-library System umetengenezwa kwa lengo la kutumika katika Taasisi nne (4) za kisheria ambazo ni Mahkama ya Zanzibar, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Afisi ya Mwanasheria Mkuu pamoja na Skuli ya Sheria ya Zanzibar.

Ukaguzi ulifanya jitihada za kutaka kuhakiki mfumo huo kwa lengo la kupima utendaji wa kazi na kuangalia ikiwa unaenda sambamba na malengo ya Taaisisi yaliyokusudiwa. Hadi ukaguzi unakamilika mfumo ulikuwa umelala haufanyi kazi licha ya kuwa gharama za shilingi 9,300,000 zilikuwa tayari zimeshalipwa kwa mtengenezaji.

Kutofanya kazi kwa mfumo huo kumesababisha Taasisi nne (4) za Kisheria kukosa huduma za kisheria zilizopangwa kutolewa kupitia mfumo, aidha kumesababisha hasara ya shilingi 9,300,000 kutokana na kukosekana kwa tija iliyokusudiwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa OR-KSUUB kufanya jitihada za makusudi za kuufufua mfumo huo, kuusimamia na kuudhibiti ili uweze kudumu na kufanya kazi kwa weledi na ufanisi na hatimae kupatikana kwa tija iliyokusudiwa.

### b) Kukosekana kwa baadhi ya taarifa za Utengenezwaji wa mfumo wa e-library System

Ukaguzi uliomba nyaraka zinazohusiana na utengenezwaji wa mfumo wa e-library System kwa lengo la kuweza kuzifanyia uhakiki ikiwa zimefuata vigezo kwa mujibu wa "TOR" pamoja na "Concept Note". Hadi ukaguzi unakamilika baadhi ya nyaraka zilizoombwa hazikuwasilishwa kwa ukaguzi, nyaraka zilizokosekana ni kama zifuatazo:-

- Signed Contract/Agreements/Statement of Commitment for maintanance.
- Inception Report.
- System Quality Assurance Report.
- User Acceptance Test Report.
- Training Manual for the system.
- Work Report.

Kukosekana kwa nyaraka hizo kumepelekea ukaguzi kushindwa kufahamu na kutoa ushauri kwa Ofisi ikiwa mfumo umetengenezwa kwa mujibu wa mahitaji ya watumiaji "user requirements", umekidhi vigezo vilivyohitajika, taratibu nzuri zilitumika katika kufanya majaribio ya utendaji kazi wa mfumo, wadau wameshirikishwa ipasavyo na mafunzo yalifanyika kwa ufanisi.

Aidha kukosekana kwa nyaraka hizo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 4.0 cha matakwa ya "TOR" na vile vile kwenda kinyume na kifungu nambari 2.3 cha Muongozo wa eGA nambari eGA/EXT/BSA/008 wa Utekelezwaji wa Miradi ya TEHAMA, wa mwaka 2020.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa (OR) KSUUB kufanya mawasiliano ya karibu na mshauri elekezi kwa kumtaka atayarishe nyaraka zote zilizokosekana kwa mujibu wa hadidu rejea na kwa mujibu wa vigezo vya kitaifa na kimataifa. Nyaraka hizo zitasaidia katika kutatua changamoto za usimamizi na uendeshaji wa mfumo zinazojitokeza pamoja na kuwepo kumbukumbu zitakosaidia katika uimarishaji wa mfumo baadae.


### 4.1.3.6 Kutokuwepo kwa leseni katika kanzidata "database" ya Mfumo wa HR-Payroll Information System

Mfumo wa HR-Payroll System hutumia "database" aina ya SQL Server 2019 kutoka kwa kampuni ya Biashara ya Microsoft ambapo kanzidata hiyo hutumika kwa ajili ya kuhifadhia taarifa zote za kiutumishi pamoja na mishahara kwa watumishi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kwa mujibu wa sera ya makubaliano ya leseni za Microsoft (End User License Agreement - EULA), ili utumie kanzidata ni lazima Taasisi ilipie leseni ya matumizi, baada ya kulipiwa kanzidata inakuwa halali na kupatiwa ulinzi, usalama na udhibiti mkubwa kutoka kwa kampuni hiyo na kulinda taarifa zilizomo dhidi ya mashambulizi ya virusi, udukuzi n.k.

Ukaguzi umebaini kwamba database ya mfumo wa HR-Payroll Information System haina leseni ya matumizi licha ya kwamba imehifadhi taarifa muhimu za watumishi na Viongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa sasa kanzidata iliyoingizwa humo inatumia leseni ya majaribio tu ambayo haina muda mrefu wa matumizi na vile vile haina usalama wa kutosha. Hali halisi ya taarifa hizo ni kama inavyoonekana katika picha hapo chini:-

**Picha Nambari 1: Kanzidata ya toleo la majaribio ambayo inamaliza muda Januari, 2024**



| | SERVER NAME | INSTALLATION_DATE | VERSION | EXPIRY DATE |
|---|---|---|---|---|
| 1 | WIN-21I9HV0KO35\MSSQLSERVER2019 | 2023-07-26 23:36:06.640 | Enterprise Evaluation Edition (64-bit) | 2024-01-22 23:36:06.640 |

Hali hii inaweza kusababisha hatari ya upotevu wa taarifa za kiutumishi na mishahara kwa viongozi na watumishi wa umma ikiwa kanzidata itashambuliwa, kuharibiwa na virusi au kudukuliwa kupitia mitandao jambo ambalo litapelekea kuingiza hasara kubwa Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa OR-KSUUB kuhakikisha unafanya jitihada za makusudi za kununua leseni ya matumizi ya kanzidata ya mfumo wa HR-Payroll System ili kuziweka taarifa zake katika hali ya usalama dhidi ya hatari zilizopo.

#### 4.1.3.7 Kutofanyika kwa usanidi katika sehemu zinazoweka kumbukumbu za shughuli za watumiaji wa kanzidata ya Mfumo "database Audit logs"


Moja kati ya sehemu muhimu zinazopewa kipaombele cha udhibiti kwenye kanzidata ni sehemu ya kuhifadhi kumbukumbu za shughuli za watumiaji "database audit logs".

Sehemu hii hurikodi shughuli "activities" zote zinazofanywa na watumiaji wa kanzidata "database administrators and database users" ambapo hutumika kwa kuangalia ushahidi endapo tukio la kihalifu likifanywa kupitia kanzidata ya mfumo.

Ukaguzi ulifanya uhakiki wa kanzidata "database" ya mfumo wa HR-Payroll Information System na kubaini kwamba sehemu ya kuhifadhi "Audit logs" haijasanidiwa (not configured) kwa ajili ya kuchunguza na kuweka kumbu kumbu za matukio yanayofanyika ndani ya kanzidata.

Picha ifuatayo inaonesha kanzidata ya mfumo wa HR-Payroll Information System haijafanyiwa usanidi (not configured) katika sehemu ya Audit logs, kwa ajili ya kurekodi shughuli zote zinazofanyika ndani ya database.

**Picha Nambari 2: Kanzidata ya Mfumo wa HR-Payroll Information System haijasanidiwa kwa ajili ya kunasa Audit Logs**



Kutofanyika kwa usanidi wa kuweka kumbukumbu za uchunguzi kwa shughuli zinazofanyika katika kanzidata kunaweza kusababisha kukosekana kwa ushahidi wa kumtambua aliyehusika endapo ikitokezea kufanyika vitendo visivyokuwa na uadilifu moja kwa moja ndani ya kanzidata kama vile wizi, udukuzi, ufutaji wa taarifa bila ya idhini, ubadilishwaji wa data n.k.


Ukaguzi unaushauri uongozi wa OR-KSUUB kuhakikisha kanzidata ya mfumo wa HR-Payroll Information System inasanidiwa ili kuweza kuchunguza, kubaini matumizi halisi na kuweka kumbukumbu za shughuli zote zinazofanyika ndani yake na akaunti yoyote inayohusika kufanya shughuli hizo. Hali hii itasaidia kupatikana kwa ushahidi wa kubaini tarehe, muda na akaunti iliyotumika kufanya kitendo kisichokuwa na uadilifu ndani ya kanzidata hiyo.

Aidha, katika kuongeza usiri, uadilifu na usalama wa kulinda taarifa za kiutumishi Ukaguzi unaushauri uongozi wa OR-KSUUB kuhakikisha unamuandaa mtu pekee atakaetunza, kusimamia na kuzifikia taarifa za uchunguzi zilizo ndani ya kanzidata za mifumo "database audit logs" ili kuepusha kuchezewa, kufutwa au kuharibiwa na wasiokuwa waadilifu.

### 4.1.3.8 Kukosekana kwa usalama katika Seva inayoendesha Mfumo wa HR-Payroll Information System (Application Server)

Ukaguzi umebaini kompyuta aina ya Seva ambayo imeingizwa Mfumo wa HR-Payroll Information System haiko salama kiutendaji "Vulnerable" kutokana na kubainika kuwa haina leseni katika "Window Operating System". Vile vile imebainika haina programu ya kuzuwia mashambulizi ya virusi, programu hatarishi na udukuzi "antivirus software" licha ya kuwa kompyuta hiyo imeungwa na mtandao wa Internet. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika picha hapo chini:-

**Picha Nambari 3 : Mapunfugu ya usalama katika Seva ya Mfumo wa HR – Payroll Information System haiko salama**




*Seva yenye mfumo wa HR-Payroll System ambayo haina leseni ya Window Operating System, badala yake inatumia ya Window ya majaribio tu, vile vile ina ujazo mdogo wa nafasi, haina antivirus na inatumia internet*

Aidha, imebainika kuwa Seva hiyo ina ujazo mdogo wa nafasi ya kuendesha mfumo wa HR-Payroll Information System kulingana na mahitaji ya mfumo wenyewe (System Requirement Specification) ambapo kwa kiasi kikubwa imesababisha mfumo kuwa na kasi ndogo ya utendaji kazi "slow performance" kwa vile mfumo huo unatumika takriban Taasisi zote za SMZ. Vile vile hali hii imepelekea baadhi ya taarifa kushindwa kuhifadhiwa kwa ufanisi ndani ya kanzidata za mfumo kama vile taarifa za application logs.

Kuwepo kwa usalama mdogo wa Seva hiyo kunaweza kusababisha hatari kubwa ya mfumo wa HR-Payroll Information System kupata mashambulizi ya virusi, udukuzi, utendaji mdogo wa kazi na hatari nyengine zisizojulikana jambo ambalo litapelekea mfumo kuharibika na hatimae kuingiza hasara Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa OR-KSUUB kufanya jitihada za kuhakikisha Seva hiyo inaekewa leseni halisi "Original Window license" katika mfumo wa uendeshaji "Operating System" na vile vile inaingizwa programu ya kusaidia kuzuwia mashambulizi na hatari mbali mbali zinazotokana mashambulizi ya mitandao kama vile virusi, udukuzi n.k. na pia kuongeza uwezo ili iweze kufanya kazi kwa ufanisi.

#### 4.1.3.9 Dosari za kiusalama zilizobainika katika Chumba cha Mitambo (Server Room)

Ukaguzi ulitembelea katika chumba cha Mitambo (Server Room) cha OR-KSUUB Unguja kilichopo katika ghorofa ya sita ambapo chumba hicho vile vile hutumika kusimamia na kuendesha mitambo ya kamera za ulinzi (CCTV Camera) zilizofungwa kwa ajili ya kuweka usalama wa Afisi. Katika chumba hicho ukaguzi umebaini uwepo wa dosari mbali mbali kama zifuatazo:-

- Mitungi ya kuzimia moto (fire extenguishers) imekwisha muda wa matumizi (expired).
- Mfumo wa kugundua na kutoa ishara ya hatari ikiwa khitilafu za moto zikitokea katika jengo haufanyi kazi "Addressable Smoke & Heat Detector and Fire Alarm System".
- Kipooza Hewa (Air Condition) kilichomo ndani ya chumba cha Seva hakifanyi kazi vizuri kutokana na kutofanyiwa "service" kwa muda mrefu.
- Kutokuwepo kwa kifaa cha usalama kinachodhibiti uingiaji wa watu mlangoni (door security device).

Hivyo, kuwepo kwa dosari za kiusalama zilizotajwa hapo juu kunaweza kusababisha upotevu wa taarifa na uharibifu wa mifumo na miundombinu ya Afisi iliyowekwa ndani ya chumba hicho.

**Aidha, kwa upande wa CCTV kamera** katika jengo la OR-KSUUB lenye ghorofa nane (8) ukaguzi umebaini kati ya kamera (16) zilizofungwa, kamera (11) zinaonesha na kamera (5) hazioneshi kutokana na changamoto mbali mbali.

Hata hivyo ukaguzi umebaini mtambo wa kuhifadhia kumbukumbu za matukio (NVR) yanayorikodiwa na CCTV kamera haufanyi kazi, kwa hivyo hakuna rikodi yoyote inayoingizwa katika mtambo huo licha ya kwamba kamera 11 zinaonesha. Jadweli lifuatalo linaonesha idadi ya kamera zilizofungwa na hali halisi ya utendaji kazi:-

## Jadweli Nambari 31: Idadi ya Kamera zilizofungwa na Afisi

| Eneo Husika | Idadi ya Kamera zilizofungwa | Idadi ya kamera zinazofanya kazi | Idadi ya kamera zisizofanya kazi |
|---|---|---|---|
| Nje ya jengo la Afisi | 7 | 4 | 3 |
| Ground Floor | 4 | 3 | 1 |
| 1st Floor – 5th Floor | 0 | 0 | 0 |
| 6th Floor | 5 | 4 | 1 |
| 7th Floor – 8th Floor | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla ya Kamera** | **16** | **11** | **5** |

Kwa mujibu wa jadweli hapo juu kunaonesha kwamba idadi ya kamera zinazofanya kazi ni kidogo kulinganisha na ukubwa wa jengo ambapo baadhi ya ghorofa hazijafungwa kamera, kwa mfano ghorofa ya kwanza hadi ya tano, na ghorofa ya saba hadi ya nane.

Vile vile ukaguzi umebaini ufungaji wa kamera haukuzingatia vipaombele vya usalama wa maeneo waliopo Viongozi Wakuu wa Afisi katika jengo hilo, kwa mfano afisi za Mhe. Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na baadhi ya Wakurugenzi zipo katika ghorofa ya nne (4) lakini hakuna kamera iliyofungwa kwenye ghorofa hiyo kwa ajili ya kuangalia usalama wao endapo tatizo lolote likitokea dhidi yao.

Kutofanya kazi kwa kamera za Afisi kunaweza kusababisha kukosekana kwa ushahidi endapo tukio lolote la wizi, uhalifu au uharibifu likitokea katika Afisi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa OR-KSUUB kuimarisha dosari zote zilizotajwa hapo juu zinazohusu CCTV kamera na chumba cha Mitambo ili kuongeza usalama, ulinzi na utendaji kazi wa vifaa vilivyomo katika chumba cha Mitambo kwani chumba hicho ni muhimu sana katika kusimamia na kuendesha mifumo na miundombinu ya Afisi.

Aidha, Ukaguzi unaushauri uongozi wa Afisi kufanya jitihada za makusudi za kutengeneza au kubadilisha mtambo wa kuhifadhia kumbukumbu za matukio ya CCTV kamera na vile vile kuongeza idadi ya ufungaji wa kamera hususan katika ghorofa ya nne (4) ambayo viongozi wakuu wa Ofisi wapo hapo.

### 4.1.4 MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU UCHUMI ZANZIBAR (ZAECA)

Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA) kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 4.1.4.1 Kukosekana kwa Mkataba wa Viwango vya Huduma (SLA Agreement) baina ya ZAECA, ZICTIA na TTCL

Mkataba wa Viwango vya huduma ni aina ya mkataba unaowekwa kati ya mtoa huduma na mteja, ukielezea viwango vya utendaji na ahadi zinazohusiana na utoaji wa huduma fulani.

Mkataba huu hua ni chombo cha kusimamia na kuhakikisha ubora wa huduma ambapo pande zote mbili zinakubaliana juu ya viwango maalum vya utendaji, mara nyingi vikiwa na vigezo vya kiufundi, muda wa kurekebisha matatizo (downtime), na mambo mengine yanayohusiana na huduma inayotolewa. Viwango vya Utendaji, Muda wa Ufikiaji (Downtime) Maelezo ya Huduma, Malipo na Adhabu, Muda wa Mkataba, Mchakato wa Kupima Utendaji.

Aidha ukaguzi uliofanyika ulibaini ZAECA haina Mkataba wa viwango vya huduma na Watoa huduma wao ambao ni ZICTIA na TTCL jambo ambalo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 4.3, nambari 4.1.6 na 4.1.7 cha Viwango bora vya kimataifa (Best Practice) ISO/IEC 20000 vinavyoelekeza uwepo wa Mkataba wa viwango vya huduma (SLA agreement) katika Huduma za TEHAMA kwenye Mashirika na Taasisi mbali mbali.

Kutokuwepo kwa Mkataba wa Viwango vya Huduma (SLA) kunaweza kuwa na athari mbali mbali haswa kwa wateja na watoa huduma, ikijumuisha kutokuwa na uhakika wa viwango vya utendaji, migogoro ya kuelewa vigezo vya huduma, kutokuwa na malalamiko yanayoweza kushughulikiwa kisheria pamoja na kutokuwa na kipimo wazi cha utendaji wa huduma fulani.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAECA kuhakikisha unaandaa utaratibu wa upatikanaji wa Mkataba wa Viwango vya huduma (SLA Agreement) kutoka kwa watoa huduma wake wote.

#### 4.1.4.2 Kutozingatiwa kwa Utaratibu wa Utengenezaji wa Mifumo ya TEHAMA (Software Development Life Cycle)

"Software Development Life Cycle – SDLC" ni mchakato wa kina unaotumika katika utengenezaji wa Programu za TEHAMA ambapo utaratibu huu wakitaalamu unajumuisha hatua tofauti ambazo hufuatwa kipindi cha uanzishwaji mpaka kumalizika kwa Mfumo husika.

Lengo kuu la SDLC ni kutengeneza mfumo unaokidhi matarajio ya watumiaji, kusaidia kutengeneza na kukamilisha Programu kwa wakati na bajeti iliyokusudiwa huku ikizingatia ubora wa mfumo husika.

Aidha, ukaguzi ulibaini kwamba utengenezaji wa mfumo wa "Case Distribution System" haukuzingatia utaratibu na mbinu za "SDLC" kwa sababu ya kukosekana kwa nyaraka mbalimbali zilizotakiwa kuwepo kama ushahidi wa kuzingatiwa kwa "SDLC".

Hali hii inakwenda kinyume na matakwa ya viwango bora kubalifu (Best practice) ISO/IEC 12207:2017 kifungu nambari 7-24, kinachozungumzia utaratibu uliobora katika hatua za utengenezaji wa Mifumo ya TEHAMA katika Taasisi, ili kuhakikisha utekelezaji ulio bora na wa uhakika wa utengenezaji wa Mifumo ya TEHAMA.

Miongoni mwa hatua za Msingi za Utengenezaji wa Mifumo ya TEHAMA ambazo hazikuzingatiwa wakati wa utengenezwaji wa Mfumo wa Case Distribution System ni pamoja na: -

- Uchambuzi na Mahitaji ya watumiaji (Requirements Analysis).
- Ubunifu wa Mfumo (System Design).
- Upimaji/ Majaribio ya Mfumo (System Testing).
- Uwasilishaji wa Mfumo (System Deployment).
- Uendeshaji na Matengenezo (Operation and Maintenance).

Kutozingatiwa kwa hatua za Kitaalamu za utengenezwaji wa Mifumo ya TEHAMA (SDLC) kunachukuwa sehemu kubwa ya kuwa ni chanzo cha matatizo na changamoto mbali mbali za mifumo ya TEHAMA ikiwemo: -

- Ucheleweshwaji wa kukamilika kwa mifumo ya TEHAMA.
- Ubora hafifu wa mifumo ya TEHAMA inayotengenezwa.

- Mifumo kutengenezwa kwa gharama kubwa zaidi ya uhalisia wake.
- Mifumo kutokukidhi mahitaji ya watumiaji.
- Kutokufikiwa kwa malengo ya Serikali katika uwekezaji kwenye TEHAMA.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAECA kuhakikisha unazingatia taratibu za utengenezwaji wa mifumo ya TEHAMA kama vile "Software Development Life Cycle (SDLC), Project Development Life Cycle (PDLC)" n.k ili kuisadia Serikali kufikia malengo ya uwekezaji kwenye TEHAMA ambayo ni kuongeza tija, ufanisi, uwazi na uwajibikaji kwa wakati.

Aidha, katika mfumo huo uliotengenezwa, ukaguzi unashauri kuandaliwa kwa nyaraka zake zote muhimu kama vile nyaraka ya mahitaji, nyaraka ya usanidi, nyaraka ya namna mfumo unavyofanya kazi (operations manual), n.k na kwamba nyaraka hizo zipatikane kwa ajili ya ukaguzi.

### 4.1.4.3 Mapungufu yaliobainika katika chumba cha Seva (Server Room)

Chumba cha Seva ni eneo maalum ambalo hutumiwa kuhifadhi na kusimamia vifaa vya kompyuta na miundombinu inayosaidia utoaji wa huduma za mtandao, uhifadhi wa data, na mifumo mengine muhimu katika Mamlaka au biashara.

Katika kufanya ukaguzi wa mifumo ya TEHAMA ya ZAECA ukaguzi ulibaini uwepo wa mapungufu mbali mbali yakiwemo kukosekana kwa mfumo wa kuzima moto, kuharibika kwa UPS inayotumika kuimarisha ulinzi juu ya mabadiliko ya umeme katika Vifaa ndani ya Seva, kutokuwepo kwa daftari la kusajili watu wanaoingia kwenye chumba cha Seva, kutokuwepo kwa kamera za ulinzi, udhaifu wa udhibiti kupitia geti/ mlangoni, kutokuwepo kwa mashine ya "Biometric" kwa ajili ya kuchukuwa kumbukumbu za watu wanaoingia, Maelezo ya kina ya dosari hizo ni kama ifuatavyo:-

**a) Kukosekana kwa mfumo wa kiautomatiki wa kuzima moto (Fire Suppression System) katika chumba cha Seva**

Ukaguzi ulibaini ZAECA kutokua na Mfumo wa dharura wa kuzima Moto katika Chumba cha Seva kilichopo ndani ya Mamlaka hiyo jambo ambalo ni kwenda kinyume na Matakwa ya Miongozo na Viwango vya kimataifa vya TEHAMA wa ISO 9001 (Fifth edition 15/9/2015) katika kifungu nambari 5.15, ambacho kinasisitiza uhitaji wa utaratibu wa udhibiti wa taarifa ili kulinda vifaa na mifumo ya TEHAMA inayohifadhiwa katika Seva na kuweza kufanya kazi hiyo

kwa masaa 24 kwa siku zote za wiki.

Kukosekana kwa mfumo wa kuzima moto katika chumba cha Seva kunaweza kusababisha hatari kwa vifaa, miundombinu na taarifa zilizo ndani ya chumba Seva kama vile ongezeko la joto na kusababisha mripuko wa moto, kuharibika kwa miundombinu na kukosa huduma, kuongezeka kwa gharama za matengenezo baada ya kutokea kwa moto n.k.

Ukaguzi unaushauri viongozi ea ZAECA Kuweka Mfumo wa kuzima moto wa kiautomatiki (fire suppression system) katika chumba cha Seva ili kuweza kulinda vifaa na mifumo ya TEHAMA inayohifadhiwa.

**b) Kutokuwepo kwa daftari la kusajili watu wanaoingia katika chumba cha Seva**

Ukaguzi ulibaini kukosekana kwa Daftari la kuweka rikodi za Watu wanaingia na kutoka katika chumba cha Seva, hali hii inaenda kinyume na viwango kubalifu vya kimataifa vya TEHAMA vinavyohitaji uwepo wa daftari maalum litakalotumika kwa ajilli ya kurikodi watu watakaoingia na kutoka katika chumba cha Seva kwa ajili ya usimamizi mzuri na udhibiti wa chumba cha Seva.

Kukosekana kwa Daftari la kuhifadhia watu wanaoingia na kutoka katika chumba cha Seva kunaweza kusababisha kushindwa kudhibiti na kufahamu aina ya watu wanaoingia na kutoka katika eneo hilo, muda pamoja na shughuli wanazofanya hali ambayo inaweza kuhatarisha usalama wa rasilimali zilizomo ndani yake.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAECA kuweka utaratibu imara kwa kuweka kumbukumbu za wanaoingia na kutoka katika chumba cha seva pamoja na kufuatilia shughuli wanazofanya ndani ya chumba hicho ili kuhakikisha kunakuwepo kwa usalama wa taarifa na miundombinu iliyomo.

**c) Udhaifu wa udhibiti wa Mlango wa chumba cha Seva kilichopo ZAECA (Absence of reinforced Door)**

Ukaguzi ulibaini ZAECA kutokuweka ulinzi wa kutosha katika Mlango wa kuingilia katika chumba cha Seva hali ambayo ni kinyume na Matakwa ya kifungu nambari 2.9.2.1 cha Muongozo wa utengenezaji wa Sera ya Ulinzi wa TEHAMA katika Afisi za Umma kutoka Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar eGAZ unaoelekeza kwamba kuwepo na udhibiti imara wa uingiaji katika vyumba vya kuhifadhia Mitambo kwa lengo la kuboresha Usalama.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAECA kuweka mlango wa geti la chuma katika chumba cha Seva pamoja na kuboresha madirisha ya chumba hicho kwa ajili ya kulinda na kudhibiti rasilimali zilizopo katika chumba hicho dhidi ya vihatarishi vinavyoweza kusababisha upotevu wa vifaa, taarifa pamoja na mifumo.

**d) Kutokuwepo kwa kifaa cha kusimamia kumbukubu za wanaoingia na kutoka katika chumba cha Seva (biometric door security device)**

Kwa mujibu wa muongozo na viwango kubalifu vya kimataifa vya TEHAMA wa ISO 9001 (Fifth edition 15/9/2015) katika kifungu nambari 7.1, 7.2, 7.3 inasisitiza uhitaji wa udhibiti wa taarifa katika sehemu za Afisi, vyumba, juu ya uwekaji wa kifaa maalum cha kuchukua kumbukumbu ya watu wanaoingia na kutoka katika chumba cha Seva, kwani kufanya hivyo kunasaidia udhibiti na usalama wa juu katika upatikanaji na ufikiaji wa mifumo na vifaa katika chumba cha Seva.

Kukosekana kwa kifaa hicho kunaweza kupelekea Mamlaka kushindwa kupata kumbukumbu sahihi za waliongia na kutoka katika chumba hicho ili kuweza kusaidia katika kufuatilia matumizi na kubaini matendo yasiyo ya kawaida.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAECA kuweka mashine ya Biometric ili kusaidia udhibiti na usalama katika upatikanaji na ufikiaji wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA katika chumba hicho.

### 4.1.4.4 Udhaifu wa udhibiti wa ufikiaji na mgawanyo wa majukumu ndani ya Mfumo wa usimamizi wa Kesi (Access control)

Miongozo ya Wakala wa Serikali Mtandao, 2022 (ICT Gudelines 2022) kifungu nambari 4.1, pamoja na kifungu nambari 3.4.4.7 cha Sera ya TEHAMA ya Taifa Zanzibar, ambacho kinazitaka Mamlaka za Umma kutengeneza utaratibu wa udhibiti wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA kwa watumiaji kwa lengo la kudumisha Usalama, Usiri, Uadilifu wa taarifa za Serikali pamoja na upatikanaji wa mifumo.


Ukaguzi ulibaini kwamba Mfumo wa Usimamizi wa Kesi (Case Distribution Sysytem) wa ZAECA una udhibiti duni wa ufikiaji katika makundi ya watumiaji wake ambapo kundi la watumiaji wa kawaida (Information Center Officer) wamepatiwa uwezo mkubwa wa ufikiaji wa Moduli zote zinazowawezesha watumiaji hao kuingiza taarifa za aina zote katika mfumo, kuona taarifa mbalimbali katika mfumo, kusanidi pamoja na kufuta taarifa mbali mbali ndani ya Mfumo huo. Hivyo kundi hili ni la "super users" ambalo linaweza kukamilisha hatua zote bila ya kumuhusisha mtu mwengine katika ngazi tofauti za uongozi wa Mamlaka.

Udhibiti duni wa ufikiaji wa mfumo, hususan mfumo wenye taarifa nyeti kama huu unaweza kupelekea kuwepo kwa dosari mbali mbali kwa Mamlaka na Serikali kwa ujumla, miongoni mwa hizo ni pamoja na: -

- Kuondoa Usiri unaotakiwa kuwepo katika taarifa mbali mbali zinazohusiana na kesi za Rushwa na uhujumu uchumi.
- Kuhatarisha Uadilifu wa taarifa za Kesi pamoja na mienendo yake katika hatua mbali mbali za upatikanaji wa haki kwa watuhumiwa.
- Kudhoofisha hali ya upatikanaji wa mfumo husika pamoja na usalama wa taarifa zilizomo.

Hali halisi ya utumiaji ya mfumo inayoonesha mtumiaji wa kawaida kupewa uwezo wa kuzifuta modeli zote ni kama inayoonekana katika picha ifuatayo:-

**Picha Nambari 4: Mfumo wa Usambazaji wa Kesi ukionesha Afisa wa Kitengo cha IC (Information Center) kufikia katika Moduli zote za Mfumo**




Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAECA kuzingatia mgawanyo wa majukumu na makundi ya watumiaji katika kufikia moduli mbali mbali za Mfumo na kuhakikisha kwamba hakuna mtu mmoja mwenye ufikiaji wa maeneo yote ya mfumo ili kuimarisha Usiri, Uadilifu, na Usalama wa taarifa mbali mbali za Kesi zinazohusiana na Rushwa na Uhujumi Uchumi.

Aidha, ili kuhakikisha kuwa mfumo unazingatia uwazi na uwajibikaji Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAECA kutengeza makundi ya watumiaji yanayowahusisha viongozi wa Mamlaka ambao pia watapatiwa ufikiaji katika mfumo ili waweze kuona na kupata taarifa zote kupitia ripoti mbali mbali kwenye mfumo.

### 4.1.4.5 Dosari ya kiusalama katika Uhifadhi wa Mfumo wa Usambaziji Kesi

Ukaguzi ulibaini kuwa Mfumo wa Usambazi Kesi umehifadhiwa katika Kompyuta ya Mamlaka kama Seva, hata hivyo Kompyuta hiyo inatumiwa na mmoja wa maafisa wa ZAECA kama kitendea kazi chake katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na miongozo ya viwango bora kubalifu vya TEHAMA (best practice) ambayo kwa sababu za kiusalama ambazo ni njia muhimu za kuhakikisha taarifa za Serikali zinaendelea kubaki na Usiri, Uadilifu na kupatikana muda wote inatakiwa Kompyuta/ Seva inayotumika kuhifadhi mifumo ya TEHAMA kuwekwa katika mazingira salama kama vile chumba cha Seva (Sever Room) ambayo yanaudhibiti wa ufikiaji unaohakikisha kila anayefikia vifaa hivyo (Kompyuta/ Seva) anafahamika muda wote na kuhifadhiwa kwa kumbu kumbu za alichofanya kupitia "audit trails/ logs" mazingira ambayo ZAECA haijaweka katika Kompyuta inayotumika kuhifadhi mfumo wa "Case Distribution".

Aidha, hali hii inaweka rehani Usiri, uadilifu na upatikanaji wa taarifa nyeti za kesi mbali mbali zinazohusu wahalifu na watuhumiwa wa masuala ya rushwa na uhujumu uchumi jambo ambalo linaweza kupelekea kuchelewesha au kukwamisha juhudi na jitihada za Serikali katika kupambana na Rushwa na Uhujumu Uchumi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAECA kuchukuwa hatua za makusudi za kuboresha mazingira ya TEHAMA katika Mamlaka ikiwemo upatikanaji wa Seva maalum itakayotumika kwa ajili ya kuhifadhi mifumo mbali mbali ya TEHAMA ya Mamlaka na kuhakikisha kwamba Seva hiyo inawekwa katika chumba maalumu cha Seva (Server Room) ambacho kitazingatia matakwa ya kiusalama, utendaji, usiri, uadilifu na upatikanaji wa mifumo katika ngazi ya Taifa na Kimataifa (best practice).

#### 4.1.4.6 Malipo ya ziada yaliyofanyika kwa wazabuni kupitia mfumo wa eProz shilingi 13, 883,600

Ukaguzi ulifanya mapitio ya taratibu za manunuzi yaliyofanywa na ZAECA kupitia mfumo wa eProz na kubaini zaidi ya asilimia 34 ya Zabuni za "Minor Value" zilitolewa na ZAECA kwenda kwa wasambazaji (suppliers) kwa ajili ya malipo ya huduma mbali mbali.

Ukaguzi ulibaini uwepo wa dosari katika mchakato wa manunuzi yaliyofanyika ikiwemo ukiukwaji wa taratibu za manunuzi ambapo ni kinyume na Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016. Baadhi ya dosari zilizobainika ni kama zifuatazo:-

a) Utoaji wa Zabuni kwa waombaji "biders" waliokuwa na bei za juu zaidi na kuwaacha waombaji waliokuwa na bei ndogo ambao walichaguliwa na mfumo na kuwekwa katika nafasi 3 bora (3 Lowest biders) bila ya kuwepo kwa sababu za msingi zenye ushahidi.

b) Mfumo wa eProz kushindwa kutumika katika kutoa taarifa za matokeo kwa waombaji zabuni hususan kwa wazabuni ambao hawakuchaguliwa (hawakushinda zabuni) ya kusambaza bidhaa zilizohitajika ili kuweka kumbu kumbu na ushahidi wa kutoridhishwa na uwezo pamoja na vigezo vyao kabla ya kuwanyima zabuni husika.

Hivyo, kutokana na dosari zilizopo hapo juu, tathmini iliyofanyika imebainisha ZAECA imefanya malipo ya ziada ya shilingi 13,883,600 kwa zabuni 15 kati ya zabuni 41 zilizofanyiwa tathmini bila ya kuzingatia matakwa ya Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma pamoja na matakwa ya mfumo wa eProz. Hali halisi ya taarifa za malipo ya ziada yaliyofanyika ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 32: Zabuni zilizotolewa kwa watoa huduma ambao bei zao ni kubwa ukilinganisha na watoa huduma waliochaguliwa na mfumo wenye bei nafuu**

| Namba | Nambari ya Zabuni | Gharama halisi za mzabuni mwenye bei ndogo kwa mujibu wa mfumo (TZS) | Gharama za aliyepewa tuzo ya zabuni (TZS) | Nafasi ya aliyepewa tuzo ya zabuni kwa mujibu wa mfumo | Ziada ya fedha (TZS) | Asilimia ya ziada (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | rfq_22651 | 150,000 | 212,000 | 4 | 62,000 | 29.25 |
| 2. | rfq_22649 | 148,000 | 210,000 | 3 | 62,000 | 29.52 |
| 3. | rfq_22648 | 596,500 | 707,500 | 2 | 111,000 | 15.69 |
| 4. | rfq_22503 | 5,015,000 | 11,512,100 | 4 | 6,497,100 | 56.44 |
| 5. | rfq_18233 | 4,761,000 | 5,475,000 | 2 | 714,000 | 13.04 |
| 6. | rfq_16914 | 385,000 | 591,000 | 5 | 206,000 | 34.86 |
| 7. | rfq_16900 | 2,457,000 | 2,700,000 | 3 | 243,000 | 9.00 |
| 8. | rfq_12147 | 1,600,000 | 2,450,000 | 2 | 850,000 | 34.69 |
| 9. | rfq_10830 | 800,000 | 850,000 | 2 | 50,000 | 5.88 |
| 10. | rfq_22540 | 600,000 | 1,680,000 | 5 | 1,080,000 | 64.29 |
| 11. | rfq_22270 | 4,277,000 | 7,880,000 | 5 | 3,603,000 | 45.72 |
| 12. | rfq_16578 | 1,800,000 | 2,200,000 | 2 | 400,000 | 18.18 |
| 13. | rfq_22245 | 210,500 | 216,000 | 2 | 5,500 | 2.55 |
| **Jumla** | | **22,800,000** | **36,683,600** | | **13,883,600** | |

Kufanyika kwa malipo ya ziada kunaweza kusababisha hasara kwa Serikali kutokana na upotevu wa fedha unaotokana na kutozingatiwa kwa Sheria na taratibu za manunuzi kupitia mfumo wa kielektroniki wa eProz. Vile vile kunaweza kusababisha dosari zifuatazo:-

- Kuondoa imani kwa wazabuni kutokana na kutopatiwa taarifa zozote kwenye mfumo kuhusiana na zabuni walizoomba ikiwa wamekosa na sababu zilizowafanya kukosa zabuni hizo.
- Kukosekana kwa tija na kupunguza ufanisi wa ununuzi na uondoshaji wa mali za umma kwa sababu ya kutozingatia taratibu zilizowekwa kupitia mfumo wa eProz.
- Kuongeza gharama kwa Serikali na kuisababishia Serikali hasara kwa kufanya manunuzi ya bidhaa na huduma kwa bei za juu zaidi ya uhalisia wa soko.
- Kuchochea mazingira ya rushwa hususan katika mazingira ambayo wazabuni wenye bei ndogo wasipopatiwa zabuni na badala yake kupewa wazabuni wenye bei za juu zaidi.

Vile vile jadweli hapo chini linaonesha taarifa nyengine ya mzabuni ambae amechaguliwa na kupewa tuzo ya zabuni kwa thamani ya shilingi 14,880,000 kwa ajili ya kusambaza huduma kwa ZAECA lakini nafasi yake kwa mujibu wa orodha ya mfumo ni mtu wa kumi na sita (16) kulingana na bei za zabuni zilizowasilishwa ambapo mzabuni mwenye bei ndogo alikuwa ni shilingi 7,636,000. Ukaguzi haukupatiwa ushahidi wa vigezo vilivyotumika kumpata mzabuni huyo.

Hali halisi ya mchakato wa zabuni ni kama inavyoonekana katika picha hapo chini:-

## Jadweli Nambari 33: Kukosekana kwa vigezo vilivyotumika kumpata mzabuni wa 16 na kuwaacha wazabuni wa nafasi za awali wenye bei nafuu.

**AWARDING DECISION: Awarded**

| Rank | Supplier | Awarding Decision | Total Price | Confirmed Price |
|---|---|---|---|---|
| 1 | MULTI HOME FURNITURE | | 7,636,000 | 7,636,000 |
| 2 | TRINITY GENERAL SUPPLIES | | 7,751,000 | 7,751,000 |
| 3 | ZAN PRINTINGS | | 7,830,000 | 7,830,000 |
| 4 | AMO COMPUTER SERVICES | | 8,336,000 | 8,336,000 |
| 5 | New Home Furniture | | 9,030,000 | 9,030,000 |
| 6 | AKHAKAMU GENERAL SUPPLIES COMPANY LIMITED | | 9,920,000 | 9,920,000 |
| 7 | SAMOI TRADER & GENERAL SUPPLY COMPANY LIMITED | | 10,112,000 | 10,112,000 |
| 8 | SALEH DECORATION | | 10,374,000 | 10,374,000 |
| 9 | Storatoet General Supply | | 11,720,000 | 11,720,000 |
| 10 | KADON COMPANY LIMITED | | 12,319,200 | 12,319,200 |
| 11 | Z & M (T) GENERAL TRADERS LIMITED | | 12,430,000 | 12,430,000 |

Page 53 of 59

Report run from: Report Area, at: 22/12/2023 12:10

| Rank | Supplier | Awarding Decision | Total Price | Confirmed Price |
|---|---|---|---|---|
| 11 | DILAIYA PRINTING AND GENERAL SUPPLIES | | 12,430,000 | 12,430,000 |
| 12 | ABRAS GENERAL TRADER | | 13,420,000 | 13,420,000 |
| 13 | KICHAN GENERAL SUPPLIERS COMPANY LIMITED | | 13,908,000 | 13,908,000 |
| 14 | 4 PEOPLE GENERAL SUPPLIER | | 14,038,000 | 14,038,000 |
| 15 | DREAM LINER GENERAL TRADERS LIMITED | | 14,330,000 | 14,330,000 |
| 16 | F & AS EQUIPE AND GENERAL | Awarded | 14,880,000 | 14,880,000 |

**Picha Nambari 5: Wazabuni ambazo wamekosa tuzo ya zabuni na hawakupewa taarifa ya sababu ya kukosa kupitia mfumo kwenye zabuni ya RFQ_2637**

Showing Result 1 - 21 of 21

RFQ: rfq_26437 - UNUNUZI WA MEZA NA VITI KWA AJILI YA OFISI YA ZAECA

| RANKING | | SUPPLIER | | TOTAL PRICE | CONFIRMED PRICE | COMMERCIAL |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 16 | | F & AS EQUIPE AND GENERAL | 0 | 14,880,000 | 14,880,000 | Accepted |
| 1 | | MULTI HOME FURNITURE | 0 | 7,636,000 | 7,636,000 | Accepted |
| 2 | | TRINITY GENERAL SUPPLIES | 0 | 7,751,000 | 7,751,000 | Accepted |
| 3 | | ZAN PRINTINGS | 0 | 7,830,000 | 7,830,000 | Accepted |
| 4 | | AMO COMPUTER SERVICES | 0 | 8,336,000 | 8,336,000 | Accepted |
| 5 | | New Home Furniture | 0 | 9,030,000 | 9,030,000 | Accepted |
| 6 | | AKHAKAMU GENERAL SUPPLIES COMPANY LIMITED | 0 | 9,920,000 | 9,920,000 | Accepted |
| 7 | | SAMOI TRADER & GENERAL SUPPLY COMPANY LIMITED | 0 | 10,112,000 | 10,112,000 | Accepted |
| 8 | | SALEH DECORATION | 0 | 10,374,000 | 10,374,000 | Accepted |
| 9 | | Storetoet General Supply | 0 | 11,720,000 | 11,720,000 | Accepted |
| 10 | | KADON COMPANY LIMITED | 0 | 12,319,200 | 12,319,200 | Accepted |
| 11 | | DILAIYA PRINTING AND GENERAL SUPPLIES | 0 | 12,430,000 | 12,430,000 | Accepted |
| 11 | | Z & M (T) GENERAL TRADERS LIMITED | 0 | 12,430,000 | 12,430,000 | Accepted |

Ukaguzi unaushauri Uongozi wa ZAECA kuhakikisha kwamba unasimamia kitengo cha Manunuzi kwa karibu na kuhakikisha kwamba taratibu za Manunuzi zinazingatiwa muda wote katika aina zote za manunuzi kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo ya manunuzi.

Aidha, kwa upande wa matumizi ya mfumo wa e-Proz ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAECA kuhakikisha kwamba unawawezesha watumishi wa Kitengo cha manunuzi kwa kupatiwa mafunzo stahiki katika baadhi ya maeneo ambayo hawana uelewa wa kutosha ili waweze kuutumia mfumo ipasavyo na kuepuka kufanya malipo ya ziada yatakayosababisha hasara kwa Serikali.

### 4.1.4.7 Kutokushindanishwa kwa watoa huduma mbalimbali kwenye Zabuni ya Ununuzi wa Huduma ya Chakula nambari RFQ_21374 yenye thamani ya shilingi 45,360,000

Ukaguzi ulibaini kwamba ZAECA haikuwaalika watoa huduma mbalimbali katika zabuni ya Ununuzi wa Huduma ya Chakula kupitia Zabuni nambari RFQ_21374 ya tarehe 07/06/2023 ambapo Kampuni ya 2R&2N Supplier ndio pekee iliyoalikwa kushiriki katika Zabuni hiyo kinyume na Sheria namabri 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 na Kanuni zake.

Ukiukwaji wa taratibu za manunuzi unaweza kupelekea uwepo wa mianya ya rushwa na uhujumu uchumi na kuisababishia Serikali hasara kwa kununua bidhaa au huduma kwa bei kubwa zisizokuwa na ushindani.

Kudhoofisha uchumi kwa kuondoa ushindani na mzunguko wa fedha kwa kupunguza wafanya biashara ambao hawapati kazi kama hiyo ya Zabuni ya kutoa huduma ya chakula.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAECA kusimamia kitengo cha Manunuzi kwa karibu na kuhakikisha kwamba watumishi wanazingatia matakwa ya Sheria na Kanuni za Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ili kufanya manunuzi yenye tija katika matumizi ya fedha za Serikali na kupunguza gharama zisizo za lazima kwa Serikali kupitia ushindani wa wazabuni na watoa huduma mbali mbali watakao wezesha kupatatikana bei shindani ambazo ni himilivu kwa Serikali.

#### 4.1.4.8 Upatikanaji hafifu wa mfumo wa manunuzi wa kielektroniki (eProz) katika mtandao wa ZAECA

Ukaguzi ulibaini kwamba mfumo wa eProz haupatikani kupitia mtandao wa ZAECA katika mazingira ya Makao Makuu ya Afisi, ambapo ukaguzi uliweza kugundua chanzo kikuu cha tatizo la kutokupatikana kwa mfumo wa eProz kupitia mtandao wa Afisi ni kuwepo kwa matumizi makubwa ya "bandwith" yanayofikia kikomo cha "bandwith" iliyolipiwa (20Mbps) na ZAECA kutoka ZICTIA yakiwa ni sababu kuu ya kukwamisha ufikiaji wa mfumo wa eProz.

Aidha, ukaguzi uliweza kufanya tathmini ya matumizi ya "internet" na kubaini kwamba ZAECA haijaweza kuzuia matumizi katika "sites" zisizokuwa na tija na zenye vihatarishi vya usalama wa taarifa za kompyuta kama vile Torrent, Netflix, Ticktok, adult sites, gambling site, download sites n.k ambazo kwa kawaida hutumia "Bandwith" kubwa na kunyima Programu nyengine kufanya kazi wakati wa masaa ya kazi.

Kukosekana kwa leseni za udhibiti na usalama katika kifaa cha ulinzi wa mawasiliano ya mtandao (sophos firewall) kunaweza kupunguza ufanisi wa Kitengo cha Manunuzi katika matumizi ya mfumo wa manunuzi (eproz)

Vile vile kuongezeka kwa gharama binafsi kwa watumishi kutokana na watumishi kutumia simu zao za mkononi kwa ajili ya kupata huduma za Internet na kuweza kuufikia mfumo wa eProz.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAECA kufanya malipo ya Leseni za kifaa cha Sophos XG Firewall ili kupata uwezo wa kufanya usanidi wa Sera za Usalama ikiwemo kuzifungia Programu ambazo zimepigwa marufuku katika Muongozo wa Internet Usage Guideline, 2022 wa eGAZ.

#### 4.1.4.9 Kutotumika kwa mfumo wa e-Office katika Afisi za Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi

Ukaguzi ulibaini kwamba ZAECA haijaanza matumizi ya mfumo wa Serikali wa Afisi Mtandao (e-Office) licha ya kupatiwa Kompyuta na "Scanner" maalumu kwa ajili ya kuendesha mfumo kwa zaidi ya miezi 4 sasa.

Aidha, ukaguzi ulibaini kwamba watumishi wa Masjala pamoja na watumishi wengine wanaotakiwa kutumia mfumo wa e-Office hawajapatiwa mafunzo ya namna ya kuutumia mfumo ambapo mpaka tunakamilisha Ukaguzi ZAECA haikuwa na mpango wa mafunzo ya mfumo ya e-Office.

Kukosekana kwa dira na mpango madhubuti wa utekelezaji wa miongozo halali ya Serikali kupitia Wakala wa Serikali Mtandao na Afisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kumepelekea mapungufu katika mipango na mikakati ya Serikali ya kutekeleza Serikali Mtandao ili kuongeza tija, ufanisi, uwazi na uwajibikaji.

Ukaguzi unashauri uongozi wa ZAECA kuhakikisha kwamba unasimamia kitengo cha Masjala na TEHAMA kwa kushirikiana na eGAZ na Mamlaka ya Nyaraka na Kumbu kumbu Zanzibar ili kuwezesha utolewaji wa mafunzo kwa watumishi wote wanaotarajiwa kutumia mfumo wa e-Office na kutekeleza mahitaji yote muhimu yatakayowezesha kuanza kutumika kwa mfumo wa e-Office katika Afisi zote za ZAECA Unguja na Pemba kwa uharaka unaostahili.

#### 4.1.4.10 Kukosekana kwa Mfumo wa Kielektroniki wa kufanya Uchunguzi wa Kimahkama (Forensic Audit Software) na kukusanya Ushahidi wa Kidijitali (Digital Evidence)

Mfumo wa Kielekroniki wa kufanya Uchunguzi wa Kimahkama (Forensic Audit Software) na kukusanya Ushahidi wa Kidijitali (Digital Evidence) ni mfumo wa Kielektroniki uliotengenezwa na kutumika kwa lengo la kuhifadhi na kusimamia ushahidi wa kesi au nyaraka nyingine muhimu zinazotumika katika Muktadha wa kimahakama. Ushahidi huu unaweza kuwa wa aina mbalimbali, ikiwa ni pamoja na nyaraka za elektroniki, picha, sauti, au taarifa nyingine inayoweza kutumika kuthibitisha na kuelezea ukweli juu ya suala fulani.

Mfumo huu unaweza kujumuisha programu, taratibu, na vifaa vinavyosaidia uhifadhi wa ushahidi kwa njia inayohakikisha usalama, uhakika, na upatikanaji wa haraka wa taarifa. Lengo kuu la mfumo wa kuchunguza ushahidi ni kutoa njia rasmi na yenye utaratibu wa kisheria wa kuhifadhi, kusimamia, na kuwezesha utumiaji wa ushahidi katika muktadha wa kisheria na kiupelelezi.

Ukaguzi ulibaini ZAECA haina Mfumo wa Kielekroniki unaotumika katika kusaidia kuchunguza ushahidi kutokana na Kesi mbalimbali zinazo ripotiwa katika Mamlaka. Hata hivyo, hadi ukaguzi unakamilika haukuweza kupatiwa njia zinazotumika kuhifadhi ushahidi wa kidijitali (Digital Evidence).

Baadhi ya nyaraka za kidijitali ambazo zinatakiwa kuwa na mfumo wa kusimamia na kulinda matumizi yake ni pamoja na: -

- Barua pepe, Maandishi na Ujumbe Mfupi (Emails, text and instant messages).
- Picha za Kidijitali na Video (Digital photographs and video footage).
- Faili za Uhasibu na Miamala (Accounting files and transactions).
- Historia ya kivinjari na kumbukumbu za mtandao (Browser history and Internet logs).
- Taarifa za Eneo (GPS tracks and location data)
- "Databases Logs"

Kukosekana kwa mfumo wa kuchunguza na kuhifadhi ushahidi wa kidijitali au kutumia mifumo isiyo rasmin kunaweza kusababisha dosari mbali mbali, hasa katika muktadha wa kimahakama, kiuchunguzi na kiupelelezi kama zifuatazo:

**Kuharibu ubora wa Ushahidi:** Hali hii inaweza kujitokeza katika mazingira ambayo ushahidi uliochukuliwa na Mamlaka ukatofautiana na ushahidi halisi japo kwa sehemu ndogo sana kama vile mkato, nukta, urefu wa sentensi, "format of data" na kupelekea ushahidi kukataliwa katika vyombo vya kutolea haki.

**Upotevu wa Ushahidi:** Kukosekana kwa Mfumo imara wa Kielekroniki unaotumika kuhifadhia Ushahidi kunaweza kupelekea kupotea kwa nyaraka na vielelezo mbalimbali ambavyo ni muhimu katika kufanikisha hatua za kupatikana kwa haki juu ya kesi fulani katika vyombo vya haki.

**Kuchelewesha Kesi na Uchunguzi:** Kutokana na upotevu na kuharibika kwa ubora wa ushahidi kunaweza kupelekea ucheleweshwaji wa Kesi na kukamilika kwa uchunguzi jambo linaloweza kuchelesha upatikanaji wa haki.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAECA kupanga bajeti itakayowezesha upatikaji wa mfumo wa Kielektroniki wa kuhifadhi ushahidi wa kidijitali kwa kuzingatia miongozo ya kitaifa na kimataifa.

### 4.1.4.11 Kukosekana kwa "Sophos Firewall" katika Afisi za Mikoa za Mamlaka ya Kuzuia na Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar

Ukaguzi ulibaini kutokuwepo kwa Firewall katika Afisi za Mikoa za Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA Regional Offices).

Hali hii inapelekea matumizi yote ya kimtandao katika Afisi za Mikoa kwa upande wa Unguja kutokuwa na usalama wa kutosha jambo ambalo ni kinyume na Matakwa ya Miongozo ya Serikali 2022, kifungu nambari 6.3.1 Kinachozitaka Taasisi za Umma kuweka njia za kiusalama katika Matumizi ya Kimtandao katika Afisi za Umma.

Kukosekana kwa kifaa cha kuweka usalama wa mtandao (Network) kunaweza kupelekea kuvuja au kudukuliwa kwa taarifa muhimu za Serikali na hivyo kusababisha hatari ya kukosekana kwa Usiri, Uadilifu, na Upatikanaji wa taarifa za Serikali zinazochakatwa, kusafirishwa na kuhifadhiwa katika mifumo na vifaa nyengine vya TEHAMA vinavyotumika ZAECA na kusababisha kupotea, kuharibiwa ama kudukuliwa kirahisi na watu wasiohusika na kutokuwa na nia njema na Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAECA kuchukuwa hatua za makusudi za kuboresha Teknolojia ya kimtandao ya Mamlaka ili kuimarisha usalama na kuongeza tija na ufanisi wa ZAECA kupitia matumizi ya TEHAMA.

### 4.1.4.12 Kutokufanyika kwa Mafunzo ya Kujikinga na Uhalifu wa Kimtandao (Cyber Security Awareness Training) kwa watumishi wa ZAECA:

Mpango wa mafunzo ya uelewa juu ya masuala ya ulinzi na usalama wa matumizi ya TEHAMA ni mpango mahsusi ulio na lengo la kuwajengea uwezo watumiaji wa mifumo pamoja na vifaa vya TEHAMA dhidi ya matokeo ya uhalifu wa kimtandao (cyber crime) pamoja na uingizwaji wa programu hatarishi "malicious software" unaoweza kuiathiri Mamlaka,

Aidha, ukaguzi ulibaini ZAECA kutokua na mpango mahsusi wa kutoa mafunzo ya usalama wa Kimtandao (Cyber Security Awareness Training) kwa watendaji wake licha ya kuwa watendaji hao hutumia vifaa vya kielektroniki, miundombinu ya Kimtandao pamoja na mifumo ya TEHAMA katika kazi zao za kila siku.

Hali hii inaenda kinyume na Matakwa ya Muongozo wa utengenezaji wa Sera za ulinzi wa TEHAMA kutoka Wakala wa Serikali mtandao Zanzibar kipengele nambari 2.8.4.1 kinachozungumzia utowaji wa elimu kuhusiana na Makosa na Usalama wa kimtandao kwa watumishi wa Taasisi za Umma katika ngazi zote.

Kushindwa kuilinda Mamlaka dhidi ya wahalifu wa mitandao (hacker) pamoja na programu hatarishi (malicious software) hali inayoweza kusababisha uvujaji wa taarifa (data breach) nyeti za Mamlaka na hivyo kuisababishia Serikali Gharama kubwa katika kupambana dhidi ya Uhalifu wa aina hiyo pamoja na kukosekana kurejeshwa kwa taarifa muhimu ambazo zilipata mashambulizi au kupotea kwa njia ya mitandao.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAECA kuandaa Mpango wa mafunzo ya Usalama wa Kimtandao kwa watumishi wake katika ngazi zote ili kuhakikisha kwamba kila mtumishi anachukuwa tahadhari za mashambulizi ya kimtandao kupitia matumizi ya mifumo na vifaa mbali mbali vya TEHAMA. Aidha, mafunzo haya yanatakiwa kutolewa angalau mara moja kila mwaka kwa watumishi wote Unguja na Pemba.

### 4.1.4.13 Kutofungwa kwa Mfumo wa Kamera za Ulinzi katika Afisi za ZAECA

Mfumo wa Kamera za CCTV unasaidia kuonesha kumbukumbu za matukio yote yanayofanyika katika mazingira ya Afisi kwa lengo la kutunza ushahidi kwa ajili ya hatua nyengine za haki kwenye vyombo husika ikiwa kumetokezea uhalifu wa aina yoyote.

Kwa kuzingatia Kifungu nambari 4.3.4 cha muongozo wa Wakala wa Serikali Mtandao (eGAZ), 2022, Taasisi inatakiwa kuhakikisha uwepo Usanifu wa Usalama wa Mamlaka (Institutional Security Architecture) ambao utahakikisha upatikanaji wa usalama wa taarifa na nyenzo muhimu za TEHAMA.

Katika kufanya mapitio ya mfumo wa Ulinzi kwa kutumia kamera katika Afisi kuu pamoja na Afisi za Mikoa za ZAECA Unguja, ili kuangalia utendaji kazi wa mfumo huo, ukaguzi ulibaini kutokufungwa kwa mfumo wa CCTV camera katika Afisi hizo licha ya kubainika katika Afisi Kuu uwepo wa vifaa vinavyoweza kuwezesha kufanya kazi kwa mfumo huo ikiwemo Mashine ya kurikodia matukio (NVR) pamoja na kamera.

Hali hii imesababisha kukosekana kwa taarifa za ulinzi na ushahidi kwa njia za kidijitali katika maeneo yote ya Afisi kuu za ZAECA yaliyopo Kilimani.

Vile vile kwa kuzingatia umuhimu wa usalama katika mazingira ya Afisi za ZAECA ambazo pamoja na mambo mengine hushikilia mali na vitu mbali mbali vya thamani kama ushahidi wa matukio ya Rushwa na Uhujumu Uchumi kutoka kwa wananchi kunaweza kuongeza hatari (risk) ya mali hizo kuharibiwa, kuibiwa, au kupotezwa ushahidi katika maeneo ya himaya ya ZAECA na hatimae kushindwa kujulikana waliohusika kuondoa ushahidi huo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAECA kuandaa mpango na kutekeleza ufungaji wa Kamera za Ulinzi kuanzia katika hatua ya kuandaa michoro ya mtandao wa Kamera hadi Nyaraka ya Usanifu wa kiusalama kwa kuzingatia miongozo ya kitaifa na kimataifa ikiwa ni hatua muhimu za kuboresha usalama na kuhakikisha upatikanaji wa ushahidi wa uhakika endapo uhalifu wa aina yoyote utatokea katika mazingira ya Afisi.

### 4.1.5 WIZARA YA UJENZI MAWASILIANO NA UCHUKUZI

Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 4.1.5.1 Kutokuwepo kwa Mifumo ya TEHAMA ya Wizara

Katika kipindi cha awamu ya nane, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefanya jitihada kubwa za kuimarisha maendeleo katika sekta ya TEHAMA kwa Taasisi za Serikali ili kurahisisha mawasiliano katika utendaji kazi kwa lengo la kutoa huduma bora kwa wananchi, kuongeza udhibiti wa ukusanyaji mapato na matumizi, kuimarisha ulinzi na usalama wa taarifa na nyaraka mbali mbali za Serikali pamoja na kuboresha miundombinu na mifumo ya mawasiliano kwa lengo la kupatikana tija na ufanisi wa kazi na huduma bora kwa Jamii.

Wakala wa Serikali Mtandao imeanzisha Mkakati wa kidijitali wa Serikali (Government Digital Strategy) kwa lengo la kuisaidia Taasisi za Umma katika kutoa huduma bora kupitia Mifumo ya TEHAMA.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi haijaanzisha na kutumia mifumo yake ya TEHAMA kwa ajili ya utendaji kazi wa Wizara hiyo. Vile vile imebainika baadhi ya mifumo Jumuishi ya Serikali ambayo inasimamiwa na Wakala wa Serikali Mtandao na kutumika kwa Taasisi zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kama vile mfumo wa e-Office, pia nayo inatumika kwa kiwango kidogo kwa watendaji wa Wizara. Hadi ukaguzi unakamilika Wizara imekuwa inafanya shughuli zake nyingi kwa kutumia njia za kawaida "manually".

Kutokuwepo kwa mifumo ya TEHAMA ya kufanyia shughuli kuu katika Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kunaweza kusababisha utendaji dhaifu wa shughuli za Wizara na kupelekea kupungua kwa ufanisi.

Aidha, kutotumika kwa mifumo ya TEHAMA ni kutounga mkono juhudi za Serikali katika kuanzisha Mkakati wa Mabadiliko ya Kidijitali kwa Serikali kwamba Taasisi za umma kutumia Mifumo ya TEHAMA.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kufanya jitihada za makusudi za kuanzisha mifumo ya TEHAMA kwa lengo la kurahisisha utendaji, utoaji wa huduma bora kwa Wananchi pamoja na kuunga mkono jitihada za Serikali za kufanya mabadiliko ya kidijitali kwa Taasisi za Umma (Government Ditigal Transformation Strategy) ili kuongezeka kwa kasi ya maendeleo endelevu nchini.

### 4.1.5.2 Kukosekana kwa Kamera za kusimamia Ulinzi na Usalama katika Wizara (CCTV)

Ukaguzi ulifanya ziara ya mapitio ya Afisi katika majengo ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi na kubaini kutokuwepo kwa kamera za kusimamia ulinzi (CCTV) na usalama wa rasilimali za Afisi pamoja wafanyakazi wa Wizara hiyo.

Kutokuwepo kwa kamera za CCTV kunaweza kusababisha uchochezi wa kujitokeza kwa vitendo vya uharibifu wa mali za afisi, uhalifu, upotevu na wizi wa mali za Afisi na kupelekea kukosekana kwa ushahidi wake na hatimae kuingiza hasara Serikali.

Vile vile kunaweza kupelekea urahisi wa kufanyika kwa vitendo visivyo na nidhamu na maadili kwa wafanyakazi ndani ya mazingira ya Afisi bila ya kubainika jambo ambalo litaweza kushusha taswira, heshima na uadilifu kwa watumishi wa Wizara.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa MOICT kutenga bajeti ya kufanya manunuzi na ufungaji wa kamera za Ulinzi (CCTV Camera) katika maeneo yote muhimu ya jengo la Wizara ili kuimarisha Ulinzi na kuhakikisha kunakuwa na Usalama wa kutosha wa mali za Afisi pamoja na wafanyakazi wake.

#### 4.1.5.3 Kukosekana kwa zana za kisasa za kufuatilia utendaji na mawasiliano ya mtandao (Modern Network Monitoring Tools).

Zana za ufuatiliaji wa mawasiliano ya Mtandao ni zana zinazoweza kufuatilia mtandao kwa wakati halisi (real time monitoring) na kutoa taarifa ya haraka juu ya utendaji kazi na hali ya Afya ya mtandao (Network health) kwa muda wa masaa 24 siku 7 za wiki. Zana hizi huruhusu Wizara kufanya ufuatiliaji wa mtandao na kudhibiti mapungu mbali mbali kabla hayajatokea (pro-active measures) na kusaidia kuongeza ufanisi wa mtandao unaopelekea kuongeza tija katika utumishi kwa matumizi ya TEHAMA.

Ukaguzi ulibaini kwamba MOICT haina zana za kufuatilia hali ya Mtandao wake (Network Monitoring system) zenye uwezo wa kutoa taarifa halisi na kwa wakati (real time) kuhusiana na matukio yanayofanyika kupitia Mtandao pamoja na utendaji kazi wa mtandao wa Wizara jambo ambalo ni kinyume na miongozo ya viwango bora kubalifu vya usalama vya kimataifa ISO/IEC 27001.

Miongoni mwa athari za moja kwa moja zinazoweza kuifika MOICT na Serikali kwa ujumla ni pamoja na zifuatazo: -

Ucheleweshwaji wa ugunduzi wa matatizo ya Mtandao na kupelekea kuchelewa kutoa ufumbuzi wa tatizo husika wakati linapotokezea kunapelekea kukwamisha utoaji wa huduma bora kwa jamii na kwa wadau mbalimbali wa Wizara.

Kukosa fursa za kufanya maboresho ya mfumo wa Mtandao kwa kukosa taarifa muhimu ambazo zingeweza kupatikana kupitia zana za ufuatiliaji wa Mtandao.

Vile vile kushindwa kubaini mapema uwepo wa changamoto na kuzipatia ufumbuzi (pro-active measures) kabla ya kuanza kujitokeza kwa athari zitakazosababishwa na changamoto hizo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha unatenga bajeti na fedha toshelevu na kununua zana za kisasa za kusimamia mfumo wa mtandao na miundombinu yake yote kwa wakati halisi (real time network monitoring tools) ili kuepusha dosari zinazoweza kutokezea.

### 4.1.6 WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI

Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa Wizara ya Maji Nishati na Madini (WMNM) kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 4.1.6.1 Kutokuwepo kwa Tovuti ya Taasisi

Sheria Nambari 12 ya Wakala wa Serikali Mtandao ya 2019, Sera ya Taifa ya TEHAMA na Sera ya Serikali Mtandao zinasisitiza juu ya haja ya kutumia TEHAMA katika uendeshaji wa shughuli za Serikali kurahisisha mawasiliano na katika utowaji wa huduma kwa jamii. Tovuti ni jukwaa muhimu linaloweza kutoa ufikiaji wa habari kwa umma, kuongeza uwazi wa shughuli za serikali, na kuwezesha mawasiliano bora kati ya serikali na wananchi.

Ukaguzi umebaini kwamba Wizara ya Maji Nishati na Madini haina Tovuti rasmi inayotumia kwa ajili ya kufikisha taarifa mbali mbali za kazi za Wizara pamoja na utekelezaji wa majukumu yake ya kila siku.

**Upatikanaji wa taarifa mbalimbali Kitaifa na Kimataifa**: Kutokuwepo kwa tovuti rasmi ya taasisi kunakwamisha upatikanaji wa taarifa mbali mbali za taasisi katika ngazi ya taifa na kimataifa jambo linaloweza kuikosesha Wizara na Serikali kwa ujumla fursa za kupata maoni ya kujenga kutoka kwa wadau mbali mbali pamoja na kukosa fursa za uwekezaji katika Sekta ya Maji,Nishati na Madini.

**Ukosefu wa Uwazi**: Kutokuwa na tovuti kunaweza kuongeza ukosefu wa uwazi na Kudhoofisha uwajibikaji katika taasisi kwa kuwa taasisi inakuwa imejifungia na kutokuweka wazi kazi zake, mipango na mikakati yake kwa umma ambayo inatakiwa kutumika kama kipimo cha utekelezaji wa majukumu ya taasisi husika kwa kipindi husika.

**Kudhoofisha Mahusiano na wadau**: Kutokuwepo kwa tovuti kunaweza kupelekea taasisi kuwa na mahusiano dhaifu na wadau wake kwa sababu ya kukosa mawasiliano ya moja kwa moja na wadau wake kote duniani.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Maji, Nishati na Madini kuchukua jitihada za lazima na kuhakikisha inakuwa na tovuti. Kwa kuzingatia mazingira ya sasa, kuwa na tovuti ni muhimu kwa taasisi kujenga na kudumisha uwepo wa dijitali unaofaa.

#### 4.1.6.2 Kutozingatiwa kwa miongozo katika Utengenezaji wa Mfumo wa Madini Management System

Kwa mujibu wa toleo la barua ya Manunuzi na ufungaji wa Mifumo na Vifaa vya TEHAMA katika sekta ya Umma, iliyotolewa tarehe 13 Julai 2021 lenye kumbukumbu namba OR/EGOV/NJ/02/VOL.VII/216 kutoka kwa Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar, sehemu ya 5(a) ya barua hiyo imezielekeza taasisi zote kuandaa mahitaji yote muhimu na nyaraka za awali za uanzishaji wa mifumo ya TEHAMA kulingana na viwango na miongozo inayotolewa na Serikali.

Hata hivyo baadhi ya miongozo ya viwango bora na kubalifu ya kimataifa ya TEHAMA ikiwemo ISO/IEC 12207, IEEE Std 1074-2018 - IEEE Standard for Developing Software Life Cycle Processes, ISO/IEC 27001 - Information Security Management System (ISMS) n.k, inataka mfumo wowote unaotengenezwa kupitia utaratibu maalumu wa kutengenezea mifumo. Software Development Life Cycle (SDLC), huu ni mchakato ambao kimsingi hutoa mbinu iliyopangwa kwa muundo, uundaji, majaribio, uwekaji na matengenezo ya mifumo.

Ukaguzi haukuweza kupatiwa nyaraka zote muhimu za mfumo wa Madini ambapo ilibainika kwamba Utengenezaji wa mfumo wa Madini (Madini Management System) haukuzingatia taratibu za kutengeneza mifumo za kitaifa na kimataifa.

Kutozingatiwa kwa utaratibu wa kutengeneza mifumo ya TEHAMA katika utengenezaji wa mfumo wa Madini kunaweza kupelekea kukosekana kwa hali ya umiliki wa mfumo kwa watumishi wa Wizara na kuonekana kama mali ya mtoa huduma (Lack of ownership of the system), hali itakayopelekea mfumo kutotumika ipasavyo na kuinyima Serikali kupata manufaa ya uwekezaji katika mfumo husika.

Kukosekana kwa matumizi endelevu ya mfumo jambo linaloweza kusababisha mfumo usiendelee mara baada ya kumalizika kwa mkataba na mtoa huduma hususani mfumo unapokabidhiwa kwa Serikali na kuisababishia Serikali hasara kubwa.

Uwepo wa mifumo mingi Serikalini isiyokuwa na tija na inayo ongeza gharama za wendeshaji kwa kuwalipa watoa huduma badala ya kutumia rasilimali watu za ndani ya Serikali.

Ukaguzi unashauri kuwa kabla ya kuunda au kununua mfumo Shirika lizingatie miongozo ya Wakala wa Serikali Mtandao pamoja na viwango bora kubalifu vya kimataifa.

Vile vile, Ukaguzi unaushauri uongozi wa WMNM kuhakikisha nyaraka zote zinapatikana wakati wa utengenezwaji wa mfumo kwa lengo la kupatikana matumizi sahihi na endelevu kwa mifumo ya TEHAMA.

#### 4.1.6.3 Ufanyikaji wa Malipo ya Mfumo wa Madini zaidi ya shilingi 877,174,447 kwa M/S Rahisi Solution pasipo kutimiza wajibu wake kwa mujibu wa Mkataba

Wizara ya Maji, Nishati na Madini iliingia mkataba na M/S Rahisi Solution Company LTD mnamo tarehe 01/04/2022 kwa huduma za utengenezaji na ufungaji wa Mfumo wa Usimamiaji Madini na huduma nyinginezo zilizoainishwa katika Mkataba huo nambari SMZ/A13/SR/2021-2022/01.

Aidha, kipengele nambari 4 (c), (d), (e) na (f) cha Hadidu Rejea za Mkataba huo kinamtaka Mtoa Huduma (M/S Rahisi Solution Company LTD) kuwasilisha Wizarani nyaraka zifuatazo kama sehemu muhimu ya mfumo wa Madini: -

i. Training Materials and User Manuals,
ii. Maintenance Details Plan, Agreement & SLA,
iii. API tha enables the prospective system to exchange information with third party systems from different stakeholders.
iv. System Requirement document,
v. System Design document,
vi. User Acceptance Test Case document,
vii. User Acceptance Certificate,
viii. User Access and Privileges Mapping document,
ix. System Configuration/ Set Up Manual document,
x. Database backup report,
xi. Reports (Inception Report, Monthly Progress Report, and Final Report)

Ukaguzi umebaini kwamba zaidi ya asilimia 92 ya nyaraka zote zilizotakiwa kutolewa na M/S Rahisi Solution kama nyenzo muhimu za kuwezesha Wizara kudhibiti na kusimamia uendeshaji wa Mfumo wa Madini hazijawahi kutolewa hadi ukaguzi unakamilika. Hata hivyo, Wizara ya Maji, Nishati na Madini imeendelea kumlipa mtoa huduma (M/S Rahisi Solution) kuanzia mwezi Juni, 2022 hadi mwezi Mei, 2023 jumla ya shilingi 877,174,447 hadi ukaguzi ukamilike kuwasilisha nyaraka hizo muhimu za umiliki, usimamizi na uendeshaji wa mfumo huo wa Madini. Hali halisi ya malipo hayo ni kama inayoonekana katika Jedwali hapo chini:-

**Jadweli Nambari 34: Malipo yaliyolipwa kinyume na makubaliano ya Mkataba wa Mfumo wa Madini zaidi ya shilingi 877,174,447**

| Mwezi | Tarehe ya Malipo | Anaka Namba | Gharama za Tozo ya Mfumo (Tshs) | VAT (Tshs) | Kiasi Halisi cha Malipo ya Ankara pamoja na VAT (Tshs) | Kiasi kilicholipwa (Tshs) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Apr-22 | - | RHSLSNWB | 24,116,100 | 3,617,415 | 27,733,515 | 155,945,850 |
| May-22 | - | RHHA2OWW | 57,205,400 | 8,580,810 | 65,786,210 | |
| Jun-22 | - | - | - | - | - | |
| Jul-22 | 07/07/2023 | RHD71NRG | 82,329,860 | 12,349,479 | 94,679,339 | 158,329,957.40 |
| Aug-22 | 07/07/2023 | RHEC33US | 81,336,785 | 12,200,518 | 93,537,303 | |
| Sep-22 | - | RHBKJ2JJ | 100,780,350 | 15,117,053 | 115,897,403 | 99,484,550 |
| Oct-22 | 07/11/2022 | RH3MG9W5 | 109,964,450 | 16,494,668 | 126,459,118 | |
| Nov-22 | - | RHK4ECNM | 104,149,500 | 15,622,425 | 119,771,925 | 83,561,876.09 |
| Dec-22 | - | RHUKM98V | 108,415,600 | 16,262,340 | 124,677,940 | 88,704,680.44 |
| Jan-23 | 07/07/2023 | RHHQ6Y7X | 115,382,350 | 17,307,353 | 132,689,703 | 158,329,957.40 |
| Feb-23 | 07/07/2023 | RH7OM3JQ | 97,040,350 | 14,556,053 | 111,596,403 | |
| Mar-23 | 20/09/2023 | RHBVYHZ | 118,954,760 | 17,843,214 | 136,797,974 | |
| Apr-23 | 10/05/2023 | RHI9CWLU | 68,985,670 | 10,347,851 | 79,333,521 | 56,988,162.24 |
| May-23 | 07/06/2023 | RH7OSZVX | 104,462,105 | 15,669,316 | 120,131,421 | 75,829,413.06 |
| **Jumla** | | | | | | **877,174,446.63** |

Aidha, wakati wa kipindi cha ukaguzi imebainika kwamba Kampuni ya Rahisi Solution iliwasilisha madai ya malipo ya jumla ya shilingi 622, 793, 713 kwa kipindi cha miezi 5 kuanzia mwezi, Julai, 2023 hadi mwezi Novemba, 2023 ikingojea taratibu za malipo japokuwa hajatekeleza wajibu wake kwa mujibu wa makubaliano rasmi na Wizara katika kuwasilisha nyaraka hizo Serikalini.

Ikiwa madai hayo yatafanyika M/S Rahisi Solution atakuwa amelipwa jumla ya shilingi 1,499,968,159 bila ya kuwasilisha nyaraka zinazohitajika za Mfumo ikiwemo nyaraka za umiliki, usimamizi, wendeshaji na udhibiti wa Mfumo wa Madini.

Aidha, kitendo cha Wizara kuendelea kufanya malipo kwa M/S Rahisi Solution pamoja na kwamba hajatekeleza baadhi ya matakwa muhimu ya Mkataba kimepelekea M/S Rahisi Solution kutokuweka uzito katika kutengeneza na kuwasilisha Wizarani nyaraka zote zinazotakiwa ili kuiwezesha Wizara kuwa na umiliki, usimamizi, wendeshaji na udhibiti wa Mfumo wa Madini.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Maji, Nishati na Madini kuchukua hatua stahiki za kisheria kuhakikisha kwamba M/S Rahisi Solution anatekeleza wajibu wake kama ilivyokubaliwa katika mkataba.

Aidha, kwa kuwa tayari M/S Rahisi Solution ameishalipwa zaidi ya shilingi 877,174,447 ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuzuia malipo zaidi kwa M/S Rahisi Solution hadi atakapotekeleza takwa la kuwasilisha nyaraka zote zilizoainishwa katika Kipengele cha 4 (c), (d), (e) na (f) katika Hadidu rejea za Mkataba huo.

#### 4.1.6.4 Kutokuzingatiwa kwa ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika Rasimu ya Mkataba baina ya Wizara na M/S Rahisi Solution

Ukaguzi umebaini kuwa Wizara ya Maji, Nishati na Madini iliiandikia barua Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuitaka kufanya mapitio ya Rasimu ya Mkataba nambari SMZ/A13/SR/2021-2022/01 uliokuwa unatarajiwa kusainiwa baina ya Wizara na Rahisi Solution, ambapo katika majibu ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kupitia barua ya tarehe 28/02/2022 nyenye marejeo nambari LD 908 VOL.II/39 Mwanasheria Mkuu wa Serikali alishauri Uongozi wa Wizara kufanya marekebisho ya Vifungu mbali mbali kama vile: -

- GCC 12.1 – Kinachozungumzia Programu ya utekelezaji wa Mfumo.
- GCC 17.1 – Kikizungumzia uwepo wa Activity schedule.

Vipengele hivi vilishauriwa kuwekwa katika Mpango Kazi wa Mradi, hata hivyo Wizara haikutekeleza hayo na badala yake iliviacha katika Mkataba kama unavyosomeka sasa.

- GCC 16 – Kutokuwepo kwa vipengele (f) na (g) ambavyo vimetajwa katika Mkataba wakati katika uhalisia havipo.

Mpaka Mkataba unasainiwa Vipengele hivi havikuwekwa kama ilivyopendekezwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

- GCC 27 – Kutokuwepo kwa kiwango cha "Penalty for lack of Perfomance" ambacho Rasimu ya Mkataba ilionesha kwamba kimeelezewa zaidi kwenye kifungu GCC 41.1 ambacho kimsingi hakikuwepo katika Rasimu ya Mkataba uliopitiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali alipendekeza kwamba kwa umuhimu wa kifungu hicho kilitakiwa kuwekwa katika Mkataba utakao sainiwa, hata hivyo Uongozi wa Wizara ya Maji, Nishati na Madini haukukiweka kifungu hicho katika Mkataba uliosainiwa baina ya Wizara na M/S Rahisi Solutions. Hali hii imechangia kusua sua kwa Utendaji wa kampuni ya M/S Rahisi Solution na kuikosesha Serikali haki zake za msingi kwa mujibu wa Mkataba.

- GCC 13.1 – Kutokuwepo kwa Kifungu cha "Contract Duration" – Mwanasheria Mkuu alibainisha kutokuwepo kwa Kifungu cha muda wa mkataba na kupendekeza kifungu hicho kuwekwa kwenye GCC.

Hata hivyo Uongozi wa Wizara haukutekeleza hayo na badala yake mkataba uliendelea kusainiwa ukiwa na mapungufu yaliyobainika.

- SCC 1.1(m) – Mwanasheria Mkuu alibaini kwamba Kifungu hiki hakikuwa kinafahamika vyema na kwamba alipendekeza kitolewe maelezo zaidi.

Hata hivyo mkataba uliendelea katika hatua za kusainiwa bila ya kufanyiwa kazi mapendekezo hayo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

- SCC 5 (7.1) – Kutofahamika vyema nani mwenye "full mandate and authority" kati ya Mmiliki wa Kampuni na Mwakilishi wa Mmiliki wa Kampuni, ambapo Mwana Sheria Mkuu wa Serikali alishauri pawekwe sawa kabla ya kusainiwa kwa Mkataba husika.

Hata hivyo haya hayakufanyiwa kazi kama yalivyotolewa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mkataba ulisainiwa kama ulivyokuwa.

Kwa ujumla kutozingatiwa kwa yaliyotolewa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni kwenda kinyume na matakwa ya Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 pamoja na Kanuni zake za 2021 jambo ambalo linaweza kuingiza hasara Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Maji Nishati na Madini kuchukua hatua za haraka kurekebisha mkataba kwa kuzingatia mabadiliko yaliyopendekezwa. Hii itahakikisha kuwa Wizara inafuata miongozo ya kisheria na itaepuka hatari za kisheria zinazoweza kutokea kutokana na kutokuzingatia mabadiliko muhimu.

### 4.1.6.5 Kutokuwepo kwa mfumo wa ulinzi wa kamera katika Vituo (checkpoint), Unguja na Pemba

Ukaguzi umebaini kutokuwepo kwa mfumo wa ulinzi wa Kamera maeneo muhimu ambayo yanatumika kila siku na yanahifadhi mali za serikali. Miongoni mwa maeneo hayo muhimu ambayo hayakufungwa Kamera ni katika vituo (checkpoint).

**Ushawishi wa uhalifu na udanganyifu:** Wafanyakazi na wafanyabiashara wanapojua kuwa hakujafungwa Kamera katika vituo hivyo kwa pamoja wanaweza kuwa na hamasa zaidi kutekeleza vitendo vya uhalifu na udanganyifu kwa makusudi kutokana na dereva kujuana na mfanyakazi au kwa njia yeyote itakayotumia bila ya kujali za kufanya hivyo, ambapo hali hii inamshawishi muhalifu kufanya uhalifu kwa kujiamini kwa kujua kuwa hakuna Kamera za ulinzi za kuchukua matukio.

**Kupunguza ufanisi wa ulinzi:** Maeneo muhimu kawaida huwa na mikakati ya ulinzi, na kamera ni sehemu muhimu ya mikakati hiyo, kutokuwepo kwa Kamera kunaweza kusababisha pengo katika ufanisi wa ulinzi na ufuatiliaji.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa WMNM kuhakikisha wanaweka udhibiti wakutosha katika vituo vya ukaguzi, kamera zina jukumu muhimu katika kuimarisha usalama, kutoa ushahidi wa matukio, na kusaidia katika kudhibiti mazingira. Kutokuwepo kwake.

#### 4.1.6.6 Kutokafanya kazi kwa baadhi ya moduli za mfumo wa Madini

Mfumo wa Madini Management umekusanya jumla ya moduli kuu kumi na tisa (19) ambazo hutumika kwa shughuli zote za mchakato mzima wa usimamiaji wa maliasili zisizorejesheka, katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuna baadhi ya moduli hazifanyi kazi licha ya kwamba mfumo unaendelea kutumika, moduli hizo ni kama zifuatazo:-

- ***Moduli ya Kuingia kwa Gari (Vehicle Entry)***

Moduli hii ilitarajiwa kuonesha magari yote yaliyoingia shimoni na kuweza kuhesabu na kutenganisha baina ya magari yaliyokuwa tayari yameshathibitishwa na yaliyokuwa hayajathibitishwa. Moduli hii imeshindwa kufanya kazi kwa sababu ya ukosekanaji wa kamera kwenye mashimo, ambapo kamera hizo zilitakiwa kufungwa na vendor kama makubaliano yanavyosema.

- ***Moduli ya Makosa (Offenses)***

Moduli hii ilipaswa kutumika kulipisha na kurikodi makosa yote yanayohusiana na maliasili zisizorejesheka yakiwemo kutoa kibali zaidi ya kimoja, kuhamisha na kusafirisha maliasili zisizorejesheka bila kibali au leseni na makosa yote yanayofanywa na madereva wa magari yaliyosajiliwa kwenye mfumo. Moduli hio kwa sasa haifanyi kazi, na inatumika Zanmalipo kama mbadala wake.

Kutofanya kazi kwa moduli hizo kunasababisha kukosekana kwa baadhi ya Taarifa muhimu kama zilivyobainishwa hapo juu jambo ambalo linaweza kupelekea mfumo kuonekana hauna tija kama ilivyokusudiwa licha ya fedha nyingi kutumika katika ulipaji wa huduma ya mfumo uwo.

Aidha, hali hii pia hupelekea hatari za usalama. Ukosefu wa uthibitishaji hufanya iwe rahisi kwa magari yasiyoidhinishwa kuingia kwenye mashimo ya kuchimba bila kutambuliwa, na kusababisha hatari ya usalama. Bila kamera, inakuwa vigumu kufuatilia na kurekodi aina za magari yanayoingia kwenye mashimo, hivyo kuifanya iwe vigumu kutekeleza itifaki za usalama.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa WMNM kufanya jitihada za makusudi ili kuweza kuukamilisha mfumo huo na katika moduli zote kwa lengo la kuweka udhibiti na usimamazi wa maliasili zisizorejesheka kama ilivyokusudiwa na hatimae kupatikana kwa tija na ufanisi wa utendaji kazi wa mfumo.

#### 4.1.6.7 Kutounganishwa kwa mashine za POS na mfumo wa Madini

POS mashine ni mashine ambazo hutumiwa na wapekuzi (inspectors) waliokuwepo kwenye kituo cha upekuzi (checkpoints) za njiani kwa ajili ya kuthibitisha vibali vya kubebea na kuhamisha maliasili zisizorejesheka. Pia POS zilitakiwa ziweze kutoa vibali vya maliasili zisizorejesheka aina ya mawe, kokoto, kifusi na udongo.

Ukaguzi umebaini kwamba POS za kwenye kituo cha upekuzi (checkpoint) za njiani hazisomani na mfumo wa Madini Management. Ambapo wakaguzi waliopo kwenye vituo (checkpoint) hushindwa kuthibitisha vibali na pia hushindwa kutoa vibali vya baadhi ya maliasili pamoja kushindwa kupunguza tani za maliasili.

**Kukosekana kwa Ufanisi wa Usimamizi:** Ukiwa na POS isiyounganishwa, usimamizi wa miamala na udhibiti wa uthibitisho unaweza kuwa mgumu. Hii inaweza kuleta changamoto katika kufuatilia na kudhibiti mchakato wa uthibitisho

**Kukosekana kwa Ufanisi wa Usimamizi:** Ukiwa na POS isiyounganishwa, usimamizi wa miamala na udhibiti wa uthibitisho unaweza kuwa mgumu. Hii inaweza kuleta changamoto katika kufuatilia na kudhibiti mchakato wa uthibitisho.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa WMNM kuchukua jitihada za kuunganisha POS na mfumo wa Madini ili kuleta ufanisi mkubwa, pamoja na kuboresha udhibiti wa miamala na huduma.

Hata hivyo, pia ukaguzi unaushauri uongozi uchukuwe hatua za kiusalama zinazopaswa kuchukuliwa kuhakikisha usalama wa mifumo na data.

#### 4.1.6.8 Udhibiti Duni wa Uingizaji Taarifa kwenye Mfumo wa Madini

Katika kukagua mchakato wa maombi ya vibali vya usafirishaji, uchimbaji na uhamishaji wa maliasili zisizorejesheka, ukaguzi umebaini dosari katika udhibiti wa uingizaji wa Taarifa kama ifuatavyo:

i. Kumruhusu muombaji kujaza taarifa atakazo kwenye eneo la ujenzi, hali ya kuwa mfumo unaweza kuwa na taarifa hizo tokea awali na muombaji akaweza kuchagua.

ii. Kumruhusu muombaji kujaza taarifa za sababu ya kibali wakati sababu za mtu kuomba kibali zinajulikana tayari. Kwa hiyo mfumo unaweza hifadhi taarifa hizo na muombaji akaweza kuchagua moja kwa moja kutokea kwenye mfumo.

iii. Kutokuwepo kwa kikomo katika ujazaji wa taarifa za maelezo zaidi ya kibali. Mfumo unamruhusu muombaji kujaza taarifa kwa jinsi anavyotaka yeye.

Hali hii inaweza kusababisha kupunguza kwa ufanisi wa mfumo  na unaweza kupelekea ugumu katika kufanya uchambuzi wa taarifa na kutoa ripoti jambo ambalo litaathiri watumiaji wa mfumo ambao wanategemea taarifa sahihi na zinazopatikana kwa urahisi.

Kwa kuzingatia  hizi, ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Maji Nishati na Madini kuweka mfumo bora wa udhibiti wa uingizaji taarifa ili kuhakikisha usahihi, usalama, na ufanisi wa mfumo wa habari ikiwemo kutumia mbinu sahihi kama vile kufanya uhakiki wa data, usimamizi wa mchakato wa uingizaji taarifa, na matumizi ya teknolojia sahihi ya usalama wa data.

### 4.1.6.9 Kujirudia kwa nambari za ankara zinazozalishwa kupitia mfumo wa Madini

Katika uchambuzi wa data zilizomo katika mfumo wa Madini, ukaguzi umebaini urudiaji wa nambari ya ankara "Invoice Number" zinazozalishwa kiotomatiki na mfumo wa Madini. Jumla ya ankara 500 zenye thamani ya shilingi 25,455,500 zimebainika kujirejea. Kati ya ankara hizo, 259 zimeshaisha muda wake (expired) na 241 ya ankara zimeshafanyiwa malipo.

Kutokana na kujirejea kwa nambari ya ankara, kunaweza kusababisha ugumu wa kufuatilia malipo kwa urahisi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Maji Nishati na Madini kwa kushirikiana na Kampuni ya M/S Rahisi Solution (Mtoa Huduma) kuhakikisha kuwa nambari za ankara zinakuwa za kipekee na zinadhibitiwa vizuri katika mfumo wa malipo ili kuepuka  hizi na kuhakikisha utendaji mzuri na udhibiti imara wa shughuli za kifedha na usimamizi wa malipo. Mchanganuo wa ankara hizo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 35: Idadi ya ankara zilizozalishwa kwa kujirejea na hali zake**

| Namba | Idadi ya Ankara | Thamani (Tsh.) | Asilimia (%) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| | 259 | 13,500,500 | 51.8 | Muda umeisha |
| | 241 | 11,955,000 | 48.2 | Zimelipiwa |
| **Jumla** | **500** | | | |

### 4.1.6.10 Udhibiti duni wa Uhakiki wa Taarifa na Malipo yanayoingizwa katika ZanMalipo

ZanMalipo ni mfumo unaotumika na WMNM kusimamia malipo na kuhifadhi taarifa zote zinazohusiana na huduma za maliasili zisizorejesheka kwa upande wa Pemba.

Katika kukagua mchakato wa maombi ya vibali usafirishaji, uchimbaji na uhamishaji wa maliasili zisizorejesheka. Ukaguzi umebaini uwepo wa udhibiti duni wa kutekeleza uthibitishaji wa uingizaji wa taarifa. Baadhi ya mapungufu yaliyobainika ni kukosekana kwa udhibiti katika uingizaji wa taarifa sahihi kwa upande wa Pemba ambapo taarifa zinazoingizwa kwa ajili ya hifadhi kuhusiana na maliasili zisizorejesheka zimebainika ya kutokuwa na mpangilio mzuri wa taarifa hizo ikiwemo taarifa za kwenye seksheni ya "Bill reference" ambapo imekuwa ikijazwa maelezo tofauti na usahihi.

Vile vile Mfumo wa ZanMalipo umebainika kumruhusu mtoa huduma kuingiza kiasi cha malipo ya huduma kwa njia ya kawaida ya mkono na sio kwa kuchagua kutoka kwenye mfumo moja kwa moja.

**Kukosekana kwa udhibiti mzuri wa uhakiki wa taarifa zilizomo ndani ya mfumo huo kunaweza kupelekea dosari zifuatazo:-**

- Kujitokeza kwa ugumu katika kufuatilia na kuchambua malipo kutokana na kushindwa kutofautisha bili mbalimbali.
- Ikiwa malipo yanahitaji kurejeshwa au kurekebishwa kunaweza kusababisha ugumu wa kubaini na kufuatilia aina ya malipo yanahusika na hatua gani za kuchukua.
- Kuingiza taarifa za mapato kwa njia ya mkono kunaongeza hatari ya uingizwaji wa taarifa za malipo zisizosahihi kutokana na kusababisha uwezekano wa kupoteza mapato au kutozingatia malipo kwa usahihi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Maji Nishati na Madini kuhakikisha kuwa mfumo wa ZanMalipo unaweka taarifa vizuri kwa mpangilio mzuri ili kuhakikisha ufanisi, uaminifu, na utendaji wa biashara unaendelea vizuri.

Kuwa na utaratibu mzuri wa kumbukumbu na mpangilio wa taarifa kunaweza kuboresha mchakato wa malipo na huduma kwa wateja, vile vile uongozi kuhakikisha njia ya malipo zinakuwa sahihi na zenye udhbiti mzuri kulingana na mahitaji ya biashara na kuzingatia ufanisi,usahihi, na usalama.

### 4.1.6.11 Dosari za kiusalama na kimazingira zilizobainika katika Chumba cha Mitambo (Control Room)

Katika kufanya mapitio ya udhibiti na kiusalama wa kimazingira katika miundombinu ya mtandao wa Wizara ya Maji Nishati na Madini ukaguzi umebaini uwepo wa mapungufu mbali mbali yanayoweza kuathiri Usiri, Uadilifu na Upatikanaji wa mifumo ya TEHAMA ya Wizara, miongoni mwa mapungufu hayo ni:

- **Udhaifu katika udhibiti wa milango ya kuingilia chumba cha Mitambo**

Ukaguzi umebaini uwepo wa udhibiti na usalama duni kwenye milango ya kuingilia katika vyumba vya kuhifadhia vifaa vya Miundombinu ya TEHAMA (server room) jambao ambalo linaweza kusababisha urahisi wa upatikanaji wa rasilimali hizo muhimu ndani ya chumba hicho pindipo watu wenye nia hasi wakiingia.

- **Uwepo wa mpangilio duni wa vifaa vya Mtandao vinavyohifadhiwa katika "cabinet/ Rack"**

Ukaguzi ulibaini kukosekana kwa mpangilio mzuri wa vifaa mbali mbaii vya Mtandao vilivyowekwa na kufanya kazi katika kabati maalumu (rack cabinet) ikiwemo waya za kusafirisha data (network cables) ambazo hazikuwa zimepangiliwa vizuri pamoja na vifaa vyengine vya mtandao, hali hii ni kwenda kinyume na miongozo ya viwango bora kubalifu (best practice), ISO/IEC 14763-2: Information technology.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Maji Nishati na Madini kupitia kitengo cha TEHAMA cha Wizara kuchukuwa jitihada za kupangilia vizuri rasilimali zote za TEHAMA zinazofanya kazi kwenye Chumba cha Seva ili kuimarisha ufanisi wa utendaji kazi wa miundombinu hiyo pamoja na kuongeza usalama katika mazingira ya chumba hicho.

### 4.1.7 MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE ZANZIBAR (ZAA)

Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar (ZAA) kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 4.1.7.1 Kukosekana kwa tija ya matumizi ya mfumo wa maegesho ya vyombo vya moto ZAA

Kwa mujibu wa viwango vilivyo bora (best practise) Taasisi zinatakiwa kuwa na mpango imara wa usimamizi na matumizi endelevu ya mifumo ya TEHAMA kwa malengo ya kuboresha ufanisi wa jumla, kuboresha matumizi ya rasilimali, kupunguza upotevu wa taarifa na kuokoa gharama kwa Taasisi.

Ukaguzi umebaini kwamba Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar haina mpango imara wa usimamizi, uendeshaji na udumishaji wa mifumo ya TEHAMA (system sustainability plan). Hali hii imebainika kutokana na kufeli kwa utendaji kazi wa mfumo wa **Parking System** ulionunuliwa kutoka kwa Kampuni ya **Beijing Construction Engineering Group Company Ltd** kwa thamani ya **USD 125,000 (approx: Tsh. 318,670,000)** na kufungwa katika Jengo la Terminal 3, ambapo Mfumo huo ulifanya kazi kwa kipindi cha mwaka mmoja na miezi miwili tu kuanzia februari 2022 hadi aprili 2023, kabla ya kubadilishwa na kuwekwa Mfumo mwengine wa **Smart Parking System** ulionunuliwa kwa gharama za shilingi **788,413,995.98** kutoka kwa kampuni ya **NPK TECHNOLOGIES LIMITED** na kuanza kazi mwezi wa Novemba 2023.

Dosari hii imesababisha Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kuingia hasara kutokana na kufeli kwa kushindwa kufanya kazi mfumo wa kwanza na kupelekea Mamlaka kununua tena mfumo mwengine wa maegesho ya gari kwa gharama tajwa hapo juu.

Aidha, kutokuwepo kwa mpango imara wa matumizi endelevu wa mifumo kunapelekea Mamlaka kuwa na mifumo mingi isiyo kuwa na tija, vile vile kukosekana kwa mpango huo kumepelekea hasara kubwa kwa serikali ambayo ingeweza kuepukika.

Ukaguzi unashauri uongozi wa ZAA kuweka mpango Imara wa kufanya tathmini ya upembuzi yakinifu kabla ya kuanza kununua mifumo na kutumia, vile vile kuishirikisha Ofisi ya Wakala wa Serikali Mtandao pamoja na Mwanasheria Mkuu katika michakato ya manunuzi na uingiaji wa mikataba kwenye Mifumo ya TEHAMA ili kupatikana mifumo yenye tija, ufanisi, endelevu na kufanya kazi kwa weledi kwenye makusanyo ya mapato ya maegesho ya vyombo vya moto.

#### 4.1.7.2 Kukosekana kwa nyaraka za utengenezaji wa mfumo wa ZAA ID pamoja na mfumo wa ZAA Car Sticker

Kwa mujibu wa muongozo wa Usimamizi wa miradi ya TEHAMA wa EGAZ 2022 kifungu 2.6 kinaeleza kwamba taratibu za utengenezaji wa mifumo inataka kwa kila mfumo utakaotengenezwa lazima uzingatie uwepo wa nyaraka zinazoonesha hatua mbali mbali zilizotumika katika utengenezaji wa mfumo.

Ukaguzi umebaini kwamba mfumo wa ZAA ID pamoja na mfumo wa ZAA Sticker haina nyaraka muhimu ambazo zinaonesha taratibu za utengenezwaji wa mifumo hiyo mpaka kukamilika kwake, Aidha ukaguzi umeshindwa kupata nyaraka zinazoonesha ukusanyaji wa maoni ya wadau katika ushiriki wao wa kutoa maoni na michango jinsi namna bora ya kutengeneza mfumo ambao utaweza kutatua changamoto mbali mbali zilizopo katika taasisi hiyo.

Kutokuwa na nyaraka za utengenezwaji wa mifumo pamoja na kutowashirikisha watendaji wa ZAA katika utengenezwaji wa Mifumo kunaweza kusababisha Kushindwa kutambua namna gani mfumo unaweza kurekebishwa endapo tatizo lolote litajitokeza kwa sababu ya kukosa nyaraka muhimu za kutengenezwa mfumo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAA uhakikishe nyaraka zote muhimu katika Mfumo utakao tengenezwa na kutumika katika Mamlaka hiyo ziwepo kwa lengo la kulinda usalama wa mfumo endapo changamoto yoyote itakapojitokeza.

#### 4.1.7.3 Mazingira duni kwenye chumba cha Sava (Server Room) Pemba

Chumba cha Seva ni chumba muhimu sana kwa kuwa kinahifadhi Kompyuta na Seva zinazoendesha mifumo na kuhifadhi taarifa za mifumo ya taasisi na vifaa mbalimbali vya TEHAMA. Kwa kuzingatia umuhumu wa usiri, uadilifu, na upatikanaji wa taarifa zinazohifadhiwa kwenye chumba cha Seva, Viwango bora kubalifu vya kimataifa vimeweka vigezo vinavyotakiwa kuzingatiwa kwenye chumba cha Seva, miongoni mwa vigezo hivyo ni pamoja na joto, hali ya unyevunyevu, udhibiti wa moto, udhibiti wa watu kwenye kuingia, uwepo wa kamera za ulinzi n.k.

Ukaguzi umebaini uwepo wa mazingira duni kwenye chumba cha Seva kilichopo ZAA Pemba, chumba hiki hakina udhibiti wa moto wa moja kwa moja (automatic fire suppresion system) kama inavyotarajiwa, udhaifu kwenye udhibiti wa mlango ambapo hakuna mashine ya kurikodi taarifa za watu wanaoingia ndani, udhaifu wa usafi wa mazingira, kutokuwepo kamera za ulinzi, chumba kimejengwa kwa kutumia maboksi (Hard board).

Miongoni mwa dosari zinazotokana na udhaifu wa udhibiti na mazingira duni ya chumba cha Seva ni pamoja na kuhatarisha usiri, uadilifu, kupunguza utegemezi wa taarifa zinazochakatwa na kuhifadhiwa kwenye chumba cha Seva. Aidha, uwepo wa mazingira duni kama vile mavumbi kwenye chumba cha Seva unatishia matumizi endelevu ya vifaa vya TEHAMA vilivyomo kwenye chumba cha Seva vilivyoigharimu Serikali fedha nyingi, kukosekana kwa mifumo sahihi ya kuzima moto kunaziweka taarifa na vifaa vyote vya TEHAMA vilivyomo ndani ya chumba cha Seva hatarini kuteketea kama ikitokea janga la moto.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuyafanyia kazi mapungufu yote yaliyobainika kwenye ukaguzi kwa muda muafaka ili kuepuka madhara yanayoweza kujitokea ambayo ni pamoja na hasara, upotevu wa taarifa.

#### 4.1.7.4 Kukosekana kwa mafunzo endelevu kwa wafanyakazi katika Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar

Kwa mujibu wa Muongozo wa ISO 27001 kifungu A.7.2.2 Kinaelekeza kwamba Wafanyakazi wa taasisi wapatiwe mafunzo endelevu yenye kuleta tija katika Nyanja tofauti ambayo yataendana na majukumu ya kazi zao.

Ukaguzi umebaini kwamba wafanyakazi wa kitengo cha TEHAMA pamoja na idara nyengine katika Mamlaka ya Viwanja vya Zanzibar (ZAA) kwa muda mrefu hawajapatiwa mafunzo yenye tija na manufaa kwa taasisi hiyo ambayo yataweza kuleta matokeo chanya ya Matumizi bora ya Mifumo ya TEHAMA.

Kukosekana kwa mafunzo ya mara kwa mara ya Usalama, Usimamizi na Uendeshaji wa mfumo kunaweza kusababisha kukosekana kwa usimamizi mzuri wa utumiaji wa mfumo na hatimae Serikali kuingia gharama za uendeshaji wa mfumo zisizo na ulazima.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar kusimamia na kuhakikisha kwamba wafanyakazi wa Mamlaka hiyo wanapatiwa mafunzo ya mara kwa mara ya matumizi bora ya mifumo ili kuweza kusimamia vizuri na kupata taaluma ya kisasa kutokana na mabadiliko ya mara kwa mara ya sayansi na teknolojia.

### 4.1.7.5 Kutokushirikishwa ipasavyo kwa wataalamu wa TEHAMA pamoja na watumiaji wa mifumo katika utengenezaji/ ununuzi wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA

Kwa mujibu wa muongozo wa Usimamizi wa miradi ya TEHAMA wa eGAZ 2022 kifungu 5.1.3 kinaeleza kwamba Kuwepo na ushirikishwaji wa wadau katika utengenezaji wa mifumo ili kuepusha uwepo wa mifumo isiyokuwa na tija.

Ukaguzi umebaini kwamba uongozi wa Mamlaka haukuwashirikisha wataalamu wake wa TEHAMA pamoja na watumiaji katika ununuzi wa mifumo pamoja na ujenzi wa miundombinu ya TEHAMA ambapo imebainika kwamba mifumo mingi iliyopo haifikii malengo kwa kukosekana utendaji kazi wa mifumo na miundombinu hiyo kama ilivyokusudiwa, miongoni mwa mifumo hiyo ni mfumo wa POSHO Plus, Parking system iliyopo Pemba, Parking System iliyokuwepo Terminal 3 ambayo ilitengenezwa katika mkataba wa BCEG, Special Airport Systems kutoka kampuni ya M/S Collin Aerospace pamoja na Mfumo wa LDCS kutoka URIELSOFT, Aidha ukaguzi umebaini kwamba Uongozi wa ZAA haukuwashirikisha wataalamu wa TEHAMA katika ujenzi wa utanuzi sehemu ya kuwasili kwa Abiria (Arrival Area) Terminal 3 ambapo kulifanyika ukarabati uliohusisha miundombinu ya TEHAMA iliyosimamiwa na wataalamu kutoka nje ya Taasisi.

Kutowashirikisha wataalamu wa TEHAMA pamoja na watumiaji wa mifumo (end users) kunapelekea kukosa nafasi ya kuweza kushauri namna bora ya utengenezaji na usimamizi wa mifumo pamoja na miundombinu ya TEHAMA na kuisababishia hasara kwa serikali kwa kutafuta mifumo mengine ambayo imekuwa na gharama kubwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar kuhakikisha kwamba kabla ya ununuzi wa mifumo ya TEHAMA kuwepo na ushirikishwaji wa wataalamu wa TEHAMA pamoja na watumiaji wa mifumo (end users) katika kushauri njia bora za ununizi wa mifumo hiyo ili kuepuka za upotevu wa mali za serikali.

### 4.1.7.6 Dosari zilizobainika katika ulinzi wa CCTV Camera ndani ya mipaka ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (ZAA) Pemba

Ukaguzi umebaini kwamba ZAA haina ulinzi imara wa mipaka yake ambapo imegundulika CCTV Camera zilizofungwa hazifanyi kazi kama ilivyokusudiwa baada ya kushindwa kutambua wizi uliofanyika wa Taa za kuongozea ndege ambazo zimefungwa ndani ya Mipaka ya uwanja huo wa Pemba.

Kushindwa kufanyakazi kwa Kamera za ulinzi ni kuhatarisha usalama wa miundombinu ya TEHAMA ambayo imewekwa katika maeneo yote ya Uwanja wa Ndege pamoja na rasilimali muhimu za Taasisi ambazo zinahitaji ulinzi imara ili kuweza kuchunguza matokeo ya uhalifu na pia kutumika kama ushahidi wa utoaji vielelezo panapo hitajika.

Ukaguzi unashauri kwamba ZAA ihakikishe Camera za ulinzi zinawekwa katika maeneo muhimu ambazo zitakuwa na uwezo wa kuhifadhi matukio kwa muda mrefu pamoja na uwepo wa Camera katika maeneo yote muhimu ili kuepusha matukio ya uhalifu katika mipaka ya viwanja hivyo.

#### 4.1.7.7 Dosari zilizobainika ambazo huathiri utendaji kazi wa kitengo cha TEHAMA

Ukaguzi umebaini dosari mbalimbali ambazo zimesababisha uzorotaji wa shughuli za kiutendaji katika kitengo cha TEHAMA ZAA, miongoni mwa dosari hizo ni Ukosefu wa Ofisi za kufanyia kazi kwa upande wa Unguja na Pemba jambo ambalo limepelekea wafanyakazi hao kufanya kazi zao katika maeneo yasio rasmin, Aidha Ukaguzi umebaini pia ukosefu wa Wafanyakazi wa Kitengo cha TEHAMA ambapo baadhi ya wafanyakazi ambao ni wataalamu wa TEHAMA wameondolewa katika nafasi zao za TEHAMA na kuwekwa sehemu ya maegesho (Parking) jambo ambalo linadumaza ufanisi wa TEHAMA katika mamlaka hiyo.

Kukosekana kwa Ofisi za kufanyia kazi kwa wafanyakazi wa TEHAMA kunaweza kupunguza ufanisi kwa watendaji wa kitengo cha TEHAMA na kusababisha ugumu katika kushughulikia changamoto za kila siku, vile vile kuondoa wafanyakazi wa TEHAMA katika nafasi zao na kuwapeleka eneo la maegesho (Parking) ni kudumaza taaluma za wafanyakazi hao na pia kuongeza mzigo kwa wafanyakazi wachache waliobaki katika kitengo hicho jambo ambalo linapelekea kwa baadhi ya kazi kufanywa na Wataalamu kutoka Taasisi za nje.

Ukaguzi unaushauri kwa uongozi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kuhakikisha kwamba wafanyakazi wa TEHAMA wanawekewa mazingira rafiki ya kufanyia kazi kwa kupatiwa afisi ambazo zitaendana na mazingira yao ya kufanyia kazi ili kuwapa hamasa wafanyakazi hao ya kuweza kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi, aidha uongozi wa ZAA unashauriwa kwamba kuwarejesha wafanyakazi wa TEHAMA katika nafasi zao na kuwatumia ipasavyo katika kuimarisha miundombinu katika Taasisi hiyo jambo litapunguza uhitaji wa wataalamu wa kufanya kazi kutoka taasisi za nje.

#### 4.1.7.8 Kukosekana kwa Muunganiko wa moja kwa moja wa Mifumo yote ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (Intergration)

Ukaguzi umebaini dosari ya kutokuunganishwa kwa mifumo ya TEHAMA ya ZAA na mifumo ya Mamlaka nyengine za Serikali ambapo mfumo wa ZAAID pamoja na Car Sticker ambayo inayokusanya mapato haijaunganishwa na mfumo wa ZANMALIPO pamoja na mifumo ya kibenki, Aidha katika Website ya ZAA ina module ya ratiba za ndege pamoja na moduli ya ubadilishaji wa fedha lakini moduli hizo hazijaunganishwa na mifumo inayohusiana na utoaji wa taarifa hizo na kupelekea moduli hizo kuwa tupu ama kuingizwa taarifa kwa njia ya kawaida.

Kutounganishwa kwa mifumo kunapelekea utoaji wa Taarifa zisizokuwa sahihi jambo ambalo ni kuitia doa mamlaka hiyo kwa wale ambao wanatembelea website ya ZAA ambapo baadhi ya taarifa zilizoingizwa hazina ukweli ndani yake.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya viwanja vya Ndege Zanzibar **(ZAA)** kufanya mchakato wa kuunganisha mifumo moja kwa moja ili kuweza kupata taarifa zilizo sahihi na kuepuka kutoa taarifa ambazo hazina usahihi ndani yake.

#### 4.1.7.9 Mapungufu yaliyobainika katika moduli ya utoaji ripoti katika Mfumo wa SAS (Special Airport System)

Mfumo wa SAS ambao ndani yake umekusanya jumla ya mifumo mitano nayo ni FIDS, LDCS, AODB, CUPPS na CUSS, mifumo ambayo hutumika ndani ya uwanja wa ndege katika usimamizi wa operesheni za ndege na taarifa zake zote.

Ukaguzi umebaini kwamba kitengo cha Marshaller kimepewa uwezo wa kuona taarifa zilizomo ndani ya mifumo ya SAS (read only) jambo ambalo limepelekea kukosa uwezo wa kuzitoa taarifa hizo kwa njia ya kuprint au kuhamisha kwa njia nyengine, vile vile taarifa hizo huhitajika kwenye kitengo cha Biashara kwa ajili ya ukusanyaji wa mapato yatokanayo na operesheni hizo za ndege lakini kitengo hicho hakikupewa uwezo wa kuingia ndani ya mfumo huo.

Kukosekana kwa ripoti zinazotokana na mfumo kunaweza kupelekea upatikanaji wa taarifa zisizo sahihi ambazo hutumiwa na Marshaller na kitengo cha biashara katika ukusanyaji wa mapato yatokanayo na operesheni za ndege.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAA kuhakikisha kwamba kitengo cha Marshaller pamoja na kitengo cha biashara kupatiwa ruhusa ya kuingia ndani ya mfumo pamoja na uwezo wa kutoa ripoti ambazo zitawezesha kutumika katika shughuli mbali mbali ndani ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege.

#### 4.1.7.10 Mapungufu yaliyobainika katika moduli ya uingizaji wa taarifa katika mifumo ya ZAA

Ukaguzi umebaini kwamba mfumo wa Car Sticker pamoja na ZAA ID inaruhusu uingizaji wa taarifa muhimu ndani ya mfumo kwa njia ya kawaida (manual) ambazo ni tarehe ya kuanza matumizi pamoja na tarehe ya kumaliza matumizi jambo ambalo linasababisha uingizaji wa taarifa zisizo sahihi na kuathiri utendaji kazi wa mfumo kwa kuongeza au kupunguza tarehe ya kumaliza kwa kitambulisho.

Uingizaji wa tarehe ya kuanza matumizi na tarehe ya kumaliza matumizi kwa njia ya kawaida ni kutengeneza mazingira yasiokuwa mazuri kwa watumiaji wa mifumo hiyo kwa sababu inawezekana ikaongezwa muda mrefu zaidi au kupunguzwa muda zaidi wakati vitambulisho vinatakiwa viwe na Tarehe maalum iliyopagwa na Uongozi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kuhakikisha mfumo wa ZAA ID pamoja na Mfumo wa Car Sticker inarekebishwa sehemu ya kuanza na kumaliza kwa matumizi ya vitambulisho ili kuondosha dosari za kuongeza ama kupunguzwa kwa muda wa matumizi.

#### 4.1.7.11 Mapungufu yaliyobainika katika miundombinu ya Mtandao (Network Kutokutofautisha Anuani ya Mtandao (Network Segmentation)

"Network Segmentation" ni mkakati wa kugawanya mtandao katika sehemu ndogo zinazojitegemea (Vlans/Segments) ili kuboresha usalama, utendaji, na usimamizi wa mtandao. Lengo kuu la "Network Segmentation" ni kuzuia upanuzi wa mashambulizi ya kimtandao na kudhibiti ufikiaji wa rasilimali za mtandao kwa njia iliyopangwa.

Ukaguzi ulibaini kuwa ZAA haijatekeleza utaratibu wa kugawa mtandao katika sehemu ndogo ndogo zinazojitegemea kwa lengo la kuboresha utendaji na usalama katika majengo ya "Terminal 1 and 2". Hali hii inakwenda kinyume na kifungu nambari 6.3.5 cha Muongozo wa Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar wa mwaka 2022 unaoelekeza taasisi za Umma kugawanya mtandao unao hifadhi mifumo muhimu (Critical System) na mtandao wa matumizi ya kawaida.

Aidha, kukosekana kwa "Network Segmentation" kumesababisha ZAA kushindwa kuwa na Mtandao wa Wageni (Guest Wi-Fi) kwa lengo la kuwawezesha wageni wa ZAA wanaokwenda katika Viwanja hiyo kama wasafiri/ wateja au wageni kuwa na ufikiaji wa huduma ya mtandao (Guest Wi-Fi services) bila kuathiri mifumo na rasilimali nyengine muhimu za Taasisi kama vile Seva n.k.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAA kuhakikisha kwamba unatekeleza" Network Segmentation" pamoja na uanzishwaji wa Mtandao kwa ajili ya wageni (Guest Wi-Fi) ambao hautakuwa na muingiliano wa moja kwa moja na mtandao mkuu wa Taasisi.

### 4.1.7.12 Kukosekana kwa zana za kisasa za kufuatilia utendaji wa mtandao (Modern Network Monitoring Tools)

Zana za ufuatiliaji wa Mtandao ni zana zinazoweza kufuatilia mtandao kwa wakati halisi (real time monitoring) na kutoa taarifa ya haraka juu ya utendaji kazi na hali ya Afya ya mtandao (Network health) kwa muda wa masaa 24 siku 7 za wiki. Zana hizi huruhusu taasisi kufanya ufuatiliaji wa mtandao na kudhibiti mapungu mbalimbali kabla hayajatokea (pro-active measures) na kusaidia kuongeza ufanisi wa mtandao unaopelekea kuongeza tija katika utumishi kwa kutumia TEHAMA. Miongoni mwa athari za moja kwa moja zinazoweza kuifika ZAA ni pamoja na ucheleweshwaji wa kubaini matatizo ya mtandao na kupelekea kuchelewa kutoa ufumbuzi wa tatizo husika hali inayoweza kukwamisha utoaji wa huduma kwa jamii. Kukosa fursa za kufanya maboresho ya mfumo wa mtandao kwa kukosa taarifa muhimu ambazo zingeweza kupatikana kupitia zana za ufuatiliaji wa mtandao.

Vile vile kushindwa kubaini matatizo na kutoa ufumbuzi kabla hayajatokea (pro-active measures) na badala yake kungojea mpaka matatizo yatokee kisha ndipo ZAA ianze kutafuta chanzo na ufumbuzi wake hali inayoweza kuchukuwa muda mrefu wananchi wakiendelea kukosa huduma muhimu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAA kuhakikisha unatenga bajeti na fedha toshelevu na kununua zana za kisasa za kusimamia mfumo wa mtandao na miundombinu yake yote kwa wakati halisi (real time network monitoring tools) kwa haraka iwezekanavyo ili kuepusha dosari zinazoweza kutokea kama zilivyoainishwa hapo juu.

#### 4.1.7.13 Kukosekana kwa usimamizi wa "Bandwidth katika Afisi za "Terminal 1 na 2".

Usimamizi wa "bandwidth" ni mbinu au mchakato wa kudhibiti matumizi ya upana wa kipimo data (bandwidth) kwenye mtandao. Lengo la "bandwidth management" ni kudhibiti, kupanga, na kutoa kipaombele cha traffic ya mtandao ili kutumika kwa njia inayofaa na kutimiza mahitaji ya mtandao kwa Taasisi.

Ukaguzi ulibaini kutokuwepo kwa utaratibu wa kudhibiti upatikanaji wa "bandwidth" kwa watumiaji katika Mamlaka ya Viwanja vya ndege Zanzibar katika afisi za "Terminal" 1 na 2. Aidha ZAA haijaweka mfumo wa kuwathibitisha watumiaji wa mtandao, jambo linalo ongeza changamoto ya upatikanaji wa huduma iliyo bora, salama na ya uhakika katika utekelezaji wa majukumu ya afisi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAA kuweka utaratibu wa kudhibiti upatikanaji wa huduma ya kimtandao upande wa Terminal 1 na 2, ikiwa ni pamoja na kuweka njia za kuwathibitisha watumiaji (User Authentication) kabla ya kuanza kupata Huduma.

#### 4.1.7.14 Mapungufu yaliyobainika katika miundombinu ya Mtandao (Network Infrastructure) katika afisi za ZAA Terminal 3

Kwa mujibu wa miongozo ya Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar kama vile "E- Government Guidelines, 2022", Internet "Usage Guidelines, 2022", Sera ya Taifa ya TEHAMA kwa taasisi za Umma ya mwaka 2013 pamoja na Miongozo ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzani (TCRA) kama vile Internet Service Providers Minimum Security Guidelines wa 2019 zinahitaji taasisi za umma kuweza kudhibiti kwa kuimarisha miundombinu ya mawasiliano ya mtandao ili kuongeza kasi ya upatikanaji wa mtandao, ufanisi na weledi wa utendaji kazi pamoja na kuongeza usalama katika matumizi bora ya mtandao.

Kwa kuzingatia mkataba wa makubaliano ya huduma za Mtandao uliotiwa saini mwezi wa Aprili 2022 baina ya Zantel na ZAA ni kwamba ZAA atapata huduma ya kutumia Mtandao wa Internet "Dedicated bandwidth Internet" yenye kasi ya 150Mbps kutoka kwa Kampuni ya Zantel ambapo kwa kila mwezi atalipia jumla ya USD 1,620.

Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kwamba ZAA amefungiwa miundombinu na kupatiwa huduma hiyo tangu mwezi wa Julai 2022 lakini haitumii huduma hiyo, na badala yake Kampuni ya DNATA ambayo ni Muwekezaji katika Uwanja wa Ndege Terminal 3 ndiyo inayotumia huduma hii bila ya makubaliano na Mtoa huduma (Zantel) na bila ya kulipia huduma hiyo.

Hivyo, ukaguzi haukupatiwa ushahidi wa nyaraka zinazohusiana na makubaliano ya kuhamisha huduma ya matumizi ya Mtandao kutoka ZAA kwenda kwa Kampuni ya DNATA jambo ambalo ni kinyume na makubaliano ya mkataba.

Kutokana na makubaliano ya bei yaliyofikiwa baina ya ZAA na Zantel katika Mkataba wa Huduma ya Mtandao ambapo kwa kila mwezi ZAA atalipia USD 1620, hivyo ZAA imetakiwa kulipa gharama zenye jumla ya USD 24,310.5 sawa na wastani wa shilingi 61,384,012.5 ($24,310.50*2,525.00) ikiwa ni deni kwa kipindi cha miezi 15 kutoka Zantel, jambo ambalo linaweza kuingiza hasara Serikali pindipo ZAA atakapolilipa deni hili bila ya kuishirikisha kampuni ya DNATA.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAA kuhakikisha kuwa unafanya ufuatiliaji wa karibu wa utaratibu wa malipo ya deni hilo kwa kuhakikisha kwamba DNATA ndio atakaewajibika kulipa deni hilo pamoja na adhabu yoyote itakayojitokeza pindipo litakapopata suluhu ya malipo.

Aidha ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAA kuongeza udhibiti na kuwa makini katika matumizi ya miundombinu na rasilimali za TEHAMA kwa shughuli za Serikali.

### 4.1.7.15 Dosari katika utoaji wa huduma za Internet kwa Kampuni za Ndege shilingi 50,373,750

Katika kufanya mapitio ya udhibiti wa miundombinu ya Mtandao wa ZAA ukaguzi ulibaini kwamba kupitia Terminal 3 ZAA inatoa huduma ya "Internet" kwa Makampuni takribani 5 ambayo ni: -

a) Luthansa
b) Air France / KLM
c) Qatar Airways
d) ZAT
e) Transword Zanzibar

Ukaguzi ulibaini kwamba ZAA haikuwa na makubaliano ya kimkataba kama vile "MoU" yaliyofunganishwa baina ya pande mbili hizo jambo lilipelekea ukaguzi kushindwa kufanya tathmini ya utekelezaji wa haki na wajibu wa kila upande katika utoaji wa huduma hiyo.

Aidha ukaguzi haukuweza kubaini kiwango cha "internet" kilichotakiwa kusambazwa kwa kila kampuni kwa mujibu wa makubaliano ili kufanya tathmini ya hali halisi, bei zilizokubaliwa na pande zote mbili, muda wa huduma pamoja na kupima utekelezaji kwa mujibu wa makubaliano hayo.

Mbali na hayo ukaguzi haukupata ushahidi wa uwepo wa malipo yoyote yaliyofanywa na Kampuni za Ndege kutokana na huduma ya Internet iliyokuwa zikipatiwa kutoka kwa ZAA.

Hivyo, baada ya kufanya mapitio ya kiwango halisi cha "internet" inayosambazwa kwa Makampuni hayo 5, na kwa kuzingatia muda ambao ZAA imekuwa ikitoa huduma hiyo, ukaguzi ulibaini kwamba ZAA imepata hasara ya zaidi ya zaidi ya USD 19,950 sawa na wastani wa shilingi 50,373,750 ($19,950.00*2,525.00) kutokana na kushindwa kutoza tozo ya huduma ya mtandao kwa kampuni hizo. Msingi wa hasara ya bei tajwa umepatikana kutokana na mlinganisho wa bei za ZICTIA zinazotozwa kwa Taasisi mbali mbali za Umma.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAA kuandaa mkakati imara wa kufanya ufuatiliaji wa madeni wanayodai kwa Kampuni za Ndege kutokana na kuwapatia huduma ya Internet ili kupata fedha kwa ajili ya kufanya shughuli zake nyengine ikiwemo kulipa madeni inayodaiwa na Taasisi mbali mbali.

Mchanganuo wa msingi wa bei za huduma za internet kutoka kampuni ya ZICTIA pamoja na madeni ambayo ZAA inadai ni kama inavyoonekana katika picha na jadweli hapo chini:-

## Picha Nambari 6: Mpangilio wa bei za huduma ya Mtandao (Internet) kutoka ZICTIA

SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

ZICTIA

Zanzibar Information Communication Technology Infrastructure Agency

SLP 1823
Mtaa wa Mazizini,
Zanzibar.
+255 24 2235784
info@zictia.go.tz

**GHARAMA ZA INTERNET**

| S/N | SERVICE LEVEL | Gharama ya Mbps moja kwa mwezi. |
|---|---|---|
| 1. | 1 Mbps - 10 Mbps | 35 USD/1Mbps |
| 2. | 11 Mbps - 50 Mbps | 30 USD /1 Mbps |
| 3. | 51 Mbps - 100 Mbps | 25 USD / 1Mbps |
| 4. | 101 Mbps and more | 20 USD /1Mbps |

## Jadweli Nambari 36: Uchambuzi wa bei na Kiwango cha huduma za "Internet" kwa Kampuni za Ndege kwa kipindi cha zaidi ya miezi 12

| Jina la Kampuni | Kiwango cha Data | Muda wa Huduma (Miezi) | Kiwango cha Huduma kwa Mwezi (ZICTIA) | Jumla ya Gharama (USD) |
|---|---|---|---|---|
| Luthansa | 10Mbps | 12 | 350 | $5,250 |
| Air France / KLM | 10Mbps | 12 | 350 | $5,250 |
| Qatar Airways | 10Mbps | 12 | 350 | $5,250 |
| ZAT | 5Mbps | 12 | 175 | $2,100 |
| Transword Zanzibar | 5Mbps | 12 | 175 | $2,100 |
| **Jumla** | | | | **$19,950** |

### 4.1.7.16 Kutozingatia utaratibu wa utowaji huduma ya kukodisha maeneo ya uhifadhi wa vifaa ya elektroniki (Collocation Services) shilingi 142,500,000

Ukaguzi ulibaini kwamba ZAA inatoa huduma ya kuhifadhi vifaa vya kielektroniki kwa makampuni binafsi ndani ya chumba cha mitambo (Control Room) kinachopatikana ndani ya Jengo la "Terminal 3". Makampuni yaliyokodishiwa maeneo ya kuhifadhi vifaa vya kielekitroniki ni pamoja na: -

- Dnata,
- Zanlink
- TTCL
- ComNet
- Fly Dubai
- Qatar Airways
- Oman Air

Aidha ukaguzi ulibaini kuwa ZAA haina makubaliano rasmi kama vile Mikataba/ MoU inayoainisha haki na wajibu wa pande zote za makubaliano kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za Manunuzi.

Aidha, ZAA haikuweza kuupatia ukaguzi nyaraka zinazothibitisha malipo kufanywa na Makapuni hayo kwa ZAA hali inayoashiria uvujifu wa mapato ya Serikali yanayotokana na huduma hiyo inayotolewa na ZAA kwa Makampuni hayo.

Kwa kutumia miongozo na Viwango vya bei za huduma ya uhifadhi wa vifaa vya kielektroniki inayotolewa na ZICTIA ukaguzi uliweza kubaini uwepo wa hasara ya zaidi ya shilingi 142,500,000 kutokana na ZAA kushindwa kuwalipisha Tozo ya huduma za uhifadhi wa mitambo "Collocation Services" kwa kampuni hizo kwa kipindi cha miezi 15.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAA kuhakikisha kuwa ina miongozo inayobainisha utoaji wa huduma hizo pamoja na malipo yake kwa mujibu wa miongozo ya Serikali. Mchanganuo wa majadweli yanayoonesha bei kulingana na miongozo ya ZICTIA ni kama inavyooenaka katika majadweli hapo chini:-

## Jadweli Nambari 37: Viwango vya gharama za uhifadhi wa vifaa vya kielekroniki (Charges for Coolocation Services) kutoka ZICTIA.

1. **Product Specifications & Tariff**

1.1 **Co-location:**

| Space | Commercial Name | One-Time cost | Monthly Recurring Cost | 20% Monthly Discount for Government |
|---|---|---|---|---|
| 1 U | Basic | 200,000.00 | 500,000.00 | 400,000.00 |
| Half Rack | Standard | 400,000.00 | 2,500,000.00 | 2,000,000.00 |
| Full Rack | Premium | 600,000.00 | 4,500,000 | 3,600,000.00 |
| | | | | |

## Jadweli Nambari 38: Huduma za kuhifadhi vifaa vya kielekroniki zinazotolewa na ZAA kwa makampuni binafsi pamoja na makadirio ya gharama kwa kipindi cha miezi 15.

| Company Name | Co-location Plan | Service Period (Months) | Service Price Per Month (Tzs) | Total Cost (Tzs) |
|---|---|---|---|---|
| DNATA | Full Rack | 15 | 4,500,000 | 67,500,000 |
| Zanlink | 1U | 15 | 500,000 | 7,500,000 |
| Comnet | 1U | 15 | 500,000 | 7,500,000 |
| Qatar Airways | Half Rack | 15 | 2,500,000 | 37,500,000 |
| TTCL | 1U | 15 | 500,000 | 7,500,000 |
| Fly Dubai | 1U | 15 | 500,000 | 7,500,000 |
| Oman Air | 1U | 15 | 500,000 | 7,500,000 |
| **Total** | | | | **142,500,000** |

### 4.1.7.17 Kutokuwepo kwa Mfumo wa Ufuatiliaji wa utendaji kazi wa vifaa katika wakati Halisi na kuripoti "Online Realtime Tracking and Reporting System".

Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (ZAA) imefunga vifaa vya kiusalama katika maeneo mbali mbali ikiwemo eneo la kupita abiria wanaosafiri kwenye Viwanja hivyo vya Unguja **(AAKIA)** pamoja na Pemba **(Pemba Airport)** ambapo ndani yake kuna mashine za ukaguzi wa abiria kama vile X-Ray scanner, CCTV Camera, Metal Detector n.k.

Ukaguzi umebaini kwamba Mamlaka ya viwanja vya Ndege haina mfumo wa ufuatiliaji wa vifaa ambao utaweza kugundua kama kifaa kina uwezo mzuri wa kufanya kazi au kina matatizo ambapo kwa upande wa Pemba Generator limeshindwa kufanya kazi wakati umeme ulipozimwa na kupelekea Abiria waliosafiri kukaguliwa (checking) kwa njia ya kawaida (manual) jambo ambalo linaweza kuleta hatari ya kiusalama wa abiria kwa kusafiri na vitu visivyofaa endapo mkaguzi atashindwa kugundua vitu hivyo, Aidha Mashirika ya Ndege yalitoa hati ya kusafiria (boarding pass) kwa njia ya kawaida (manual) na vile vile kushindwa kutumia computer zao ambazo zina taarifa zote muhimu za abiria na vile vile Kamera za ulinzi zilishindwa kufanya kazi kwa kukosa umeme jambo ambalo linaweza kupelekea hatari kubwa za kiusalama.

Dosari za kiusalama zilizotajwa hapo juu zinaweza kusababisha hatari ya kiusalama wa abiria kwa kusafiri na vitu ambavyo haviruhusiwi kisheria.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar kuongeza usalama na kuboresha kwa ujumla katika sehemu zote za Mamlaka hiyo na kuhakikisha kwamba mashine za kuzalisha umeme (generators) ziweze kufanya kazi muda wote ambapo kutatokea hilitafu ya umeme ili vifaa vya ulinzi vifanye kazi kwa muda wote kama ilivyokusudiwa.

### 4.1.8 TAASISI YA VIWANGO ZANZIBAR (ZBS)

Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 4.1.8.1 Kutokuwepo kwa muongozo wa kusimamia utekelezaji wa Miradi ya TEHAMA (ICT Project Management Policy/ Guideline)

Kinyume na matakwa ya Miongozo ya Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar pamoja na viwango bora kubalifu vya TEHAMA, Ukaguzi ulibaini kwamba ZBS haina muongozo wa kusimamia utekelezaji wa Miradi ya TEHAMA.

Kukosekana kwa muongozo huu kunaweza kupelekea Taasisi kukosa thamani ya fedha zinazowekezwa katika miradi ya TEHAMA kuathiri matumizi endelevu ya mifumo, kutofanyika majaribio ya mifumo kabla ya kuanza kutumika rasimi katika kazi za uzalishaji, kukosekana kwa mpango wa kudhibiti gharama za miradi na kusababisa miradi kutumia fedha nyingi zisizo akisi uhalisia n.k.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZBS kusimamia utengezwaji wa muongozo wa kusimamia utekelezaji wa miradi ya TEHAMA kwa kuzingatia miongozo ya eGAZ na viwango bora kubalifu vya TEHAMA kwa uharaka unaostahili na kuhakikisha kwamba muongozo huo unatumika katika utekelezaji wa miradi mbali mbali ya TEHAMA ya ZBS.

#### 4.1.8.2 Udhaifu wa udhibiti wa kimazingira katika miundombinu ya mtandao wa ZBS

Katika kufanya mapitio ya udhibiti wa kimazingira katika miundombinu ya mtandano wa ZBS tulibaini uwepo wa mapungufu mbalimbali yanayoweza kuathiri Usiri, Uadilifu na Upatikanaji wa mifumo ya TEHAMA kinyume na miongozo ya viwango bora kubalifu vya TEHAMA (best practice), miongoni mwa mapungufu hayo ni: -

Uwepo wa mpangilio duni wa waya za mtandao (ethernet cables) katika makabati (cabinates/ racks) yaliyopo kwenye afisi za ZBS Chake Chake. Hali hii inachangia kuongeza ugumu wa utatuzi wa changamoto za mtandao katika miundombinu ya mtandao wa ZBS. Aidha, udhaifu huu unaweza kudhoofisha ufanisi wa mtandao katika mawasiliano hususani pale "Fiber Optic Cables" zinapokunjwa kunjwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZBS kuzingatia miongozo ya viwango bora kubalifu (best practice) katika kufanya mpangilio wa vifaa na nyaya za mtandao ambapo kila kifaa na aina ya nyaya za mtandao zina utaratibu wake wa "handling" katika kabati (cabinet) za taasisi ikiwa ni pamoja na kuzipatia utambulisho kwa kuziwekea majina au kodi (codes) zinazozitambulisha ili kufahamika kutoka kwenye Seva/ Rack mpaka kwenye "face plate", aidha, kwa upande wa usimamizi na matunzo ya "fiber optic cables" ni lazina ziwe handled kwa kuzingatia "how delicate they are" kwenye utendaji kazi wake.

### 4.1.9 KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA

Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 4.1.9.1 Kutokufanyika kwa mafunzo ya Mfumo wa ZAMIS

Kwa mujibu wa makubaliano ya Mkataba wa utengenezaji wa Mfumo wa ZAMIS kifungu 8.2 (ix), kimeeleza kwamba "DataVision itatoa mafunzo kwa wafanyakazi juu ya nanma ya uendeshaji wa mfumo, uhifadhi wa taarifa (Backup), kusanidi (configure) na kadhalika.

Ukaguzi umebaini kwamba Kampuni ya DataVision haijatoa mafunzo kwa wafanyakazi wa Kamisheni juu ya matumizi bora ya mfumo wa ZAMIS jambo ambalo limepelekea watendaji wa Kamisheni kushindwa kutambua namna bora ya matumizi ya mfumo huo.

Kushindwa kutoa mafunzo ya namna bora ya kutumia mfumo wa ZAMIS ni kwenda kinyume na makubaliano ya utengenezaji wa mfumo kifungu namba 8.2(ix) ambapo kampuni hiyo imeelekeza kwamba itatoa mafunzo kwa wafanyakazi wa Kamisheni juu ya namna bora ya matumizi ya mfumo wa ZAMIS.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Zanzibar kuhakikisha kwamba Kampuni ya DataVision inatoa mafunzo kwa watendaji wake juu ya namna bora ya matumizi ya mfumo ambao utatumika katika shughuli mbalimbali za kamisheni hiyo.

#### 4.1.9.2 Kukosekana kwa Seva ya kuhifadhia mifumo ya TEHAMA

Ukaguzi umebaini kwamba Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Zanzibar haina Seva ya kuhifadhia mifumo, ambayo ingetumika kuhifadhia mifumo, kufanya majaribio ya mifumo kabla ya kutumika rasmin (live enviroment), kufanya mafunzo ya mifumo kwa watumishi wa Taasisi, kufanya uhifadhi wa taarifa za mifumo (System Backup) na kadhalika.

Kukosekana kwa Seva ya uhifadhi wa mifumo katika Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana kumepelekea mifumo ya Kamisheni kuhifadhiwa katika Taasisi ya ZICTIA na mifumo mengine kuwekwa katika domain ya Taasisi na endapo ikitokea sehemu za kuhifadhia mifumo hiyo imeharibika Kamisheni itashindwa kupata kumbukumbu zilzomo ndani ya mifumo hiyo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana kuhakikisha kwamba kunapatikana Seva ya kuhifadhia mifumo (Application Server) pamoja na seva ya kuhifadhia kumbukumbu za Mifumo (backup server) ili kuweka udhibiti kamili wa Taarifa za wakfu zitakazoingizwa ndani ya Mifumo hiyo.

#### 4.1.9.3 Kukosekana kwa nyaraka muhimu za Utengenzwaji wa Mfumo

Kwa mujibu wa Muongozo wa eGA nambari **eGA/EXT/BSA/008** wa Utekelezwaji wa Miradi ya TEHAMA, wa mwaka 2020 unahitaji mradi wa TEHAMA unapotekelezwa lazima ufuate taratibu na mbinu "Methodology" ya Project Development Life Cycle (PDLC) . Mbinu hiyo imekusanya hatua tofauti za mchakato wa utengenezwaji wa mfumo.

Aidha, kifungu nambari 2.3 cha muongozo huo kimefafanua kwamba kwa kila hatua kutakuwa na matayarisho ya nyaraka ambazo zitasaidia katika utengenezwaji, uendeshaji, usimamizi na udumishaji wa mfumo.

Baada ya kukamilika kwa mradi kutakuwa na mpango wa kusimamia na kudumisha mradi ili kuweza kufanya kazi kwa ufanisi na kuendelea kutoa huduma bora kama ilivyokusudiwa.

Ukaguzi uliomba nyaraka mbali mbali za utengenezwaji wa mfumo wa ZAMIS pamoja na mfumo wa Hajj fund, lakini hadi ukaguzi unakamilika baadhi ya nyaraka hazikuweza kupatikana. Miongoni mwa nyaraka zilizokosekana ni kama zifuatazo:-

- Ripoti ya Pendekezo la Mradi (Project Proporsal Report / Business Case) kuhusiana na uanzishwaji wa Mfumo inayoeleza kwa ufupi hatua mbali mbali za utengenezwaji wa mfumo pamoja na kuchambua kwa kina gharama zote za fedha zitakazotumika kwenye kila kipengele cha mradi huo (Project Breakdown Cost).
- Ripoti ya kufanyika kwa Tathmini ya Vihatarishi vya Mradi (Risk Assessment Report).
- Mpango wa kusimamia, kuzikabili na kuziepuka hatari zinazoweza kujitokeza kwenye utekelezaji wa Mradi (Risk Management Plan).
- Ripoti ya hali ya Mradi iliyofikia (Progress Project Report) pamoja na gharama zilizokuwa zimetumika kabla ya kumalizika kwa mradi huo wa utengenezwaji wa mfumo kwa mujibu wa kifungu cha 6.4(a) cha Masharti Maalum ya Mkataba (SCC).
- Ripoti ya uthibitisho wa kukubalika kwa utendaji kazi katika majaribio ya mifumo (UAT Report).

- Ripoti ya Kuhakiki Ubora wa Mfumo (Quality Assurance Report) kwa mujibu wa Mpango wa kusimamia Ubora (Quality Management Plan) uliopo.
- Kodi za kutengenezea Mfumo "Source Codes".
- Barua ya kukubalika Mfumo (Acceptance Letter).
- Muongozo wa mtumiaji wa Mfumo (Application User Manual).

Kukosekana kwa nyaraka hizo kunatoa ishara kwamba kuna udhaifu katika mchakato wa utengenezwaji wa mfumo wa TEHAMA kutokana na kutokuzingatiwa kwa Muongozo wa utekelezaji wa miradi ya TEHAMA wa eGA nambari **eGA/EXT/BSA/008** pamoja na miongozo ya kimataifa ya utengenezwaji wa Mifumo ya TEHAMA (SDLC).

Aidha, kukosekana kwa nyaraka hizo kunaweza kusababisha hatari (risk) ya kutengenezwa mifumo isiyokuwa na tija na ufanisi wa utendaji kazi na kupelekea kushindwa kufikia malengo yaliyokusudiwa jambo ambalo linaweza kusababisha Afisi kuingia gharama za ziada za marekebisho ya mfumo na hatimae kuingiza hasara Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kamisheni ya Wakfu kuhakikisha unazingatia na kufuata kikamilifu miongozo na viwango vinavyokubalika kitaifa na kimataifa katika utekelezaji wa miradi ya TEHAMA. Vile vile, Afisi kuhakikisha nyaraka zote zinazohusika kwenye mfumo zinatengenezwa na kuwekewa kumbukumbu kwa kila hatua ili kupatikana ufanisi katika usimamizi na udumishaji wa mifumo ya TEHAMA ya Afisi.

#### 4.1.9.4 Kuchelewa kukamilika kwa Mradi wa utengenezwaji wa Mfumo

Kwa mujibu wa makubaliano ya utengenezwaji wa mfumo wa ZAMIS yaliyosainiwa tarehe 12 Novemba, 2019 kati ya kampuni ya Data Vision International Limited na Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Zanzibar ambapo kupitia mpango kazi (Revised work plan) wa utengenezaji wa mfumo umeeleza kwamba ifikapo March, 2021 mfumo huo uwe umekamilika kwa ajili ya matumizi.

Ukaguzi umebaini kwamba Mfumo wa ZAMIS haujaanza kutumika hadi sasa kutokana na mapungufu mbali mbali yanayoukabili mfumo huo ambapo imebainika kwamba baadhi ya module hazifanyi kazi na kupelekea changamoto ya kutokamilika kwa usajili wa warithi wa mali za marehemu.

Kushindwa kukamilisha utengenezaji wa mfumo kwa wakati ni kwenda kinyume na makubaliano ya utengenezaji wa mfumo huo ambapo hadidu rejea (TOR) ya utengenezaji wa mfumo wa ZAMIS kifungu namba 4.2 kimeeleza muda wa kukamilika kwa mfumo ni miezi tisa kuanzia utengeneza mpaka kutumika kwake.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana kuhakikisha kwamba mfumo wa ZAMIS unaanza kutumika kama makubaliano ya mkataba yanavyoelekeza ili kuepuka kwenda kinyume na makubaliano hayo.

#### 4.1.9.5 Dosari zilizobainika katika utengenezaji wa Nambari za Malipo (Control Number) zinazotolewa kutoka katika Mfumo wa ZAMIS

Usajili wa mirathi katika mfumo wa ZAMIS haukamiliki mpaka malipo ya fomu ya Tirka yafanyike ambayo ni shilingi 2,000 malipo ambayo yanalipwa kupitia Nambari ya Malipo (Control Number) inayotolewa na mfumo wa ZAMIS na inakuongoza ufanye malipo kupitia namba ya kampuni 40070.

Ukaguzi umebaini kwamba Nambari ya Malipo (Control Number) inayotolewa na mfumo wa ZAMIS haitokani na mfumo wa Serikali wa Malipo (ZanMalipo), vile vile nambari hiyo kama utafanya malipo kupitia bank au mitandao ya simu malipo yako hayatafanyika jambo ambalo linapelekea mfumo kushindwa kuendelea na maombi ya ufunguaji wa fomu ya Tirka. Hali halisi ya ufanyaji wa malipo katika mfumo inaonekana katika picha hapo chini:-

**Picha Nambari 7: Muongozo wa namna ya kufanya malipo katika mfumo wa ZAMIS**




Utengenezaji wa nambari za malipo (control number) kinyume na mfumo wa ukusanyaji wa kielektroniki wa mapato (ZanMalipo) ni kwenda kinyume na muongozo wa **"Kutayarisha Mpango wa Bajeti wa Serikali Kuu"** wa mwaka wa fedha 2023/2024 kifungu namba 2.5(i) kimeeleza kwamba malipo yote ya Serikali yapitie katika mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji wa mapato ZanMalipo, vile vile kufanya hivyo kunaweza kusababisha hatari ya upotevu wa mapato ya Serikali kwa kufanyika malipo nje ya account husika ya Kamisheni.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kamisheni ya Wakfu kuhakikisha kwamba malipo yoyote yatokanayo na Mali ya Amana yapitie katika mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji wa mapato wa ZanMalipo ili kuepusha upotevu na uvujaji wa mapato ya Serikali.

### 4.1.9.6 Kutokukabidhiwa kwa Kodi Asili "Source Code" za Mfumo wa ZAMIS kwa Kamisheni ya Wakfu

Kwa mujibu wa makubaliano ya Mkataba wa utengenezaji wa Mfumo wa ZAMIS kifungu 8.2 (x) kimeeleza kwamba "Miongoni mwa Majukumu ya DataVision ni pamoja na kutoa ama kukabidhi kodi asili (source code) za mfumo wa ZAMIS kwa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana.

Ukaguzi umebaini kwamba Kampuni ya DataVision haijakabidhi kodi asili za mfumo wa ZAMIS ambapo kwa sasa mmiliki halali wa source code hizo ni Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana sio mali ya DataVision.

Kushindwa kukabidhi source code hizo ni kwenda kinyume na makubaliano ya Mkataba wa utengenezaji wa Mfumo wa ZAMIS ambapo kampuni ya DataVision imeweka wazi kwamba itakabidhi source code za mfumo wa ZAMIS kwa Kamisheni ya Wakfu, vile vile kutokukabidhi source code za mfumo wa ZAMIS ni kuonesha kwamba mfumo sio mali ya Kamisheni ya Wakfu isipokuwa umiliki wa Mfumo huo upo kwa DataVision.

Ukaguzi unaikumbusha Kamisheni ya Wakfu kutambua kwamba Source Code za Mfumo wa ZAMIS ni mali yao hivyo basi uongozi wa Kamisheni uhakikishe kwamba uwasilishwaji wa Source Code za mfumo huo unatekelezwa kikamilifu na kukabidhiwa rasmi kwa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana.

### 4.1.9.7 Kukosekana kwa mazingira ya kufanya Majaribio (Test Environment) kwa mifumo ya WAKF

Kwa mujibu wa viwango vinavyokubalika **(Best Practice)** vinaelekeza kwamba kuwepo na mazingira ya kufanya majaribio ya mfumo kabla ya kuanza kutumika kwa lengo la kutambua na kurekebisha hitilafu zozote zinazoweza kuathiri utendaji kazi mzuri wa mfumo au kuathiri matumizi ya mtumiaji. Vile vile ikitokezea mabadiliko katika mfumo, kwanza hutakiwa kufanyiwa majaribio katika mazingira ya majaribio (Test environment) ambapo mfumo wa majaribio unakuwepo pamoja na miundombinu yake, vile vile majaribio yote yanayofanyika huwekewa kumbukumbu za matokeo yake kwa ajili ya kuboresha mfumo katika utendaji wake.

Ukaguzi umeshindwa kupata ushahidi wa uwepo wa mfumo wa mazingira ya majaribio (Test Environment) kwa Mifumo yote ya WAKF jambo ambalo lingepelekea kusaidia sana kufanyiwa maboresho kutokana na mabadiliko yanayojitokeza.

Kukosekana kwa mazingira ya kufanyia majaribio (Test environment) kwa Mifumo ya WAKF ni kwenda kinyume na miongozo inayokubalika (Best Practice) na vile vile kunaweza kusababisha kuchelewa kufanyiwa maboresho ya hitilafu zinazojitokeza kwenye Mfumo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa WAKF kuhakikisha kwamba kunakuwa na mazingira ya Majaribio (Test Enviroment) ambayo yatatoa fursa ya kuona changamoto mbali mbali zitakazojitokeza ndani ya mfumo ili ziweze kutatuliwa na kurahisisha matumizi bora ya mfumo huo.

#### 4.1.9.8 Kutokufanya kazi kwa baadhi ya moduli za mfumo wa ZAMIS

Mfumo wa ZAMIS umekusanya jumla ya moduli kumi na sita (16) ambazo hutumika kwa shughuli zote za usajili wa mali za mirathi ya Kiislamu, katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa baadhi ya moduli hazifanyi kazi vizuri licha ya kwamba mfumo unaendelea kutumika, moduli hizo ni kama zifuatazo:-

- ***Moduli ya kutoa Ripoti "Reporting Module***

Moduli hii ilitarajiwa kutoa ripoti za taarifa za warithi wa Marehemu ikiwemo taarifa za mali za marehemu, idadi ya warithi wa marehemu, madeni ya marehemu, taarifa za kibenki za marehemu, taarifa za wanaodaiwa na marehemu n.k.

Aidha, moduli hii ilitarajiwa kuweza kutoa ripoti hizo kwa vipindi tofauti vinavyohitajika kama vile kwa mwezi, miezi mitatu, miezi sita, kwa mwaka n.k ambapo ripoti hizo zilitarajiwa kupatikana katika mifumo tofauti kama vile mfumo wa pdf, spreadsheet, text file, JSON file, html file, Word file n.k, ukaguzi umebaini kwamba moduli ya ripoti haiwezi kutoa ripoti za jumla kwa marehemu waliosajiliwa ndani ya mfumo.

Hivyo kutokana na kutofanya kazi vizuri kwa moduli hii kunapelekea WAKF kutoweza kupata ripoti za aina tofauti kama zilivyotajwa hapo juu.

- ***Moduli ya usajili katika mfumo wa ZAMIS***

Ukaguzi umebaini kwamba moduli ya usajili ndani ya mfumo wa ZAMIS haipatikani mpaka mtumiaji aanze kujaza taarifa za marehemu kama keshasajiliwa ama bado na endapo marehemu hayumo ndani ya mfumo ndipo moduli ya usajili inapojitokeza na kukupa fursa ya kuanza kujisajili.

- ***Uwepo wa kitufe cha Religion (Dini) wakati wa usajili wa marehemu***

Ukaguzi umebaini kwamba wakati wa usajili wa mirathi, Mfumo wa ZAMIS unakulazimisha kuingiza dini (Religion) ambapo ndani yake kuna jumla ya dini tofauti wakati marehemu huwa ni wa kiislamu wanaoruhusiwa kuingizwa ndani ya mfumo.

Kutofanya kazi vizuri kwa moduli hizo kunasababisha kukosekana kwa baadhi ya Taarifa muhimu kama zilivyobainishwa hapo juu jambo ambalo linaweza kupelekea mfumo kuonekana hauna tija kama ilivyokusudiwa licha ya fedha nyingi kutumika katika utengenezwaji wake.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa WAKF kufanya jitihada za makusudi ili kuweza kuukamilisha mfumo huo katika moduli zote kwa lengo la kuweka taarifa za kiutumishi na bajeti kama ilivyokusudiwa na hatimae kupatikana kwa tija na ufanisi wa utendaji kazi wa mfumo.


#### 4.1.9.9 Mfumo kuonyesha ujumbe unaohusiana na tatizo la kiufundi “Error Message”

Ukaguzi umebaini Mfumo wa ZAMIS umekuwa ukionesha ujumbe wa tatizo la kiufundi kila baada ya muda wakati mtumiaji anapokuwa katika shughuli zake za matumizi ya mfumo huo. Kiuhalisia ujumbe huo wa makosa “error message” hutokea wakati mtumiaji atakapoendea na utaratibu wake wa kujisajili ndani ya mfumo wa ZAMIS. Ujumbe huo unajitokeza katika moduli zifuatazo:-

- Moduli ya Applicantion: Ndani yake kuna moduli mbili lakini moduli ya Applicant list ndani yake kuna kitufe cha Action ambacho kina moduli ya “edit” na “view”, ukibonyeza module ya View mfumo unashindwa kuendelea na kutoa ujumbe (“An error has occured”).
- Moduli ya Deceases: Ndani yake kuna jumla ya moduli saba lakini ni moduli mbili tu zinazofanya kazi nazo ni “Request new form” pamoja na “Heirs List” nyengine ukizifungua zinaleta ujumbe wa “An error has occured”.
- Moduli ya Tirka: Ndani yake kuna jumla ya moduli nne, moduli ya Tirka ndio inafanya kazi zilizobaki ukizifungua zinaleta ujumbe wa (“An error has occured”).
- Moduli ya Will: Ndani yake kuna jumla ya moduli tano ambazo zote hazifanyi kazi na zinaleta ujumbe wa (“An error has occured”).

Hali halisi ya ujumbe unaojitokeza wakati wa utumiaji wa mfumo ni kama unavyoonekana katika picha ifuatayo:-

**Picha Nambari 8: Ujumbe wa "An error has occured unaojitokeza wakati wa utumiaji wa mfumo**




Kushindwa kwa mfumo kufanya kazi kama ilivyokusudiwa ni kutengeneza mazingira ambayo yanaweza kukwamisha juhudi za Kamisheni katika azma yake ya kutumia mfumo ambapo lengo la kutumia mfumo ni kusajili na kuhifadhi taarifa za mirathi ya marehemu wa kiislamu.


Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kamisheni ya Wakfu kuhakikisha kwamba mfumo wa ZAMIS unatumika kama ilivyokusudiwa kwa kusimamia kikamilifu uondoshaji wa changamoto zote zinazoukabili mfumo ambazo zimepelekea mfumo kushindwa kufanya kazi kama ilivokusudiwa.

### 4.1.9.10 Mfumo unashindwa kuingiza taarifa za nyuma za marehemu

Baada ya kukamilika kwa mirathi taarifa za marehemu zinahifadhiwa katika Ofisi za Kamisheni ya Wakfu kama kumbukumbu za miradhi ambapo kama kunatokea changamoto yoyote kwa warithi basi taarifa hizo hutumika kwa kusaidia kuondosha changamoto hizo.

Ukaguzi umebaini kwamba mfumo wa ZAMIS hauna moduli ambayo itawezesha kuingizwa kwa kumbukumbu za mirathi ambazo mchakato wa usajili umeshakamilika ambapo kumbukumbu hizo zipo katika Afisi ya Wakf na zimehifadhiwa sehemu maalum ya kuweka kumbukumbu kwa njia ya mafaili na taarifa hizo hutumika pale ambapo kutajitokeza changamoto yoyote ya mirathi kwa watoto ama wajukuu wa marehemu. Aidha, ZAMIS inaruhusu uingizwaji wa taarifa za mtumiaji mpya ambapo itampa nafasi ya kufungua nambari ya mtumiaji (User account) na kuanza usajili wa kufungua kesi za mirathi. Hali halisi ya ukurasa unaonyesha namna ya mtumiaji wa mfumo anavyoweza kuanza kujisajili ni kama inavyoonekana katika picha hapo chini:-

**Picha Nambari 9: Ukurasa unaonyesha namna ya mtumiaji anavyoanza kujisajili ndani ya Mfumo.**





Kushindwa kuingiza taarifa za marehemu waliopita katika mfumo wa ZAMIS ni kuufanya mfumo huo kutofikia malengo yaliyokusudiwa na WAKF ambayo yalihitaji kupatikana kwa mfumo utakaoweza kuhifadhi nyaraka zote za marehemu kwa njia ya mfumo wa TEHAMA.

Ukaguzi unashauri kwamba WAKF ihakikishe mfumo wa ZAMIS unatengenezewa mazingira ya uwepo wa moduli ambayo itawezesha kuhifadhiwa kwa kumbukumbu za mirathi za marehemu waliopita ili kuiwezesha taasisi hiyo kufikia malengo yake ya kuwa na mfumo wa TEHAMA kama ilivyokusudiwa.

### 4.1.9.11 Mfumo kuchanganya baadhi ya Taarifa za warithi wa marehemu

Ukaguzi umebaini kwamba mfumo wa ZAMIS unachanganya taarifa za warithi wa marehemu waliokuwemo ndani ya mfumo ambapo imebainika kwamba mtumiaji mpya anapojisajili ndani ya mfumo wa ZAMIS atahitajika kuingiza taarifa za warithi wa Marehemu (Hierst list) ambazo zinapatikana katika moduli ya Marehemu (Deceases) katika sehemu ya Heirst List ambapo anahitajika kuingiza orodha ya majina ya marehemu mfumo una chapisha majina ambayo mtumiaji mpya sio ya kwake ambayo yanatokana na mtumiaji mwengine ambae taarifa hizo amekwisha zijaza ndani ya mfumo.

**Picha Nambari 10: Picha inaonesha majina ya warithi waliojitokeza wakati wa usajili wa mfumo**




| Sn | FullName | Gender | Phone | ID Type | ID No | Actions |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Rauhiyya Othman Ali - 0254118899 | FEMALE | 0254118899 | ZANID | 25880014 | Actions |
| 2 | Asha Machano Juma - 0772030606 | MALE | 0772030606 | ZANID | 5053427892101 | Actions |
| 3 | YUSSUF HUSSEIN PANDU - 0773213061 | MALE | 0773213061 | ZANID | 20119000 | Actions |
| 4 | MUSSA OMAR HAJI - 0777638393 | MALE | 0777638393 | ZANID | 9000190 | Actions |

Uchanganyikaji wa taarifa katika mfumo wa ZAMIS hali hii hupelekea kujitokeza kwa changamoto ya usahihi wa taarifa na hatimae kuleta taharuki kubwa kwa warithi wa mali za marehemu pamoja na kupunguza weledi na ufanisi wa utendaji kazi wa mfumo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa WAKF ufanye mapitio ya kina juu ya usahihi wa taarifa pamoja na ufanyajikazi wa mfumo wa ZAMIS ili kutatua changamoto za uchanganyikaji wa Taarifa, ikumbukwe kwamba mfumo wa ZAMIS ndio pekee utakao kuwa na jukumu la kusimamia na kuhifadhi mirathi ya kiislamu.


### 4.1.9.12 Kukosekana kwa Sera pamoja na muongozo wa matumizi ya Neno siri (Password Management Policy)

Kwa mujibu wa Hadidu Rejea (TOR) ya utengenezaji wa mfumo wa ZAMIS, kifungu cha 6 kimeeleza namna ya usimamizi wa Neno siri la mfumo ambapo ndani yake kuna vifungu vifuatavyo:-

- Kifungu 6.1 kimeelezea sera ya nenosiri (Password policy).
- Kifungu 6.1.1 ubadilishwaji wa nenosiri.
- Kifungu 6.1.2, kinaeleza ukubwa wa nenosiri la kuingia ndani ya mfumo.
- Kifungu cha 6.1.3 mahitaji ya nenosiri, ambapo itahitaji kuweka alama, nambari pamoja na herufi za nenosiri.

Ukaguzi umebaini kwamba Kampuni ya DataVision International Limited imeshindwa kwenda sambamba na hadidu rejea (TOR) katika usimamizi wa neno siri, jambo ambalo limepelekea kutokidhi vigezo vya uwepo wa nenosiri kwa kushindwa kuweka vigezo vya ukubwa wa nenosiri (Password), uingizaji wa alama (symbol), herufi pamoja na nambari, ambapo kwa sasa mfumo unaruhusu kuingiza nenosiri lisilozingatia mchanganyiko wa nambari, herufi na alama.

**Picha Nambari 11: Picha inaonesha nenosiri la kuingia ndani ya mfumo wa ZAMIS ambalo ni namba kuanzia moja mpaka nne (1234)**



Kukosekana kwa muongozo wa nenosiri (password policy) kunahatarisha usalama wa taarifa zilizomo ndani ya mfumo kwa kukosekana kwa usalama madhubuti wa ufikiaji wa mfumo ambapo kunaweza kusababisha ongezeko la kuathiriwa kwa nenosiri (password) kutoka kwa wavamizi wa mfumo (intruders).

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kamisheni ya Wakfu kuhakikisha kwamba kunapatika muongozo wa nenosiri na vile vile kuitaka kampuni ya DataVison kulitengeneza vizuri nenosiri ndani ya mfumo wa ZAMIS litakaloendana na matakwa ya sera na muongozo wa nenosiri ili kuimarisha usalama wa kuingia ndani ya mfumo.

### 4.1.9.13 Kukosekana kwa Mfumo wa ZAMIS kwa kutumia Mobile Application

Kwa mujibu wa mkataba wa utengenezaji wa Mfumo kati ya Kamisheni ya Wakf na Kampuni ya DataVision kifungu cha 8.2 g (viii) kinaelezea kwamba kampuni ya DataVision itatengeneza mfumo utakaofanya kazi kwenye simu za mkononi (Mobile Application System) ambao utarahisisha katika ufikiaji wa mfumo kwa wepesi.

Ukaguzi umebaini kwamba Kampuni ya DataVision haijatengeneza mfumo unaofanya kazi kwenye simu za mkononi (Mobile Application System) ambao ungeweza kurahisisha katika usimamizi wa shughuli mbali mbali za utendaji kazi wa mfumo wa ZAMIS.

Kushindwa kutengeneza mfumo unaofanyakazi kwenye simu za mkononi (Mobile Application System) ni kwenda kinyume na makubaliano ya kimkataba ya utengenezaji wa mfumo kati ya Kamisheni ya Wakf na Kampuni ya Datavision ambapo Kamisheni imeshindwa kufikia lengo la kurahisisha utoaji wa huduma kwa wahusika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kamisheni ya Wakfu kuhakikisha kwamba unasimamia kikamilifu makubaliano ya mkataba ikiwemo suala la utengenezwaji wa mfumo unaofanyakazi kwenye simu za mkononi (Mobile Application System) ili kuepuka kwenda kinyume na makubaliano ya mkataba huo.

#### 4.1.9.14 Ukiukwaji wa taratibu za utengenezaji wa Mfumo wa Hajj Found (System Development Life Cycle)

Kwa mujibu wa Viwango vinavyokubalika (Best Practise) vinaitaka taasisi kabla ya kutengeneza mfumo lazima ipitie katika hatua muhimu za utengenezaji wa mfumo (System Development Life Cycle) ambazo zinaelezea hatua muhimu za kufuatwa kabla ya kutengenezwa mfumo. Aidha, nyaraka zote za Mfumo zitatakiwa kutengenezwa na kuekewa kumbukumbu kwa kila hatua ya uandaaji wa Mfumo huo.

Mfumo wa Zanzibar Hajj Found ni mfumo muhimu kuwepo katika Kamisheni ya Wakfu ambao utaweza kuondosha changamoto mbali mbali zinazojitokeza katika usimamizi wa shughuli za Hijja kwa Mahujaji wote wa Zanzibar, ikumbukwe kwamba Kamisheni ya Wakfu ndio msimamizi na mratibu mkuu wa Shughuli zote za Hijja.

Ukaguzi umebaini kwamba Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana inaendelea na mchakato wa utengenezaji wa mfumo wa Zanzibar Hajj Found, aidha ukaguzi umeshindwa kupata nyaraka zozote zinazohusiana na utengenezwaji wa mfumo huo ambazo huelezea utaratibu mzima utakaotumika katika utengenezaji wa mfumo kuanzia hatua ya awali mpaka kukamilika kwake.

Utengenezaji wa mfumo usiozingatia taratibu unaweza kusababisha madhara ya kutokukamilika kwa mfumo kutokana na kubainika kwa changamoto nyingi kulikosababishwa na kukiukwa kwa hatua muhimu za utengenezaji wa mfumo ikiwemo hatua ya ukusanyaji wa maoni ya watumiaji, uandaaji wa nyaraka za mfumo, muda wa kuanza na kumalizika kwa mfumo n.k.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana kuhakikisha kwamba mfumo wa Zanzibar Hajj Found unafuata utaratibu wa hatua muhimu za utengenezaji wa mfumo (System Development Life Cycle) ikiwemo kuandaa nyaraka zote zinazohitajika katika uanzishaji, usimamizi na udumishaji wa mfumo huo ili kuepuka kuwa na mfumo usiokuwa na tija kwa Taasisi.

### 4.1.10 MAMLAKA YA MAPATO ZANZIBAR (ZRA)

Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

## Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi

### 4.1.10.1 Kutoshirikishwa kikamilifu Kitengo cha TEHAMA cha ZRA katika mchakato wa Utengenezwaji wa Mfumo wa ZIDRAS

Kwa mujibu wa utaratibu unaokubalika (best practice) kwenye uanzishwaji wa Miradi ya Mifumo ya TEHAMA kwa Taasisi za Umma unahitaji kuwepo kwa ushirikishwaji uliokamilika kwa watumiaji na wasimamizi wa Mifumo wa TEHAMA kuanzia hatua za awali hadi hatua za mwisho za utengenezaji wa Mifumo ya TEHAMA. Vivile taratibu zinahitaji wasimamizi wa ndani wa mfumo wa TEHAMA kupatiwa elimu kuhusiana na aina ya kodi asili (source codes) zilizotumika kutengeneza mifumo, lugha na jukwaa lililotumika kwenye utengenezaji wa Mifumo (programming language & framework/platform) na vile vile kupatiwa mazingira ya majaribio ya kutengeneza Mifumo (Test Environment) ili kuwaandaa vyema wasimamizi kwa kuwapatia uelewa mkubwa wa kusimamia, kuendesha na kudumisha Mifumo hiyo ili kupunguza gharama kubwa za utegemezi pindipo watakapokabidhiwa rasmi baada ya kukamilika hatua za utengenezwaji.

ZIDRAS ni mfumo wa TEHAMA uliotengenezwa na wataalamu wa ICT kutoka Kampuni ya UBX chini ya usimamizi wa eGAZ, ambapo eGAZ ilisaini mkataba na UBX kwa ajili ya utengenezwaji wa Mfumo huo utakaotumiwa na ZRA kwa shughuli kuu za biashara ya makusanyo ya kodi. Aidha mfumo wa ZIDRAS, umekuja ili kuondosha changamoto na dosari za kiutendaji na kiusalama zilizokuwa zikitokea katika Mfumo wa awali wa ZITAS.

Ukaguzi uliofanyika ulibaini kuwa kitengo cha TEHAMA cha Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) hakikushirikishwa kikamilifu katika mchakato wa utengenezwaji wa Mfumo wa ZIDRAS ambapo imebainika mchakato huo ulikuwa ukifanyika baina ya eGAZ na UBX pekee kwa kipindi kirefu cha utengenezwaji licha ya kuwa Wasimamizi wakuu wa mfumo huo baada ya kukamilika ni Kitengo cha TEHAMA cha ZRA.

Hadi ukaguzi unakamilika, mfumo wa ZIDRAS ulikuwa umeanza kutumika kwa kipindi cha zaidi ya miezi sita nyuma kwa baadhi ya Taasisi lakini Kitengo cha TEHAMA hakikuwa na uelewa juu na Usimamizi, Uendeshaji, Udumishaji na hali ya Usalama wa taarifa za makusanyo ndani ya mfumo pamoja na kanzidata yake.

Kutoshirikishwa kikamilifu kwa Kitengo cha TEHAMA katika michakato ya utengenezwaji wa mifumo ya ndani ya Mamlaka kunaweza kusababisha wataalamu wa ndani ya Kitengo cha TEHAMA kushindwa kudhibiti mifumo ya Mamlaka kikamilifu na kuondokewa na ari, imani, morali na nguvu ya kusimamia mifumo hiyo jambo ambalo litapelekea kushindwa kutoa msaada wa kiufundi kwa watumiaji wa mifumo ndani ya Afisi na hatimae kusababisha kuzorota kwa kazi, kuendelea kutegemea watu wa nje ya Mamlaka jambo ambalo litachochea kuongeza gharama za uendeshaji na kuingiza hasara Serikali bila ya kupatikana tija iliyokusudiwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) katika Miradi yake ijayo kuchukuwa jitihada kubwa za kuhakikisha watendaji wake wa Kitengo cha TEHAMA wanashirikishwa kikamilifu kwenye michakato yote ya Miradi ya TEHAMA inayohusiana na Mamlaka ili kuepusha dosari zinazoweza kujitokeza baadae na kuigharimu Mamlaka na Serikali kutokana na udhaifu unaoweza kujitokeza kwenye Usimamizi, Uendeshaji na Udumishaji wa Mifumo na Miundombinu ya TEHAMA ya Mamlaka.

### 4.1.10.2 Dosari katika utendaji kazi wa Mfumo wa ZIDRAS

Ukaguzi ulifanya mapitio ya Mfumo wa ZIDRAS kwa lengo la kuhakiki na kutathmini ufanisi wa utendaji kazi wa mfumo hususan katika eneo la usalama na michakato ya usimamizi wa makusanyo ya kodi. Licha ya mfumo kuendelea kufanya kazi kwa zaidi ya miezi sita baada ya kukamilika kwa utengenezwaji wake, hadi ukaguzi unakamilika ulibaini kuwepo kwa dosari za kiutendaji katika mfumo huo, baadhi ya dosari hizo ni kama zifuatazo:-

- **Kushindwa kufanya kazi kwa moduli ndogo ya Uhakiki wa Marejesho ya Kodi (Tax Return Vetting)**

Katika Mfumo wa ZIDRAS, moduli ndogo ya Uhakiki wa Marejesho ya Kodi (Tax Return Vetting) imegawika katika vipengele (section) vikuu viwili ambavyo ni Marejesho ya Ushuru wa Ndani (Domestic Tax Return - DTR) na Marejesho ya Mapato Yasiyo ya Kodi (Non Tax Income Return - NTR). Ukaguzi ulibaini kuwa kipengele cha Marejesho ya Mapato Yasiyo ya Kodi (NTR) hakiwezi kuonyesha taarifa zozote kuhusiana na mapato yasio ya kodi, jambo ambalo linawapa ugumu watendaji wa Idara ya NTR wanapohitaji kupata taarifa za Mapato yasiyo ya Kodi kutoka kwenye mfumo wa ZIDRAS. Hali hii husababisha watendaji hao kutumia kipengele chengine cha Marejesho ya Ushuru wa Ndani (DTR) ili kuweza kuzivuta data za NTR na kuzipata taarifa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zao.

- **Kutokuwepo kwa moduli ya kuweka Taarifa za makusanyo ya Ndege Binafsi (Private Charters)**

Ukaguzi ulibaini kuwa Mfumo wa ZIDRAS hauna moduli/sehemu ya kuingiza taarifa za mapato (marejesho) kutoka kwa Kampuni zenye kutumia ndege Binafsi na sio Ndege za Biashara. Hali hii hupelekea taarifa za makusanyo kwa ndege hizo kuingizwa kwa njia ya kawaida kwenye mfumo wa zamani wa ZITAS kutokana na Mfumo mpya wa ZIDRAS kukosa sehemu za kuingiza Taarifa za Ndege hizo.

- **Kutokufanya kazi kikamilifu kwa moduli ya Ripoti kwenye Mfumo wa ZIDRAS**

Ukaguzi ulibaini kuwa moduli ya Ripoti katika mfumo wa ZIDRAS bado ina changamoto ya utendaji kazi kutokana na kushindwa kutoa ripoti muhimu za makusanyo ya mapato na madeni. Baadhi ya ripoti ambazo bado hazipatikani katika mfumo wa ZIDRAS ni pamoja na Ripoti za Marejesho ya Ritani, Ripoti za Madeni, Ripoti za Walipa kodi kwa Kila mwezi, miezi mitatu, miezi sita, mwaka, Ripoti za makusanyo ya kila siku zinazotokana na huduma za tozo za Viwanja vya Ndege na ada za usalama n.k.

- **Mfumo kushindwa kutoa taarifa za ukumbusho "Notification Message" kwa Walipakodi kuhusu tarehe zao za kuwasilisha Ritani zinapofika (due date)**

Ukaguzi umebaini kuwa ZIDRAS haiwezi kuwakumbusha wateja kwa kutumia njia ya barua pepe, SMS au njia nyingine yoyote kuhusu kuwasilisha marejesho yao pindipo tarehe za malipo zitakapofikiwa jambo ambalo ni kinyume na mahitaji ya mfumo.

- **ZIDRAS kushindwa kuchuja na kuonyesha taarifa kwa mujibu wa mahitaji ya watumiaji wa Mfumo**

Ukaguzi umebaini kwamba baadhi ya Kampuni za Ndege kama KLM, QATAR, FLY DUBAI, KENYA, UGANDA, TURKISH na ETHIOPIA tayari zimetoa tamko rasmi kwa Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) kwamba Kampuni hizo zitalipia ada za tozo (ushuru) kwa kutumia shilingi ya Kitanzania (Tsh.) na sio Dola ya Kimarekani (USD).

Hata hivyo, Mfumo wa ZIDRAS unashindwa kubagua taarifa za malipo ya USD na malipo ya Tshs. Katika moduli ya NTR, na badala yake huonyesha aina zote mbili za taarifa za malipo (Tsh & USD) katika sehemu ya Ritani za Ushuru wa Uwanja wa Ndege, hivyo wakati mwingine inaleta mkanganyiko wa taarifa za mapato kwa upande wa watendaji wa Idara ya NTR ambao hushughulika na Taarifa hizo wakati wanapofanya kazi ya kuthibitisha na kuidhinisha taarifa za malipo.

Kuwepo kwa changamoto hizo kunaweza kusababisha kutopatikana kwa ripoti sahihi zinazotolewa na ZIDRAS na hatimae kukosekana kwa tija na ufanisi wa utendaji wa Mfumo huo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZRA kuhakikisha kuwa mfumo wa ZIDRAS unafanyiwa marekebisho haraka iwezekanavyo kutokana na mapungufu yote yaliyobainika ili kuweza kutumika kwa ufanisi na kupatikana kwa tija iliyokusudiwa.

### 4.1.10.3 Dosari katika Ukusanyaji wa Mapato yatokanayo na Kodi za Bandari na Viwanja vya Ndege

Moja kati ya aina za mapato yanayokusanywa na ZRA ni Mapato Yasiyo ya Kodi (Non Tax Revenues) ambapo mapato hayo hutokana na vyanzo mbali mbali kama vile Ada za Bandari na Uwanja wa Ndege, Ada za leseni, Ada za Usajili wa Vyombo vya Moto n.k.

Mapato yasiyo ya kodi hukusanywa kila mwezi kupitia taarifa zinazowasilishwa ZRA (Files Returns) kutoka kwa Wateja wake ambao ni Kampuni za Meli za Abiria na Migizo, Kampuni za Ndege, waombaji wa leseni za udereva, wanaosajili vyombo vya moto n.k.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba taarifa nyingi za mapato (File Retuns) zinazoingizwa kwenye mfumo wa ZIDRAS kuhusiana na makusanyo ya ada za Bandari na Uwanja wa Ndege hazina uhakika wa usahihi wake kutokana na taarifa hizo kukusanywa na kuingizwa kwenye mfumo wa ZIDRAS kwa njia ya kawaida (manually) badala ya kupitia muunganiko wa mifumo (systems integration).

Hali hii imebainika kutokana na kuwepo kwa tofauti baina ya taarifa za idadi ya abiria zinazowasilishwa kutoka kwa Wateja (Airlines & Marine Ferries) kupitia "Manifest" na taarifa za abiria zinazowasilishwa na watendaji wa ZRA kwa njia ya "Excel Files" kutoka maeneo hayo ya makusanyo (Uwanja wa Ndege na Bandarini) jambo ambalo ZRA hupata tabu katika kuthibitisha usahihi wa taarifa hizo.

Aidha hali hii imetokana na kukosekana kwa muunganiko wa moja kwa moja (integration) baina ya Mfumo wa ZIDRAS na mifumo ya wateja wanaolipa ada za Bandari (Kampuni za Meli na Ndege).

Kuwepo kwa utofauti kwenye taarifa za abiria wanaosafiri kunaweza kusababisha ZRA kushindwa kufikia malengo ya makusanyo yasiyo ya kodi kutokana na kutopatikana kwa taarifa sahihi jambo ambalo linaweza kuingiza hasara kwa Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZRA kufanya jitihada za kuunganisha moja kwa moja mfumo wa ZIDRAS pamoja na mifumo ya wateja wao wanaolipa ada za bandari (Kampuni za Meli na Ndege) ili kupatikana taarifa sahihi za abiria waliosafiri na hatimae kuepuka udanganyifu unaoweza kujitokeza kwenye taarifa za abiria kutokana na mchakato huo kufanyika manually kwa sasa.

#### 4.1.10.4 Dosari katika Muunganiko wa Mfumo wa ZIDRAS na Mfumo wa Ikram Sealine Company

Ukaguzi ulifanya uhakiki wa muunganiko (Integration) uliopo baina ya Mfumo wa ZIDRAS na Mfumo wa Meli ya **Ikram Sealine Company** kwa lengo la kuangalia aina gani ya taarifa za makusanyo zinazoingia kwenye mfumo wa ZIDRAS kutoka kwenye mfumo wa Ikram Sealine Company.

Kwa mujibu wa maelezo ya watendaji wa Idara ya NTR kutoka ZRA taarifa za makusanyo zilizohitajika kuunganishwa kwenye mfumo wa ZIDRAS ni pamoja na taarifa za makusanyo yatokanayo na idadi ya abiria waliosafiri, makusanyo yanayotokana na migizo (cargo and parcels) pamoja na taarifa za magari yaliyopakia mizigo (Freight Shipping Trucks).

Dosari iliyobainika katika muunganiko huo ni kwamba mfumo wa Ikram Sealine Company unaingiza taarifa za makusanyo ya mizigo midogo midogo tu (parcel) na sio taarifa zote kwa mujibu wa makubaliano ya uunganishwaji kama vile taarifa za idadi ya abiria waliosafiri na idadi ya mizigo mikubwa (cargo).

Hali hii husababisha kuwepo kwa upotevu wa mapato kutokana na kutopatikana kwa taarifa za idadi ya abiria wanaosafiri, idadi ya mizigo (cargo) iliyosafirishwa pamoja na taarifa za magari yaliyopakia mizigo katika Meli hiyo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZRA kufanya jitihada za makusudi za kuhakikisha taarifa zote za makusanyo ya Meli ya Ikraam Sealine zinaingizwa katika Mfumo wa ZIDRAS jambo ambalo litapelekea kuimarika kwa makusanyo na hatimae Serikali kupata fedha nyingi za maendeleo.

#### 4.1.10.5 Kuchelewa kuunganishwa kwa Mifumo ya Makusanyo ya Mapato ya Kampuni ya AZAM, ZAN FAST FERRIES na Mfumo wa ZIDRAS

AZAM MARINE na ZAN FAST FERRIES ni miongoni mwa kampuni kubwa zilizopo Zanzibar zinazofanya biashara ya usafirishaji wa abiria na mizigo yao kupitia njia ya Bahari (Coastal Travel).

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Kampuni hizo bado zinakwepa kuunganisha mifumo yao yenye taarifa za makusanyo ya abiria na mizigo pamoja na mfumo wa ZIDRAS, badala yake taarifa zao huziwasilisha ZRA kwa njia ya kawaida (manually) kupitia 'manifest paper' zilizojazwa kwa mkono. Aidha, imebainika kwamba hii ni moja kati ya mbinu zinazotumiwa na kampuni hizo kukwepa kodi kwa kutokuwasilisha idadi halisi ya abiria waliosafiri pamoja na mizigo iliyomo jambo ambalo ZRA hushindwa kufahamu na hupata changamoto nyingi katika kubaini idadi halisi ya abiria waliosafiri pamoja na mizigo yao.

ZRA kushindwa kutambua idadi halisi ya makusanyo inayohitajika kupatikana kutokana na makusanyo ya Kampuni hizo kunapelekea kushindwa kufahamu mapato halisi na hatimae kujitokeza kwa upotevu wa mapato kwa Serikali.

Ukaguzi unashauri uongozi wa ZRA kwa kushirikiana na uongozi wa Shirika la Bandari na Serikali kuchukuwa jitihada za makusudi za kuyataka makampuni ya AZAM MARINE, ZAN FAST FERRIES na nyenginezo kuunganisha moja kwa moja mifumo yao na Mfumo wa kukusanya Mapato wa ZRA kwa utaratibu maalum ili taarifa za abiria, mizigo na nyenginezo zinazohitajika ziweze kuingizwa kwenye mfumo wa ZIDRAS na kupatikana mapato halisi.

#### 4.1.10.6 Kukosekana kwa leseni ya Kanzidata ya Mfumo wa ZIDRAS (Oracle Database)

Oracle, kama mifumo mingine iliyotengenezwa na makampuni mbalimbali duniani, huwa na makubaliano maalum katika matumizi ya kanzidata zake za aina ya "Oracle Database".

Kanzidata hizo ili zitumike kwa matumizi ya biashara katika taasisi za Umma na Kampuni binafsi zinapaswa kulipiwa leseni halali ya matumizi. Baada ya kulipiwa leseni Oracle Database inakuwa halali kutumika kibiashara, kupata ulinzi, usalama na inaimarisha udhibiti mzuri wa taarifa zinazoingizwa ndani yake kutokana na vitendo vya uhalifu vinavyofanywa dhidi ya kanzidata hiyo, kwa kupata "online updates and security patches" kupitia mtandao.

Aidha, ukiukwaji wa masharti ya leseni ya matumizi kwa taasisi zinazotumia database hiyo unaweza kusababisha taasisi za umma au kampuni binafsi kuingia katika hatari ya kukosa usalama wa taarifa zake zilizomo na vile vile kuweza kushtakiwa mahakamani ikibainika.

Kwa mujibu wa kifungu nambari 3.16 cha Toleo la 2 la Sera ya TEHAMA ya ZRB ya mwaka 2021 kinachohusu **Usimamizi Bora wa TEHAMA** kinaeleza kwamba "Mifumo yote (programu zote) ya ZRA lazima iwe na makubaliano halali ya leseni ambayo yataendana na Sera Kuu ya Programu".

Aidha kifungu nambari 5.2 cha sera hiyo kinachohusu **General Software** kinaeleza yafuatayo: -

- Watumiaji wa mifumo lazima watii hakimiliki "copy rights" na matakwa ya leseni "licensing restrictions" pamoja na Sera za ZRA zinazotumika. Rasilimali za TEHAMA haziwezi kutumika kwa kukiuka hakimiliki au masharti ya makubaliano yoyote ya leseni.
- ZRA itatumia programu zenye leseni ambapo Idara ya TEHAMA inawajibika kushughulikia utoaji leseni katika programu hizo kwa usahihi na zilizosasishwa.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba ZRA imekuwa ikitumia kanzidata ya Oracle (Oracle Database) iliyounganishwa na Mfumo Mkuu wa Makusanyo ya Mapato (ZIDRAS) kwa muda mrefu ambapo taarifa zote za makusanyo ya mapato ya walipakodi zinahifadhiwa ndani ya kanzidata hiyo kupitia mfumo wa ZIDRAS.

Dosari iliyobainika ni kwamba kanzidata hiyo imekuwa ikitumika kuhifadhia taarifa za makusanyo ya mapato ya walipakodi bila ya kuwa na leseni ya matumizi kwa kipindi kirefu (expired licences) jambo ambalo linapelekea taarifa za walipakodi kuwa katika hatari kubwa ya kukumbwa na athari kutokana na kutokuwepo kwa ulinzi imara na usalama katika matumizi ya kanzidata hiyo.

Baadhi ya athari zinazoweza kuikumba ZRA kutokana na kutumia kanzidata isiyo na leseni ya matumizi ni kama vile kufutika kwa taarifa za makusanyo ya walipakodi zilizoingizwa, kushambuliwa na virusi au programu hatarishi, kuvamiwa au kudukuliwa kupitia wizi wa mitandao na hatimae kuingizia hasara Serikali.

Aidha, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na vifungu vya sera ya TEHAMA ya ZRA vilivyonakiliwa hapo juu pamoja na kukiuka Makubaliano ya Leseni ya Mtumiaji kwa Kampuni ya Oracle (End User Lisence Agreements - EULAs) ambapo inaweza kusababisha dhima kubwa kwa ZRA.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar kuhakikisha unafanya jitihada za makusudi za kununua leseni halali za matumizi ya rasilimali zote za TEHAMA zinazotumika kwa Taasisi hiyo ikiwemo mifumo, kanzidata, programu pamoja na miundombinu ya TEHAMA ili kuziweka taarifa zake katika hali ya usalama.

#### 4.1.10.7 Tathmini ya Miundombinu ya Mtandao (Review of Network infrastructure)

Ukaguzi ulifanya mapitio ya miundombinu ya Mtandao (Network Infrastructures) na kubaini uwepo wa Swichi aina ya CISCO Small Business 200 zinazotumiwa na Mamlaka kwa shughuli za mawasiliano ya usafirishaji wa taarifa (data) kupitia mifumo yake ya ZIDRAS na VFMS.

Hata hivyo, ukaguzi umebaini Swichi hizo zimepitwa na wakati ambapo muda wake wa mwisho wa matumizi (End of Life) ni tarehe 04 Oktoba, 2018 na muda wa mwisho wa kupatiwa msaada wa sasisho (End Of Life Support) ni tarehe 31 Oktoba, 2023.

Kuendelea kutumia miundombinu hiyo kunaweza kuathiri hali ya upatikanaji na ufikiaji wa taarifa za kwenye mifumo, aidha kunaweza kuhatarisha usalama wa mifumo ya ndani ya Mamlaka kama vile Mfumo wa VFMS, ZIDRAS na mifumo mingine inayotumika kwa matumizi ya ndani na nje ya Mamlaka.

Matumizi ya vifaa vilivyopitwa na wakati haviwezi tena kupokea sasisho (updates) za kiusalama mtandaoni, na hivyo kuwa na uwezekano wa kuathiriwa na wavamizi wa nje wa kupitia mitandao.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) kuhakikisha kuwa unanunua na kufunga vifaa na miundombinu ya kisasa ya mtandao ili kuimarisha ulinzi na usalama wa taarifa dhidi ya mashambulizi yanayotokana na vihatarishi vya mtandao na hatimae kupatikana kwa ufanisi wa utendaji kazi wa vifaa na miundombinu hiyo.

### 4.1.11 MFUKO WA HIFADHI YA JAMII (ZSSF)

Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

## Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi

### 4.1.11.1 Dosari katika Maboresho ya Mfumo wa FuMIS

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ZSSF imefunga mkataba na Kampuni ya Real Tech Limited terehe 28 Novemba, 2022 wenye nambari SMZ/F0308/C/NCB/2021-2022/06 uliogharimu shilingi **195,290,000** pamoja na VAT kwa ajili ya uboreshaji wa Mfumo Mkuu unaosimamia Mafao ya Wanachama wa ZSSF (FuMIS).

Kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba kazi hiyo ya maboresho ilitakiwa kufanyika kwa kipindi cha miezi sita (6) kuanzia tarehe 01 Disemba, 2022 hadi tarehe 30 Mei, 2023. Hadi ukaguzi unakamilika mnamo mwezi wa Novemba, 2023 kazi hiyo ilikuwa bado haijakamilika ukizingatia kwamba kuna miezi sita (6) mengine ya ziada ilikuwa tayari imeshapita bila ya kuwepo kwa mkataba wa nyongeza (addendum). Licha ya kuongezeka kwa muda huo ukaguzi umebaini kuwa ZSSF haikujumuisha kipengele cha kutoa adhabu (penalt) au tozo kwa mtoa huduma pindipo akishindwa au akichelewa kukabidhi kwa wakati kazi hiyo kwa mujibu wa mkataba.

Kutokamilika kwa maboresho hayo kunapelekea kuchelewa kupatikana kwa huduma bora zilizotarajiwa kutolewa kwa wanachama wa Mfuko kutokana na kufanyika kwa maboresho hayo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZSSF kupitia Idara ya TEHAMA kufuatilia kwa kina juu ya sababu za ucheleweshwaji wa maboresho ya mfumo wa FuMIS na kuweka mpango imara wa kufanya upembuzi yakinifu na kuondoa dosari zote zilizopo ambazo zinakwaza kwa njia moja au nyengine zoezi la ukamilishaji wa Mfumo huo.

### 4.1.11.2 Mapitio ya mfumo wa kugundua, kutoa ishara na kuzima moto (Fire Detection and Suppression System)

Mfumo wa kugundua na kuzima Moto (Fire Detection and Suppression System - FDSS), ni mfumo wa kisasa ambao umejumuisha vifaa na miundombinu mbali mbali yenye uwezo wa kubaini chanzo cha moto (fire detection), kutoa ishara ya hatari ya moto (fire alarm) na vile vile kuweza kuzima moto wakati unapotokea kwenye majengo mbali mbali (fire extenguisher).

Faida kuu ya Mfumo huu ni kuweza kubaini mapema, kutoa ishara kwa binadamu na kuweza kuuzima moto wenyewe (automatic) bila ya kuingiliwa na binaadamu wakati janga la moto linapotokea katika jengo au eneo la Afisi, ambapo pia husaidia kwa kiasi kikubwa kuzima moto maeneo ambayo binaadamu hatoweza kuyafikia mapema wakati wa dharura ya moto.

ZSSF imefanikiwa kuweka teknolojia na miundombinu ya mfumo wa kugundua, kutoa ishara na kuzima moto (FDSS) katika Ofisi zake mbali mbali ikiwemo chumba cha Seva na Mitambo ya Mawasiliano (Datacenter) kilichopo katika Makao Makuu Kilimani Unguja, Vile vile miundombinu hiyo imefungwa katika Afisi ya Pemba pamoja na Hoteli ya Mkoani Pemba.

Hata hivyo, katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba pamoja na ZSSF kuweka vifaa na miundombinu ya kisasa ya kuzima moto lakini kumekuwa na uhaba kwa miundombinu hiyo kufanyiwa huduma za matengenezo na maboresho kwa wakati "services and maintanance". Hadi ukaguzi unakamilika baadhi ya miundombinu hiyo ilikuwa bado haijafanyiwa maboresho kwa kipindi cha zaidi ya mwaka mmoja.

Kushindwa kufanya huduma za matengenezo na maboresho kwa wakati kwenye mifumo ya kuzimia moto kunaweza kusababisha mifumo hiyo kutoweza kufanya kazi ipaswavyo kama ilivyotarajiwa pindipo janga au dharura ya moto ikitokea katika majengo ya ZSSF, jambo ambalo litapelekea kujitokeza kwa uharibifu mkubwa wa vifaa, mali na taarifa za afisi na hatimae kuingiza hasara Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZSSF kuhakikisha unaandaa na kutekeleza vizuri mkakati wa kusimamia mfumo na miundombinu ya uzimaji wa moto katika majengo yake na vile vile kufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika vifaa hivyo kwa lengo la kuhakikisha vinafanya kazi ipasavyo pamoja na kuvifanyia huduma za maboresho na matengenezo "services and maintanance" kwa wakati ili kuweza kudumisha utendaji kazi wa vifaa hivyo.

### 4.1.11.3 Dosari katika Mchakato wa Usimamizi wa Matukio (Inadequate Incident Management Process)

ZSSF ni moja kati ya Taasisi zilizofanikiwa kwa kiasi kikubwa katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutumia mifumo na miundombinu mbali mbali ya TEHAMA kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli zake za Mfuko.

Ukaguzi ulifanya ufuatiliaji kwa ofisi zake zote kuhusiana na njia zinazotumika katika kuripoti na kusimamia matukio na changamoto za kwenye mifumo kuanzia hatua zinapojitokeza, hatua ya ufuatiliaji hadi hatua ya kupatiwa ufumbuzi na kubaini uwepo wa udhaifu katika mchakato mzima wa usimamizi wa matukio na utatuzi wa changamoto za mifumo.

Aidha, ukaguzi umebaini kwamba ZSSF kwa kiasi kikubwa bado inaendelea kutumia utaratibu wa njia ya kawaida (manual) kupitia uandishi wa madokezo, simu na mahojiano ya moja kwa moja katika kukusanya changamoto za mifumo kutoka kwa watumiaji na kuwasilishwa Idara ya TEHAMA kwa ajili ya ufumbuzi ambapo changamoto hizo hutakiwa kuekewa kumbukumbu na kupangiwa vipao mbele vya kufanyiwa kazi kwa mujibu wa uhalisia wake, umuhimu wake, madhara yake, tarehe na muda ulioripotiwa na Idara ya Mtumiaji.

Ni maoni ya mkaguzi kuwa utaratibu wa utendaji kazi wa uongozi unahitaji kuimarishwa kwani siku hizi kuna njia za kiotomatiki za kudhibiti Mchakato ambao huleta majibu ya haraka kwa changamoto, dosari na hatari mbalimbali zinazoweza kujitokeza na kuripotiwa na wafanyakazi.

Aidha, imebainika kutokuwepo kwa mkataba wa utoaji wa huduma (SLA) baina ya Idara ya TEHAMA na Vitengo vengine vya watumiaji wa mifumo katika Mfuko (Business Units) jambo ambalo linaweza kupelekea kutokuwepo kwa maelewano mazuri katika utoaji na upatikanaji wa huduma za kibiashara.

Kuendelea kutumia njia ya kawaida (manual system) kunaweza kusababisha Mfuko kupungua ufanisi wake katika utendaji kutokana na mifumo iliyopo kushindwa kufanyiwa marekebisho kwa wakati juu ya changamoto, dosari na Vihatarishi mbali mbali vinavyoweza kujitokeza na kuripotiwa na wafanyakazi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZSSF kuanzisha utaratibu wa kutumia mfumo wa TEHAMA (Helpdesk System) ikiwa kama dawati kuu kwa ajili ya kupokea, kukusanya, kusimamia na kuwasilisha matukio na changamoto na Vihatarishi vyote vinavyojitokeza kwenye mifumo ili kuwezesha watumiaji wa mifumo (system users) katika tawi lolote la ZSSF kuripoti moja kwa moja kwenye Idara ya TEHAMA kwa lengo la kufanyiwa kazi haraka iwezekanavyo na kubakia kumbukumbu zote za taarifa zake.

Zaidi ya hayo, makubaliano ya kiwango cha huduma (SLA) kati ya Idara ya TEHAMA na vitengo vya Biashara yanapaswa kutekelezwa ili kudumisha uwajibikaji na utatuzi wa matukio kwa wakati.

Vile vile uongozi wa Mfuko kwa kushirikiana na Idara ya TEHAMA unashauriwa kuandaa mkakati maalum wa kupitia, kuchambua, kufanyia tathmini na kuzitatua hatari zote zilizopo katika mifumo na miundombinu ya TEHAMA ya Mfuko kwa kuzingatia umuhimu na aina ya hatari zilizobainika.

#### 4.1.11.4 Udhaifu katika utendaji kazi wa Mifumo ya ZSSF kwa upande wa Pemba

Ukaguzi ulifanya uhakiki wa utendaji kazi wa mifumo ya ZSSF kwa upande wa Pemba na kubaini kuwa kasi ya utendaji kazi wa mifumo kwa Pemba ni ndogo (slow speed). Hali hii imesababishwa na kuwepo kwa udhaifu katika miundombinu iliyotumika kuunganisha mawasiliano ya mtandao (VPN Connection) kutoka kwa kampuni ya Zanlink.

Aidha imebainika kunapokuwa na changamoto ya hali ya hewa kwa mfano uwepo wa mvua kubwa hupelekea mifumo kushindwa kupatikana na kutumika kwa ufanisi.

Kuwepo kwa udhaifu katika miundombinu ya mawasiliano ya mtandao kunaweza kusababisha kupungua kwa ufanisi wa utendaji kazi wa Mfuko kwa upande wa Pemba na hatimae kupelekea kujitokeza kwa malalamiko kwa watumishi wa ZSSF kwa upande wa Pemba na wanachama kutokana na huduma duni zinazoweza kutolewa na Mfuko kwa upande wa Pemba zilizosababishwa na changamoto ya mawasiliano ya mtandao.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZSSF kuweka na kutumia njia mbadala ya miundombinu ya Mkonga wa Taifa kutoka ZICTIA (Fiber Connectivity and Infrastructure) kwa upande wa Pemba kama ilivyoungwa katika Ofisi za Zanzibar kwa lengo la kuendelea kupatikana huduma bora na ya uhakika, yenye kasi kubwa (higher speed) na iliyo salama (secure) dhidi ya mashambulizi na vihatarishi vinavyotokana na mitandao (cyber attacks).

### 4.1.12 SHIRIKA LA UMEME ZANZIBAR (ZECO)

Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 4.1.12.1 Ukosefu wa uidhinishaji katika michakato ya mfumo wa SUPRIMA

Kifungo nambari 2.1 (1) (i) cha Mwongozo wa Serikali Mtandao kwa Maendeleo, Upataji, Uendeshaji na Utunzaji wa maombi ya Serikali Mtandao, eGA/EXT/APA/005 ya mwenzi Machi 2020, inazitaka taasisi za umma zinazoanzisha mifumo kuhakikisha kuwa mifumo hiyo inakidhi mahitaji yao ya biashara ya kitaasisi.

Katika mapitio ya udhibiti wa matumizi ya mfumo wa SUPRIMA ili kuthibitisha kutosheleza kwake na ufanisi ukaguzi ulibaini kasoro zifuatazo;

(i) **Kutokuwepo kwa uidhinishaji wa kuzalisha tokeni ambazo hazilipiwi "free issue tokens":** Tokeni ambazo hazilipiwi hutengenezwa kwa mkono "manually" na Mshika Fedha mkuu "chief cashier". Mambo yanayosababisha uzalishaji wa tokeni hizi ni pamoja na ubadilishaji wa mita mpya za umeme ambazo zimezidi uniti hamsini ambapo kikawaida mita mpya huwa na unit hamsini, wakati mita imefanyiwa majaribio kabla ya usakinishaji "installation" na kukosea kununua uniti. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa mchakato wa idhini umewekwa kwa mkono "manually" ili kuhakikisha uhalali wa hatua iliyofanywa.

(ii) **Kutokuwepo kwa uidhinishaji wa kusimamia deni la mteja** Mazingira yanayosababisha deni la mteja ni pamoja na deni la uniti hamsini ambalo hutozwa kwa kila mita mpya ya umeme, na deni la mteja hutokea wanaposhindwa kulipa gharama zote za kuunganisha umeme yaani kuunganishwa umeme kwa mkopo. Madeni haya huingizwa kwenye akaunti zao za mita ili wakati wanaponunua umeme, deni linakatwa kwa wakati huo huo.

Kutokuwepo kwa idhini ya kuzalisha tokeni zisizolipiwa "free issue token" kunaweza kusababisha uzalishaji wa tokeni kwa mtu asiye na haki kwa makusudi au bila kukusudia, hivyo kupoteza mapato ya Serikali. Vile vile kunaweza kusababisha kutoza deni kwa mtu asiye na haki kwa makusudi au bila kukusudia, hivyo kupoteza mapato ya Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZECO kuhakikisha kwamba uidhinishaji unawekwa na kutekelezwa kwenye mfumo.

#### 4.1.12.2 Kutokuwepo kwa muunganisho kati ya mfumo wa mapato wa EQUILLIUM na mfumo wa uhasibu wa SAP ERP kwa usimamizi wa madeni

Kifungu nambari 2.1.3.4 (ii) cha viwango vya Serikali Mtandao kwa maendeleo, ununuzi, uendeshaji, na matengenezo ya matumizi ya Serikali Mtandao, 2018 inahitaji kwamba hati ya uchambuzi wa mahitaji kwa maendeleo au ununuzi ifikirie sifa za ubora, ikiwa ni pamoja na interface ya mfumo wa nje na huduma au moduli ya programu.

Wakati tunakagua mfumo wa EQUILLIUM tumebaini mapungufu tofauti ikiwa ni pamoja na mfumo wa EQUILLIUM haurekodi moja kwa moja "automatically" madeni, hasa bili zisizolipwa. Kwa hiyo, mchakato wa kurekodi madeni ya jumla katika mfumo wa SAP unategemea kwa kiasi kikubwa kuingizwa kwa kumbukumbu kwa mkono "manually", ambayo inaweza kusababisha makosa na kutofautiana.


Kutounganishwa kwa mifumo hii kunaweza kusababisha kushindwa kurekodi moja kwa moja "automatically" madeni katika mfumo wa SAP, kunapelekea kutegemea "manual journal entries", ambapo kunaweza kuleta hatari kwa usahihi na uadilifu wa kifedha. Pia inaweza kusababisha makosa katika taarifa za kifedha, ikiwemo kuongezeka au kupungua kwa madeni. Hitilafu hizi zinaweza kuhatarisha uwazi wa kifedha, kuzuia maamuzi ya kifedha.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZECO kuunganisha mifumo kati ya mfumo wa malipo wa EQUILLIUM na mfumo wa ripoti za kifedha wa SAP ili kuwezesha kurekodi moja kwa moja madeni katika mfumo wa SAP kutoka kwenye mfumo wa EQUILLIUM; na vile vile kufanya upatanisho "reconciliation" wa madeni mara kwa mara kati ya mifumo miwili ili kuhakikisha uwiano na usahihi katika taarifa za kifedha.

### 4.1.12.3 Mfumo wa SUPRIMA kutoweza kujaza ada ya usajili kiotomatiki


Kifungu nambari 2.2.1.1 (i) cha Mwongozo wa Serikali Mtandao kwa Maendeleo, Upataji, Uendeshaji na Utunzaji wa maombi ya Serikali Mtandao, eGA/EXT/APA/006 ya mwenzi Machi, 2020 inazitaka taasisi za umma zinazoanzisha mifumo kuhakikisha kuwa mifumo hiyo inakidhi mahitaji yao ya biashara ya kitaasisi.

Mapitio ya mchakato wa usajili wa wateja katika mfumo wa SUPRIMA, ilibainika kuwa, mfumo huo, kama ulivyoundwa kwa sasa, hauna uwezo wa kuweka kiasi cha ada ya usajili kiotomatiki licha ya kuwa kiasi hicho kinajukilikana kwa mujibu wa miongozo. Upungufu huu husababisha wafanyakazi kulazimika kuingiza ada wenyewe wakati wa usajili wa wateja. Kielelezo hapo chini kinaonyesha uwekaji wa ada ya usajili kwa mikono.




Picha ifuatayo inafafanua athari za mfumo wa SUPRIMA kutoweza kujaza ada ya usajili kiotomatiki.

| New Connection Total/ Registration Fee | Occurrence of Amount |
|---|---|
| Customer Unpaid/ Zero Amount | **28103** |
| Customer paid below 8000 TZS | **89** |
| Customer Paid an exact 8000 | **39031** |
| Customer Paid above 8,000 TZS | **483** |




Njia ya kuingiza ada ya usajili kwa mikono inaweza kusababisha kuongezeka kwa makosa ya kibinadamu, kama vile viwango vya ada visivyo sahihi au maingizo ambayo hayajapokelewa. Pia hali hii inasababisha kuzorota kwa kazi, kwani wafanyakazi inawalazimu kuingiza ada ya usajili kila wanapofanya usajili hali ya kuwa taarifa hivyo inajulikana. Zaidi ya hiyo, ukosefu wa otomatiki unaweza kusababisha ucheleweshaji na kuzuia ufanisi wa jumla wa taratibu za kukusanya ada.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZECO kuhakikisha kuwa Mfumo wa SUPRIMA usanidiwe kwa mujibu wa miongozo ili kurejesha ada za usajili kiotomatiki; na kufanya majaribio na ufuatiliaji wa mara kwa mara wa mchakato wa kiotomatiki ili kudumisha ufanisi na kutegemewa kwake.

#### 4.1.12.4 Utoaji wa faini ya malipo ya umeme kwa wateja waliochelewa kwa kutumia "manually"

Kifungu nambari 2.2.1.1 (i) cha Mwongozo wa Serikali Mtandao kwa Maendeleo, Upataji, Uendeshaji na Utunzaji wa maombi ya Serikali Mtandao, eGA/EXT/APA/006 ya mwenzi Machi, 2020 kinazitaka taasisi za umma zinazoanzisha mifumo kuhakikisha kuwa mifumo hiyo inakidhi mahitaji yao ya biashara ya kitaasisi.

Wakati wa ukaguzi wa mfumo wa EQUILLIUM wa wateja wa malipo ya baada ya kupata huduma "postpaid customers", ilibainika kuwa utoaji wa adhabu yaani faini kwa malipo yaliyochelewa hufanywa kwa mikono "manually". Kwa mujibu wa utaratibu huo, wateja wanapaswa kulipishwa bili za matumizi yao ya umeme, na ikiwa malipo hayatapokelewa baada ya muda uliowekwa, ambao umepangwa kuwa siku 21 kutoka wakati wa bili, usambazaji wa umeme hukatwa. Baadaye, wafanyakazi huingia kwenye mfumo wao wenyewe ili kuzalisha bili za adhabu, kazi ambayo inaweza kuendeshwa kiotomatiki.

Utoaji wa faini kwa mikono "manually" unaweza kusababisha hatari ya ucheleweshaji wa utoaji huduma, kupelekea kufanyika kwa makosa, na kuongezeka kwa mzigo wa kazi kwa wafanyakazi. Mbinu hii inaweza kusababisha utoaji wa faini/adhabu usiolingana, na hivyo kuathiri ufanisi wa jumla wa mchakato wa bili na malipo. Pia huongeza hatari ya kutoziangalia akaunti zilizochelewa, na kusababisha hitilafu za kifedha.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Umeme Zanzibar kuhakikisha kuwa Mfumo wa Equillium usanidiwe ili kuzalisha bili za adhabu kiotomatiki "automatically" kwa malipo yaliyochelewa kulipwa ndani ya muda uliowekwa pamoja na kufanya majaribio na kufuatilia mara kwa mara mchakato wa kiotomatiki ili kudumisha ufanisi na kutegemewa kwake.

#### 4.1.12.5 Ubadilishwaji wa madeni unaofanyika kwa mkono "manual" kwa wateja wa mikopo kwenye mfumo wa SAP

Kifungu nambari 2.2.1.1 (i) cha Mwongozo wa Serikali Mtandao kwa Maendeleo, Upataji, Uendeshaji na Utunzaji wa maombi ya Serikali Mtandao, eGA/EXT/APA/006 ya mwenzi Machi 2020, inazitaka taasisi za umma zinazoanzisha mifumo kuhakikisha kuwa mifumo hiyo inakidhi mahitaji yao ya biashara ya kitaasisi.

Katika ukaguzi wa mfumo wa SAP, ukaguzi uliangalia kuhusu wateja wa mikopo wa umeme, ingawa aina ya mteja inachaguliwa ipasavyo wakati wa usajili ili kutofautisha kati ya wateja wa fedha taslimu na wa mikopo, ukaguzi uibaini, licha ya kuwa kiwango cha deni huingizwa kwenye mfumo wa SAP lakini bado inahitajika kuingiza tena kwa mkono "manually" kiwango hicho hicho kwenye mfumo wa SUPRIMA hali ya kuwa mifumo hiyo miwili imefanyiwa uunganishwaji "Intergration".

Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa mifumo ya SAP na SUPRIMA imeunganishwa kwa kiasi "partially integrated" kwa ajili ya uhamisho wa kiotomatiki wa taarifa za usajili wa wateja kutoka kwa SAP hadi mfumo wa SUPRIMA, lakini mchakato wa madeni bado haujaunganishwa kikamilifu, hali hii imetokana na hitilafu ya muundo "Design limitation" vile vile kutojumuishwa katika usanidi wa muunganisho "integration configuration".

Uingiliaji kati wa kibinafsi "Manual interventions" unaweza kuongeza uwezekano wa makosa, ucheleweshaji, na uwezekano wa kutofautiana katika akaunti za wateja. Hii inaweza kuathiri usahihi wa jumla wa rekodi za fedha na malipo ya wateja, na hivyo kusababisha taarifa potofu za kifedha, upotevu wa mapato na kutoridhika kwa wateja.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Umeme Zanzibar kuhakikisha mchakato wa muunganisho "intergration process" kati ya SAP na SUPRIMA uharakishwe ili kujumuisha mchakato wa madeni ya wateja wa mikopo. Kufuatilia kwa haraka muunganisho huu kutaboresha mchakato wa ulipaji madeni, kupunguza hitaji la masasisho ya mikono, na kuongeza ufanisi kwa ujumla. Hata hivyo Shirika lihakikishe linafanya majaribio na ufuatiliaji wa mara kwa mara ili kuhakikisha ujumuishaji huo unaondoa changamoto na kuboresha usahihi wa akaunti za wateja.

### 4.1.12.6 Maombi ya Ununuzi kufanyika kwa mkono "manually"

Kwa mujibu wa kifungu nambari 2.2.1.1 (i) cha Mwongozo wa Serikali Mtandao kwa Maendeleo, Upataji, Uendeshaji na Utunzaji wa maombi ya Serikali Mtandao, eGA/EXT/APA/006 ya mwezi Machi, 2020 inazitaka taasisi za umma zinazoanzisha mifumo kuhakikisha kuwa mifumo hiyo inakidhi mahitaji yao ya biashara ya kitaasisi.

Wakati wa ukaguzi, tulibaini kuwa ombi la ununuzi hufanywa kwa mikono, licha ya uwepo wa moduli hiyo katika mfumo wa SAP, lakini haitumiki kwa ununuzi wa bidhaa badala yake, inatumika kwa kuombea vifaa kutoka ghalani, ambayo inakwenda kinyume na muongozo wa eGA/EXT/APA/006 ya Machi, 2020.


Upelekaji wa hati halisi kwa ajili ya uidhinishaji bila ya kutumia njia ya otomatiki unaweza kusababisha ucheleweshaji, hasa ikiwa waidhinishaji hawapatikani ofisini. Ucheleweshaji huu unaweza kuathiri muda wa manunuzi na kuathiri ratiba ya jumla ya mradi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika kuongeza uhamasishaji na utoaji wa Mafunzo, vile vile Shirika kupanga vipindi vya mafunzo ili kuwaelimisha wafanyakazi kuhusu manufaa ya moduli ya SAP na jinsi inavyoweza kurahisisha kazi zao.

### 4.1.12.7 Mfumo kukosa udhibiti wa kubadilisha taarifa

Kwa mujibu wa kifungu nambari 2.2.1.1 (i) cha Mwongozo wa Serikali Mtandao kwa Maendeleo, Upataji, Uendeshaji na Utunzaji wa maombi ya Serikali Mtandao, eGA/EXT/APA/006 ya mwenzi Machi, 2020 kinazitaka taasisi za umma zinazoanzisha mifumo kuhakikisha kuwa mifumo hiyo inakidhi mahitaji yao ya biashara ya kitaasisi.

Katika mchakato wa kupitia mfumo wa SAP ili kutathmini gharama zinazohusiana na kuunganishiwa umeme, ilibainika kuwa gharama za kuunganisha umeme zinaweza kubadilishwa na mpimaji bila kuhitaji idhini "Approval" kutoka kwa mtu yeyote au mkuu wa kitengo anayehusika na kutoa idhini hiyo. Kwa hivyo, gharama hizi zinaweza kubadilishwa na mfumo unaruhusu hatua zinazofuata kuendelea bila pingamizi.




| # | Item Code | Item Name | Quantity | Price | VAT Code | Total (LC) | GL Account | G/L Account Name | Discount % | Info Dept. | Items Sale Type |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | DS-CW-001 | XLPE 2X25MM2 (ABC WIRE) | 30 | 2,500.00 | OVAT15 | TZS 75,000.00 | 42101 | Connection Materials | -200.00 | Service Line | Discounted Items |
| 2 | DS-PL-010 | GALVANIZED PIPE 2M (ROOF POLE) | 1 | 40,000.00 | OVAT15 | TZS 40,000.00 | 42101 | Connection Materials | 0.00 | Service Line | Discounted Items |
| 3 | DS-CL-001 | TENSION CLAMP 2X25 | 2 | 7,700.00 | OVAT15 | TZS 15,400.00 | 42101 | Connection Materials | 0.00 | Service Line | Discounted Items |
| 4 | DS-AS-034 | TEE-OFF (CONNECTOR )(PC CLAMP) | 4 | 10,000.00 | OVAT15 | TZS 40,000.00 | 42101 | Connection Materials | 0.00 | Service Line | Cash Items |
| 5 | DS-MT-035 | SINGLE PHASE PRE PAID METER (M | 1 | 110,250.00 | OVAT15 | TZS 110,250.00 | 42101 | Connection Materials | 0.00 | Service Line | Cash Items |
| 6 | DS-CW-067 | NEUTRAL SCREEN ALUMINIUM WIRE | 5 | 10,320.00 | OVAT15 | TZS 51,600.00 | 42101 | Connection Materials | 0.00 | Service Line | Cash Items |
| 7 | DS-CW-010 | TWIN FLAT WITH EARTH 10MM2 | 1 | 7,100.00 | OVAT15 | TZS 7,100.00 | 42101 | Connection Materials | 0.00 | Service Line | Cash Items |
| 8 | DS-CL-017 | WALL CLAMPS | 2 | 0.00 | OVAT15 | | 42101 | Connection Materials | 0.00 | Service Line | Discounted Items |
| 9 | DS-CL-018 | POLE CLAMPS | 2 | 0.00 | OVAT15 | | 42101 | Connection Materials | 0.00 | Service Line | Discounted Items |
| 10 | DS-SC-008 | COACH SCREW -2" (FOR ROOF POLE | 4 | 0.00 | OVAT15 | | 42101 | Connection Materials | 0.00 | Service Line | Discounted Items |
| 11 | DS-AS-049 | FISHERS (ROOF POLE) | 4 | 0.00 | OVAT15 | | 42101 | Connection Materials | 0.00 | Service Line | Discounted Items |
| 12 | DS-BT-001 | PIG TAIL HOOK (FOR ROOF POLE) | 1 | 0.00 | OVAT15 | | 42101 | Connection Materials | 0.00 | Service Line | Discounted Items |
| 13 | DS-BT-009 | BOLT & NUTS -2" (FOR ROOF POLE | 1 | 0.00 | OVAT15 | | 42101 | Connection Materials | 0.00 | Service Line | Discounted Items |
| 14 | SRV-0002 | NEW CONNECTION FEE | 1 | 500.00 | OVAT15 | TZS 500.00 | 42101 | Connection Materials | 0.00 | Service Line | Cash Items |
| 15 | | | | | OVAT0 | | | | 0.00 | | Cash Items |

Marekebisho yasioidhinishwa ya gharama za kuunganisha umeme yanaweza kusababisha hitilafu za kifedha, na kuathiri bajeti nzima. Vile vile kutokuwepo kwa mchakato wa uidhinishaji husababisha ukosefu wa uangalizi, uwezekano wa kuruhusu marekebisho ya kiholela ambayo huenda yasioanishwe na kanuni pamoja na kusababisha kutofautiana kwa tathmini ya gharama, na kusababisha mkanganyiko na migogoro kati ya wadau.

**Ukaguzi unalishauri Shirika la Umeme kufanya yafuatayo:-**

- Kuanzisha mchakato wa uidhinishaji rasmi kwenye mfumo ambapo marekebisho yoyote ya gharama za kuunganisha umeme lazima yakaguliwe rasmi na kuidhinishwa na mamlaka iliyoteuliwa, kama vile meneja wa mradi au mkuu wa idara husika.
- Kuhakikisha uwazi katika mchakato wa tathmini ya gharama kwa kuandika mabadiliko yoyote yaliyofanywa na mpimaji na kutoa mantiki ya wazi ya marekebisho hayo.
- Kuweka miongozo na vigezo vilivyo wazi vya kurekebisha gharama za kuunganisha umeme.
- Kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa mchakato wa tathmini ya gharama ili kutambua na kurekebisha marekebisho yoyote ambayo hayajaidhinishwa, kukuza uwajibikaji na kuzingatia taratibu zilizowekwa.

### 4.1.12.8 Mfumo kutokuwa na uwezo wa kutoa ripoti kulingana na mahitaji ya Taasisi

Wakati wa mapitio ya mifumo ya SUPRIMA na EQUILLIUM, ukaguzi ulibaini kwamba mifumo hiyo haiwezi kutoa baadhi ya ripoti kulingana na mahitaji ya Taasisi. Hii inaashiria kwamba kuna upungufu katika utendaji kazi wa mifumo hiyo kwa kutokidhi mahitaji mahususi ya utoaji taarifa zilizoagizwa na taasisi hivyo, huwalazimu kutoa ripoti nje ya mfumo kwa ajili ya kazi zao za kila siku. Zifuatazo ni ripoti ambazo haziwezi kutolewa na mifumo hiyo:-

i. Orodha ya mita zote zilizobadilishwa ambazo zinajumuisha yafuatayo (sababu ya kubadilisha mita, maelezo ya mita, muanzishaji wa maombi ya kubadilishiwa mita, na idhini). Hii ni kwa mifumo ya SUPRIMA na EQULLIUM.

ii. Ripoti ya tokeni zilizotolewa bila malipo na jina la mwidhinishaji. Hii ni kwa SUPRIMA.

iii. Ripoti ya bili zinazozalishwa kwa wateja waliotumia umeme kinyume na taratibu "wizi wa umeme" pamoja na wafanyakazi wanaohusika.

iv. Ripoti ya faini inayotolewa kwa wateja wa kulipia kabla na baada ya kupata huduma ya umeme "prepaid and post-paid customers" ikiwa ni pamoja na majina ya wafanyakazi wanaohusika na EQUILLIUM na SUPRIMA na orodha ya wateja wote wa umeme na ushuru wao.

Kuwepo kwa dosari hii kunaweza kusababisha mfumo kutokuwa na uwezo wa kutoa ripoti kulingana na mahitaji ya taasisi na kukwamisha utoaji wa maamuzi ya taasisi, vile vile kusababisha hatari ya kutofuata miongozo ya kitaasisi na mahitaji ya udhibiti. Bila ripoti sahihi na kwa wakati kunapelekea utendaji kazi usio na ufanisi ambao unaweza kutokea, kwani wadau wakuu wanakosa taarifa muhimu za kupanga na kufanya uchambuzi wa taarifa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika kufanya marekebisho ya mfumo ili kupata ripoti inayolingana na mahitaji mahususi ya Shirika, vile vile kutoa mafunzo kwa watumiaji wa mfumo ili kuboresha uelewa na umuhimu wa kazi za ripoti na kuhakikisha matumizi bora pamoja na kuweka mpango wa matengenezo ya mfumo ili kushughulikia mapungufu yoyote ya programu au hitilafu zinazoathiri uwezo wa kutoa ripoti.

### 4.1.12.9 Kutokuwepo kwa nyaraka muhimu za uanzishaji na usimamizi wa mradi wa AMR (Billing and Head System)

Kwa mujibu wa miongozo ya eGA ya utekelezaji wa Mradi wa TEHAMA wa Serikali inaitaka Taasisi ya Umma kuanzisha nyaraka za mradi wa TEHAMA ambayo itasaidia kusimamia, kudhibiti na kubaini changamoto mapema ambayo hupelekea wasimamizi wa mradi na wadau kufanya maamuzi ya kimkakati katika kipindi chote cha maisha ya mradi.

Wakati wa ukaguzi, tuliomba nyaraka mbalimbali za mradi wa "Billing and Head system" lakini hadi tunakamilisha ukaguzi, hatukuweza kupata nyaraka hizo. Miongoni mwa nyaraka zilizoombwa ambazo hazikupatikana kwa ukaguzi ni;

- Nyaraka rasmi ya pendekezo la utekelezaji wa mfumo wa AMR "Proposal for AMR system implementation".
- Nyaraka rasmi ya Mradi "Project charter".
- Nyaraka rasmi ya Utafiti yakinifu "Approved Feasibility study".

- Nyaraka rasmi ya mahitaji ya Mtumiaji "Approved User requirements documents".
- Nyaraka rasmi ya usanidishaji wa Mfumo.
- Nyaraka rasmi ya Ripoti za mafunzo ya Mfumo zilizoidhinishwa kwa vikundi tofauti vya watumiaji.
- Nyaraka rasmi ya Ripoti za Jaribio la Kukubalika kwa Mtumiaji (UAT).
- Nyaraka rasmi ya Mpango wa uendelevu wa Mfumo.
- Nyaraka rasmi ya Cheti cha kukamilika kwa Mradi.

Kukosekana kwa Nyaraka muhimu kunaweza kusababisha mchakato wa usimamizi wa mradi kuchelewa kukamilika jambo ambalo linapelekea kuathiri mpango mkuu wa ukamilishaji wa utengenezwaji, usimamizi na uendeshaji wa mradi. Kama inavyoonyeshwa kwenye ratiba ya mradi, mradi ulianza mwaka 11/19/2021 na ulitarajiwa kukamilika 7/20/2022, lakini hadi tunamaliza ukaguzi Novemba 29, 2023 mradi haujakamilika.

Zaidi ya hayo, husababisha kukosekana kwa uwajibikaji kwa washiriki wa timu ambao hawaelewi majukumu yao.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Umeme kuhakikisha unaboresha njia za mawasiliano ndani ya timu ya mradi ili kuhakikisha kuwa nyaraka zote muhimu zinatengenezwa, zimeidhinishwa, na kuwashirikisha wanaohusika. Vilevile Shirika linashauriwa kuanzisha kamati ya uendeshaji wa mradi "project steering committee"" ambayo itasaidia kufuatilia mradi huo pamoja na kuhakikisha uwepo wa nyaraka zote muhimu wakati wa kuanza kwa mradi.

#### 4.1.12.10 Usimamizi duni wa Mradi wa Mfumo wa AMR

Kwa mujibu wa kifungu nambari 2.3.4 cha Viwango na miongozo ya utekelezaji wa mradi wa TEHAMA wa Serikali kinatoa jukumu la ufuatiliaji na udhibiti wa mradi na utekelezaji wa mradi ili matatizo yanayoweza kujitokeza yaweze kutambuliwa kwa wakati na hatua za kurekebisha zichukuliwe inapobidi. Mchakato wa ufuatiliaji na udhibiti ni pamoja na kupima shughuli zinazoendelea za mradi na vigezo vya mradi kwa kuangalia ("cost, effort, scope, etc.") dhidi ya mpango wa mradi na msingi wa utendaji wa mradi, kwa hiyo inabainisha nini kifanyike ili mradi urudi kwenye mstari wake wa awali na kwa wakati.

Ukaguzi ulibaini kutotosheleza kwa usimamizi wa mradi wa TEHAMA kwa mfumo wa AMR kutokana na kutokuwepo kwa ratiba ya mradi inayoakisi awamu ya mradi iliyopo wakati wa ukaguzi. Ingawaje ratiba ya mradi iliyopokelewa na ukaguzi ilionesha mradi ulitakiwa kukamilika mwaka 2022 jambo ambalo lilifanya iwe vigumu kutabiri ni lini mradi huo utakamilika kutokana na kutokuwepo kwa ratiba nyengine ambayo inaakisi ratiba ya mradi. Zaidi ya hayo, Shirika halina ripoti ya utendaji wa mradi na usimamizi wa hatari, pamoja na nyaraka muhimu za mradi.

Hali hii inaweza kusababisha athari zifuatazo Timu ya mradi zinaweza kukosa mwelekeo, na kusababisha juhudi zisizo sawa na kupelekea kutozingatia malengo muhimu. Vile vile Wadau wanaweza kukosa taarifa za kutosha, na hivyo kusababisha kutoridhika na uwezekano wa kushindwa kwa mradi. Zaidi ya hayo, washiriki wa timu wa mradi wanaweza wasijue majukumu yao, na kusababisha ucheleweshaji na utekelezaji wa mradi usioridhisha.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Umeme Zanzibar kuhakikisha kwamba watu wanaosimamia miradi wana ufahamu wa kutosha wa usimamizi wa mradi kwa kufuata sheria na kanuni za Serikali. Vile vile uongozi ubainishe majukumu na wajibu kwa wanaohusika na mradi na uhakikishe kuwa washiriki wa timu wanaelewa michango yao binafsi pamoja na kuhakikisha uwepo wa nyaraka zote muhimu wakati wa kuanza kwa mradi.

### 4.1.13 WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII ZANZIBAR (ZCSRA)

Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa Wakala wa Matukio ya Kijamii Zanzibar (ZCSRA) kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 4.1.13.1 Kutozingatiwa kwa Taratibu za kukusanya Mahitaji ya watumiaji (User Requirements)

Katika mapitio ya mfumo wa CRVS, ukaguzi umebaini kuwa mfumo wa CRVS bado haujakamilika utengenezwaji wake kwa baadhi ya moduli zilizomo, licha ya kuwa mpango wa utengenezaji wa mfumo kwenye mradi huo (project schedule) unaonesha kuwa mradi umekamilika. Hali hii imejitokeza kutokana na kukosekana kwa ufanisi katika utaratibu wa kukusanya mahitaji ya utengenezwaji wa mfumo huo kwa watumiaji ikiwemo kutoshirikishwa ipasavyo wadau wa mfumo huo.

Kutozingatiwa ipasavyo kwa taratibu za kukusanya mahitaji ya mtumiaji wa mfumo kunaweza kupelekea kucheleweshwa kwa mchakato wa maendeleo ya utengenezwaji wa usimamizi wa mfumo, na kujitokeza kwa hatari ya kuanzisha mifumo ambayo haiendani na matarajio na mahitaji ya watumiaji (end users) jambo ambalo litapelekea kupatikana mifumo isiyokuwa na tija kwa taasisi na kuingiza hasara Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii kuhakikisha unafuata taratibu zilizobora za uanzishwaji wa mifumo ya TEHAMA pamoja na kukusanya mahitaji ya watumiaji kwa ufanisi na weledi ili kuhakikisha kuwa mifumo inatengenezwa kwa mujibu wa mahitaji na hatimae kupata mifumo yenye ufanisi katika utendaji kazi na kufikia malengo yaliyokusudiwa.

### 4.1.13.2 Kuwepo kwa tofauti ya taarifa baina ya Mfumo wa CRVS na kumbukumbu za Vitabu

Ukaguzi umebaini uwepo wa hitilafu ya tofauti ya takwimu za taarifa baina ya Mfumo wa Vizazi na Vifo (CRVS) na takwimu za vitabu vya matukio ya kijamii.

Tofauti hizi zinaweza kusababisha dosari katika utendaji na ufanisi wa udhibiti wa taarifa za matukio ya kijamii na pia zinaweza kuathiri usahihi wa ripoti zinazotolewa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar kuchukua hatua za haraka ili kufuatilia na kurekebisha dosari zinazobainika katika mifumo pamoja na taarifa za kwenye vitabu ili kuhakikisha kunakuwepo na uwiano wa taarifa za mfumo zinazoendana na taarifa za vitabu. Aidha, ukaguzi unaushauri uongozi wa ZCSRA kuimarisha taratibu za udhibiti wa ndani ili kuzuia hitilafu zinazoweza kujitokeza baadae kwenye mifumo na kwenye nyaraka nyengine za Wakala.

Jadweli hapo chini linaonesha mchanganuo wa utofauti wa kumbukumbu za matukio ya kijamii baina ya mfumo wa CRVS na Vitabu kwa kipindi cha mwezi wa Agosti, 2022 kutoka katika Wilaya ya Mjini, Unguja.

**Jadweli Nambari 39: Tofauti ya takwimu za Taarifa kati ya Mfumo wa CRVS na Vitabu**

| Aina ya Taarifa | Mfumo | Vitabu | Tofauti |
|---|---|---|---|
| Vizazi | 1359 | 950 | 409 |
| Vifo | 159 | 476 | 317 |

## 4.1.14 MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI ZANZIBAR (ZURA)

Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

### 4.1.14.1 Kukosekana kwa Mpango wa Matengenezo wa kuzuia uharibifu (Preventive Maintenance Plan)

Katika ukaguzi uliofanyika ZURA Unguja na Pemba ilibainika kwamba ZURA haina mpango wa matengenezo wa kuzuia uharibifu wa vifaa na vitendea kazi mbali mbali ikiwemo mifumo na miundombinu ya TEHAMA.

Mpango huu huainisha ratiba ya matengenezo ya vifaa/ vitendea kazi husika kulingana na vigezo mbali mbali ambavyo taasisi husika itaviona vinafaa kwa makundi tofauti kama vile hali ya vifaa, umri wa vifaa, kiwango cha matumizi ya vifaa, unyeti wa vifaa, gharama na umuhimu wa vifaa husika n.k.

Lengo la mpango wa matengenezo ni kuhakikisha kwamba vifaa vyote vya Taasisi ambavyo vinagharimu fedha nyingi kuvinunua vinatumika katika namna endelevu kwa muda uliopangwa na kuepusha hasara kwa Serikali kupitia ununuzi wa vifaa vyengine kama hivyo kwa sababu ya ubovu wa vifaa vilivyopo uliosababishwa na kukosa matengenezo ya kuzuia uharibifu mara kwa mara kulingana na mpango husika.

Kukosekana kwa mpango huo kumepelekea ZURA kuwa na vifaa mbali mbali vilivyoharibika na kushindwa kutengenezwa kwa Unguja na Pemba ambapo vifaa hivyo vimejumuisha Printers, Kompyuta, UPS, Kamera za Ulinzi za CCTV, mtandao (Network), routers, vipoza joto (ACs) n.k, ambavyo vimeharibika na kukosekana kwa utaratibu na ratiba rasmi wa matengenezo yake na kukosekana kwa tija na kupunguza ufanisi wa Shirika katika utekelezaji wa majukumu yake.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZURA kuandaa mpango wa matengenezo ya kuzuia uharibifu na kuhakikisha unafuatwa kwa kutenga rasilimali fedha na muda kwa ajili ya utekelezaji mipango husika kwa wakati.

Aidha, kwa upande wa vifaa ambavyo tayari vimekwisha haribika tunashauri vifanyiwe tathmini ya ubovu ili kubaini kama vinaweza kutengenezwa au vinahitaji kubadilishwa na kuchukua hatua stahiki mara moja ili kurejesha hali ya utendaji wa Taasisi na kuongeza tija na ufanisi.

#### 4.1.14.2 Kukosekana kwa Mpango wa Kusimamia Matukio ya TEHAMA (ICT Incident Management Plan)

Mpango wa usimamizi wa matukio (Incident Management Plan) ni utaratibu maalumu wa utambuzi, usajili, uhakiki, ufuatiliaji na utatuzi wa matukio mbali mbali ya TEHAMA katika Miundombinu na Vifaa vya TEHAMA pamoja na Programu Tumizi ambayo yanaweza kuathiri utendaji wa Taasisi kupitia TEHAMA na kuondoa Usiri, Uadilifu na Upatikanaji wa Taarifa mbali mbali za Serikali kwa wakati.

Ukaguzi umebaini kwamba ZURA haina Mpango rasmi wa kusimamia matukio ya TEHAMA katika kutambua, kusajili, kuhakiki, kufuatilia, kutatua na kutunza kumbu kumbu za matukio mbali mbali ya TEHAMA, tofauti na matakwa ya Kifungu nambari 9.2.2 cha ZURA ICT Guideline pamoja na matakwa ya miongozo ya viwango bora kubalifu vya TEHAMA kama vile **ISO/IEC 27001 Clause 10.2**. Hali hii inaweza kusababisha ucheleweshwaji wa kubaini na kutatua changamoto za TEHAMA.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati kusimamia uandaaji wa mpango wa kusimamia matukio ya TEHAMA kwa kuzingatia miongozo ya kitaifa na kimataifa (best practice) na kuhakikisha kwamba mpango huo unatumika katika usimamizi wa matumizi ya Miundombinu, vifaa na Programu zote za TEHAMA katika taasisi.

#### 4.1.14.3 Utekelezaji wa Mradi wa kutengeneza mfumo wa ZIRS nje ya muda wa mkataba

Kwa mujibu wa Mkataba nambari ISPG/DRMNRG/ZNZ/AFDB/QCBS/10/2019 uliongiwa baina ya mtoa huduma na Afisi ya Rais Fedha na Mipango kwa niaba ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (ZURA), Mkataba huo ulisainiwa tarehe 29/05/2020 na ambapo ulitakiwa kuanza kutekelezwa ndani ya siku 15 ambayo ni sawa na tarehe 13/06/2020 na kwamba ulitakiwa kukamilika ndani ya miezi 6 kuanzia tarehe 13/06/2020 sawa na tarehe 12/12/2020.

Ukaguzi umebaini kwamba sehemu kubwa ya mradi huu ilitekelezwa nje ya muda wa mkataba, yaani mradi huu ulitekelezwa pasipokuwa na mkataba hai kuanzia tarehe 13/12/2020 mpaka tarehe 30/12/2022 mradi ulipokamilika, sawa na ucheleweshaji wa mradi kwa zaidi ya miaka 2 na siku 18.

Aidha, hadi ukaguzi unakamilika haukupatiwa "addendum" ya kuongeza muda wa mkataba ili kuhalalisha kazi za mradi kuendelea kufanyika na Serikali kuwa na nguvu za kisheria za kuidhinisha malipo ya Mtoa huduma, hali hii inaweza kupelekea athari mbali mbali kwa Serikali/ Umma na mtoa huduma ikiwemo ukiukwaji wa Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 pamoja na kanuni zake kwa kuidhinisha malipo kwa mtoa huduma pasipokuwa na mkataba hai. Vile vile kunaweza kupelekea kuchelewesha manufaa ya mradi husika kwa ZURA hali iliyoikosesha ZURA fursa ya kupata tija na kuongeza ufanisi kwa kipindi chote ambacho mradi ulichelewa jambo ambalo linaweza kuongeza gharama za utekelezaji wa mradi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZURA kwa kushirikiana na uongozi wa Afisi ya Rais Fedha na Mipango kuhakikisha kwamba unazingatia matakwa ya Sheria za Nchi katika Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma bila kujali chanzo cha fedha zinazotumika kutekeleza kazi/ mradi husika kwakuwa Sheria za Nchi hazibagui aina ya chanzo cha fedha.

### 4.1.14.4 Kutokamilika kwa Utengenezwaji wa Mfumo wa Usimamizi wa Malalamiko (CMS)

"Software Development Life Cycle – SDLC" ni mchakato wa kina unaotumika katika utengenezaji wa Programu za TEHAMA ambapo utaratibu huu wakitaalamu unajumuisha hatua tofauti tofauti ambazo hufuatwa kipindi cha uanzishwaji mpaka kumalizika kwa Mfumo husika. Hatua hizo zikijumuisha: -

- Uchambuzi na Mahitaji ya Mfumo (Requirements Analysis).
- Ubunifu wa Mfumo (System Design).
- Matengenezo ya Mfumo (System Development).
- Upimaji (Testing).
- Uwasilishaji wa Mfumo (System Deployment).
- Uendeshaji na Matengenezo (Operation and Maintenance).

Lengo kuu la SDLC ni kuzalisha programu inayokidhi matarajio ya wateja, kusaidia kuzalisha programu kwa wakati uliokusudiwa pamoja na kusaidia kupatikana kwa programu ndani ya bajeti iliopangwa.

Aidha, ukaguzi umebaini kutokufuatwa kwa utaratibu wa utengenezaji wa mifumo ya TEHAMA (SDLC) katika utengenezaji wa Mfumo wa Malalamiko wa Mamlaka ya udhibiti wa huduma za Maji na Nishati (ZURA).

Hali hii inakwenda kinyume na matakwa ya viwango bora kubalifu (Best practice) **ISO/IEC 12207:2017 Clauses 7-24** pamoja na kifungu nambari **7.0** cha ZURA ICT guideline, kinachozungumzia utaratibu uliobora katika hatua za utengenezaji wa Mifumo ya TEHAMA katika Taasisi au Mashirika, ili kuhakikisha utekelezaji uliobora na wa uhakika wa utengenezaji wa Mifumo ya TEHAMA.

Kutokana na kutokuzingatiwa kwa taratibu za utengenezaji wa mifumo ya TEHAMA (SDLC) katika matengenezo ya Mfumo wa Malalamiko (Complaint Management System), kumesababisha kutokukamika kwa hatua za matengenezo ya Mfumo husika kwa kipindi kirefu ambapo matengenezo ya awali yalianza mnamo mwaka 2020.

Baadhi ya vipengele muhimu ambavyo bado havijakamilika katika utekelezaji wa Mfumo wa "Complaint Management System" inajumuisha moduli zifuatazo;

- Uwezo wa Mlalamikaji kutuma ombi lake mwenyewe kupitia Mtandao.
- Uwezo wa Mhandisi wa ZURA kuona na kuweka "Update" juu ya lalamiko Fulani.
- Uwezo wa Mfumo kutuma SMS za kawaida kwa walalamikaji kuonyesha kupokelewa kwa malalamiko yao.
- Uwezo wa Mfumo kumuwezesha Mlalamikaji kuingiza taarifa ya muendelezo wa lalamiko lake.
- Uwezo wa Mfumo kutoa ripoti za utekelezaji wa utatuzi wa malalamiko ya Wananchi.

Hali hii inaonesha udhaifu kwa Kitengo cha TEHAMA cha ZURA kutokana na kutofanya upembuzi yakinifu wa mahitaji ya watumiaji wa mifumo (user requirements) kabla ya kuanza kutengeneza mfumo huo jambo ambalo limepelekea kuchelewa kukamilika kwa Mfumo husika.

Aidha, Kutokukamilika kwa mfumo katika wakati muafaka kunaweza kupelekea kujitokeza kwa ongezeko la gharama za ziada zisizotarajiwa na hatimae kutofikia malengo na kutopatikana tija iliyokusudiwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZURA kufuata njia za Kitaalamu katika matengenezo ya Mifumo ya TEHAMA ili kuendana sambamba na matakwa ya miongozo bora kubalifu ya Kitaifa na Kimataifa.

#### 4.1.14.5 Kukosekana kwa nyaraka muhimu za Utengenzwaji wa Mifumo ya ndani ya TEHAMA

Katika kufanya Mapitio ya Mifumo ya TEHAMA iliotengenezwa na Mamlaka ya Udhibiti ya Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), Ukaguzi umebaini kukosekana kwa nyaraka muhimu za utengenezwaji wa mifumo hiyo, ambapo mpaka kumalizika kwa ukaguzi ZURA ilishindwa kutupatia nakala za nyaraka mbali mbali zilizotumika katika michakato ya utengenezaji wa mifumo tajwa hapo chini: -

- Mfumo wa usimamizi wa Malalamiko (Complaint Management System (CMS))
- Mfumo wa usimamizi wa Rasilimali Watu (Human Resource - Instify Management System (HRMIS)

Miongoni mwa nyaraka zilizohitajika kwa ajili ya ukaguzi ambazo hazikupatikana ni pamoja na nyaraka zifuatozo: -

1. Approved User Requirements Documents
2. Approved Project Plan or Project Schedule
3. Approved Project Cost Management Plan.
4. Approved User Acceptance Testing (UAT) reports.
5. Approved System Configuration Documents.
6. Approved System Operations Manual/ document.
7. System training Reports for different user groups.
8. User matrix documents.
9. Approved System sustainability plan.

Kukosekana kwa Nyaraka muhimu za utengenezaji wa Mifumo ya TEHAMA kunaenda kinyume na matakwa ya kifungu nambari **2.5** cha Muongozo wa viwango vya mahitaji ya uanzishwaji wa programu za TEHAMA kutoka Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar (eGAZ), pamoja na viwango bora kubalifu (Best Practice) **ISO/IEC/IEEE 15289:2011.** Ambayo imeweka umuhimu wa utengenezaji wa nyaraka mbali mbali katika hatua tofauti za utengenezaji wa programu za TEHAMA.

Utaratibu wa kutengeneza Mifumo ya TEHAMA pasipo kuzingatia uwepo wa nyaraka muhimu kunachangia katika kupatikana kwa Mifumo isiyokuwa na tija katika taasisi, kupatikana kwa Mifumo iliyokosa ufanisi katika utendaji kazi pamoja na kupatikana kwa Mifumo inayochukua mda mrefu kukamilika.

Ambapo kwa ujumla hali hii inachangia katika kudumaza maendeleo ya TEHAMA katika Taasisi za Umma pamoja na kuongezea Serikali mzigo na hasara ya kudhamini mifumo isiokua rasmi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZURA kuhakikisha unafuata njia za kitaalamu katika kutengeneza mifumo ya TEHAMA ya ndani, kama inavyoelekezwa kupitia miongozo mbali mbali ya kitaifa na kimataifa.

### 4.1.14.6 Mapungufu yaliyobainika katika Mradi wa Ufungaji wa chumba cha kuhifadhia Mitambo (Mini Data Center) ZURA

Mradi wa Usambazaji na Ufungaji wa vifaa kwa ajili ya chumba kidogo cha kuhifadhia mitambo (Mini Data Center) ulitekelezwa kupitia Mkataba nambari **SMZ/FO118/W/NCB/2021/22/20,** baina ya Mamlaka ya Udhibiti wa huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) na Kampuni ya Neymon Investiment LTD, ambapo mradi huo uligharimu kiasi cha shilingi 177,000,000.

Mradi huo ulianza mnamo tarehe 1 Oktoba, 2022 na kumalizika tarehe 30 Novemba, 2022 ambapo ulijumuisha usambazaji wa vifaa na ufungaji wa mifumo ifuatayo:-

- Ufungaji wa sakafu ya chuma ilioinuliwa (Steel Raised Floor Tiles).
- Ufungaji wa Mfumo wa kufuatilia hali ya kimazingira ya chumba cha kuhifadhia Mitambo (Monitoring System).
- Ufungaji wa Mfumo wa hali ya hewa (Air conditional System).

- Ufungaji wa Mfumo wa Umeme na Mfumo wa umeme wa hakiba ( Main Power System and Redundant Power Supply).
- Ufungaji wa Mfumo wa Ulinzi kwa kutumia Kamera (Surveillance System).
- Ufungaji wa Mfumo wa kudhibiti uingiaji wa chumba cha kuhifadhia Mitambo (Door Access Control).
- Uwekaji wa Mazingira Bora ya mpangilio wa waya za mawasiliano katika chumba cha mitambo (Cable Management).
- Utayarishaji wa Nyaraka za Matumizi kwa ajili ya chumba cha Kuhifazia Mitambo (Documentation and Control).

Katika utekelezaji wa Mradi huu ukaguzi umebaini mapungufu mbali mbali yanayoendana kinyume na matakwa ya Mkataba wa Mahitaji na Ufafanuzi wa kiufundi (Requrement and Technical Specification) kama ifuatavyo:-

- **Kutofanya Kazi kwa Mfumo wa Ufatiliaji wa hali ya kimazingira ya Chumba cha Seva**

Kwa kuzingatia matakwa ya Mkataba uliosainiwa baina ya ZURA na Mtoa Huduma katika kipengele nambari 7 cha Waraka wa Vipimo vya Mahitaji na Ufafanuzi wa kiufundi (Requirement and Technical Specification) kinachozungumzia uwekaji wa mfumo wa ufatiliaji ambao utakua na uwezo wa kufatilia hali halisi katika chumba cha Mitambo ikiwemo kufatilia hali ya joto, mzunguko wa hewa, uwezo wa kugundua uvujaji wa maji, ufuatiliaji wa usalama, ufuatiliaji wa hali ya nishati na umeme, uwezo wa kugundua uwepo wa moshi nakadhalika.

Ukaguzi umebaini kwamba mfumo wa kufuatilia hali ya hewa katika "Mini Data Center" haujakamilika kwa mujibu wa mkataba japokuwa mtoa huduma ameshalipwa fedha zote, aidha ukaguzi umebaini kutokufungwa kwa baadhi ya vifaa muhimu ambavyo ni: -

- "Screen Monitor" ya inchi 55 iliyokusudiwa kuonesha hali halisi ya hewa katika chumba hicho.
- "Sensors" ambazo kazi yake ni kufuatilia kiwango cha joto, kiwango cha umeme na mzunguko wa hewa na kupeleka taarifa hizo kwenye "Screen Monitor" kwa ajili ya kufanyiwa kazi.

Kutokufanya kazi kwa Mfumo wa ufatiliaji wa hali ya kimazingira katika chumba cha kuhifadhia Mitambo kunaweza kusababisha kuharibika kwa vifaa vilivyomo ndani ya chumba hicho kutokana na kuongezeka kwa joto kali pindipo mfumo huo ukiharibika na kushindwa kutoa ripoti na ukumbusho (notification) kwa wakati.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZURA kufanya uhakiki wa kina kabla ya kupokea miradi ya TEHAMA kutoka kwa wakandarasi katika hatua za kuhakikisha utekelezaji wa Mradi kwa mujibu wa makubaliano. Aidha, ukaguzi unaushauri uongozi wa ZURA kufunga Skrini za ufatiliaji wa mfumo kwa lengo la kuondoa athari zitakazoweza kujitokeza kutokana na kukosa tarifa za hali ya chumba cha seva kwa wakati husika.

### 4.1.14.7 Dosari katika mfumo wa Ulinzi wa kamera (CCTV camera system)

Mfumo wa Kamera za CCTV unasaidia kuonesha kumbukumbu za matukio yote yanayofanyika katika mazingira ya Afisi kwa lengo kuu la kutunza ushahidi kwa ajili ya hatua nyengine za Mashtaka kwenye vyombo vya kutoa haki ikiwa kumetokezea uhalifu wa aina yoyote.

Kwa kuzingatia Kifungu namba 4.3.4 cha muongozo wa Serikali Mtandao wa mwezi Machi mwaka 2022, Taasisi inatakiwa kuhakikisha uwepo Usanifu wa Usalama wa Taasisi (Institutional Security Architecture) amabo utahakikisha upatikanaji wa usalama wa Taarifa na nyenzo muhimu za TEHAMA.

Kwa kuzingatia hayo Ukaguzi umebaini dosari mbali mbali katika mfumo wa Ulinzi kwa kutumia Kamera katika Ofisi za ZURA upande wa Unguja na Pemba kama zifuatazo;

### I. Kutokufanya kazi kwa Asilimia 22.2 za kamera katika Ofisi Kuu ya ZURA Unguja

Katika kufanya mapitio ya mfumo wa Ulinzi kwa kutumia kamera katika Ofisi kuu za ZURA Unguja, ili kuangalia utendaji kazi wa mfumo huo, Ukaguzi umebaini uwepo wa Kamera 12 kati ya 54 sawa na asilimia 22.2 ambazo hazifanyi kazi kwenye jengo la ZURA Unguja. Hivyo kusababisha kukosekana kwa tarifa za ulinzi na ushahidi kwa njia ya kamera katika maeneo hayo kwa kipindi kisichopungua miezi 6.

Hata hivyo ukaguzi ulishindwa kupatiwa ushahidi juu ya hatua zilizochukuliwa katika utengenezaji wa Kamera zilizoharibika. Jambo linaloenda kinyume na kifungu nambari **10.5 cha ZURA ICT GUIDELINE** kinachohitaji uwepo wa utaratibu endelevu wa kufanya matengenezo ya nyenzo za TEHAMA hali hiyo inaweza kusababisha dosari zifuatazo:-

**Uhalifu Usiothibitishwa:** Bila kamera za ulinzi, ni vigumu kuthibitisha uhalifu na kuchukua hatua dhidi ya wale wanaohusika. Kamera zinasaidia katika kurekodi matukio ya uhalifu na kuwafanya wahalifu wawe na wakati mgumu kuepuka kukamatwa pamoja na kupinga mashtaka.

**Kupotea kwa Mali**: Kamera za ulinzi zinasaidia kulinda mali za thamani za Ofisi. Kutokuwepo kwa ulinzi wa kamera kunaweza kutengeneza mwanya wa wizi wa mali za Taasisi na hivyo kusababisha upotevu na hasara kubwa kwa Taasisi na Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZURA kuhakikisha kwamba unayafanyia kazi mapungufu yote yaliyobainika katika hoja hii.

### 4.1.14.8 Kusitishwa kwa Mfumo wa Kuchunguza (Scanning) Mafuta ya kimagendo na Uchakachuaji (Fuel Marking System) ZURA

Ukaguzi umebaini uwepo wa usitishwaji wa Mfumo uliokua ukitumika katika Kupima na kuhakikisha Nishati ya Mafuta inayopatikana kwa Wananchi imefata Sheria na Taratibu zilizoekwa katika Nchi. Mfumo huo ulianza kufanya kazi mnamo tarehe 1 Novemba, 2022. Kwa kuzingatia makubaliano yaliofikiwa katika zabuni yenye kumbukumbu namba **SMZ/FO118/NC/ICB/2019-20/17** ya Huduma ya upimaji wa mafuta ilitarajiwa kumaliza muda wake mnamo 31 Octoba, 2023.

Aidha ukaguzi ulishindwa kujiridhisha njia madhubuti zilizowekwa na ZURA katika kuhakikisha zinasaidia Serikali katika kuzuia na kupambana na vitendo vya kimagendo vya Mafuta katika visiwa vya Unguja na Pemba baada ya kusitisha matumizi ya mfumo wa upimaji wa Mafuta (Fuel Marking Sysytem).

**Kupungua makusanyo ya Kodi za Serikali:** Kutokana na kukosekana kwa njia ya kuthibitisha uhalali wa Mafuta endapo yakifikishwa katika vituo vya kuuzia mafuta (Filling Stations) Hii inaweza kupelekea mafuta hayo kupanda na hivyo kupunguza Pato la Serikali linaloingia kupitia Tozo zitokanazo na uingizaji wa Mafuta.

**Kuhatarisha Usalama wa vyombo vya Wananchi na kuingizia Serikali Hasara ya Fidia:** Kukosekana kwa njia madhubuti za kupambana na uingizwaji wa mafuta bila ya kufata taratibu katika nchi kunaweza kuchangia kwa kiasi kikubwa kupatikana kwa mafuta yasiokidhi vigezo na hivyo kupelekea uharibifu katika vyombo vinavyotumia mafuta hayo, Hali hio inaweza kuisababishia Serikali mzigo wa ulipaji wa fidia endapo ikibainika mafuta yaliotumika ndio chanzo cha matatizo yaliojjitokeza.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZURA kutengeneza mikakati thabiti ya kuzuia na kudhibiti upatikanaji wa huduma za maji na nishati katika viwango vilivyo tarajiwa ili kufikia lengo la utengenezwaji wa Mamlaka hii na Serikali.

### 4.1.14.9 Kutokufanya kazi kwa Mfumo wa kukagua vihatarishi (Walthrough Scanners)

Mfumo wa kukagua vihatarishi ni mfumo wa kiusalama unaotumika kuchunguza vihatarishi ambavyo vimeambatana na mtu wakati wa kuingia katika maeneo tofauti ikiwemo katika Viwanja vya Ndege, vituo vya Treni, majengo ya Serikali na kadhalika.

Ukaguzi umebaini mfumo huo haukuwahi kutumika kwa kuchunguza vihatarishi (Walkthrough scanner) katika lango kuu la kuingilia katika jengo la Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) tokea kipindi cha kukamilika kwa uwekwaji wa Mfumo huo mnamo mwaka 2020.

Aidha, ukaguzi ulishindwa kujiridhisha kutokana na kutopatiwa vielelezo vya uwepo wa kompyuta inayohifadhi na kuonesha uchambuzi wa matukio ya watu wanaopita na kukaguliwa na Mfumo huo wa kiusalama, hii ni kutokana na kutokuepo kwa sehemu iliokusudiwa kuwekwa kwa seva ya kuongoza Mtambo huo (Control Center).

Vile vile, ukaguzi ulishindwa kujiridhisha kutokana na kutopatikana vielelezo vinavyoonesha uwepo wa mafunzo yaliopatiwa wataalam (Security personel) kwa lengo la kuongoza na kusimamia Mfumo huo wa Ulinzi.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na lengo la Serikali la kuwekeza katika Mifumo ya kisasa ambayo ina lengo la kutumika katika kuboresha huduma za kiusalama katika ofisi na majengo ya Serikali.


Ukaguzi unaushauri uongozi kuhakikisha utekelezaji wa matumizi ya mifumo ya usalama ya ndani kwa lengo la kuboresha uendeshaji na kulinda usalama kama ilivyo kadiriwa

#### 4.1.14.10 Udhaifu katika udhibiti wa utoaji wa Leseni kupitia Mfumo wa ZIRS

Baada ya kufanya mapitio ya Mfumo wa ZIRS na kuangalia hatua zinazotumika katika utowaji wa Leseni za uendeshaji wa Biashara za Mafuta kwa Wadau wa ZURA, Ukaguzi umebaini uwepo wa udhaifu katika udhibiti wa upatikanaji wa Leseni hizo, ambapo mfumo unamuwezesha Mtumishi wa ZURA kuwa na uwezo wa kuiona na kuipakua Nyaraka ya Leseni kabla ya kukamilika kwa hatua za malipo. Hali hii inaweza kupelekea uwepo wa mianya ya rushwa na kuikosesha Serikali mapato kwa mtumishi asiyekuwa muadilifu kwa kupakuwa na kumkabidhi mteja nyaraka ya leseni kabla hajafanywa malipo.

Aidha, ukaguzi umebaini Mfumo kutokua na uwezo wa kubaini endapo Leseni iliyopakuliwa na kutumika katika vituo vya mafuta kuwa imekamilika katika hatua za  malipo au laa.

**Picha Nambari 12: Leseni ambayo haijamaliza taratibu za malipo katika mfumo wa ZIRS ambapo Afisa wa ZURA ana uwezo wa kuipakua kabla ya kufanyiwa malipo**




Ukaguzi unaushauri uongozi  wa ZURA kuhakikisha unaongeza udhibiti katika eneo hili kwa kuhakikisha kwamba Leseni inaonekana katika mfumo baada ya kukamilisha hatua za Malipo, na kwamba leseni ikishatolewa katika mfumo mara ya kwanza (original) na kama itatakiwa kutolewa tena kwa mara nyingine itambulike kama nakala (Copy 1,2,3 etc.).


Aidha, kuwekwe mgawanyo wa majukumu ambapo afisa anayehusika na leseni pekee ndo aweze kuona leseni pale inapokamilika katika hatua ya Malipo.

### 4.1.14.11 Kujirudia kwa Taarifa zinazoingizwa kwenye Mfumo wa ZIRS (Data Redundancy)

Kujirudia kwa taarifa kwenye mfumo ni kitendo cha kuwepo kwa nakala nyingi za taarifa zinazofanana ndani ya Mfumo au Kanzidata. Hali hii inaweza kutokea kutokana na utaratibu mbaya wa kuhifadhi au kurekodi Taarifa ambapo taarifa hio hujirudia mara nyingi bila sababu ya msingi.

Ukaguzi umebaini baadhi ya taarifa za Mfumo wa ZIRS zinajirudia bila ya sababu maalum kama inavyoonekana katika picha hapo chini:-

**Picha Nambari 13: Hali ya takwa la mfumo la kuingiza taarifa kuhusiana na kituo cha Mafuta wakati wa ukaguzi ingawa taarifa hizo zilishaingizwa katika mfumo wakati Kituo husika kinasajiliwa**




Wingi wa taarifa zinazofanana ambazo zinajaza nafasi ya kuhifadhi taarifa katika Seva (storage) na kupelekea kuongeza gharama za uwendeshaji wa mifumo ya kielektroniki kwa kulazimisha manunuzi ya Seva kubwa zaidi ili kukabiliana na mahitaji makubwa ya nafasi za kuhifadhi taarifa bila sababu za msingi.

“Sloweness” ya mfumo mara kwa mara inayosababishwa na wingi wa taarifa ambazo hazina msingi katika mfumo pamoja na ugumu wa kusimamia ubora wa taarifa mbali mbali zinazopatikana katika mfumo ikiwa ni pamoja na kusasisha taarifa ikiwa kuna nakala nyingi za data inayohusiana na taarifa hiyo.


Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZURA kuhakikisha unaweka utaratibu bora wa kuhifadhi “re-use” taarifa mbali mbali ndani ya mfumo katika hatua tofauti za mfumo matumizi na uingizaji wa data.

Aidha, Ukaguzi unashauri ZURA kuhakikisha kwamba taarifa zote zinazoingizwa katika mfumo zinazingatia sifa ya ubora na ukamilifu (quality and complete data) ili zitumike kuisaidia Serikali kufanya maamuzi sahihi kwa wakati.

#### 4.1.14.12 Kuwepo kwa Taarifa zisizo sahihi ndani ya Mfumo (incorrect data)

Kwa kuzingatia kifungu nambari 4.1.1(c) cha muongozo wa Wakala wa Serikali Mtandao wa mwezi Machi, 2022, kinachozitaka Taasisi za Umma kuhakikisha uwepo wa utaratibu wa upatikanaji na uingizaji wa taarifa bora na sahihi ndani ya Mifumo ya TEHAMA. Ukaguzi umebaini uwepo wa baadhi ya taarifa zisizo sahihi ndani ya mfumo wa ZIRS kama ilivyoambatanishwa katika picha hapo chini.

**Picha Nambari 14: Eneo la kijiografia kinapopatikana Kituo cha Mafuta cha Bavuai ambapo mfumo unaonesha Kituo hicho kikiwa karibu na eneo la "Chwaka Police Station" tofauti na uhalisia ambao ni kwamba Kituo husika kinapatikana eneo la "Mombasa Unguja" umbali wa zaidi ya kilomita 34.5 kutoka eneo linalosomeka katika mfumo**




Uwepo wa taarifa ambazo hazina usahihi katika mfumo wa ZIRS unaweza kuathiri ubora wa maamuzi yanayofanywa na Serikali kutokana na taarifa zilizomo ndani ya mfumo na kuondoa utegemezi wa mifumo ya TEHAMA katika kuongeza tija na ufanisi. Aidha, hali hii inakwenda kinyume na miongozo halali ya Serikali kama ilivyoonukuliwa hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZURA kuhakikisha unaweka utaratibu bora wa kuthibitisha (review) usahihi wa taarifa zinazoingizwa kwenye mfumo kabla ya "posting" ili kuhakiki ubora na ukamilifu wa taarifa husika kila hatua ya matumizi ya mfumo.

### 4.1.14.13 Mapitio ya Mfumo wa Usimamizi wa Malalamiko (Complaint Management System)

Mfumo wa CMS ni mfumo uliotengenezwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (ZURA) kwa lengo la kuiwezesha Mamlaka kuhifadhi na kufuatilia malalamiko ya Wananchi kuhusiana na changamoto za upatikanaji wa huduma za Maji na Nishati.

Kwa kuzingatia matakwa ya Miongozo ya Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar ya Machi, 2022 (ICT Guidelines), Miongozo ya Wakala wa Serikali Mtandao ya Utengenezaji wa Mifumo ya Kielekroniki pamoja na Viwango kubalifu (Best practice), Ukaguzi umebaini Dosari mbali mbali katika mfumo wa Usimamizi Malalamiko (CMS) kama ilivyoelezewa hapo chini: -

### 4.1.14.14 Dosari katika utowaji wa Ripoti za Mfumo wa usimamizi wa malalamiko (CMS)

Ripoti za mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano TEHAMA ni nyenzo muhimu ambazo zinaweza kutoa ufahamu na taarifa kuhusu utendaji, usalama, na mwenendo wa mfumo na shughuli fulani ndani ya Taasisi.

Ripoti hizi zinaweza kutolewa kwa viongozi wa juu, timu za IT, na wadau wengine, na zinaweza kujumuisha Ripoti za Utendaji, Ripoti za Mafanikio na kadhalika.


Aidha, ukaguzi umebaini kutokupatikana kwa ripoti zilizo sahihi kutoka ndani ya mfumo wa Malalmiko wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati ambapo ripoti zinazopatikana ndani ya Mfumo haziakisi uhalisia na ripoti za utekelezaji wa kitengo cha Uhusiano wa Umma ZURA.

Hali hii inaenda kinyume na Matakwa ya Kifungu nambari 5.1 cha Muongozo wa TEHAMA wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (ZURA ICT GUIDELINE) kinachozitaka Taasisi kuweka utaratibu wa kuhakikisha upatikanaji wa Tarifa za Uhakika, Sahihi na zilizokamilika.


### Jadweli Nambari 40: Utofauti baina ya ripoti zinazopatikana kutoka kwenye mfumo wa Malalamiko (CMS) na Taarifa zinazopatikana kutoka kwenye ripoti za Utekelezaji wa Kitengo cha Uhusiano wa Umma ZURA

| | Idadi ya Malalmiko Yote Yaliyosajiliwa | Idadi ya Malalamiko Yaliyofanyiwa Kazi (Resolved) | Idadi ya Malamiko Yanayoendelea Kufanyiwa Kazi (On Progress) |
|---|---|---|---|
| **Ripoti Kutoka Katika Mfumo** | 77 | 0 | 76 |
| **Ripoti Ya Utekelezaji Kutoka Kitengo Cha (Pr)** | 90 | 65 | 25 |
| **UTOFAUTI** | **13** | **65** | **51** |

### Mchoro Nambari 3: Utofauti wa Ripoti za Mfumo wa (CMS) na Ripoti halisi za utekelezaji Kitengo cha (PR)



**Picha Nambari 15: Muhtasari wa Ripoti ya Malalamiko kutoka katika Mfumo wa Malalamiko wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati**




**Kukosa Taarifa Muhimu za Uendeshaji:** Ripoti za mfumo zinasaidia kutoa taarifa muhimu kuhusu uendeshaji wa mfumo na shughuli za uzalishaji na utendaji katika Taasisi. Kukosa ripoti kunaweza kufanya iwe vigumu kutambua hali ya uendeshaji, utendaji na ufuatiliji wa majukumu katika Taasisi.

**Kukosa Kugundua Mapema Matatizo:** Ripoti za mfumo zinaweza kutoa ishara za mapema kuhusu matatizo au makosa yanayotokea. Kukosa ripoti kunaweza kuchelewesha ugunduzi wa matatizo na hivyo kusababisha madhara makubwa baadae.

Ukaguzi unaishauri ZURA kuhakikisha mifumo inauwezo wa kutoa ripoti zenye uhalisia na Sahihi ili kuisaidia Serikali katika hatua za Kufanya Maamuzi kupitia Taarifa zinazopatikana kutokana na Mifumo ya TEHAMA.

### 4.1.14.15 Kutofanya kazi ipasavyo "Logs/ Audit Trails" ndani ya Mfumo wa ZIRS

"Logs/ Audit trails" ni rikodi za kumbukumbu za matukio yanayofanyika katika mfumo yanayojumuisha usanidi na matumizi ya mfumo katika miamala mbali mbali muda wote mfumo unapotumika au kufanyiwa mabadiliko. "Audit trails" hutumika kama njia mbadala ya kusimamia Usiri, Uadilifu, Usalama na Upatikanaji wa taarifa za Serikali muda wote.

"Audit logs" zinahusisha nakala za taarifa za miamala yote inayofanyika katika mfumo ambazo zinaweza kuwa katika hatua ya kanzidata na programu tumizi, aidha, "audit trails" zinahusisha nakala za taarifa za mabadiliko yanayofanyika katika mfumo kwenye usanidi au kufuta (delete) taarifa fulani katika mfumo. Miongoni mwa taarifa zinazohifadhiwa kwenye "audit trails" ni pamoja na mtumiaji wa mfumo (user), aina na muamala/ mabadiliko ya yaliyofanyika, tarehe na muda, na mabadiliko yoyote yaliyofanywa kwenye kanzidata au programu tumizi (mfumo).

Ukaguzi umebaini kuwa mfumo wa ZIRS haujawezeshwa kikamilifu kuchukua na kutunza "audit trails" za maeneo mbali mbali kama vile "user logs" yaani "filter user logs based on the time frame".

Aidha, ukaguzi umebaini mfumo kupitia kipengele cha "Logs" kilichowekwa hakina uwezo wa kuonyesha kumbukumbu zaidi ya rikodi 50, ambazo hazijitoshelezi katika kufuatilia tukio/ jambo fulani lililotokea katika mfumo kwa kipindi angalau cha mwaka mmoja.

**Kukwamisha ufuatiliaji na tathmini ya matukio yanayoweza kutokea kwenye mfumo:** Bila "logs/ audit trail" toshelevu zenye wigo mpana wa kupata nakala za matukio ya mfumo (event viewer logs) na matukio ya kanzidata (database logs) kwa kipindi cha angalu mwaka mmoja inakuwa vigumu kufuatilia na kutathmini shughuli zilizofanyika katika mifumo na kanzidata. Hii inaweza kuchochea utendaji wa matukio maovu ya aina mbali mbali ikiwemo ubadhirifu wa fedha za umma katika mfumo pasipo kubainika.

**Ukosefu wa Uwajibikaji:** Uwepo wa audit trail husaidia katika kutambua ni nani aliyesababisha au kuhusika na shughuli ama ubadhirifu fulani. Bila rekodi hizi, uwajibikaji unakuwa mgumu kuthibitisha.

**Kupungua kwa Usalama:** Audit trail husaidia katika kugundua shughuli zisizotarajiwa au za kutiliwa shaka. Kutowezeshwa kwa kumbukumbu hizi kunaweza kusababisha hatari zaidi ya usalama kwani itakuwa vigumu kubaini shughuli za kushukiwa za kimtandao au udanganyifu.

**Kukosa Uthibitisho kwa Madhumuni ya Kisheria:** Katika mazingira mengi, kama vile kufuata sheria za ulinzi wa data au kanuni za usalama wa mifumo, audit trail ni muhimu kutoa uthibitisho kwa madhumuni ya kisheria. Kutoweka kwa rekodi hizi kunaweza kusababisha kutothibitisha kufuata kwa sheria na kanuni hizo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZURA kutekeleza mgawanyo wa majukumu kwa mujibu wa matakwa ya viwango bora kubalifu vya TEHAMA pamoja na miongozo ya kitaifa ili kuhakikisha kwamba kila mtumiaji wa mfumo anapewa ufikiaji wa mfumo kwa kuzingatia majukumu yake ya msingi pamoja na "Segregation of Duties (SoD)" kwa lengo la kuimarisha usiri, uadilifu, upatikanaji wa taarifa pamoja na usalama wa mifumo ya TEHAMA.


### 4.1.14.16 Dosari ya kiusalama katika upatikanaji wa Mfumo wa Usimamizi wa Malalamiko (SSL Certificate issue)

SSL (Secure Sockets Layer) Certificate, ni cheti cha kidigitali kinachothibitisha utambulisho wa tovuti au Mfumo na kutoa usimamizi wa uhusiano salama (encrypted) kati ya mtumiaji na seva ya Mfumo. SSL hutumika kuboresha usalama wa mawasiliano kwenye tovuti na Mifumo ambapo huzuia uwezekano wa watu wasiokuwa na nia njema kusoma au kuharibu taarifa inayopitishwa baina ya mtumiaji na Seva.

Ukaguzi umebaini Mfumo wa (CMS) kutokuekewa SSL certificate ilio hai na hivyo kuhatarisha mawasiliano yanayofanyika baina ya Mtumiaji na Seva kupitia Mtandao.

Hali hii inaendana kinyume na kifungu **nambari 4.3.4** cha Muongozo wa Serikali Mtandao eGAZ wa mwezi machi, 2022, kinachohitaji uwepo wa utaratibu utakao hakikisha usalama wa Tarifa na mawasiliano baina ya Mtumiaji na Seva.

**Picha Nambari 15: Upatikanaji wa Mfumo wa Usimamizi wa Malalamiko (Complaint Managent system) kupitia mtandao (WAN) bila ya kua na "SSL certificate" iliokua hai**




**Ukosefu wa Usalama wa Mawasiliano:** Mifumo isiyo na SSL certificate hutuma data bila ya kuwa na usalama imara (encryption) ambapo hali hii inaweza kufanya mawasiliano kati ya mtumiaji na Mfumo kuwa wazi kwa watu wa tatu (Third parties), ambapo watakua na uwezo wakuvuruga faragha na kudukua habari za watumiaji.

**Kupungua kwa Imani ya Wateja:** Watumiaji wanaweza kuwa na wasiwasi kuhusu kutoa taarifa zao za kibinafsi kwenye tovuti ambayo haioneshi ishara za usalama "SSL certificates" na "https://" kwenye URL. Hii inaweza kusababisha kupungua kwa imani na kuondoka kwa walalamikaji.

Ukaguzi unaishauri ZURA kuhakikisha inaweka utaratibu mzuri wa kiusalama katika kufikia mifumo yao, ili kuboresha usalama wa taarifa zinazosafirishwa baina ya mtumiaji na Seva.

#### 4.1.14.17 Kukosekana kwa zana za kisasa za kufuatilia utendaji wa Mtandao (Modern Network Monitoring Tools)

Zana za ufuatiliaji wa Mtandao ni zana zinazoweza kufuatilia Mtandao kwa wakati halisi (real time monitoring) na kutoa taarifa ya haraka juu ya utendaji kazi na hali ya Afya ya Mtandao (Network health) kwa muda wa masaa 24 siku 7 za wiki. Zana hizi huruhusu taasisi kufanya ufuatiliaji wa Mtandao na kudhibiti mapungufu mbali mbali kabla hayajatokea (pro-active measures) na kusaidia kuongeza ufanisi wa mtandao unaopelekea kuongeza tija katika utumishi kwa kutumia TEHAMA.

Kinyume na matarajio ya wadau wa ZURA nchini pamoja na miongozo ya viwango bora kubalifu **ISO/IEC 27001(A.18)** Ukaguzi umebaini kwamba ZURA haina zana za kufuatilia hali ya Mtandao wake (Network Monitoring system) yenye uwezo wa kuifahamisha hali halisi kwa wakati (real time) ya Mtandao.

Kwa kuzingatia umuhimu wa Mifumo pamoja na miundomimbinu ya kimtandao inayopatikana ndani ya ZURA mfano Mfumo wa HRMIS pamoja na CMS.

ZURA ilitarajiwa iwe na uwezo wa kufuatilia na kufahamu kwa wakati halisi hali ya upatikanaji wa mifumo husika ili kuhakikisha kwamba hakuna mfumo utakao kuwa "down" bila ya ZURA kuwa na taarifa ili kutoa taarifa stahiki kwa watumiaji wa mifumo hiyo kabla tatizo halijatokea na kuweka mikakati mahususi ya kupata ufumbuzi wake kwa haraka.

Ucheleweshwaji wa ugunduzi wa matatizo ya Mtandao na kupelekea kuchelewa kutoa ufumbuzi wa tatizo husika hali inayoweza kukwamisha utoaji wa huduma kwa jamii katika taasisi mbali mbali za umma.

Kukosa fursa za kufanya maboresho ya mfumo wa Mtandao kwa kukosa taarifa muhimu ambazo zingeweza kupatikana kupitia zana za ufuatiliaji wa Mtandao.

Kushindwa kubaini matatizo na kutoa ufumbuzi kabla hayajatokea (pro-active measures) na badala yake kungojea mpaka matatizo yatokee kisha ndo ZURA ianze kutafuta chanzo na ufumbuzi wake hali inayochukuwa muda mrefu wakati taasisi za umma zikiendelea kukosa huduma muhimu za ufikiaji wa mifumo yao.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZURA kuhakikisha unatenga bajeti ya kutosha ya kununua zana za kisasa za kusimamia mfumo wa Mtandao na Mifumo ya TEHAMA pamoja na miundombinu yake yote kwa wakati halisi (real time network monitoring tools) kwa haraka iwezekanavyo ili kuepusha athari zinazoweza kutokea kama zilivyoainishwa.

### 4.1.15 BARAZA LA USIMAMIZI WA LESENI ZA BIASHARA (BRLC)

Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa Baraza la Usimamizi wa Leseni za Biashara (BRLC) kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 4.1.15.1 Matumizi ya fedha yasiyokuwa na tija shilingi 22,140,000

Ukaguzi ulibaini kwamba Baraza la Usimamizi wa Leseni ya Biashara Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023 lilifanya mafunzo ya matumzi ya Mfumo wa NOBS kwa wafanyakazi wake tofauti ikiwemo watendaji wa TEHAMA kwa gharama za takriban shilingi 22,140,000.

Dosari iliyobainika ni kwamba tangu kumalizika mafunzo hayo kwa zaidi ya mwaka mmoja sasa mfumo huo haujawahi kutumika na wala haujulikani hatima yake. Hali hii ni kuitia hasara Serikali kutokana na kutotumika kwa mfumo huo kwa vile watendaji waliofundishwa matumizi ya mfumo wanaweza kusahau na kupelekea kuhitaji mafunzo mengine wakati wa kuanza matumizi ya mfumo huo jambo ambalo litakosa tija ya kufanyiwa mafunzo ya awali.

Aidha, kukosekana kwa ufanisi wa matumizi ya mfumo huo kunaweza kusababisha upotevu wa fedha na rasilimali za umma.

Ukaguzi unaishauri Serikali kupitia Baraza la Udhibiti wa Usimamizi wa Mfumo wa Utoaji Leseni kufuatilia na kuchukuwa hatua stahiki kwa kushirikiana na Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar za kuhuwisha utekelezaji wa mfumo huo na kuinusuru Serikali kutopata hasara.

#### 4.1.15.2 Dosari za kiusalama zilizobainika katika chumba cha Seva (Server Room)

Chumba cha Seva ni eneo maalum ambalo hutumiwa kuhifadhi na kusimamia vifaa vya kompyuta na miundombinu inayosaidia utoaji wa huduma za mtandao, uhifadhi wa data, na mifumo mengine muhimu katika taasisi au biashara.

Kwa mujibu wa Muongozo wa eGAZ wa mwaka 2022 katika kifungu cha 4.3.2 unaelekeza taasisi kutekeleza usalama wa TEHAMA kwa kuweka usalama katika taasisi kwa kufuata Miongozo ya Wakala wa Mtandao Serikalini.

Ukaguzi ulibaini kuwa Baraza la Udhibiti wa Mfumo wa Utoaji wa Leseni (BLRC) kutokufunga Kamera za ulinzi maeneo yote ya Baraza.

Kutokufungwa kwa Kamera maeneo yote ya ofisi kunapelekea kukosekana kwa usalama madhubuti na jambo ambalo linaweza kupelekea wahalifu kushawishika kufanya vitendo vya wizi na uhalifu na hatimae kushindwa kupatikana ushahidi wa matukio yaliyofanyika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Usimamizi wa Leseni za Biashara (BLRC) kuona umuhimu mkubwa wa kuhakikisha kwamba maeneo muhimu ya ulinzi yanawekwa Kamera na kuhakikisha zinafanya kazi kwa ufanisi ili kudumisha usalama na ufuatiliaji wa kutosha.

#### 4.1.15.3 Kutokuwepo kwa mitungi ya kuzima moto (Fire Extinguisher) katika Afisi ya BLRC

Kwa mujibu wa Miongozo wa viwango kubalifu vya kimataifa vya TEHAMA inaelekeza uwepo wa ulinzi wa muda wote katika Afisi.

Ukaguzi uliweza kubaini ya kwamba afisi ya BLRC kutokuwa na Mitungi ya kuzimia moto (Fire Extinguishers), kwani uwepo wa mitungi ya kuzimia moto katika ofisi ni sehemu muhimu ya hatua za usalama za kuzuia na kudhibiti moto na pia ni njia ya haraka ya kuanza kukabiliana na moto kabla ya kuenea pamoja na kudhibiti moto kabla ya wazima moto kufika eneo la tukio.

Kutokuwepo kwa mitungi ya kuzimia moto katika vyumba vya ofisi kunaweza kusababisha hatari kwa usalama wa wafanyakazi na mali zao. Miongoni mwa hatari hizo ni kama zifuatazo: -

- Kuchelewesha Kukabiliana na Moto wakati wa dharura.
- Kuongezeka kwa Uharibifu wa Mali Bila mitungi ya kuzimia moto, moto unaweza kusambaa haraka na kusababisha uharibifu mkubwa wa mali na vifaa vya ofisi.

- Hatari kwa Usalama wa Wafanyakazi: Wafanyakazi wanaweza kuwa katika hatari kubwa wakikosa nyenzo za kuzima moto kwa haraka. Hii inaweza kusababisha majeraha na hali mbaya kwa usalama wao.
- Kupoteza Imani ya Wafanyakazi: Wafanyakazi wanaweza kupoteza imani kwa usimamizi ikiwa wanajiona hawalindwi ipasavyo dhidi ya hatari za moto.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Udhibiti wa usimamizi wa Mfumo wa Utoaji wa Leseni (BLRC) kuona umuhimu mkubwa wa kuhakikisha kwamba wanaweka mitungi ya kuzima moto, kwani mitungi ya moto ni sehemu muhimu ya mikakati ya usalama wa moto katika mazingira ya ofisi na inaweza kutoa kinga muhimu dhidi ya hatari za moto. Uwepo wa mitungi ya moto ni muhimu kwa kufuata Miongozo ya usalama wa moto na mahitaji ya kisheria yanayohitaji mazingira ya ofisi kuwa na njia za kukabiliana na moto.

Hata hivyo, ni muhimu sana kuhakikisha kuwa mitungi hii inatunzwa vizuri, kusasishwa mara kwa mara, na wafanyakazi wanapewa mafunzo ya kutosha juu ya matumizi yake. Hatua hizi zinasaidia kujenga mazingira salama ya kufanyia kazi na kuzuia athari mbaya za moto.

### 4.1.16 BARAZA LA MANISPAA YA MJINI

Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa Baraza la Manispaa ya Mjini kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 4.1.16.1 Kukosekana kwa bajeti ya TEHAMA

Sera ya TEHAMA ya Zanzibar ya mwaka 2013 sehemu ya 4.8.1.2. inaelekeza kwamba, kila taasisi ya umma itatenga fedha za kutosha kwenye bajeti zake za kila mwaka kwa ajili ya manunuzi ya TEHAMA, matengenezo ya vifaa vya TEHAMA, mifumo na mitandao kwa ajili ya mabadiliko ya haraka ya Teknolojia.

Ukaguzi ulibaini kwamba Baraza la Manispaa Mjini halikutenga bajeti ya TEHAMA kwa mwaka wa fedha 2022/2023 jambo ambalo ni kinyume na matakwa ya Sera ya Taifa ya TEHAMA na kupelekea kudhoofisha ubunifu, uvumbuzi na ukuaji wa TEHAMA ndani ya utumishi wa Umma.

Kukidumaza Kitengo hicho kiutendaji na kusababisha kutokufikia malengo yake ya kusaidia na kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya Kitengo cha TEHAMA.

Vilevile, kukosekana kwa mafunzo ya mara kwa mara kwa watumiaji wa mifumo (system users) pindipo yanapotokezea mabadiliko ya uboreshaji na uimarishaji wa mifumo.

Aidha, Baraza la Manispaa Mjini kushindwa kuwajengea uwezo wataalamu wa ndani wa kitengo cha TEHAMA ili kuweza kusimamia na kuimarisha mifumo ya taasisi kwa kupitia wataalamu wa ndani, na sio kutegemea makampuni ya nje ambayo yanaongeza hasara kwa Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Manispaa Mjini kuzingatia maelekezo yaliyowekwa kwenye Sera ya TEHAMA ya Taifa ya mwaka 2013 kwenye kutenga fedha za kutosha kupitia bajeti za kila mwaka. Aidha, tunalishauri Baraza kuweka Programu ya TEHAMA kwenye bajeti zake huku ikionesha mchanganuo wa kila kipengele (Sub Programs) ili kuongeza uwazi na uwajibikaji wa Kitengo cha TEHAMA kwa kuwezesha ufuatiliaji wa utekelezaji wa bajeti husika kwa uwazi zaidi.

### 4.1.16.2 Dosari katika Uchambuzi wa Data zilizomo katika Mfumo wa Ukusanyaji Taarifa za Mapato (MUTM)

Ili kudhibiti makusanyo ya mapato na kuhakikisha kwamba malengo/bajeti za ukusanyaji wa mapato yanaenda sambamba na mapato halisi yanayokusanywa, Serikali iliamua kuanzisha mfumo maalum wa ZanMalipo kwa ajili ya kuzalisha namba za Udhibiti (Control Number) ambazo huunganishwa na mifumo mbalimbali ya ukusanyaji wa mapato ikiwa ni pamoja na mfumo wa MUTM unaotumika Baraza la Manispaa Mjini.

Kupitia mfumo wa MUTM, afisa anaekusanya mapato kwa kutumia POS au kompyuta huingiza taarifa za makusanyo kutoka kwa mteja mmoja mmoja kwa kuzingatia chanzo cha mapato ambapo mwisho wa siku ya kazi mkusanyaji anatakiwa kuwasilisha makusanyo ya siku hiyo katika mfumo wa kielektroniki, kitendo kinachopeleke kusoma taarifa kwenye mfumo Mkuu wa kutengeneza namba za Udhibiti ambazo baada ya hapo kuletwa kwenye mfumo wa MUTM kwa ajili ya kuenda kufanya malipo benki.

Hata hivyo ukaguzi baada ya kuzifanyia uchambuzi data hizo katika mfumo wa MUTM ulibaini kuwa na dosari zifuatazo: -

### 4.1.16.3 Mfumo wa MUTM kushindwa kufikia kiwango cha ukusanyaji wa mapato ya maegesho yaliyokusanywa na kampuni ya ECONEX mwaka 2021/2022

Baada ya kutoka kwa ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Baraza la Manispaa Mjini lilichukuwa uamuzi wa kukusanya mapato yao yote kwenye mfumo wao na kuachana na kampuni ya ECONEX ambao awali walipewa jukumu la kukusanya makusanyo yote ya maegesho katika maeneo yote ya Baraza la Manispaa Mjini.

Ukaguzi ulibaini kwamba mnamo tarehe 02/09/2022 Baraza la Manispaa Mjini lilianza kukusanya mapato yake yote mwenyewe kupitia mfumo wake unaofahamika kwa jina la Mfumo wa Ukusanyaji wa Taarifa za Mapato (MUTM). Hata hivyo licha ya Baraza la Manispaa Mjini kuwa na mfumo huo lakini limeshindwa kufikia kiwango cha makusanyo ya mapato ya maegesho ambacho kilikuwa kinakusanywa na kampuni ya ECONEX, hivyo kampuni ya ECONEX ilikusanya jumla ya mapato ya maegesho shilingi 771,227,500 kuanzia mwezi wa Septemba, 2021 hadi Juni, 2022 wakati Baraza la Manispaa Mjini kupitia mfumo wa MUTM lilikusanya jumla ya mapato ya maegesho shilingi 566,902,500 kwa mwaka wa fedha 2022/2023 sawa na asilimia 73.51 ya makusanyo ya mapato ya maegesho yaliyokusanywa na kampuni ya ECONEX mwaka 2021/2022, ambapo hali hii imepelekea kusababisha kukusanya mapato pungufu ya kiasi cha shilingi 204,325,000.

Kutofikia kiwango cha makusanyo ya mapato kinachotarajiwa kunaweza kusababisha athari mbalimbali kwa Baraza, miongoni mwa athari hizo ni pamoja na upungufu wa mapato na kupelekea kuzorota kwa kazi za Baraza kwa kushindwa kufanya kazi kwa ufanisi, pia unaweza kusababisha uhaba wa rasilimali za kutekeleza sera na mipango, na hivyo kupunguza ufanisi wa utawala.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Manispaa Mjini kufanya tathmini ya maeneo ya maegesho ili kutambua athari za maeneo yasiyotozwa na kufanya maamuzi sahihi kwa maslahi mapana ya Serikali, kuyaainisha maeneo yote kwenye mfumo pamoja na kuweka mipango iliyo imara na inayotekelezeka katika kufikia malengo ya makusanyo ya maegesho ya kila mwezi.

Ni muhimu kwa uongozi wa Baraza la Manispaa Mjini kutekeleza mikakati ya makusanyo ya mapato kwa ufanisi ili kuepuka dosari hizo. Hii inaweza kujumuisha maboresho katika mifumo na kuimarisha uwezo wa kukusanya mapato. Mchanganuo wa tofauti ya mapato hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 41: Tofauti ya Mapato yaliyokusanywa baina ya ECONEX na MUTM kwa mwaka wa fedha 2022/2023

| Mwezi wa makusanyo | Mapato Halisi Yaliyokusanywa Na Econex 2021/2022 (Tsh) | Mapato Halisi Yaliyokusanywa na Mfumo wa MUTM 2022/2023 (Tsh) | Tofauti ya Mapato (Tsh) | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|
| Septemba | 95,891,500 | 54,835,500 | 41,056,000 | 57.2 |
| Oktoba | 102,305,000 | 68,384,000 | 33,921,000 | 66.8 |
| Novemba | 101,334,000 | 58,828,500 | 42,505,500 | 58.1 |
| Disemba | 106,008,000 | 63,256,500 | 42,751,500 | 59.7 |
| Januari | 70,100,000 | 53,916,000 | 16,184,000 | 76.9 |
| Febuari | 62,288,000 | 55,621,000 | 6,667,000 | 89.3 |
| Machi | 67,301,000 | 57,482,000 | 9,819,000 | 85.4 |
| Aprili | 50,000,000 | 50,622,000 | -622,000 | 101.2 |
| Mei | 55,000,000 | 58,397,500 | -3,397,500 | 106.2 |
| Juni | 61,000,000 | 45,559,500 | 15,440,500 | 74.7 |
| **Jumla Kuu** | **771,227,500** | **566,902,500** | **204,325,000** | 73.51 |

### 4.1.16.4 Kutokukamilika kwa taarifa muhimu za miamala iliyotengenezewa nambari za Ankara

Ukaguzi ulibaini kuwa katika miamala ya nambari za Ankara ambayo inatengenezwa na Maafisa wa Baraza la Manispaa Mjini inakosa taarifa muhimu za kukamilika kwa miamala hiyo, na hatimae miamala hiyo inatengenezwa bila ya kuwa na taarifa muhimu kama vile jina la mlipaji pamoja na kiwango cha fedha anachotakiwa kulipa.

Kukosekana kwa taarifa muhimu katika miamala iliyotengenezewa nambari za ankara kunapelekea kuwepo kwa mwanya wa udanganyifu na wizi katika ukusanyaji wa mapato, kutoa taarifa zisizokuwa na usahihi kwa watumiaji, uwepo wa ugumu wa kufunga mahesabu ya siku, mwezi na mwaka ya taasisi, upotevu wa pesa za makusanyo ya mapato na kupelekea hasara kwa Serikali. Aidha, kukosekana kwa taarifa hizo muhimu katika miamala tofauti inapunguza imani ya utumiaji wa mfumo wa MUTM kwa wakusanyaji wa mapato.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Manispaa Mjini kuchukua hatua za haraka kuweza kuhakikisha wanashirikiana kwa pamoja na Wizara ili kuondoa tatizo hili, kwani linaathiri mchakato mzima wa ukusanyaji wa mapato katika Baraza na kupelekea kutoa taarifa zisizokuwa sahihi.

Orodha ya miamala iliyotengenezewa nambari za Ankara ambayo haijakamilika taarifa zake katika Baraza la Manispaa Mjini ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 42: Miamala iliyofanyika kwa kupitia Ankara zenye mapungufu**

| Nam | Ankara Namba | Tarehe | Mlipaji | Malipo | Mkusanyaji | Hali |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | 200270028404 | 09-09-22 | Hadiya Ali Haji | - | Hadiya Ali Haji | Pending |
| 2. | 200270028760 | 13-09-22 | - | 30,000 | Awezae Said Abdalla | Paid |
| 3. | 200270047682 | 18-01-23 | - | 30,000 | Awezae Said Abdalla | Created |
| 4. | 200270047977 | 19-01-23 | - | 30,000 | Awezae Said Abdalla | Created |
| 5. | 200270048237 | 20-01-23 | - | 30,000 | Awezae Said Abdalla | Created |

### 4.1.16.5 Uwepo wa idadi kubwa ya miamala ya nambari za udhibiti ambayo imepitiwa na muda wa matumizi (expired)

Nambari za udhibiti zinapotengenezwa na kukaa kwa muda mrefu (kulingana na muda wa kuisha matumizi) zinakuwa hazifanyi kazi tena kwa miamala hiyo baada ya kupitiwa na muda wa matumizi (expired), hivyo basi Baraza la Manispaa Mjini linakuwa na ukomo wa nambari za udhibiti mara tu zinapotengenezwa ambazo hukaa kwa mwezi mmoja tu na baada ya hapo haitumiki tena kwa ajili ya malipo na kupelekea kutengenezwa kwa nambari nyengine.

Ukaguzi ulibaini uwepo wa miamala mingi iliyotengenezewa nambari za udhibiti ambazo zimepitiwa na muda wa matumizi (expired), ukaguzi ulibaini uwepo wa idadi kubwa wa nambari za Ankara zilizopitiwa na muda wa matumizi katika Baraza la Manispaa Mjini ambazo ni 3,743 zenye thamani ya shilingi 1,838,936,212. Hali hii inaonesha kuwa nambari hizi zinachelewa kufanyiwa malipo kwa wakati au kutokufanyiwa malipo kabisa.

Uwepo wa idadi kubwa wa nambari za Ankara ambazo zimepitwa na muda wa matumizi kunapelekea kujitokeza kwa dosari kubwa katika ulipaji kwani miamala hiyo huchelewa kulipwa kwa wakati au kutokulipwa kabisa hali ambayo inakosesha mapato kwa Baraza la Manispaa Mjini na kusababisha kukusanya mapato pungufu ya matarajio yaliyowekwa na kupelekea kuzorota kwa kazi za Baraza.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Manispaa Mjini kuhakikisha wanapunguza uwepo wa nambari za Ankara ambazo zimepitwa na muda wa matumizi kwa kuwapa na kutoa elimu kwa walipaji ili kuwahamasisha kuweza kulipa kwa wakati. Aidha, ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Manispaa kutoa huduma zilizo bora kwa wateja wake ili kulipia huduma zao kwa wakati na kuweza kukusanya mapato kwa wingi na kwa wakati kulingana na matarajio ya Baraza.

#### 4.1.16.6 Uwepo wa muamala mmoja kujirejea mara nyingi zaidi wenye nambari ya udhibiti inayosomeka "0" na kukaa "Pending"

Katika kufanya uchambuzi wa data tulizozipokea kutoka kwa Baraza la Manispaa ya Mjini, ukaguzi ulibaini uwepo wa muamala mmoja ambao unajirejea mara nyingi zaidi wenye nambari ya udhibiti inayosomeka zero "**0**" ambayo si miongoni mwa mfumo wa nambari za udhibiti wa Baraza la Manispaa Mjini.

Wakati tunaendelea na uchambuzi wa data hizo, ukaguzi ulibaini ya kuwa muamala huo mmoja umejirejea mara **787** kwa thamani ya shilingi **472,200,000** ambapo miamala yote hiyo imekaa katika hali ya "Pending".

Hali hiyo inaweza kusababisha hatari kubwa ya kupotea kwa mapato na kusababisha mfumo kupungua ufanisi na weledi wa kazi kwani watumiaji wa mfumo huweza kupoteza imani na mfumo kutokana na kutoa taarifa zisizo sahihi hali itakayopelekea kuisababishia Serikali hasara, pamoja na kupoteza fursa kwa wawekezaji na wadhamini tofauti kuja kusaidia katika taasisi hio.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Manispaa Mjini kuweza kuchukua juhudi za makusudi kuweza kuwasiliana na kushirikiana na Wizara ili kulipatia ufumbuzi tatizo hili kwa ajii ya kunusuru kutoa taarifa zisizokuwa na usahihi kwa watumiaji pamoja na kuathiri utendaji mzima wa Baraza la Manispaa Mjini. Ukaguzi pia unashuri uongozi wa Baraza kuhakikisha unafanya majaribio ya mifumo yao kabla ya kuanza kutumika ili kupunguza na kuondoa matatizo kama haya ambayo yana athari kubwa katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

#### 4.1.16.7 Uwepo wa idadi kubwa ya miamala ya nambari za udhibiti ambayo hali yake inasomeka "created"

Utengenezaji wa nambari za udhibiti katika mifumo kupitia taasisi mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kawaida inakuwa na hali (status) ya "Paid", "Expired", "Pending" pamoja na "Cancel". Lakini katika hali isiyo ya kawaida ukaguzi ulibaini uwepo wa miamala ya nambari ya udhibiti ambayo hali yake (status) inasomeka "Created" mpaka leo, ambapo jumla ya miamala ipatayo **7,922** yenye thamani ya shilingi **6,782,231,924** ilibainika kuwa na hali hiyo.

Uwepo wa idadi kubwa ya miamala yenye hali hiyo unatia shaka juu ya usahihi wa taarifa za makusanyo na mapato yanayokusanywa na Baraza la Manispaa ya Mjini jambo ambalo linaweza kusababisha hasara kwa Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Manispaa Mjini kuchukua juhudi za makusudi za kuwasiliana na kushirikiana na Wizara ili kuweza kulipatia suluhisho tatizo hili kwa ajii ya kunusuru kutoa taarifa zisizokuwa na usahihi kwa watumiaji kwani kufanya hivyo ni kusaidia Serikali juu ya juhudi zinazochukuliwa za kuimiarisha mifumo ya kifedha ya ukusanyaji wa mapato ili kupunguza na kuondoa tatizo la wizi wa fedha za wananchi, na kupelekea kuongezeka kwa miradi ya maendeleo inayokwenda kwa kasi katika uongozi uliopo madarakani.

#### 4.1.16.8 Uwepo wa utofauti wa makusanyo ya mapato yaliyotumia "Control number" kulinganisha na mapato ya ripoti ya benki

Ukaguzi ulibaini kuwa kuna baadhi ya mapato yameingia benki bila ya kutumia "control number" kupitia akaunti ya Baraza la Manispaa Mjini iliyopo katika benki ya PBZ yenye nambari **0404007000**. Hivyo basi kwa mujibu wa data tulizopewa za nambari ya udhibiti kutoka Baraza la Manispaa Mjini kwa mwaka wa fedha 2022/2023 tulibaini jumla ya mapato yote yaliyofanyika kwa kutumia nambari ya udhibiti katika mfumo wa MUTM ni kiasi cha shilingi **3,542,991,128.00** ambayo ni tofauti na mapato yalioingia katika benki ya kiasi cha shilingi **3,738,771,962.45** na kupelekea upungufu wa kiasi cha shilingi **195,780,834.45.**

Kukusanya mapato bila ya kutumia "control number" kunaweza kusababisha dosari mbali mbali, miongoni mwa dosari hizo ni kama zifuatazo:-

- Kupoteza ufuatiliaji: "Control number" husaidia Baraza kufuatilia malipo yanayohusiana na huduma au bidhaa fulani. Kukosa kutumia "control number" kunaweza kufanya iwe vigumu kufuatilia mapato yako au kubaini malipo yanayofanyika.
- Kuchelewesha uhakiki: Kama hakuna "control number" taratibu za uhakiki wa malipo zinaweza kuwa ngumu, ambapo inaweza kusababisha kucheleweshwa kwa huduma au bidhaa unayoilipia.
- Hatari ya kupotea kwa malipo: Kuna hatari kubwa ya kupotea kwa malipo, kama kuna hitilafu au kutoelewana itakuwa vigumu kuthibitisha malipo yako.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Manispaa Mjini kuweza kutumia nambari ya udhibiti kwa mapato yote yanayokusanywa kupitia akaunti husika ili kuweza kudhibiti mapato hayo pamoja na kuweza kurahisisha kazi ya kufunga mahesabu kwa wakati na kuweza kupata taarifa zilizo sahihi na zenye uhakika.

### 4.1.16.9 Kukosekana kwa mfumo wa kiautomatiki wa kuzima moto (fire suppression system) katika chumba cha Seva kilichopo Baraza la Manispaa Mjini

Miongoni mwa muongozo wa viwango kubalifu vya kimataifa vya TEHAMA wa ISO 9001 (Fifth edition 15/9/2015) katika kifungu nambari 5.15 inasisitiza uhitaji wa udhibiti wa taarifa, ili kulinda vifaa na mifumo ya TEHAMA inayohifadhiwa katika chumba hicho kwa masaa 24, mifumo na vifaa hivyo hugharimu fedha nyingi na kupelekea ulazima wa ulinzi dhidi ya moto ili kuhakikisha usiri, uadilifu na upatikanaji wa taarifa zinazohifadhiwa katika chumba cha Seva muda wote.

Kukosekana kwa mfumo wa kuzima moto katika chumba cha Seva kunaweza kuwa na dosari kubwa na hatari kwa vifaa vyote na data ndani ya chumba hicho. Miongoni mwa dosari hizo ni pamoja na:-

- Ongezeko la joto: Ongezeko la joto linaweza kusababisha vifaa vya kompyuta kufanya kazi vibaya au hata kuharibika kabisa.
- Kupoteza huduma: Kukosekana kwa mfumo wa kuzima moto kunaweza kusababisha kukatika kwa huduma zilizopo kwenye Seva hizo, hii inaweza kuathiri shughuli za biashara na huduma za mtandao.

- Gharama kubwa za kurekebisha: Kurejesha chumba cha Seva baada ya moto kunaweza kugharimu sana, hii ni pamoja na gharama za kurejesha vifaa, kuanzisha upya miundombinu, na gharama za kupoteza biashara au huduma.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Manispaa Mjini kuweza kutumia mfumo wa kuzima moto (fire suppression system) katika chumba cha Seva ili kuweza kulinda vifaa na mifumo ya TEHAMA inayohifadhiwa.

Kwa kuzingatia athari hizi, ni muhimu kuhakikisha kuwa mfumo wa kuzima moto ni sehemu muhimu ya hatua za usalama katika mazingira ya chumba cha seva. Mifumo ya kuzima moto kawaida hujumuisha matumizi ya vifaa vya kuzima moto, detectors za moto, na mifumo ya kuondoa moshi kwa haraka. Pia, mipango ya dharura na mafunzo ya wafanyakazi juu ya hatua za kuchukua wakati wa dharura ni muhimu.

### 4.1.16.10 Mapitio ya Kamera zilizopo Baraza la Manispaa Mjini

Kwa mujibu wa muongozo wa eGAZ wa mwaka 2022 katika kifungu cha 4.3.2 unaelekeza taasisi kutekeleza usalama wa TEHAMA kwa kuweka usalama katika taasisi kwa kufuata miongozo ya Wakala wa Serikali Mtandao Serikalini. Kwa upande wa CCTV kamera katika jengo la Baraza la Manispaa Mjini, ukaguzi ulibaini kati ya kamera (14) zilizofungwa, kamera (12) zinaonesha na kamera (2) hazioneshi kutokana na changamoto mbali mbali.

Hata hivyo imebainika kuwa kuna kamera ambayo haijafungwa ipo katika chumba cha TEHAMA ambapo awali ilikuwepo lakini iliibiwa na kupatikana ingawaje mpaka hivi sasa haijarejeshwa sehemu husika. Jadweli lifuatalo linaonesha mchanganyo wa idadi ya kamera zilizofungwa na hali halisi ya utendaji kazi: -

## Jadweli Nambari 43: Idadi ya kamera zilizofungwa katika Baraza la Manispaa Mjini

| Eneo Husika | Idadi ya Kamera zilizofungwa | Idadi ya kamera zinazofanya kazi | Idadi ya kamera zisizofanya kazi |
|---|---|---|---|
| Jengo la Mkurugenzi (Ground Floor) | 3 | 3 | 0 |
| Jengo la Mkurugenzi (1st Floor) | 7 | 6 | 1 |
| Jengo la Mahakama (Ground Floor) | 0 | 0 | 0 |
| Jengo la Mahakama (1st Floor) | 3 | 3 | 0 |
| Jengo la Mapato (Ground Floor) | 1 | 0 | 1 |
| Jengo la Mapato (1st Floor) | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla ya Kamera** | **14** | **12** | **2** |

Kwa mujibu wa jadweli hapo juu linaonesha kwamba idadi ya kamera zinazofanya kazi ni kidogo kulinganisha na ukubwa wa jengo ambapo baadhi ya sehemu muhimu kama jengo la Mapato halijafungwa kamera.

Vile vile ukaguzi ulibaini ufungaji wa kamera haukuzingatia vipaombele vya usalama wa maeneo waliopo Viongozi Wakuu wa Afisi katika jengo hilo, kwa mfano afisi za Utoaji wa nambari za udhibiti (Control Number), ofisi za leseni, ofisi za maegesho na sehemu nyengine muhimu, lakini hakuna kamera iliyofungwa kwenye maeneo hayo kwa ajili ya kuangalia usalama wao endapo tatizo lolote likitokea zidi yao.

Kutofanya kazi kwa kamera za Afisi kunaweza kusababisha kukosekana kwa ushahidi endapo tukio lolote la wizi, uhalifu au uharibifu likitokea katika Afisi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Manispaa Mjini kuimarisha dosari zote zilizotajwa hapo juu zinazohusu CCTV kamera na ili kuongeza usalama, ulinzi na utendaji kazi wa vifaa vilivyomo katika Baraza.

Aidha, ukaguzi unaushauri uongozi wa Afisi kufanya jitihada za makusudi za kutengeneza CCTV kamera ambazo hazifanyi kazi na ambazo bado hazijafungwa, na vile vile kuongeza idadi ya ufungaji wa kamera katika maeneo yote muhimu.

### 4.1.17 SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA ZANZIBAR (ZSTC)

Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC) kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 4.1.17.1 Mitungi ya kuzima moto iliyopitwa na wakati (Expired Fire Extinguisher)

Kwa mujibu wa kifungu nambari 85 cha Sheria nambari 8 ya Afya na Usalama Kazini ya mwaka 2005 kinachoelekeza kwamba katika maeneo yote ya kazi patakuwepo na nyenzo za kuzimia moto za kutosha zinazofaa ambazo zitawekwa katika maeneo yanayofikia/ kupatikana kirahisi (readly accessible) kwa kuzingatia mazingira husika na zitakuwa zinafanyiwa maboresho (maintained).

Ukaguzi ulibaini kwamba baadhi ya Mitungi ya kuzimia moto (Fire Extinguishers) iliyowekwa katika maeneo mbali mbali ya Afisi za ZSTC Unguja na Pemba imemaliza muda wake wa matumizi kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 44: Hali ya kupita muda wa matumizi wa mitungi ya kuzimia moto katika afisi mbali mbali za ZSTC Unguja na Pemba**

| ZSTC Office | Date of Service of Fire Extinguisher | Date of Next Service of Fire Extinguisher | Period without Valid Fire Extinguisher |
|---|---|---|---|
| ZSTC HQ | Jan. 2019 | Dec. 2019 | 4 Years |
| Wete | Mar. 2019 | Feb. 2020 | 3.7 Years |
| Mkoani | Mar. 2019 | Feb. 2020 | 3.7 Years |
| Makonyo (Kiwandani) | Jul. 2022 | Jun. 2023 | 3 Months |

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZSTC kufanya tathmini ya hali halisi ya nyenzo za kuzimia moto ikijumuisha mifumo ya kugundua na kuzima moto (fire detectors and extinguishing system), mitungi ya kuzima moto katika maeneo mbali mbali ya afisi za ZSTC Unguja na Pemba ili kubaini ukubwa wa tatizo na kuweka mipango thabiti itakayotekelezwa na Taasisi ili kuhakikisha kwamba mapungufu yote yaliyoibuliwa na ukaguzi huu pamoja na hayo yatakayobainika katika tathmini yanafanyiwa kazi kwa wakati ili kulinda rasilimali za Serikali pamoja na kuimarisha usalama wa watumishi.

### 4.1.17.2 Kutofanyika kwa tathmini ya mahitaji ya mafunzo na mpango wa mafunzo ya TEHAMA kwa watumishi

Mipango ya TEHAMA kwenye taasisi ni mpango ambao unajumuisha mafunzo ya TEHAMA kwa watumishi walioainishwa na Taasisi husika.

Ukaguzi ulibaini kwamba Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC) kutokufanya tathmini ya mahitaji ya mafunzo ya TEHAMA na kutoandaa mpango wa mafunzo hayo kwa watumishi jambo ambalo ni kwenda kinyume na kifungu namba 4.2.1.2 (c) cha Sera ya Taifa ya Mtandao ya mwaka 2012 ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar kuhakikisha wanafanya tathmini ya mahitaji ya mafunzo na ujuzi na kuandaa mpango wa mafunzo utakaotekelezwa kila mwaka kwa uharaka unaostahili na kuona kwamba tija na ufanisi vinaongezeka mwaka hadi mwaka.

### 4.1.17.3 Kutokuwepo kwa utekelezaji wa bajeti kwa upande wa Kitengo cha TEHAMA kutokana na kutoingiziwa fedha

Sera ya TEHAMA ya Zanzibar ya mwaka 2012 kifungu nambari 4.8 imezielekeza taasisi juu ya utekelezaji wa ufanisi wa Serikali ya kielektroniki unategemea fedha za kutosha kutoka katika bajeti ya Taifa au msaada wa wafadhili, ambapo kila taasisi ya umma itatenga fedha za kutosha kwenye bajeti zake za kila mwaka kwa ajili ya manunuzi ya TEHAMA, matengenezo ya vifaa vya TEHAMA, mifumo na mitandao kwa ajili ya mabadiliko ya haraka ya Teknolojia.

Bajeti ni mchakato wa kuweka mipango ya mapato na matumizi ambayo kwa ujumla inachangia kupatikana kwa tija kwenye usimamizi wa matumizi ya fedha za umma, katika kitengo cha TEHAMA bajeti inasaidia mgawanyo sahihi wa rasilimali fedha kwenye kitengo, kurahisisha upimaji wa ufanisi wa kitengo, kuwezesha ufuatiliaji (monitoring) wa utendaji kazi wa kitengo, kusaidia uwekaji wa malengo, kuboresha ufanyaji wa maamuzi na kuongeza hamasa kwa wafanyakazi.

Ukaguzi ulibaini kwamba Kitengo cha TEHAMA kilitenga takribani shilingi 270,000,000 kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021, pia kilitenga takribani shilingi 319,710,000 kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022, vilevile Kitengo cha TEHAMA kilitenga takribani shilingi 228,759,000 kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023, Dosari iliyobainika na Ukaguzi ni kuwa katika miaka yote mitatu ya fedha licha ya Kitengo cha TEHAMA kuwasilisha bajeti yake hiyo lakini mpaka kufikia Juni, 2023 kitengo hiki hakijawahi kuingiziwa fedha yoyote ya bajeti.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar kuzingatia maelekezo yaliyowekwa kwenye Sera ya TEHAMA ya Taifa ya mwaka 2013 kwenye kutenga fedha za kutosha kupitia bajeti za kila mwaka.

Aidha, Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika kuwaingizia fedha Kitengo cha TEHAMA kwenye bajeti yake huku ikionesha mchanganuo wa Pemba na Unguja (Sub Programs) ili kuongeza uwazi na uwajibikaji wa Kitengo cha TEHAMA kwa kuwezesha ufuatiliaji wa utekelezaji wa bajeti husika kirahisi ukilinganisha na hali ilivyo kwa sasa.

Hata hivyo, tunashauri uongozi wa ZSTC kuifanya TEHAMA kuwa miongoni mwa vipaumbele vyake katika Taasisi kwa kuweka mipango na mikakati ya TEHAMA itayowezesha taaisisi kufikia malengo yake ya kuongeza uwazi, uwajibikaji, ufanisi na upatikaji wa tija inayotarajiwa na Serikali ya awamu ya nane kupitia TEHAMA.

#### 4.1.17.4 Mapitio ya Mfumo wa Rasilimali Watu (Human Resource Management Information System)

Ukaguzi ulifanya mapitio ya Mifumo ya ZSTC kwa kuangalia udhibiti wa taarifa uliopo ndani na nje ya mifumo hiyo. Baadhi ya mifumo mikuu iliyopitiwa kwa mwaka wa fedha 2022-2023 ni pamoja na Mfumo wa Rasilimali Watu (Human Resource Management Information System), Mfumo wa Financial Information Management System (FIMS), Mfumo wa Statistical Data Management Information System (SDMIS), mfumo wa ZANMALIPO, mfumo wa TIGOPESA na Tovuti ya Afisi.

Katika ukaguzi uliofanyika wa mfumo wa HR-Management Information System imebainika kwamba mfumo bado una mapungufu mengi katika utendaji kazi wake ambapo mapungufu hayo yasipofanyiwa kazi yanaweza kuathiri ufanisi wa mfumo na kusababisha kukosekana kwa tija iliyokusudiwa. Baadhi ya mapungufu yaliyobainika ni kama ifuatavyo: -

- **Kukosekana kwa muunganiko baina ya Human Resource Management Information System na Biometric Attendance System**

Kwa mujibu wa muongozo wa viwango kubalifu vya kimataifa vya TEHAMA unazitaka taasisi zote kuweza kuweka muunganiko wa mifumo ambayo inahitajika kuonana ili kuweza kurahisisha kazi katika taasisi.

Ukaguzi ulibaini kutokuwepo kwa muunganiko baina ya Mfumo huo wa HRMIS na Mfumo wa Mahudhurio wa Alama za Vidole (Biometric Attendance System) ambao ZSTC hutumia kwa ajili ya kusimamia mahudhurio ya watumishi wao. Muunganiko wa mifumo hiyo ungeweza kusaidia na kurahisisha kazi za Utumishi kama vile upatikanaji wa taarifa sahihi za mahudhurio ya wafanyakazi, kutokana na kujulikana kwa hesabu ya siku za mahudhurio na muda wa mahudhurio ya kazini.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZSTC kuunganisha mifumo hiyo (Human Resource Management Information System na Biometric Attendance System) ili kuweza kupatikana ufanisi, tija na kurahisisha kazi za Afisa Utumishi katika Taasisi.

- **Matumizi hafifu ya Mfumo wa HRMIS**

Ukaguzi ulibaini kuwa katika mfumo wa Human Resource Management Information System, kuna moduli 1 ambayo haijawahi kutumiwa tokea mfumo huo uanze kufanya kazi mwaka 2017 mpaka tunakamilisha ukaguzi huu. Hii ni sawa na asilimia 12 ya Moduli zote za mfano wa HRMIS, Moduli ilizobainika kuwa haijawahi kutumiwa ni moduli ya ***"Training and Operator Performance."***

Moduli ya "Training and Operator Performance" ilitakiwa kutumika kwa ajili ya kuratibu maswala ya mafunzo na upatikani wa ripoti mbali mbali kufuatilia utendaji kazi kwa lengo la kuongeza tija na ufanisi kwenye Taasisi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC) kuhakikisha unasimamia kwa karibu matumizi ya mfumo wa HRMIS ili kuhakikisha kwamba Moduli zote zilizonunuliwa kwa fedha za Umma zinatumika kama ilivyokusudiwa ili kusaidia kuongeza tija na ufanisi.

- **Mfumo kutokuwa na uwezo wa kuthibitisha usahihi wa data (data validation)**

Miongoni mwa muongozo wa viwango kubalifu vya kimataifa vya TEHAMA wa ISO 9001 (Fifth edition 15/9/2015) katika kifungu nambari 8.3.4 (d) inazitaka taasisi kuipitia mifumo yote baada ya kukamilika kwa kuifanyia majaribio kwa kila moduli ili kugundua mapungufu ya moduli hizo.

Ukaguzi ulibaini kuwa mfumo hauwezi kutambua wala kubaini usahihi wa taarifa kwa ulinganisho wa tarehe ya kuzaliwa na tarehe ya kuajiriwa kwa mfanyakazi, kwa mfano tunapoziingiza taarifa za mfanyakazi ambaye amezaliwa tarehe 01/01/2000 na pia tukaingiza tarehe ya kuajiriwa 01/01/2002, basi mfumo itampokea mfanyakazi huyo aliyeajiriwa akiwa na umri wa miaka miwili (2) na kuweza kumpatia stahiki zake zote za mshahara ingawaje kaajiriwa lakini akiwa chini ya umri wa miaka 18. Aidha, mfumo unashindwa kutambua muundo maalum wa nambari ya utambulisho wa Zan Id, NIDA pamoja na passport na kupelekea kuingizwa tarakimu zisizo halali zilizozidi muundo wa vitambulisho husika kwa mfano Muundo wa Zan Id unapokea tarakimu tisa (9) lakini mfumo unaruhusu kupokea zaidi ya tarakimu hizo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar kuupitia mfumo kwa kuufanyia majaribio na maboresho katika maeneo mbali mbali kulingana na miongozo ya kitaifa na kimataifa na kuhakikisha kwamba unakidhi vigezo vilivyowekwa vya utendaji, usalama, usiri na upatikanaji.

### 4.1.17.5 Mapitio ya Mfumo wa Financial Information Management System (FIMS)

Katika ukaguzi ilibainika kwamba ZSTC ina Mfumo unaojulikana kwa jina la Financial Management Information System, ambao umeanzishwa na Shirika la ZSTC kwa lengo la kuimarisha utendaji katika idara ya Uhasibu, kuingiza na kuhifadhi taarifa za kifedha za Shirika na kutoa ripoti za uhasibu na fedha. Aidha, Mfumo huo umetengenezwa na Kampuni ya Dobea Group LTD kupitia makubaliano baina yake na Shirika la Biashara la Taifa Zanzibari (ZSTC) mnamo tarehe 15 Machi, 2019 kwa gharama ya TZS 6,000,000. Hata hivyo, ukaguzi ulifanya mapitio ya mfumo kwa lengo la kuangalia ukamilifu wa mfumo pamoja na usahihi wa taarifa mbali mbali zilizomo na utendaji kazi wa mfumo ambapo zilibainika dosari mbali mbali kama inavyofafanuliwa hapo chini;

- **Kutotumiwa kwa baadhi ya moduli zilizomo katika mfumo**

Ukaguzi ulibaini kuwa katika mfumo wa Financial Management Information System kuna baadhi ya moduli ambazo hazijawahi kutumiwa tokea mfumo huo uanze kufanya kazi mpaka ukaguzi unakamilika. Mfano wa moduli zilizobainika kuwa hazijawahi kutumiwa ni pamoja na moduli ya kuingiza makadirio ya mapato ***(Revenue Budget).***

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC) kuyafanyia kazi mapungufu hayo.

- **Mfumo kutokuwa na uwezo wa kuthibitisha usahihi wa makadirio ya fedha (validation) pamoja na udhibiti wa kibajeti (budget control)**

Ukaguzi ulibaini kuwa mfumo hauwezi kutambua/kubaini usahihi wa makadirio ya fedha na udhibiti wa kibajeti, kwa mfano mfumo unaweza kuruhusu kufanya matumizi ya fedha yaliyozidi makadirio yaliyowekwa (over budget expenditure) bila ya kutoa taarifa yoyote itakayokujulisha kuwa umezidi kiwango cha bajeti iliyoidhinishwa, au umezidi kiwango cha fedha zilizopo katika akaunti ya benki na kukuzuiya kuendelea katika hatua nyengine."

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC) kuyafanyia kazi mapungufu hayo.

- **Mfumo kutokuwa na uwezo wa kutoa ripoti za makadirio ya mapato (Revenue Budget reports)**

Kwa mujibu wa "Term of Reference (TOR)" ya mfumo wa Financial Management Information System wa Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar katika PART F (a) ambapo inautaka mfumo uweze kutoa ripoti ya makadirio ya mapato "Able to produce Budget statements".

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC) kuyafanyia kazi mapungufu hayo.

- **Mfumo kutokuwa na uwezo wa kutoa ripoti ya "Goods Received Notes" (GRN)**

Miongoni mwa muongozo ya viwango kubalifu vya kimataifa ya Uhasibu ni pamoja na kuwa na hati ya kuthibitisha kupokea bidhaa au vifaa kutoka kwa mteja. "Goods Received Notes", ni hati inayothibitisha kupokea kwa bidhaa au vifaa na inaweza kuwa sehemu muhimu ya usimamizi wa hesabu na udhibiti wa manunuzi, hivyo basi ukaguzi ulibaini kuwa mfumo hauna uwezo wa kutoa ripoti inayothibitisha kupokelewa kwa bidhaa (Goods Received Note).

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC) kuyafanyia kazi mapungufu hayo.

- **Kutoshirikishwa kwa kitengo cha TEHAMA katika mchakato wa utengenezaji wa mifumo**

Kwa mujibu wa "Terms of Reference (TOR)" ya mfumo wa Financial Management Information System wa Shirika la ZSTC, PART D (Activities and Expected Output) kipengele cha "Testing and Evaluation" pamoja na "Training and Documentation" imekitaka kitengo cha TEHAMA kushirikishwa kikamilifu katika utengenezwaji wa mfumo.

Ukaguzi ulibaini kuwa kitengo cha TEHAMA hakikushirikishwa kikamilifu katika utengenezwaji wa mfumo huo. Kutoshirikishwa kwa kitengo cha TEHAMA wakati wa utengenezaji na matumizi ya mfumo wa fedha, kunapelekea kusababisha matatizo kadhaa na changamoto katika biashara au Shirika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC) kuandaa mpango kazi na kuwajengea uwezo wataalamu wa TEHAMA katika maeneo ya "Technical" ya mfumo ili kuwawezesha kufanya usimamizi wa mfumo huu. Vile vile kuhakikisha kwamba nyaraka zote muhimu za mfumo huu zinaandaliwa na zinapatikana katika Taasisi ili kuwezesha matumizi endelevu ya mfumo huu. Pamoja na kushirikisha ipasavyo na kujengewa uwezo wataalamu wa TEHAMA ili kuweza kusimamia mifumo husika kwa namna ambayo ni endelevu na kwa gharama nafuu.

- **Mfumo kutoa taarifa zisizo na usahihi kwa baadhi ya moduli wakati unapohitaji kuchuja (search) taarifa hizo**

Kwa mujibu wa "Term of Reference (TOR)" ya mfumo wa Financial Management Information System wa Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar katika PART TWO (3) ambapo inautaka mfumo uwe na uwezo wa upatikanaji wa taarifa zilizo sahihi.

Ukaguzi ulibaini kuwa mfumo hautoi majibu ya usahihi kulingana na taarifa inayohitajika katika moduli, kwa mfano katika kutoa ripoti ya fedha ya mapato sehemu ya "Period" inayotakiwa ilete kipindi cha miezi inaleta taarifa za kiwango cha fedha (amount) badala ya period.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC) kuyafanyia kazi mapungufu hayo.

- **Kukosekana kwa uthibitishaji na uidhinishaji wa taarifa za mapato na matumizi zinazoingizwa kwenye Mfumo**

Ukaguzi ulibaini kuwa mfumo wa Financial Management Information System hauna uwezo wa kuthibitisha taarifa za kifedha zinazoingizwa ndani ya mfumo. Uthibitishaji wa taarifa ndani ya mfumo ni muhimu sana hasa kwa mfumo wa fedha kama huu, kwani taarifa za kifedha zinazothibitishwa zinakuwa zipo salama ambapo kunaweza kuzuia upatikanaji usio sahihi kwa kuzuia watu wasiohitajika kuingiza taarifa au kupata rasilimali za mfumo, kuongeza ubora wa data kwa kuhakikisha kuwa taarifa zinaingizwa kwa usahihi na kwa mujibu wa viwango vilivyowekwa hii inaweza kuzuia makossa na kuboresha usahihi wa data, kuaminika kwa taarifa kwa watumiaji na wadau kwa kuwa na uhakika kwamba taarifa zinazoonekana zimepitia mchakato wa kuthibitisha na ni za kuaminika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC) kuyafanyia kazi mapungufu hayo.

- **Mfumo kutokufanya Kodi ya Ongezeko la Thamani ya (VAT) pamoja na fedha taslimu zilizotolewa kwa matumizi ya muda mfupi (Imprest)**

Ukaguzi ulibaini kuwa  mfumo wa Financial Management Information System wa ZSTC haujumushi hesabu za uzuiaji wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) pamoja na Fedha taslimu zilizotolewa kwa matumizi ya muda mfupi (Imprest) jambo ambalo hupelekea hesabu ya Kodi za Ongezeko la thamani kufanywa nje ya mfumo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar kuweza kuufanyia marekebisho mfumo ili uweze kufanya Kodi ya Ongezeko la Thamani.

### 4.1.17.6 Mapitio ya mfumo wa Statistical Data Management Information System (SDMIS)

Mfumo wa SDMIS ni mfumo ambao umeanzishwa na Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar mwaka 2018. Mfumo huu umetengenezwa kupitia mkataba wa tarehe 05 Juni, 2018 wenye thamani ya kiasi cha shilingi **30,500,000** uliofungwa baina ya JK IT Consultancy pamoja na Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar.

Lengo la kuanzishwa kwa mfumo wa SDMIS ni kuweka kumbukumbu mbali mbali zinazohusiana na taarifa za biashara, aina za huduma wanazotoa pamoja na taarifa nyingine zinazohusiana na Shirika, vile vile una lengo la kuliwezesha Shirika kufuatilia na kupata taarifa wakati wanapozihitaji.

Ukaguzi ulipitia kipengele kimoja badala ya chengine katika mfumo huo na kuweza kubaini mapungufu mbali mbali kama yafuatayo:--

- **Kasi ndogo ya uingizaji wa taarifa ndani ya mfumo wa Statistical Data Management Information System**

Baada ya kupitia mfumo wa uwekaji wa kumbukumbu za taarifa za Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC) ukaguzi ulibaini mfumo huo umejumuisha moduli tofauti zenye kujitegemea ambazo zinafanya kazi ya kuweka taarifa kutoka katika idara tofauti, ambapo baadhi ya moduli taarifa zake zimeingizwa miaka mingi nyuma na kupita kipindi kirefu bila ya kuingizwa taarifa nyengine ambazo zilitakiwa ziwemo. Baadhi ya moduli hizo ambazo taarifa zake zimesitishwa kuingizwa kwa muda mrefu ndani ya mfumo ni pamoja na moduli ya "Auditor" ambapo taarifa zake za mwisho kuingizwa ni za mwaka wa fedha 2017/2018, moduli ya "Business" katika kipengele cha "Shrinkage", taarifa za mwisho kuingizwa ni za mwaka wa fedha 2017/2018, moduli ya "CDF" katika kipengele cha "Estimates" taarifa za mwisho kuingizwa ni za mwaka wa fedha 2017/2018, "Task force" taarifa za mwisho kuingizwa ni za mwaka wa fedha 2021/2022, moduli ya "Procurement" katika kipengele cha kurikodi mabadiliko ya fedha ambapo taarifa za mwisho kuingizwa ni za tarehe 03/02/2020.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC) kuhakikisha moduli zilizomo katika mfumo wa SDMIS zinafanya kazi kikamilifu na kutumika katika kuweka taarifa za Shirika muda wote ili kuongeza tija na ufanisi wa kazi za kuchakata data, kuhifadhi kumbukumbu na kutoa taarifa zilizo sahihi zinazohusiana na Shirika.

- **Mfumo kuchukua nakala za taarifa (dublication of data) zaidi ya mara moja**

Baada ya kuupitia mfumo wa Statistical Data Management Information System, ukaguzi ulibaini kwamba katika moduli ya "Business" kipengele cha "Porter" mfumo unaruhusu kusajili Mchukuzi mmoja zaidi ya mara moja, ikiwa na maana ya kwamba mfumo hauna uwezo wa kutambua kwamba Mchukuzi husika amekwisha sajiliwa na ukazuiya usajili wake kwa mara ya pili, jambo ambalo linapelekea mfumo kukubali kuchukua nakala za taarifa zaidi ya moja.

Kwa mfano wakati wa kumuingiza Mchukuzi taarifa zake inaruhusu kuingiza taarifa ya kitambulisho chake ambapo unaweza kumsajili mchukuzi zaidi ya mmoja kwa kutumia kitambulisho kimoja. Hii inaonesha ya kwamba mfumo hauna ufunguo wa msingi (primary key) katika moduli ya usajili wa Wachukuzi yenye uwezo wa kutofautisha taarifa za kipekee na kuepusha urudiaji wa taarifa katika mfumo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar kuupitia mfumo huu ili kuzibaini nakala zote za taarifa zilizomo kwenye mfumo.

- **Kutokutumiwa kwa baadhi ya moduli zilizomo katika mfumo**

Kwa mujibu wa muongozo wa viwango kubalifu vya kimataifa vya TEHAMA unazitaka taasisi zote kuweza kutumia mifumo yote kikamilifu kwa kuzingatia mahitaji ya mfumo.

Ukaguzi ulibaini kuwa katika mfumo wa Statistics Management System kuna baadhi ya moduli ambazo hazijawahi kutumiwa tokea mfumo huo uanze kufanya kazi mpaka ukaguzi unakamilika. Mfano wa moduli zilizobainika kuwa hazijawahi kutumiwa ni pamoja na moduli ya Clove Seeding Distribution, Attendence, Buying, Vouching, Farmer ID, Product Purchase, Local sales".

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC) kuyafanyia kazi mapungufu hayo yaliyobainika.

- **Mfumo kutokuwa na moduli ya Mikopo ya Wafanyakazi**

Kwa mujibu wa "Term of Reference (TOR)" ya mfumo wa "Statistical Data Management Information System" kutoka ZSTC, ambapo katika ukurasa wake wa 3 kipengele cha "Suggested Requirements and Features" kimeorodhesha moduli ambazo zinatakiwa ziwemo katika mfumo, miongoni mwa orodha hizo ni pamoja na moduli ya "Mikopo ya Wafanyakazi" iliyoorodheshwa katika namba 17.

Ukaguzi ulibaini kuwa moduli ya Mikopo kwa Wafanyakazi haimo katika mfumo, hali ambayo mfumo unashindwa kufikia malengo yake kutokana na kuwa hauwezi kutoa taarifa za mikopo za wafanyakazi wake.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar kuweza kuipitia mifumo kwa kulinganisha mahitaji yote yaliyotajwa kutoka kwenye "Terms of Reference" ili kuwezesha mfumo kufanyakazi kikamilifu na kukamilika kwa kila hatua. Hii itasaidia kuweza kubaini kasoro na mapungufu yaliyomo katika mfumo.

- **Mapitio ya mfumo wa ZANMALIPO**

ZanMalipo ni mfumo wa usimamiaji ukusanyaji wa mapato ya Serikali ambao una lengo la kurahisisha ulipaji wa huduma za umma kwa kumuwezesha mlipaji kupata njia mbalimbali na rafiki za kufanya malipo kama vile kulipa kwa kutumia simu za kiganjani, Benki na Mawakala wa malipo. Ili kudhibiti makusanyo ya mapato na kuhakikisha kwamba malengo/bajeti za ukusanyaji wa mapato yanaenda sambamba na mapato halisi yanayokusanywa, Serikali iliamua kuanzisha mfumo maalum kwa ajili ya namba za udhibiti (Control Number) ambazo huunganishwa na mifumo mbalimbali ya ukusanyaji wa mapato. Hivyo, mfumo huu unatarajiwa kuwa na kumbukumbu zote za mapato yote ya Shirika yaliyopita katika mfumo huo kwa utaratibu wa kutumia nambari za udhibiti (Control Numbers).

Ukaguzi ulipitia kipengele kimoja badala ya chengine katika mfumo huo na kuweza kubaini mapungufu mbali mbali kama yafuatayo :-

- **Mfumo wa ZANMALIPO kutounganishwa na "Point Of Sale" (POS)**

Miongoni mwa muongozo wa viwango kubalifu vya kimataifa vya TEHAMA wa ISO 9001 (Fifth edition 15/9/2015) katika kifungu nambari 5.1.1 (c) ni kuhakikisha taasisi kuweza kuunganishwa kwa mifumo kulingana na mchakato wa biashara wa taasisi.

Katika nchi nyingi, Serikali hutumia nambari ya udhibiti kwa ajili ya malipo ya kodi, ada, na tozo mbalimbali. Hii inasaidia kurikodi malipo na kuhakikisha uwajibikaji. Nambari ya udhibiti (Control number) mara nyingine inaweza kutumiwa pamoja na mfumo wa ufuatiliaji wa malipo (ZanMalipo) ili kuhakikisha kuwa malipo yameshughulikiwa kwa usahihi na kuthibitishwa kwa wakati.

Inaweza pia kuwa na jukumu muhimu katika kuzuia udanganyifu wa malipo na kutoa usalama wa ziada katika mchakato wa malipo. Kwa mfano, unaweza kuipata kwenye ankara au risiti ya malipo na kutumia namba hiyo kuthibitisha kuwa malipo yamepokelewa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar kuona umuhimu kwa kuzingatia njia za kuboresha mchakato wa malipo, ikiwa ni pamoja na kuunganisha mfumo na "Point of Sale" ili kuweza kusomana taarifa zitakazofanyika za malipo ya kila siku kupitia vituo hivyo.

- **Mauzo ya Karafuu nje ya nchi (Bulk Sales) kutotumia "Control Number"**

Nambari ya udhibiti (Control Number) hutumika kwa kudhibiti, kufuatilia, na kurikodi malipo kwa njia inayoweza kufuatiliwa na kuhakikisha uwajibikaji katika Shirika.

Ukaguzi ulibaini kuwa zaidi ya asilimia 98 ya mauzo ya Karafuu yanafanyika nje ya mfumo wa ZANMALIPO ambayo ni "Bulk Sales" kwenda nje ya nchi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Biashara la Taifa kufanya tathmini ya faida na hasara za kufanya malipo nje ya mfumo wa ZanMalipo na kuchukuwa hatua stahiki kwa wakati ili kuimarisha uwazi na uwajibikaji pamoja na upatikanaji wa taarifa na takwimu sahihi kwa wakati.

- **Baadhi ya makusanyo ya mapato kufanyika bila ya kutumia Nambari za Udhibiti shilingi 130,498,235.58 na USD 1,249**

Serikali iliamua kuanzisha mfumo maalum kwa ajili ya namba za Udhibiti (Control Number) ambazo huunganishwa na mifumo mbalimbali ya ukusanyaji wa mapato. Hivyo, mfumo huu wa ZANMALIPO unatarajiwa kuwa na kumbukumbu zote za mapato yote ya Shirika yaliyopita katika mfumo huo kwa utaratibu wa kutumia nambari za udhibiti (Control Numbers).

Ukaguzi ulibaini kuwa kuna baadhi ya miamala ya malipo imefanyika bila ya kutumia "nambari za udhibiti" kupitia akaunti ya ZSTC ya "TZS" iliyopo katika benki ya PBZ yenye nambari **0404078000**, pamoja na akaunti ya "Dollar" iliyopo katika benki ya PBZ yenye nambari **0400662000**.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar kuweza kutumia control namba kwa mapato yote yanayokusanywa kupitia akaunti husika ili kuweza kudhibiti mapato hayo.

Miongoni mwa miamala iliyobainika imefanyika bila ya kufuata utaratibu uliowekwa na Shirika wa kukusanya mapato kwa kutumia "nambari za udhibiti" ni ile ya uuzaji wa karafuu nje ya nchi kwa wingi (bulk) kama ilivyoelezewa katika hoja nambari 32(ii), pamoja na miamala mengine ya ukusanyaji wa mapato kama zifuatazo katika jadweli:--

## Jadweli Nambari 45: Miamala ambayo haijatumia nambari ya udhibiti

| Tanzanian Shillings (TZS) – PBZ ACC NO. 0404078000 01/01/2023 - 30/06/2023 | | | |
|---|---|---|---|
| **S/N** | **Date** | **Transaction Details** | **Amount** |
| 1 | 10/01/23 | CASH DEPOSIT MOHD ALI JUMA FROM Mlandege Branch | 50,000,000 |
| 2 | 10/01/23 | CASH DEPOSIT MOHD ALI JUMA FROM Mlandege Branch | 40,000,000 |
| 3 | 16/01/23 | CASH DEPOSIT MOHD ZANZIBAR ID CARD- 0- TANZANIA, UNITED REPUBLIC- 1- INVESTMENTS PROFITS MOHD ALI JUMA FROM Mlandege Branch | 6,615,000 |
| 4 | 16/1/23 | CASH DEPOSIT mohd ali Juma FROM Mlandege Branch | 3,000,000 |
| 5 | 26/1/23 | CASH DEPOSIT ROSHMYA LOGISTICS COMPANY FROM IB Lumumba | 1,104,000 |
| 6 | 07/2/23 | CASH DEPOSIT ATHUMAN JUMA FROM IB Lumumba | 3,500,000 |
| 7 | 11/2/23 | CASH DEPOSIT JASMIN FROM IB Lumumba | 1,445,000 |
| **Tanzanian Shillings (TZS) – PBZ ACC NO. 0404078000 01/01/2023 - 30/06/2023** | | | |
| **S/N** | **Date** | **Transaction Details** | **Amount** |
| 9 | 22/2/23 | TAX BANK – Transfer AA/CASH_DEPOSIT/POS11 1317/RT222013630645/RIY ADHA GENERAL TRD/CASH_DEPOSIT | 744,000 |
| 10 | 09/3/23 | CASH DEPOSIT OCL OCEAN SHIPPING LINE FROM Malindi Branch | 1,091,000 |
| 11 | 06/4/23 | CASH DEPOSIT MIHD ALI JUMA FROM Mlandege Branch | 7,000 |
| 12 | 07/4/23 | CASH DEPOSIT AJE MARINE LTD FROM Mlandege Branch | 690,190.58 |
| 13 | 24/4/23 | CASH DEPOSIT KISWAHILI NA UTAMADUNI FROM Kariakoo Branch | 493,400 |
| 14 | 03/5/23 | TAX BANK – Transfer AA/CASH_DEPOSIT/POS11 1327/RT222017467068/ BRA IN CGS/CASH_DEPOSIT | 1,595,000 |
| 15 | 16/5/23 | CASH DEPOSIT ABDULSAMAD SAID AHMED FROM Forodhani Branch | 2,914,700 |
| 16 | 16/5/23 | CASH DEPOSIT ALI ABUU MACHANO FROM Forodhani Branch | 445,195 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 17 | 17/5/23 | CASH DEPOSIT<br>RUKIYAF ROM IB Lumumba | 1,377,000 |
| 18 | 01/6/23 | CASH DEPOSIT MOHD ALI JUMA FROM Mlandege Branch | 14,000 |
| 19 | 10/6/23 | CASH DEPOSIT SWAHILI SOFT<br>TECHNOLOGIES FROM IB Mpirani | 3,000,000 |
| 20 | 28/6/23 | CASH DEPOSIT<br>MGENIFROM Mlandege Branch | 307,750 |
| 21 | 30/6/23 | CASH DEPOSIT IMPREST KARAFUU FROM Mlandege Branch | 5,155,000 |
| | | **TZS** | **130,498,235.58** |
| **United State of America Dollar (USD) – PBZ ACC NO. 0400662000 01/01/2023 - 30/06/2023** | | | |
| **S/N** | **Date** | **Transaction Details** | **Amount** |
| 1 | 16/1/23 | CASH DEPOSIT NASSOR RAMADHAN JUMA FROM IB Mpirani | 206 |
| 2 | 20/1/23 | CASH DEPOSIT NASSOR<br>RAMADHAN JUMAFROM IB Mpirani | 100 |
| 3 | 23/1/23 | CASH DEPOSIT NASSOR<br>RAMADHAN JUMAFROM IB Mpirani | 220 |
| 4 | 26/1/23 | CASH DEPOSIT NASSOR<br>RAMADHAN FROM IB Mpirani | 194 |
| 5 | 28/1/23 | CASH DEPOSIT NASSOR<br>RADHAN JUMA FROM IB Mpirani | 90 |
| 6 | 31/1/23 | CASH DEPOSIT NASSOR<br>RAMADHAN JUMA FROM IB Mpirani | 114 |
| 8 | 12/2/23 | CASH DEPOSIT NASSOR<br>RAMADHAN FROM IB Mpirani | 145 |
| | | **USD** | **1,249** |

### 4.1.17.7 Mapitio ya mfumo wa TIGOPESA

Mfumo wa tigopesa wanaotumia Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar ni mfumo unaotumika kwa ajili ya ulipaji wa wakulima na wauzaji wa karafuu visiwani Zanzibar, mfumo huu hupitisha miamala mikubwa ya kila siku na kuwalipa wakulima hali ambayo ZSTC wanatakiwa kuweza kuutumia kwa kuzingatia umuhimu wake kwa kurahisisha usalama wa fedha nyingi wanazopokea wakulima na wauzaji wa karafuu katika vituo maalumu vya kununulia karafuu vilivyowekwa na shirika la ZSTC.

Ukaguzi ulipitia mfumo huu na kujua namna unavyofanyakazi, na kuweza kubaini mapungufu mbali mbali kama vile mfumo kutokuwa na uwezo wa kutoa ripoti zinazoonesha kilo zilizonunuliwa, mfumo kuchukua majina mawili ya muuzaji kwa ajili ya kuhakikiwa na kufanyiwa malipo.

- **Mfumo wa tigopesa kukosa taarifa muhimu za ununzi wa Karafuu kupitia mtandao wa simu**

Miongoni mwa viwango kubalifu vya kimataifa ni kuweza kuwa na taarifa muhimu za kujitosheleza katika mfumo ili kukizi mahitaji na malengo ya mfumo kama ilivyotarajiwa.

Ukaguzi ulibaini kuwa mfumo wa tigopesa hautoi ripoti za muhimu za ununuzi wa karafuu, kwa mfano mfumo kutokuwa na uwezo wa kubaini taarifa za kilo ambazo zimenunuliwa kwa siku, wiki, mwezi na hata msimu mzima, kwani ni muhimu kufuatilia manunuzi yanayofanyika ya kila siku ndani ya mfumo ukizingatia kuwa uhitaji wa kujua ni kilo ngapi zimenunuliwa, ni muhimu zaidi kwa sababu ya kuweza kuthibitisha na kuhakiki kwa urahisi zaidi taarifa za mnunuzi kwa kulinganisha na uhalisia katika mabuku, risiti na karatasi ya mpimaji wa karafuu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar kuweza kukaa pamoja na wahusika waliowapa huduma ya tigopesa ili kuweza kuimarisha udhibiti wa mfumo na kuimarisha huduma zake kwa ufanisi zaidi kulingana na matakwa na mahitaji wanayotaka Shirika ili kuweza kupata huduma iliyo bora zaidi na yenye uhakika kwa sababu ni mfumo ambao unalipa fedha nyingi kwa wakulima wa karafuu.

- **Mfumo kuonyesha majina mawili pekee ya muuzaji kutoka kwenye tigo kwa ajili ya kuhakikiwa na kufanyiwa malipo**

Miongoni mwa viwango kubalifu vya kimataifa ni kuhakikisha kuwa mfumo wa malipo unawekewa usalama na ulinzi kwa kuhakikisha uhakiki wa taarifa unajitosheleza kikamilifu ili kufanya malipo yaliyo na uhakika na usahihi kwa muuzaji.

Ukaguzi ulibaini kuwa mfumo wa tigopesa unapoingiza namba ya simu ya muuzaji kwa ajili ya kufanyiwa malipo, namba inakuja na majina mawili pekee, ambapo mfumo unaonyesha jina la mwanzo na jina la mwisho.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar kuweza kuchukua hatua za haraka zaidi kuwasiliana na watoa huduma ili kuhakikisha kuwa mfumo unachukua majina yote matatu ambayo yanakuwemo kwenye namba ya simu kwa ajili ya kuhakikiwa na kufanyiwa malipo kwa njia ya simu, ukizingatia kuwa majina mengi ya wakazi wa Zanzibar yanafanana. Hali hii itasaidia kupunguza changamoto nyingi za kimfumo na kupelekea kuongezeka kwa wauzaji wanaotaka kulipwa kupitia mtandao wa simu hali ambayo itapunguza ulipaji wa fedha taslimu (Cash) na kuweza kudhibiti usalama.

#### 4.1.17.8 Mapungufu yaliobainika katika chumba cha Seva (Server Room)

Ukaguzi ulitembelea chumba cha Seva cha ZSTC kwa upande wa Unguja na Pemba na kubaini uwepo wa mapungufu mbali mbali katika vyumba hivo ikiwemo kukosekana kwa mfumo wa kuzima moto, kutokuwepo kwa kamera za ulinzi, udhaifu wa udhibiti kupitia geti la mlangoni, kutokuwepo kwa mashine ya "Biometric" kwa ajili ya kuchukuwa kumbukumbu za watu wanaoingia na kutoka, udhaifu wa usalama katika dirisha la chumba cha Seva, mazingira duni ya chumba cha Seva kiusafi, mpangilio wa vitu, hali ya joto na mavumbi.

Hali hii inakwenda kinyume na miongozo ya viwango bora kubalifu (best practice) kama vile ISO 9001 (Fifth edition ya 15/9/2015) katika kifungu nambari 5.15 pamoja na, miongozo ya kitaifa inayotolewa na Wakala wa Serikali Mtandao (eGAZ).

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZSTC kuchukuwa jitihada za kufanyia kazi dosari hizi ili kuondokana na mazingira yasiyo salama katika chumba cha Seva jambo ambalo linaweza kuhatarisha usalama wa rasilimali za TEHAMA zilizo ndani ya chumba hicho.

#### 4.1.17.9 Dosari zilizobainika katika mfumo wa "CCTV Camera katika jengo la Shirika

"CCTV Camera" ni chombo cha kufuatilia na kurikodi matukio kwa madhumuni ya kuimarisha usalama na ufuatiliaji wa matukio mbali mbali kwa kutunza ushahidi wa kuaminika zaidi.

Katika kufanya ukaguzi wa mifumo ya TEHAMA ya ZSTC ukaguzi ulibaini uwepo wa mapungufu mbali mbali yakiwemo kuharibika kwa mashine inayotumika kuhifadhia taarifa za matukio (NVR), kuharibika kwa Screen inayotumika kuonyesha taarifa zinazorikodiwa, kutokufungwa kwa kamera katika baadhi ya maeneo muhimu, pamoja na kutorejeshwa kwa kamera ambayo ilifunguliwa kwa ajili ya matengenezo ya afisi.

Aidha, imebainika baadhi ya maghala yanayohifadhiwa rasilimali za karafuu kutofungwa mifumo ya Ulinzi wa Kamera ili kuweza kuongeza udhibiti na usalama dhidi ya vitendo vya wizi, upotevu, ubadhirifu au uharibifu unaoweza kufanyika kwenye rasilimali hizo.

Uwepo wa dosari hizi ni kwenda kinyume na miongozo ya viwango bora kubalifu vya TEHAMA inayosimamia masuala ya usalama kwa njia za Kidijitali pamoja na miongozo ya kitaifa hasa ikizingatiwa kwamba shughuli kuu za kibiashara za ZSTC ni kununua, kuchakata na kuuza mazao mbali mbali kama vile Karafuu, Mchai chai n.k ambazo zina mazingira ya vihatarishi (risks) vinavyoweza kuathiri upatikanaji wa faida na utoaji wa huduma endelevu kwa umma.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZSTC kufanya tathmini ya thamani halisi ya mapato yanayozalishwa kutokana na mazao tajwa kwa kulinganisha na gharama za ununuzi na usimamizi wa vifaa vya ulinzi vya kamera na hatimae kuchukuwa hatua muafaka za kufunga kamera hizo ili kuimarisha ulinzi na usalama wa maeneo yanayohifadhiwa bidhaa hizo.

Aidha, ukaguzi unaushauri uongozi wa ZSTC kuhakikisha kwamba kazi hii inafanywa na wataalamu wenye weledi na uzoefu wa kutosha ili Serikali ipate thamani ya fedha katika utekelezaji wa maboresho haya na kwamba kabla ya kutekeleza ni muhimu kila mpango ukawa kwenye maandishi na ripoti za utekelezaji zipatikane kwa ajili ya ukaguzi kulingana na itakavyohitajika.

## 4.1.18 OFISI YA RAIS FEDHA NA MIPANGO (MOFP)

Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango (MOFP) kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

### 4.1.18.1 Matumizi yasiyokuwa na tija ya fedha za Umma zaidi ya USD 838,590 wastani wa shilingi 2,180,334,000 kwa ajili ya utengenezaji wa mfumo wa National Online Business System (NOBS)

Kwa mujibu wa Muongozo wa eGA nambari **eGA/EXT/BSA/008** wa Utekelezwaji wa Miradi ya TEHAMA, wa mwaka 2020 unahitaji mradi wa TEHAMA unapotekelezwa lazima ufuate taratibu na mbinu "Methodology" ya Project Development Life Cycle – PDLC. Mbinu hiyo imekusanya hatua tofauti za mchakato wa utengenezwaji wa mfumo.

Aidha, kifungu nambari 2.3 cha muongozo huo kimefafanua kwamba kwa kila hatua kutakuwa na matayarisho ya nyaraka ambazo zitasaidia katika utengenezwaji, uendeshaji, usimamizi na udumishaji wa mfumo.

Ukaguzi ulibaini kwamba mnamo tarehe 15/11/2019 Ofisi ya Rais Fedha na Mipango (MOFP) ilisaini mkataba nambari ISPG/ZNZ/AfDB/SSB/01/2019 na Kampuni ya M/S Norway Registers Development, as Lokketangen 20B, No.1331, Sandvika, Norway kwa ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa ajili ya utengenezwaji wa mfumo wa kielektroniki ujulikanao kama Integrated National Online Business Management System (NOBS) kwa muda wa miezi 12, ambapo mfumo huo ulitakiwa kuwa tayari mnamo tarehe 12/12/2020 kwa gharama ya USD 838,590 sawa na wastani wa shilingi 2,180,334,000.

Mfumo huo ulikusudiwa kuwa na lengo la kurahisisha kazi, kuimarisha udhibiti wa utoaji wa leseni, kuongeza uwazi na uwajibikaji na kuboresha utunzaji wa kumbu kumbu za biashara kwa zaidi ya taasisi nne (4). Miongoni mwa Taasisi hizo ni Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA), Kamisheni ya Utalii Zanzibar (ZCT), Baraza la Udhibiti Mfumo wa Utoaji wa Leseni (BLRC), na Wakala wa Kusajili Biashara Zanzibar (ZBPRA).

Aidha, ukaguzi ulibaini kwamba tangu kusainiwa kwa mkataba huo hadi ukaguzi unakamilika ni zaidi ya miaka minne (4) ambapo mfumo huo wa NOBS haujakamilika utengenezwaji wake na kuanza kutumika kufanya kazi ili kufikia malengo yaliyokusudiwa. Hali hii imechangiwa na kukosekana kwa usimamizi mzuri wa Mradi wa Utengenezwaji wa Mifumo huo unaoendelea kutengenezwa na kuisababishia Serikali hasara ya fedha ambazo zingeweza kutumika kwa kusaidia utatuzi wa changamoto mbali mbali zilizopo.

Kwa upande mwingine ukaguzi ulifahamishwa kwamba Ofisi ya Rais Fedha na Mipango ilikwisha kabidhi usimamizi na uwendeshaji wa mfumo wa NOBS kwa Wakala wa Serikali Mtandao (eGAZ) tangu mwaka 2021/2022 na kwamba ilitarajiwa mpaka kufikia sasa eGAZ ingekuwa tayari imechukuwa hatua stahiki kuhusiana na mfumo huo ili kupunguza hasara.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kwa kushirikiana na Wakala wa Serikali Mtandao kuhakikisha kwamba unafuatilia kwa kina kadhia hii ili kuwezesha ukamilishaji wa mfumo wa NOBS kulingana na malengo yaliyokusudiwa na hatimae kupatikana kwa tija iliyopangwa (value for money).

#### 4.1.18.2 Udhibiti duni katika chumba cha Seva cha Afisi ya Rais Fedha na Mipango (MOFP)

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa udhibiti duni wa chumba cha Seva ambapo chumba hicho hakina udhibiti wa moja kwa moja wa moto (automatic fire suppression system) na pia kutokuwepo kwa Kamera za ulinzi (CCTV Camera) jambo ambalo ni kinyume na miongozo ya viwango bora kubalifu vya kimataifa. Hali hii inaweza kuhatarisha usalama wa vifaa, mifumo na miundombinu inayotumika katika kuendesha seva za Ofisi pindipo ikitokea janga la moto katika mazingira ya Ofisi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kufanya jitihada za kuchukuwa hatua muafaka ili kuweza kutatua changamoto hiyo iliyojitokeza kwenye chumba cha Seva.

#### 4.1.18.3 Kutokufanyakazi kwa Kamera za Usalama katika Kituo cha Kujikinga na Maafa (Disaster Recovery Site)

Ukaguzi ulifanya mapitio ya eneo la kuendeleza huduma za mtandao na biashara ya baada ya maafa (Disaster Recovery Site) la Ofisi ya Rais Fedha na Mipango liliopo Makunduchi na kubaini kwamba kuwa mashine ya kuhifadhi matukio yanayorikodiwa na CCTV Camera (NVR) haifanyi kazi. Hivyo, hakuna kumbukumbu yeyote ya matukio ya ndani wala ya nje ya eneo hilo inayoweza kutunzwa na kutumiwa kwa ajili ya kufuatia usalama wa eneo hilo.

Kutokufanyakazi kwa kifaa hicho kunaweza kusababisha upungufu katika ulinzi, usalama na ufuatiliaji wa matukio yanayofanyika kwenye mazingira ya eneo hilo jambo ambalo linaweza kusababisha kushindwa kupatikana ushahidi kwa aliyehusika pindipo janga au tukio lolote la kihalifu likitokea kwenye mazingira ya eneo au chumba hicho.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuhakikisha kuwa mtambo wa kutunza kumbukumbu zinazorikodiwa kwenye CCTV Camera (NVR) unarekebishwa haraka au kuekwa mtambo mwengine utakaokuwa na uwezo na vigezo imara vya kuhifadhia kumbukumbu za rikodi za Kamera za CCTV ili kuimarisha ulinzi na usalama wa vifaa na rasilimali zilizopo kwenye eneo hilo.

#### 4.1.18.4 Mfumo wa IFMIS kushindwa kukata Kodi ya Zuio Kiautomatiki (Automatic Withholding Tax)

Ukaguzi umebaini kuwa hati za malipo zinazotengenezwa na wahasibu katika Mfumo wa IFMIS kwa ajili ya malipo ya huduma mbali mbali zinazotolewa na watoa huduma hazikatwi Kodi ya zuio Kiautomatiki ambapo inamlazimu Mhasibu kukokotoa mahesabu ya kodi nje ya Mfumo kwa njia ya kawaida (manually) na baadae kupunguza kwenye fedha za malipo husika kwa ajili ya mchakato wa malipo.

Hali hii inaongeza uwezekano wa kufanyika makosa ya kibinadamu (human errors) wakati wa kufanya ukokotoaji wa mahesabu ya Kodi ya zuio na kupelekea mtoa huduma kukatwa fedha nyingi zaidi au pungufu ya kiwango stahiki na hatimae kusababisha hasara kwa Serikali.

Aidha, kukokotoa Kodi ya zuio kwa njia ya kawaida ni miongoni mwa sababu zinazochangia kuchelewesha malipo ya Kodi ya Zuio kwa Mamlaka ya Mapato na kuikosesha Serikali Mapato kwa wakati.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kupitia kwa Ofisi ya Muhasibu Mkuu wa Serikali kuhakikisha unasimamia kikamilifu Usanidi wa Mfumo wa IFMIS na kuhakikisha kwamba unawezeshwa kukata Kodi ya Zuio Kiautomatiki kwa haraka iwezekanavyo ili kuleta tija.

### 4.1.19 SHIRIKA LA BANDARI ZANZIBAR (ZPC)

Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa Shirika la Bandari Zanzibar (ZPC) kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

**MAPITIO YA MRADI WA e-Port**

Shirika la Bandari Zanzibar lilisaini hati ya makubaliano na kampuni ya Fortris na Wartsila tarehe 24/04/2022 kwa ajili ya uanzishwaji wa Mradi wa e-Port kwa thamani ya USD 6,569,143.31 kwa muda wa miaka mitatu (36 months) ambapo mradi huo umejumuisha utengenezwaji wa mifumo mitano (5) ya TEHAMA iliyounganishwa kwa pamoja na kutumika kwa shughuli kuu za Bandari. Mifumo hiyo ni Terminal Operating System (TOS), Enterprise Resource Planning (ERP), Fleet Fuel Management System (FFMS), Vessel Traffic System (VTS).

Aidha, mifumo hiyo ilijumuisha portal moja inayojulikana kwa jina la e-Portal. Katika kufanya mapitio ya mradi huo ukaguzi umebaini kuwepo kwa mapungufu mbali mbali kama ifuatavyo: -

#### 4.1.19.1 Kutokamilika kwa mfumo wa mizani (Weghtbridge Operations) wa kupima uzito wa mizigo

Mfumo wa mizani bandarini ni mfumo unaotumiwa katika Bandari au Vituo vya Usafirishaji wa mizigo ili kupima uzito wa mizigo inayoingia au kutoka nchini kwa lengo la kukadiria tozo zinazotakiwa kulipwa kulingana na uzito wa mizigo husika. Mfumo huu una umuhimu mkubwa sana katika kulinda barabara na madaraja yanayojengwa kwa gharama kubwa ili kudhibiti miundombinu hiyo kuharibika kutokana na uzito mkubwa wa magari ya mizigo yanayopita barabarani.

Kwa mujibu wa mkataba baina ya ZPC na Kampuni ya Fortris, Kifungu nambari 2, kipengele kidogo 2.2.8 (a-d) cha "SRS" na kama ilivyo ainishwa katika mpango kazi wa mradi (Project Schedule) kwamba mfumo wa "weghtbridge operations" utakuwa ni sehemu na utajumuishwa katika mfumo wa Terminal Operating System (TOS).

Ukaguzi ulibaini kwamba mfumo wa "weightbridge operations" haujakamilika hadi ukaguzi unamalizika jambo ambalo ni kinyume na mpango kazi pamoja na matakwa ya mkataba husika.

Aidha hali hii inatia shaka juu ya maandalizi yote yaliyofanywa na ZPC katika kuhakikisha kwamba mahitaji yote muhimu ya kutekeleza mfumo huo yamekamilika ikiwa ni pamoja na kutambua maeneo yatakayofungwa mashine hizo za kupima uzito wa mizigo, pamoja na wataalamu watakaohusika kuendesha mfumo na mashine hizo.

Vile vile kuchelewa kukamilika kwa utengenezaji wa Mfumo wa "Weightbridges Operation" pamoja na mashine zake kunapelekea kuendelea kujitokeza kwa mapungufu katika ukusanyaji wa tozo zinazotokana na upimaji wa uzito wa mizigo jambo ambalo linaweza kuingiza hasara Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Bandari ZPC kusimamia kwa ukaribu utekelezaji wa mkataba huu na kuhakikisha kwamba mfumo wa kupima mizigo (Weightbridge operations) unakamilika kwa haraka ili kuweza kukusanya tozo zinazotokana na uzito wa mizigo inayoshushwa bandarini na hatimae kufanikisha lengo la ukusanyaji wa mapato lililokusudiwa.

Aidha, kwa kuwa muda wa utekelezaji wa mfumo huu umeshamalizika ukaguzi unaushauri uongzozi wa ZPC kuchukuwa jitihada za makusudi za kufuatilia chanzo cha uchelewaji wa ukamilishaji wa mfumo huo kwa kukaa chini na Msambazaji (Fortris) ili kuchukuwa hatua stahiki za kurekebisha dosari kwa lengo la kupatikana mfumo huo hatimae kupatikana huduma iliyokusudiwa.

#### 4.1.19.2 Kutokamilika kwa moduli ya upangiliaji wa makasha (containers) kwenye Bandari ya Malindi (Yard Operations) katika mfumo wa TOS

Moduli ya "Yard Operations" ni sehemu ya mfumo wa TOS wenye jukumu la kusimamia na kuratibu upangiliaji wa mizigo mbali mbali kama vile magari na makasha (containers) katika eneo la "yard" ya bandari. Lengo ni kuongeza tija na ufanisi, kuboresha usalama wa watumishi na mizigo, na kusimamia rasilimali mbali mbali kama vile vitendea kazi kwa ufanisi zaidi. Kama ilivyo ainishwa katika "SRS" za mfumo wa TOS Kifungu nambari 2 kipengele kidogo cha 2.2.4. Kinyume na matakwa ya mkataba ulioingiwa baina ya Shirika la Bandari Zanzibar na Kampuni ya Fortris, ukaguzi umebaini kwamba Shirika halijafanikiwa kutekeleza moduli ya "Yard Operations" mpaka sasa pasipo kuwa na sababu za msingi.

Kutokamilika kwa moduli hii kunaashiria kwamba kuna hatari ya muda wa mkataba kumalizika kabla ya kutekelezwa kwa moduli hiyo muhimu katika mfumo wa TOS.

Ukaguzi unalishauri Shirika la Bandari kuchukuwa hatua stahiki za kusimamia na kufuatilia kwa karibu ili kubaini chanzo cha ucheleweshaji na kuchukuwa hatua stahiki kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba na kwa mujibu wa Sheria zilizopo.

#### 4.1.19.3 Kutokumalizika kwa Mfumo wa Vessel Traffic System (VTS)

Mfumo wa Vessel Traffic System (VTS) ni mfumo wa usimamizi wa "traffics" za Meli ambao unalenga kuimarisha usalama na kuongeza ufanisi wa usafirishaji wa baharini hapa Zanzibar. VTS hutumia teknolojia ya hali ya juu kufuatilia mienendo ya meli na vyombo vengine vya majini katika eneo la Bandari.

Kwa kuzingatia mkataba wa makubaliano wa utengenezwaji wa mfumo huu ambao ulisainiwa mnamo Aprili 24, 2022, pamoja na mpango kazi wa Mradi wa e-Port (Project Plan) mfumo wa VTS ulitakiwa kuanza tarehe 23/05/2022 na kumalizika tarehe 15/06/2023 ambapo hadi ukaguzi unakamilika mfumo huo bado ulikuwa haujamaliza kutengenezwa na kutoa huduma iliyokusudiwa.

Aidha, ukaguzi umebaini kwamba baadhi ya vifaa vilivyohitajika kufungwa na kutumika sambamba na mfumo huo pia havijawasilishwa na Kampuni iliyohusika kusambaza (Vendor). Baadhi ya vifaa vilivyokuwa havijawasilishwa ni pamoja na Rada za mawasilano za kutafuta meli n.k.

Kutokamilika kwa mfumo huo pamoja na kutowasilishwa kwa vifaa muhimu vinavyotegemewa kufanya kazi katika mfumo huo kunaweza kusababisha kupungua kwa usalama wa usafiri majini kutokana na Shirika kushindwa kufuatilia mienendo ya vyombo vya baharini kama vile Meli, Majahazi na Boti za abiria, mashua pamoja na Maharamia ambao wanaweza kufanya uhalifu katika eneo la mzingo wa bandari.

Aidha, kukosekana kwa mfumo huo wa VTS, kunaweza kusababisha Meli kushindwa kusimamiwa ipaswavyo na kupata udhibiti mzuri wa "traffics" na kupelekea kuchelewa kuingia/ kutoka kwenye Bandari hali ambayo inaweza kuzalisha hasara kwa meli hizo na Serikali kwa ujumla.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Bandari Zanzibar kufanya tathmini ya kina ya changamoto zote zinazokwamisha utekelezaji wa mfumo wa VTS na kuweka mikakati na mipango mahsusi kwa kushirikiana na Kampuni ya Fortris na wadau wengine wanaohusika ili kusaidia mfumo kukamilka kwa haraka.

Aidha, kwa kuzingatia ukweli kwamba sehemu kubwa ya mfumo huu haijafanyiwa kazi ukaguzi unaushauri uongozi wa ZPC kuchukuwa jitihada za makusudi kuharakisha ukamilishaji wa mfumo huo ili kupunguza hasara inayoendelea kutokana na kutopatikana kwa tija iliyokusudiwa.

#### 4.1.19.4 Ucheleweshwaji wa Mfumo wa FFMS katika Mradi wa "e-Port"

Ukaguzi umebaini kwamba mfumo wa FFMS ulianza kutengenezwa tarehe 22/08/2022 ambapo ulitakiwa kukamilika ndani ya miezi 4 hadi tarehe 02/12/2022, hii ni kwa mujibu wa mpango kazi ulioainishwa kwenye "Project Charter" ambayo ni nyaraka muhimu katika kusimamia mradi wa e-Port na kuhakikisha Serikali inapata thamani ya Fedha zilizoekezwa kupitia mkataba ulioingiwa baina ya Shirika la Bandari na kampuni ya Fortris. Hata hivyo, hadi ukaguzi unakamilika mfumo huo ulikuwa bado haujamaliza kutengenezwa na ulikuwa umeshachelewa kwa zaidi ya miezi nane (8) kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba.

Kutokukamilika kwa Mfumo huo kunapunguza wigo wa kusimamia upatikanaji wa Mafuta kwa ajili ya matumizi ya shughuli za Shirika, pamoja na kupunguza uwezo wa kufuatilia matumizi ya mafuta hayo katika vyombo mbali mbali vinavyo milikiwa na shirika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Bandari Zanzibar kufanya jitihada za kukamilisha utengenezwaji wa Mfumo wa FFMS ili kuweza kutumika na kupatikana tija iliyokusudiwa.

#### 4.1.19.5 Kutokutengenezwa kwa Mfumo wa Enterprise Resource Planning (ERP)

ERP ni mfumo wa Kiutawala wenye jukumu kuu la kusimamia masuala ya mapato na matumizi, rasilimali watu, mali za Shirika, manunuzi, mishahara, stoo, pamoja na kuandaa hesabu za kila mwisho wa mwaka ndani ya Shirika. Kwa mujibu wa taarifa za "e-Port Project Charter" Mfumo wa ERP ulianza kutengenezwa tarehe 15/05/2022 na kutakiwa kukamilika tarehe 13/11/2022. Hadi ukaguzi unakamilika ilibainika mfumo huo haujamaliza utengenezwaji wake na ulishachelewa kwa zaidi ya miezi 9 ambapo hatua iliyopo (current status) haikuweza kufahamika wazi kutokana na uwepo wa tofauti za taarifa baina ya "Vendor" na Shirika kwenye kazi zilizofanyika na zile zilizobakia kwa mujibu wa mkataba.

Kutokana na kubainika uchelewaji huo ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Bandari kufuata Sheria za manunuzi kwa kufanya tathmini ya chanzo cha ucheleweshwaji wa mkataba na kuchukuwa hatua stahiki kwa upande unaohusika ikiwa ni pamoja na kutoza faini kwa mtoa huduma kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba ili kuepusha hasara inayoendelea kujitokeza.

#### 4.1.19.6 Dosari katika ununuzi wa Rasilimali za TEHAMA shilingi 927,962,200

Shirika la Bandari Zanzibar lilisaini hati ya makubaliano ya mkataba na Kampuni ya ZAN IT Solution Co. Ltd wenye kumbukumbu nambari SMZ/F.123/GNCB/202-22 ya tarehe 30 /08/2022 kwa thamani ya shilingi 927,962,200 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na rasilimali mbali mbali za TEHAMA za Shirika.

Dosari iliyobainika katika mchakato wa ununuzi huo ni kutoshirikishwa kikamilfu kwa Kitengo cha TEHAMA cha Shirika katika hatua za uandaaji wa vigezo sahihi vilivyokuwa vikihitajika katika ununuzi wa rasilimali hizo kwa mujibu wa mkataba na mahitaji ya Shirika, ambapo vigezo (Specifications) vilitolewa na kuingizwa kwenye mkataba vilitoka Idara ya Ununuzi na sio Idara ya TEHAMA kama ilivyohitajika kwa mujibu ya uhalisia wa manunuzi hayo, vile vile ilibainika baadhi ya vifaa vya TEHAMA havikutolewa vigezo kabisa kwenye mkataba.

Hali hii imesababisha kununuliwa vifaa kinyume na matakwa na mahitaji ya Shirika ambapo baadhi ya vifaa vilivyonunuliwa vimebainika kuwa na uwezo mdogo wa utendaji kazi kulinganisha na mifumo ya Shirika. Miongoni mwa vifaa vya TEHAMA vilivyobainika kuwa na vigezo tofauti ni pamoja na Desktop All in One, UPS backup, pamoja na Wireless Access Points.

Aidha baadhi ya vifaa vilivyowasilishwa kinyume na vigezo ni "Microsoft Office Standard 2019, Ms. Office Pro Plus 2013" wakati viliyohitajika vilikuwa ni "Microsoft Office 365".

Vile vile Antivirus zilizotakiwa zilikuwa "Bitdefender Total Security 2021 build 26.0.7.41 64 bits" wakati zilizosambazwa na kupokelewa ni "ESET Internet security".

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Bandari kuweka utaratibu wa ndani wa manunuzi utakaohakikisha kwamba manunuzi ya vifaa vyote vya TEHAMA yanashirikisha wataalamu wa TEHAMA katika hatua zote ikiwa ni pamoja na kufanya mapitio ya mkataba kabla ya kupatiwa mzabuni ili kuhakikisha kwamba vipengele vyote vilivyohitajika vimejumuishwa kwa usahihi na ufanisi.

### 4.1.19.7 Kukosekana kwa ripoti ya ukaguzi (inspections) wa vifaa vilivyopokelewa

Miongoni mwa taratibu za manunuzi ni pamoja na kufanya ukaguzi (inspection) wa kitaalamu ili kuhakikisha kwamba vifaa vilivyonunuliwa na kuwasiliswa na Mzabuni vinakidhi matakwa ya mkataba zoezi linalofuatiwa na uandishi wa ripoti ya ukaguzi " inspection Report" huo.

Ukaguzi umebaini kwamba Ripoti ya ukaguzi wa vifaa vilivyopokelewa (Inspection Report) haikuandaliwa ili kuweza kubaini hali halisi ya idadi na vigezo vya vifaa vilivyoagizwa na vilivyopokelewa jambo ambalo linaweza kusababisha kujitokeza kwa upotevu wa vifaa vilivyonunuliwa kutokana na kutowasilishwa kwa idadi kamili na hatimae kuingiza hasara Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Bandari kufuatilia kwa karibu utendaji kazi wa kitengo cha manunuzi katika mchakato huo na kuhakikisha kwamba taratibu zote za manunuzi zinazingatiwa kwa manunuzi yote ya Shirika.

### 4.1.19.8 Dosari katika Mashine za ukaguzi wa mizigo na abiria bandarini

Katika ukaguzi uliofanyika ZPC imebainika uwepo wa mapungufu mbali mbali kwenye vitendea kazi ambayo yalichangia kuathiri ufanisi wa Bandari hususan kwenye eneo la kuhudumia abiria. Miongoni mwa mapungufu hayo ni kubainika kwa mashine za kukagulia mizigo ambazo hazifanyi kazi kwa muda mrefu. Vile vile kubainika kwa baadhi ya mashine ambazo hazipo rafiki katika utendaji wake wa kuchunguza na kukagua mizigo ya abiria wa kawaida (CX100100T1).

Hali hii inaweza kusababisha kukosekana kwa ufanisi katika utendaji kazi wa mashine hizo na kupelekea kujitokeza kwa dosari mbali mbali za kiusalama katika kazi za ukaguzi wa abiria na mizigo yao.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Bandari kuchukuwa jitihada za makusudi za kufanya marekebisho ya haraka kwa mashine zilizoharibika pamoja na kununua mashine zilizokuwa rafiki kwa watendaji wa bandari ili kupatikana tija iliyokusudiwa na kuongeza usalama wa abiria na mizigo yao.

### 4.1.19.9 Dosari katika uunganishwaji wa Mifumo ya e-Port

Kwa mujibu wa mpango kazi (implementation plan) wa mradi wa E-Port, mfumo wa TOS ulitakiwa kuanza kufanyiwa kazi tarehe 23/05/2022 na kukamilika tarehe 03/02/2023, mpaka tunakamilisha ukaguzi mwezi Septemba, 2023 mfumo wa TOS ulikuwa haujakamilika ikiwa umechelewa kwa zaidi ya miezi 7 ambayo ni sawa na asilimia 78 ya ucheleweshwaji wa mradi katika eneo hili.

Mapungufu haya yamebainika kutokana na kukosekana kwa "integration" ya TOS na mifumo mengine ambayo inahusiana katika kukamilisha shughuli za bandari ikiwemo malipo huduma, baadhi ya mifumo ni pamoja na ZANMALIPO, TANCIS-TRA, Container Management System (CMS)-SHIPCO, ERP-ZPC n.k hii ni kwa mujibu wa kifungu nambari 2, kifungu kidogo 2.5 kwenye "System Requirement Specification (SRS)"

Kwa upande wa wadau wa ZPC kama vile SHIPCO na Wakala wa kuondoa mizigo (Clearing and Forwarding Agents) mfumo wa TOS ulitakiwa kuwa na kipengele cha kuwawezesha kupata taarifa mbali mbali zinazowahusu jambo ambalo halijafanyiwa kazi kwenye mfumo wa TOS na kuwalazimu kutafuta taarifa hizo katika mifumo mingine kama vile TANCIS.

Kukosekana kwa integration baina ya mfumo wa TOS na mifumo mengine kama ilivyoainishwa hapo juu kumepelekea uwepo wa dosari mbali mbali ikiwemo kufifisha uwazi na uwajibikaji, kupunguza tija na ufanisi wa Shirika na wadau wake, kupunguza imani kwa watumiaji wa huduma za Bandari za Zanzibar na kuathiri mapato ya Serikali n.k.

Kwa kuwa kuna ucheleweshwaji mkubwa wa utekelezaji wa mkataba huu baina ya Shirika la Bandari na kampuni ya Fortris ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Bandari kufuata Sheria za manunuzi kwa kufanya tathmini ya chanzo cha ucheleweshwaji wa mkataba na kuchukuwa hatua stahiki kwa upande unaohusika ikiwa ni pamoja na kutoza faini kwa mtoa huduma ama kuchukua hatua za kinidhamu kwa watumishi ikiwa wao ndio chanzo cha tatizo.

### 4.1.20 MAMLAKA YA UWEKEZAJI WA VITEGA UCHUMI ZANZIBAR (ZIPA)

Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa Mamlaka ya Uwekezaji wa Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA) kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 4.1.20.1 Kukosekana kwa mfumo wa fedha (Financial System) Kwa Wahasibu wa Pemba

Ukaguzi umegundua kuwa kwa upande wa Unguja Muhasibu anatumia mfumo wa "Quick Book" kuchakata taarifa zake za fedha lakini kwa upande wa Pemba hakuna mfumo wowote wa kielektroniki badala yake taarifa za fedha zinahifadhiwa na kuchakatwa kwa mikono "manually".

Kuingiza taarifa za fedha kwa mikono kunaweza kupelekea kuongeza uwezekano wa makosa ya kibinadamu wakati wa kuingiza taarifa na kuchakata taarifa hizo na kupelekea kukosekana kwa ufanisi, na kasi ndogo ya utendaji wa kazi na usalama mdogo wa taarifa za kifedha tofauti na mfumo ambao huja na hatua za usalama ili kulinda taarifa nyeti.

Ukaguzi unaishauri ZIPA, kuhakikisha kuwa kunakuweko na mfumo wa fedha kwa wahasibu wa Pemba ili kurahisisha kazi zao.

#### 4.1.20.2 Kutumika chumba cha Seva kama Afisi ya TEHAMA

Ukaguzi umebaini kuwa ZIPA inatumia chumba cha Seva (Server Room) kama Afisi ya wafanyakazi wa kitengo cha TEHAMA. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na viwango bora kubalifu (Best Practice) vinavyotaka vyumba hivyo kutenganishwa kutokana na sababu kadhaa za kiusalama.

Chumba cha seva kinahitaji mazingira maalum kama vile joto na unyevunyevu uliodhibitiwa ili kuhakikisha vifaa vya seva na mitambo ya mtandao inafanya kazi vizuri. Mazingira haya yanaweza kuwa tofauti na mazingira yanayofaa kwa watu wanaofanya kazi Afisini. Hivyo wanaweza kuzima au kupunguza nguvu ya kiyoyozi ili ilingane na mahitaji yao wakati huo huo haitoendana na mahitaji ya Seva na vifaa vyengine jambo linaloweza kupelekea kuviuwa vifaa hivyo.

Aidha, Chumba cha seva kina vifaa vya msingi vya taasisi na data nyeti. Inahitaji hatua za usalama zaidi ili kuzuia upatikanaji usioidhinishwa, wizi au uharibifu. Kwa kuwatenganisha, ZIPA inaweza kutoa ulinzi wa ziada kwa rasilimali za chumba hicho kwa kuzuwia kuingia na kutoka watu wasio husika na chumba hicho.

Lakini pia, Seva na vifaa vingine vya mtandao huunda kelele kutokana na shughuli yao ya mara kwa mara na mifumo yao ya baridi. Kelele hii inaweza kuwa kero kwa wafanyakazi wa Afisi na inaweza kuathiri uzalishaji wao na ustawi. Kwa kuwatenganisha, tatizo hili la kelele linaweza kupunguzwa au kutatuliwa.

Ukaguzi unaishauri ZIPA, kutenganisha chumba cha Seva na Afisi ya watendaji wa TEHAMA ili kuweza kuendana na miongozo ya viwango bora duniani lakini pia kuepuka madhara yanayoweza kujitokeza kwa kukiwacha chumba hicho kama kilivyo kwa sasa.

#### 4.1.20.3 Mfumo wa ZIEW kutounganishwa na mfumo wa BPRA

Katika mapitio ya mfumo wa ZIEW ukaguzi umebaini kuwa mfumo huo umewekwa sehemu ya kujaza nambari za usajili wa biashara za BPRA lakini haujaunganishwa na mfumo wa BPRA ili kubaini kama muekezaji amesajiliwa na kupatiwa kibali cha biashara.

Kutounganishwa mfumo huo na mfumo wa BPRA kunapelekea mfumo huo kutobaini kama nambari hizo zilizoingizwa ni sahihi au sio sahihi lakini pia inailazimu ZIPA kuzichukua na kuzipeleka katika Afisi za BPRA kwa njia ya kawaida (manually) ili kutambua usahihi na uhalali wa usajili wake.

Njia hii inapelekea usumbufu na kutumia muda mwingi zaidi ambao ungeweza kuokolewa kama mifumo hiyo ingeliunganishwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZIPA, kuhakikisha kuwa inaunganisha mfumo huo na mfumo wa BPRA ili kurahisisha utambuzi wa usajili wa biashara za wawekezaji.

#### 4.1.20.4 Mfumo wa ZIEW kutokuwa na akaunti ya Muhasibu na Mkaguzi wa ndani

Ukaguzi umepitia mfumo wa ZIEW na kubaini kuwa kuna akaunti takribani sita tu zinazotumika ndani ya mfumo huo. Hata hviyo, pamoja na mfumo huo kuwa na uwezo wa kukusanya mapato na kutoa ripoti ya mapato ukaguzi ulibani kuwa hakuna akaunti ya muhasibu wala akaunti ya Mkaguzi wa ndani.

Mfumo kutokuwa na akaunti ya Muhasibu wakati unakusanya mapato unaweza kusababisha muhasibu kushindwa kutekeleza wajibu wake wa kufuatilia mapato lakini pia kupata ugumu wakati wa kufanya upatanisho wa kibenki (bank reconciliation). Aidha kutokuweko kwa akaunti ya mkaguzi wa ndani kunapekea mfumo kushindwa kukaguliwa vizuri na kupata ushauri unaoweza kuleta tija na maboresho ya mfumo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZIPA, kuhakikisha kuwa unawatengenezea akaunti za mfumo wafanyakazi wote wanaostahili kuwa na ufikiaji wa mfumo huo kwa mujibu wa majukumu yao wakiwemo muhasibu na mkaguzi wa ndani.

#### 4.1.20.5 Kukosekana kwa "module" ya ripoti katika mfumo wa ZIEW

Katika mapitio ya mfumo wa ZIEW ukaguzi umebaini kuwa mfumo hauna sehemu rasmi ya module ya ripoti. Hivyo, hakuna njia rahisi ya kawaida ya kutoa ripoti kutokana na kukosekana kwa kipengele hicho sehemu ya mbele ya mfumo "front-end"

Moja katika vitu muhimu vya mfumo ni ripoti kama matokeo ya uchakataji wa taarifa zilizoingizwa hivyo mfumo huo kutokuwa na "module" hiyo kunailetea shida ZIPA kupata taarifa za kilichoingizwa katika taasisi jambo ambalo halitarajiwi katika mfumo wowote.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZIPA, kurekebisha mapema tatizo hilo ili mfumo huo ulete tija stahiki kwa ZIPA.

#### 4.1.20.6 Khitilafu za Mfumo wa ZIEW baina ya malipo ya USD na TZS

Ukaguzi umebaini kuwa mfumo wa ZIEW una hitilafu ya kurikodi Fedha kuwa za Kitanzania (TZS) pindipo fedha inayolipowa ni USD.

Uwepo wa dosari hiyo unaweza kupelekea mfumo kuonekana unahifadhi kiasi kidogo cha fedha za mapato (understate) na kupelekea kujitokeza makosa kwenye ufungaji wa hesabu za mwisho wa mwaka za Taasisi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZIPA, kurekebisha tatizo hilo kabla ya kuanza kujitokeza kwa madhara kwenye mchakato wa ufungaji wa hesabu za mwisho wa mwaka.

#### 4.1.20.7 Mfumo wa ZIEW kuonyesha kupokea fedha za USD wakati taarifa za kibenki kuonesha kupokea fedha za Shilingi ya Tanzania

Ukaguzi umebaini takribani miamala nane (8) iliyoonesha kulipiwa USD 2,900 ndani ya mfumo ambazo zimeonekana kulipwa kwa fedha za kitanzania zenye jumla shilingi 7,112,000. Aidha ukaguzi umebaini kuwa kuna akaunti mbili za benki za NMB ambayo moja ni fedha za kitanzania yenye namba: 22910053601 na nyengine ni ya dola za kimarekani yenye namba: 22910053602 hivyo hakukuwa na haja ya kuziweka dola za kimarekani katika akaunti hiyo ya fedha za kitanzania.

Kuziweka fedha za kimarekani katika akaunti ya fedha za kitanzania kwa kuzibadilisha thamani kunaweza kupelekea upungufu wa fedha za kigeni lakini pia hii inaashiria udhibiti mdogo wa fedha za kigeni.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZIPA kufanya mapitio ya mfumo wa ZIEW kubaini mapungufu yaliyo orodheshwa na ukaguzi na kuyatafutia utatuzi ili kuzuwia madhara yanayoweza kujitokeza.

### 4.1.21 WAKALA WA CHAKULA DAWA NA VIPODOZI ZANZIBAR (ZFDA)

Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar (ZFDA) kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

### 4.1.21.1 Kukosekana kwa Mikataba ya Mifumo ya TEHAMA iliyopo ZFDA

Ukaguzi ulibaini kwamba ZFDA ina takribani mifumo 5 ya TEHAMA inayotumika katika kutekeleza utendaji wa Taasisi ambayo ilitengenezwa kwa nyakati na malengo tofauti, mifumo hiyo ni ZFDA Portal/IMS, LIMS, POS, Pharma Covigilance System na Clinical Trials.

Aidha, ukaguzi ulibaini kwamba mifumo yote 5 kama ilivyoainishwa hapo juu haina Mikataba wala nyaraka rasmi ya makubaliano kati ya watengenezaji wa mfumo husika na ZFDA. Kukosekana kwa Mikataba au nyaraka rasmi za makubaliano kati ya pande hizo mbili kumepelekea kukwamisha ukaguzi kwa kuwa ukaguzi umeshindwa kufahamu matarajio na makubaliano yaliyowekwa kabla ya kutengenezwa kwa mifumo husika ambayo yangetumika kama kipimo cha kutathmini utekelezaji wake ili kuhakikisha kwamba maslahi ya Serikali yanalindwa wakati wote.

Miongoni mwa taarifa muhimu zilizokosekana ambazo zilitarajiwa kuwemo katika mikataba ni pamoja na gharama za utengenezwaji wa mifumo husika, muda uliotumika katika utengenezaji wa mifumo, hadidu rejea za mahitaji ya watumiaji wa mfumo, upeo na mawanda ya mfumo, malengo ya mfumo, wajibu na majukumu kwa kila upande n.k.

Ukaguzi unaushauri uongozI wa ZFDA kuhakikisha kwamba unachukuwa hatua za makusudi  zitakazowezesha upatikanaji wa nyaraka rasmi za makubaliano au Mikataba ya utengenezaji wa mifumo tajwa hapo juu bila kujali aina ya ufadhili (financing arrangements) wa Miradi ya kutengeneza Mifumo ya TEHAMA kwa ajili ya matumizi ya kazi za ZFDA, yaani iwe gharama za utengenezaji wa mfumo husika zimetolewa na Serikali au wahisani wa maendeleo, jambo hili lina umuhimu mkubwa katika ulinzi na usalama wa Taarifa za Serikali zinazoingizwa, kuchakatwa, kusafirishwa na kuhifadhiwa katika mifumo hiyo.

### 4.1.21.2 Udhaifu uliobainika katika Vyumba vya Seva na udhibiti wa vifaa vya TEHAMA

Ukaguzi umebaini madhaifu kadhaa katika vyumba vya Seva na udhibiti wa vifaa vya TEHAMA kwa ujumla kama ifuatavyo: -

Vyumba vyote vya Seva Unguja na Pemba havina mfumo wa kuzimia moto (fire suppression system) unaostahili kwa vyumba hivyo badala yake kuna "fire extinguisher "ambazo sio rafiki kwa vyumba vya Seva na hata hivyo vyote vimepitwa na muda wa matumizi tangu Disemba, 2022.

Kwa upande wa Afisi ya Wete - Pemba vifaa vyote muhimu vya TEHAMA (Network switches, NVR, PBX) vimefungwa ndani ya Afisi ya Katibu Muhtasi wa Mkurugenzi ambapo hakuna mazingira rafiki kwa vifaa hivyo kutokana na kutokuweko kipooza hewa, uingiaji wa mavumbi na usumbufu wa ufikiaji kwa ajili ya marekebisho.

Aidha, kwa upande wa Unguja na Pemba ukaguzi umebaini kuwa mitambo ya kuhifadhi na kuendeshea kamera za ulinzi (NVR na DVR) inadhibitiwa na kuendeshwa ndani ya Afisi za wakurugenzi jambo ambalo ni kinyume na viwango bora kubalifu kwani hali hii inadhoofisha ulinzi na usalama kwa njia ya Kamera za Ulinzi ambapo Kiongozi huyo akisafiri afisi yake hufungwa na kukwamisha ufuatiliaji wa matukio kwa kadri yanavyojitokeza. Hata hivyo, ni wazi kwamba Kiongozi hana mafunzo stahiki wala muda wa kufuatilia matukio yanayoendelea kutokea kupitia Kamera za ulinzi (real time reviews).

Mapungufu haya hupelekea ufuatiliaji hafifu wa matukio na usumbufu katika kuvifanyia ukarabati vifaa hivyo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZFDA kuhakikisha kwamba mapungufu yote yaliyobainika yanatatuliwa kwa kuzingatia miongozo ya kitaifa na kimataifa kwa wakati.

#### 4.1.21.3 Mapungufu yaliyobainika katika ukaguzi wa mizigo na ukusanyaji wa mapato katika Bandari za Wete, Mkoani, Wesha na Mkokotoni

Ukaguzi ulibaini kuwepo kwa changamoto kadhaa katika utekelezaji wa kazi za ukaguzi wa mizigo ya Chakula, Dawa na Vipodozi ambayo inatakiwa pia kulipiwa kwa mujibu wa Sheria, miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na:-

Kutokuwepo kwa mashine ya utambuzi wa mizigo (scanner) kwa ajili ya kurahisisha zoezi la kubaini aina ya mizigo inayokuwemo katika shehena zinazopakiwa katika vyombo vya moto kwa ajili ya kutolewa nje ya Bandari kutoka kwenye Meli za Mizigo jambo ambalo hupelekea wakaguzi wa ZFDA kufanya ukaguzi wa mizigo kwa kutumia mikono na macho pekee.

Hali hii inapelekea kuwepo kwa mwanya mkubwa wa kuingiza bidhaa, vyakula na madawa yaliyokuwa chini ya viwango na kuhatarisha usalama wa wananchi kutokana na kuingizwa sokoni bidhaa hizo.

Aidha, katika mahojiano yaliyofanywa na watumishi wa ZFDA katika Bandari ya Wete ilibainika kwamba kuna baadhi ya wafanyabiashara wasiokuwa waadilifu wanatumia nyaraka ya "Bill Order (Control Number)" kutolea mizigo bila ya kulipia Benki au kwa Wakala wa Benki na kwamba nyaraka hiyo pia ndiyo inayotumika kama risiti ya malipo kuonesha kwa walinzi wanaokuwepo getini ambao nao huwaruhusu ama kwa kutokufahamu au kwa maslahi yao binafsi.

Hali hii inaweza kuwa chanzo kikuu cha uwepo wa "Control Numbers" takribani 180 zenye thamani ya shilingi **34,531,875.64** katika mwaka wa fedha 2022/20233 ambazo hazikulipiwa, sawa na asilimia 14 ya makusanyo yote yaliyopatikana kupitia mfumo wa ZanMalipo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZFDA kufanya mapitio ya utaratibu unaotumika katika utambuzi wa mizigo/ shehena za mizigo ili kuainisha mianya yote iliyopo ya kukwepesha ukaguzi wa Chakula, Dawa na Vipodozi na kuandaa mpango mahsusi utakaoshirikisha Shirika la Bandari na Mamlaka nyengine za Serikali katika utekelezaji wake ili kukomesha utoroshaji wa mizigo hiyo bila kukaguliwa na bila kulipia tozo husika.

Aidha, kwa upande wa ukwepaji wa kulipia tozo husika kwa kutumia "Bill Order" Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZFDA kutoa elimu kwa maafisa wanaokuwa getini pamoja na vyombo vya ulinzi na usalama ili kuwajengea uwezo walinzi na maafisa husika namna ya kubaini nyaraka rasmi inayotakiwa kutumika kutoa mizigo inayokaguliwa na ZFDA Bandarini ili kuondoa uwezekano wa kuruhusu shehena kutolewa nje ya Bandari bila ya kulipiwa kinyume na Sheria.

Kwa upande wa "Control Numbers" zilizopitwa na muda bila kulipiwa, zenye thamani ya shilingi 34,531,875.64 ukaguzi unaushauri uongozi wa ZFDA kufanya uchunguzi ili kubaini sababu za kutolipiwa kila "Control Number" ili kuainisha chanzo na kuchukuwa hatua stahiki kwa wote waliosababisha upotevu wa mapato ya Serikali kwa mujibu wa sheria.

### 4.1.21.4 Mapungufu yaliyobainika katika Mfumo wa IMS/ZFDA Portal

Mfumo wa IMS/ ZFDA Portal ni mfumo mama katika mifumo mitano inayotumiwa na ZFDA. Hata hivyo, ukaguzi umebaini mapungufu kadhaa katika mfumo ambayo yanapelekea kupunguza ufanisi na ubora wa mfumo huo. Mapungufu yaliyobainika ni kama yafuatayo: -

Eneo la mteja kujaza "TIN number" halijaunganishwa na mfumo wa TRA Pamoja na eneo la kujaza "Registration number" halijaunganishwa na mfumo wa BPRA ili kutambua usahihi wa nambari hizo zitakapoingizwa na mteja.

Mfumo unamruhusu mteja kutengeneza nambari yenye nywila (password) zenye tarakimu nne tu kinyume na "ZFDA Security Manual" kifungu nambari 3.9(i) kinachotaka tarakimu za nywila ziwe kuanzia nane lakini pia ziwe na mchanganyiko wa herufi, nambari na alama ili kuziongezea usalama akaunti hizo.

Mfumo kutokuwa na tofauti ya makundi ya akaunti za watumiaji wa mfumo baina ya wafanyakazi wa ZFDA na wateja wanaojisajili. Ikiwa akaunti zote zinaonekana kwa usawa inapelekea ugumu kuzijua akaunti za wafanyakazi au wateja peke yao lakini pia, inaleta ugumu kuziendesha akaunti hizo na kuzifanyia ukaguzi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZFDA kutatua changamoto hizi kwa haraka kwa kushirikiana na wadau mbali mbali kulingana na changamoto husika ili kuepusha athari zinazoweza kujitokeza ikiwa mapungufu hayo hayatatatuliwa kwa haraka.

### 4.1.21.5 Mapungufu yaliyobainika katika mfumo wa LIMS

Laboratory Information Management System (LIMS) ni moja katika mifumo ya ZFDA ambao unatumiwa kusajili sampuli za maabara. Mfumo huu umebaini kuwa na mapungufu kadhaa wakati wa ukaguzi kama yafuatayo: -

Kutoingizwa kwenye mfumo taarifa za Vipimo vya maabara inavyofanyiwa ZFDA na taasisi nyengine kwa mikataba midogo (Subcontracted Laboratory Tests). Kukosekana kwa taarifa hizi kwenye mfumo kunazifanya taarifa hizo kutokuwa kamili. Hivyo, mfumo hauwezi kutoa ripoti sahihi ya majaribio yote ya maabara yaliyofanywa chini ya usimamiza wa ZFDA.

Mfumo kukubali kumuweka "Analyst" huyo huyo kuwa "Checker" kwa wakati mmoja kitu ambacho hakitakiwi kufanyika. Kutokana na mmoja anafanya kazi na mwengine anatakiwa aipitie kazi hiyo haiwezi kuwa sahihi kuwezekana kuwa mtu mmoja.

Mfumo kushindwa kuweka "analysis" kwa makundi yao (Dawa, Chakula na Vipodozi) na badala yake wanatokea wote kwa pamoja jambo ambalo linapelekea usumbufu na upotevu wa wakati wa kuwachagua.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZFDA kutatua changamoto hizi kwa haraka kwa kushirikiana na wadau mbali mbali kulingana na changamoto husika ili kuepusha athari zinazoweza kujitokeza ikiwa mapungufu hayo hayatatatuliwa kwa haraka.

### 4.1.22 KAMISHENI YA UTALII ZANZIBAR (ZTC)

Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa Kamimeshi ya Utalii Zanzibar (ZTC) kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 4.1.22.1 Kutofanyika kwa ukaguzi wa ndani wa TEHAMA

Kwa Mujibu wa taratibu zilizo bora za sera za TEHAMA (ICT Policies Best Practises) zinahitaji mkaguzi wa ndani kufanya ukaguzi wa masuala ya TEHAMA kwa kutumia sera na miongozo ya kitaifa na kimataifa.

Ukaguzi ulibaini ya kwamba Kitengo cha ukaguzi wa ndani cha Kamisheni ya Utalii Zanzibar hakina utaratibu wa kufanya ukaguzi katika maeneo ya TEHAMA kwa lengo la kuhakikisha vifaa, miundombinu na mifumo ya TEHAMA ya Kamisheni inafanya kazi kwa mujibu wa vigezo na miongozo ya TEHAMA iliyopo.

Kutofanyika kwa ukaguzi wa ndani wa TEHAMA katika Kamisheni kunaweza kupelekea kujitokeza kwa hatari za kiusalama katika vifaa, miundombinu na mifumo ya TEHAMA, kwa mfano uhalifu wa mtandao, udukuzi, upotevu wa taarifa n.k.

Vile vile kunaweza kusababisha hasara kubwa kwa Serikali pindipo dosari za kiufundi zikitokea na kushindwa kubainika mapema na ukaguzi wa ndani katika mifumo na miundombinu ya TEHAMA.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar kuhakikisha unafanya ukaguzi wa ndani wa masuala ya TEHAMA ili kuimarisha usalama, kuongeza ufanisi na weledi wa utendaji kazi wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA ya Taasisi.

#### 4.1.22.2 Uhaba wa Kompyuta kwa Kamisheni ya Utalii Pemba

Katika ukaguzi uliofanyika ilibainika kwamba Kamisheni ya Utalii Pemba ina idadi ya wafanyakazi 16 ambao hutekeleza majukumu yote ya kusimamia kazi za utalii kwa upande wa Pemba kupitia zana za kisasa kama vile kompyuta za afisi n.k.

Aidha, ukaguzi ulibaini kwamba kati ya kompyuta saba (7) zilizopo, kompyuta sita (6) ni nzima na kompyuta moja (1) mbovu. Hali hii imepelekea baadhi ya watumishi kukosa kompyuta za kufanyia kazi na kusababisha kujitokeza kwa usumbufu katika utendaji wa kazi zao.

Kuwepo kwa uhaba wa kompyuta za kufanyia kazi katika Kamisheni kunapelekea kuchelewa kumalizika kazi kwa wakati kutokana na kompyuta hizo kutumika kwa awamu, jambo ambalo linapelekea kupungua kwa ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya kazi kwa watumishi wa Kamisheni.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kamisheni ya Utalii kufanya tathimi ya mahitaji halisi ya vitendea kazi vyote muhimu ikiwemo Kompyuta na kutenga bajeti na fedha za kutosha kununua vitendea kazi vyote vinavyohitajika ili kuhakikisha kwamba kunakuwa na ufanisi na utoshelevu wa vitendea kazi katika Taasisi.

#### 4.1.22.3 Kutokuwepo kwa bajeti ya Kitengo cha TEHAMA

Sera ya Serikali Mtandao Zanzibar ya mwaka 2012 kifungu nambari 4.8 imezielekeza taasisi juu ya Utekelezaji wa ufanisi wa Serikali ya kielektroniki unategemea fedha za kutosha kutoka katika bajeti ya Taifa au msaada wa wafadhili, ambapo kila taasisi ya umma itatenga fedha za kutosha kwenye bajeti zake za kila mwaka kwa ajili ya manunuzi ya vifaa vya TEHAMA, matengenezo ya vifaa vya TEHAMA, mifumo na mitandao kwa ajili ya mabadiliko ya haraka ya Teknolojia.

Katika kitengo cha TEHAMA bajeti inasaidia mgawanyo sahihi wa rasilimali fedha kwenye kitengo, kurahisisha upimaji wa ufanisi wa kitengo, kuwezesha ufuatiliaji (monitoring) wa utendaji kazi wa kitengo, kusaidia uwekaji wa malengo, kuboresha ufanyaji wa maamuzi na kuongeza hamasa kwa wafanyakazi.

Ukaguzi ulibaini kwamba Kitengo cha TEHAMA cha Kamisheni ya Utalii Unguja na Pemba hakikuwa na bajeti ya matumizi na usimamizi wa kitengo cha TEHAMA. Hivyo basi, Kukosekana kwa bajeti kunaweza kuwa na athari mbali mbali katika utawala wa kiteknolojia na Habari.

Kutokuwepo kwa bajeti ya Kitengo cha TEHAMA kunaweza kupelekea kutokezea athari zifuatazo: -

- Kukidumaza Kitengo hicho kiutendaji na kusababisha kutokufikia malengo yake ya kusaidia na kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya Kitengo cha TEHAMA.
- Kukosekana kwa mafunzo ya mara kwa mara kwa watumiaji wa mifumo (system users) pindipo yanapotokezea mabadiliko ya uboreshaji na uimarishaji wa mifumo.
- kushindwa kuwajengea uwezo wataalamu wa ndani wa kitengo cha TEHAMA ili kuweza kusimamia na kuimarisha mifumo ya taasisi kwa kupitia wataalamu wa ndani.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kamisheni ya Utalii kuzingatia maelekezo yaliyowekwa kwenye Sera ya TEHAMA ya Taifa kwa kutenga bajeti na fedha za kutosha kila mwaka kwa ajili ya kazi na mipango mikakati ya TEHAMA ili kuweza kufikia malengo ya Serikali katika kuweka Serikali Mtandao kwenye utumishi wa umma.

### 4.1.22.4 Kutokuwepo kwa mfumo wa kielektroniki kwa ajili ya kuendeshea shughuli za uratibu na udhibiti utalii

Ukaguzi ulibaini kwamba Kamisheni ya Utalii Zanzibar haina mfumo wa kielektroniki kwa ajili ya kuendeshea shughuli za uratibu na udhibiti wa Utalii ili kuimarisha upatikanaji wa taarifa, uwazi, uwajibikaji pamoja na kuimarisha udhibiti wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

- Kukosekana kwa taarifa kamili na sahihi za hali ya utalii Zanzibar ikijumuisha ukubwa wa Sekta ya Utalii, mtawanyiko (demographic) wa huduma za utalii Unguja na Pemba, mchango halisi wa utalii katika uchumi wa Zanzibar, ukuaji wa Sekta ya Utalii na matarajio ya mchango wa utalii katika uchumi siku za mbeleni, takwimu sahihi na za kutegemewa za wadau wa Sekta ya Utalii nchini n.k.

- Kukosekana kwa usahihi wa mahesabu ya tozo za malazi (accommodation) kwasababu ya kutumia njia za kawaida (manually) katika kutambua kiasi kinachotakiwa kulipwa watoa huduma za malazi.
- Kukosa ufanisi katika kazi jambo linalosababishwa na kufanya kazi zote kwa njia za kawaida (manually) na kupelekea kutumia muda mrefu kutekeleza kazi kidogo.
- Kukosekana kwa tija inayotarajiwa katika kuchangia ukuaji wa uchumi wa nchi kwa kuwa Zanzibar inategemea zaidi mchango wa Sekta ya Utalii katika uchumi wake.
- Udhibiti duni wa mapato yanayokusanywa na Kamisheni ya Utalii.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kamisheni ya utalii kutenga bajeti na fedha toshelevu zitakazoiwezesha Kamisheni ya Utalii kusanifu, kuunda na kutekeleza mfumo wa kielektroniki utakao zingatia majukumu ya msingi (core functions) ya Kamisheni na kuhakikisha kwamba mfumo huo unakuwa na uwezo wa kudhibiti ukusanyaji wa mapato kwa kutumia njia mbali mbali kama vile "Point of Sales Machine (PoS)", mitandao ya simu (Mobile Network Operators–(MNOs), Mabenki, na kwamba mfumo uunganishwe (integrated) na mifumo mengine muhimu kama vile ZANMALIPO, ZIDRAS, ZAN ID, NIDA, Uhamiaji n.k.

Aidha, kwa kuzingatia ukubwa wa mfumo huu ukaguzi unaushauri uongozi wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar kuhakikisha kwamba Serikali inapata thamani ya fedha zitakazowekezwa katika utekelezaji wa mradi huu kwa kuajiri mtaalamu aliyebobea katika masuala ya kusimamia utekelezaji wa miradi ya TEHAMA kama huu (Project Manager) ambaye atahakikiksha kwa Maslahi ya Serikali kwa upana wake yanazingatia kuanzia hatua za awali kabisa za kuandaa Zabuni, Mahitaji ya Taasisi na mahitaji ya watumiaji wa mfumo (Institution and User Requirement), mahitaji ya TEHAMA ya kitaalamu (ICT Technical requirements) pamoja na mahitaji ya Wadau wengine kama vile eGAZ – ZANMALIPO, ZCSRA – Zan ID, Wakala wa Usajili wa Biashara Zanzibar, ZRA – ZIDRAS, Baraza la usimamizi udhibiti wa utoaji wa Leseni n.k.

#### 4.1.22.5 Kutotumika kwa mfumo wa e-Office katika Afisi za Kamisheni ya Utalii Pemba

Ukaguzi ulibaini kwamba Kamisheni ya Utalii Pemba bado hawajaanza kutumia mfumo wa kupokea na kutuma barua kwa njia ya mtandao (e-Office) ili kufanikisha malengo ya Serikali yaliyokusudiwa (Serikali Mtandao) yenye nia ya kuongeza ufanisi na tija katika mawasiliano kwa njia ya barua na mzunguko wa mafaili licha ya matumizi ya mfumo huo kuendelea katika Afisi za Kamisheni Unguja tangu tarehe 21/09/2022. Hivyo basi kutotumia mfumo wa e-office kwa taasisi ya Kamisheni ya Utalii Pemba kunapelekea kuzorotesha mpango wa Serikali wa kudumisha Serikali mtandao na kupambana kuondoa utendaji wa shughuli za kiserikali kwa njia ya "manual".

Utendaji wa shughuli za kiserikali kwa njia ya "manual" kunaweza kupelekea athari mbali mbali kama vile uvujaji wa taarifa za Serikali, ucheleweshaji wa taarifa kwa kufika kwa wakati, upotevu wa taarifa unaweza kufanywa na watumishi ama kwa bahati mbaya au kwa kudhamiria.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kamisheni ya Utalii kutekeleza miongozo hiyo halali ya Serikali inayotolewa na Wakala wa Serikali Mtandao kupitia Afisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa kuhakikisha kwamba inaweka mazingira yote wezeshi kama vile kutoa mafunzo kwa watumiaji wote, kununua vifaa vyote vinavyohitajika na kufanya mawasiliano wa eGAZ ili kufungiwa mfumo kwa haraka iwezekanavyo.

#### 4.1.22.6 Kutokamilika kwa wakati utengezaji wa Tovuti ya Kamisheni ya Utalii Zanzibar iliyogharimu zaidi ya shilingi 35,521,200

Tovuti za Serikali ni moja ya zana muhimu za TEHAMA zinazotumiwa na Taasisi katika kutoa taarifa kwa umma kuhusiana na huduma mbali mbali zinazotolewa na taasisi husika.

Mnamo tarehe 21/06/2022 Kamisheni ya Utalii Zanzibar ilisaini hati ya makubaliano ya mkataba na Kampuni ya M/s Falnet Group of Technologies Limited kwa ajili ya utengenezwaji wa Tovuti ya Kamisheni kupitia Zabuni namba SMZ/JO2/CT/DP/2021-22/01 yenye thamani ya shilingi 35,521,200 ambapo Mtoa Huduma alitakiwa kukamilisha kazi hiyo na kukabidhi Tovuti kwa Kamisheni ndani ya miezi mitatu (3) ambapo ni tarehe 20/08/2022.

Hadi ukaguzi unakamilika, zaidi ya miezi 15 Tovuti hiyo haijakamilika na bado ipo katika majaribio (testing) ili kubaini mapungufu na kuyafanyia kazi.

Kuchelewa kukamilika kwa mradi huo kunapelekea kuwanyima fursa wadau mbali mbali wa Kamisheni ya kupata taarifa za msingi kuhusiana na taarifa muhimu zinazohusu Kamisheni.

Aidha, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Muongozo wa Utengenezaji, Uendeshaji na Usimamizi wa Tovuti za Serikali, toleo la 1.0 mwaka 2022, ambapo aya ya 7.1 inaelekeza kuwa tovuti zote zihifadhiwe kwenye kituo kikuu cha kuhifadhi taarifa cha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar kuhakikisha unamsimamia kwa karibu Mtoa Huduma (M/s Falnet Group of Technologies Limited Company) na kulinda maslahi mapana ya Serikali kwa kutekeleza vipengele vya Mkataba hususani katika vipengele vya adhabu inayotokana na kutokamilisha utakelezaji wa mkataba kwa wakati.

Aidha, Kamisheni inashauriwa kuhakikisha kwamba Tovuti hii inakidhi matakwa ya Ubora na vigezo vyote kama vilivyotolewa katika Muongozo wa Utengezaji, Usimamizi na Wendeshaji wa Tovuti za Serikali Zanzibar, 2022.

Kwa upande mwingine, kwa kuwa muda wa mkataba huu umekwishapita ukaguzi unaushauri uongozi wa Kamisheni ya Utalii kufuata hatua za kisheria ili kuhuisha mkataba husika ili kwamba uwe halali mbele ya macho ya Sheria kwa kuwa ikitokea kuna mgogoro wowote Serikali haitakuwa na nguvu za Kisheria kwenda Mahakamani au katika vyombo vyengine vya kutoa haki na kupelekea kupoteza haki zake na kupata hasara.

### 4.1.23 OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ

Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

## Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi

### 4.1.23.1 Kutokuwepo kwa ushahidi wa Umiliki wa mfumo mpya wa MUTM

Mfumo Mpya wa MUTM umepatikana kupitia Mkataba wa Matengenezo ya Mfumo uliofungwa baina ya Chuo cha Mipango (IRDP) Mwanza (Mteja) pamoja na Kampuni ya Jam Solution (Mtoa Huduma) kwa thamani ya shilingi 350,000,000 ambapo mkataba huo ulitiwa saini tarehe 06 Septemba 2022.

Kwa kuzingatia mifumo ya TEHAMA ni mali na inapaswa kuwekwa katika daftari la Mali za Kudumu, ukaguzi umebaini kuwa utaratibu uliotumika ni kinyume na kifungu Nambari 62 na 64 cha Sheria nambari 6 ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021, ambapo inaelekeza taasisi za Umma kutumia mbinu sahihi za upatikanaji wa mali za umma na kutunza nyaraka zinazothibitisha kuwa mali zinamilikiwa kisheria.

Kwa kuzingatia kwamba Mkataba haujaitambua Wizara kama ni mmiliki halali wa mfumo huo, ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara, kuanzisha mchakato wa kupata umiliki kutoka kwa IRDP aliyeingia Mkataba wa utengenezaji wa mfumo huo ili kuutambua mfumo huo kama Mali ya Umma ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mujibu wa Sheria ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma.

### 4.1.23.2 Kutokuwepo kwa Kifungu cha Uanzishwaji wa Makubaliano ya "Escrow"

Ukaguzi umebaini kwamba mkataba wa Utengenezaji wa Mfumo mpya wa MUTM haukujumuisha kipengele cha Uanzishwaji wa Makubaliano ya Escrow, ambapo ni makubaliano ya kulinda na kutunza viasili vya mifumo kwa Wakala wa Escrow hadi kukamilika kwa utekelezaji wa mkataba wa utengenezaji wa mifumo hiyo.

Kushindwa kusimamia ulinzi na usalama wa viasili vya mfumo mpya wa MUTM, kunatoa fursa kwa mtengenezaji wa mifumo (Jam Solution) kuendelea kuvitumia (re-uses) viasili hivyo kwa kuviboresha (customization) kwa ajili ya manufaa ya kibiashara.

Ili kudumisha uendelevu wa mfumo wa MUTM, ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya TAMISEMIM kwa kushirikiana na Chuo cha Mipango (IRDP) kufanya maboresho ya Mkataba kwa kuweka nyongeza ya kifungu cha uanzishwaji wa Makubaliano ya Escrow ili kuhakikisha usalama na upatikanaji wa viasili vya mfumo wa MUTM wakati itakapohitajika.

#### 4.1.23.3 Kutokubainishwa kwa uwazi wa Hakimiliki ya ubunifu wa viasili vya mfumo (source codes)

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kifungu nambari 4 cha mkataba wa utengenezaji wa mfumo mpya wa MUTM hakijatosheleza katika kubainisha Hakimiliki ya viasili vya mfumo uliotengenezwa.

Kutokubainisha umiliki wa viasili vya mifumo, kunatoa fursa kwa mtengenezaji (Jam Solution) kuendelea kuwa na udhibiti wa mfumo hadi baada ya kumalizika kwa utekelezaji wa mkataba huo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Viwango vya Utengezaji, Upatikanaji, Uendeshaji na Utunzaji wa Mifumo ya Serikali Mtandao (Hati Na. eGAZ/EXT/ESG/003), aya nambari 2.2.2.1.3 ambapo inaelekeza mkataba lazima uwe na kifungu kinachotoa umiliki wa viasili vya programu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya TAMISEMIM kuhakikisha unazingatia ulinzi wa hakimiliki ya viasili vya mfumo mpya wa MUTM katika mkataba kama ilivyoelekezwa kupitia kifungu nambari 3(1)(b) cha Sheria ya Hakimiliki ya Zanzibar ya 2003, pamoja na muongozo wa viwango kupitia hati nambari eGAZ/EXT/ESG/003.

#### 4.1.23.4 Kutokufanyika kwa zoezi la uhamisho wa data (Data Migration) kwa ajili ya matumizi ya mfumo mpya wa MUTM

Ukaguzi ulibaini kuwepo kwa mfumo mpya wa Ukusanyaji wa taarifa za Mapato (MUTM) ulioanza kutumika kuanzia Septemba 2023, lakini hadi ukaguzi unakamilika zoezi la uhamisho wa data halijafanyika.

Hali hiyo imepelekea kuwa na mifumo miwili (2) ya taarifa za mapato kwa mwaka wa fedha 2023/2024, ambapo MUTM ya zamani itaripoti taarifa za mapato ya mwezi wa Julai hadi Agosti, 2023 na MUTM mpya itaripoti taarifa za mapato mwezi wa Septemba, 2023 hadi 30 Juni, 2024 kufanya hivyo kunaweza kuzalisha taarifa za mapato zisizo na usahihi na kupelekea kuwapotosha watumiaji wa taarifa hizo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya TAMISEMIM kuhakikisha kwamba zoezi la uhamisho wa data za mfumo linatekelezwa ipasavyo kwa ajili ya kuwezesha mfumo wa MUTM mpya uliyopo sasa, kuzalisha taarifa za mapato yaliyokusanywa kupitia MUTM ya zamani na hivyo kuepusha matumizi ya mifumo miwili kwa wakati mmoja.

#### 4.1.23.5 Kuwepo kwa akaunti zisizo na wamiliki (generic accounts)

Katika kupitia watumiaji, ukaguzi umebaini kuwepo kwa akaunti zinazotumika kuufikia mfumo ambazo hazibainishi watumiaji halisi wanaomiliki akaunti hizo.

Kuwepo kwa akaunti hizo, kunatoa fursa kwa mtu yoyote kuzitumia (shared account) na kuingia ndani ya mfumo, na inapelekea kushindwa kubainisha mtu halisi aliyeitumia akaunti hiyo kufanya miamala isiyostahiki kwa ajili ya kumuwajibisha. Jedwari lifuatalo linaonyesha hali halisi ya akaunti zisizotambulika

**Jadweli Nambari 46 : Akaunti zisizotambulika ndani ya mfumo wa MUTM**

| S/N | UserID | Jina Kamili | Mtumiaji | Jukumu | Taasisi | Hali |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 0T9Z23 | MAPATO MAPATO MAPATO | mapatomaghb@tamisemim.go.tz | Mkusanyaji | BARAZA LA MANISPAA MAGHARIB B | active |
| 2 | 2E8RRH | MAPATO MAPATO MAPATO | mapatowete@tamisemim.go.tz | Afisa mapato | BARAZA LA MJI WETE | active |
| 3 | 75ZHDN | MAPATO MAPATO MAPATO | mapatomicheweni@tamisemim.go.tz | Afisa mapato | HALMASHAURI YA WILAYA MICHEWENI | active |
| 4 | 8XJFC4 | MAPATO MAPATO MAPATO | mapatochake@tamisemim.go.tz | Afisa mapato | BARAZA LA MJI CHAKECHAKE | active |
| 5 | CHSK35 | MUANGALIZI MAGH B | muangalizimaghb@tamisemim.go.tz | Muangalizi msaidizi | BARAZA LA MANISPAA MAGHARIB B | active |
| 6 | CX1XZT | MAPATO MAPATO MAPATO | mapatomjini@tamisemim.go.tz | Afisa mapato | BARAZA LA MANISPAA MJINI | ACTIVE |
| 7 | G7VS8P | ADMIN ADMIN ADMIN | adminmagha@tamisemim.go.tz | Afisa mapato | BARAZA LA MANISPAA MAGHARIB A | active |
| 8 | G9L0KJ | MAPATO MAPATO MAPATO | mapatokaska@tamisemim.go.tz | Afisa mapato | BARAZA LA MJI KASKAZINI A | active |
| 9 | J0DKC4 | ADMIN ADMIN ADMIN | adminmjini@tamisemim.go.tz | Afisa mapato | BARAZA LA MANISPAA MJINI | active |
| 10 | U2SKND | MUANGALIZI MKUU | info@tamisemim.go.tz | Muangalizi mkuu | OR-TAMISEMIM | active |
| 11 | VX450H | ADMIN ADMIN ADMIN | adminmaghb@tamisemim.go.tz | Afisa mapato | BARAZA LA MANISPAA MAGHARIB B | active |
| 12 | X12S6I | MAPATO MAPATO MAPATO | mapatomagha@tamisemim.go.tz | Afisa mapato | BARAZA LA MANISPAA MAGHARIB A | ACTIVE |

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara, Mabaraza ya Manispaa, Miji na Halmashauri kuhakikisha kwamba kila mtumiaji anasajiliwa kwa kutumia utambulisho wake halisi, ili kubainisha watumiaji watakaotumia vibaya akaunti zao kwa ajili ya uwajibikaji.

#### 4.1.23.6 Kutokuwepo kwa sera za usimamizi wa mashine za POS (Ving'amuzi)

Mfumo wa MUTM umeunganishwa na kufanya kazi katika mashine za POS (Ving'amuzi) zinazotumiwa na wakusanyaji wa mapato (collectors).

Ukaguzi umebaini jumla ya POS 371 zinafanyakazi bila ya kuwepo kwa sera za usimamizi ambazo zinatoa muongozo wa namna bora ya utumiaji wa mashine hizo.

Kutokuwepo kwa sera za usimamizi wa mashine za POS, zinazoweka udhibiti wa miongozo (directive controls) kunatoa nafasi ya matumizi mabaya ya mashine hizo na kupelekea upotevu wa fedha za makusanyo ya mapato.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuandaa sera za usimamizi wa matumizi bora ya mashine za POS kwa lengo la kuweka udhibiti imara katika matumizi ya mashine hizo ili kuongeza ufanisi katika kukusanya mapato katika Mabaraza ya Manispaa, Miji na Halmashauri.

#### 4.1.23.7 Kuwepo kwa mashine za POS zinazotumika bila ya kuthibitika katika mfumo wa MUTM

Katika ukaguzi, tumebaini kuwepo kwa mashine za POS zilizosajiliwa ambazo hazina nambari ya siri (secretcode) inayotumika kuthibitisha (validate) uwepo wa mfumo wa MUTUM ndani ya mashine hizo.

Kuwepo kwa dosari hiyo, kunatoa taaswira ya kwamba mashine hizo zinaweza kutumika kukusanya mapato kwa mfumo mwengine na hivyo taarifa za mapato kutokuonekana katika mfumo wa MUTM.

**Jadweli Nambari 47: Mashine za POS zinazofanyakazi ambazo hazijathibitishwa kupitia mfumo wa MUTM**

| s/n | posid | imeinumber | secretcode | pstatus | instituteid | installcode | Institution |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 22 | 359457090850818 | NULL | active | 1627039650094 | E856Y | Manispaa ya Magharibi B |
| 2 | 33 | 359457090844076 | NULL | active | 1627039292863 | TKV0P | Manispaa ya Magharibi A |
| 3 | 247 | 353007063320756 | NULL | active | 1627819993457 | 6OYWU | Baraza la Mji Chakechake |
| 4 | 376 | 861899059832686 | NULL | active | 1627820028474 | M4SE7 | Baraza la Mji Kaskazini A |
| 5 | 380 | 861899059832769 | NULL | active | 1627820028474 | YCEHC | Baraza la Mji Kaskazini A |
| 6 | 404 | 862595062903238 | NULL | active | 1627819746330 | RIGP6 | Halmashauri W/ Kusini |

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara, Mabaraza ya Manispaa, Miji na Halmashauri kufanya zoezi la mapitio ya mashine za POS ili kuhakikisha kwamba POS zote zinasoma mfumo wa MUTM na kuripoti taarifa za mapato yaliyokusanywa kama ilivyokusudiwa.

### 4.1.24 OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI

Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

## Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi

### 4.1.24.1 Kukosekana kwa Mpango rasmi wa kufanya mabadiliko katika mifumo ya TEHAMA ya OCGS (Systems Change Management Plan)

Mpango wa kufanya mabadiliko hutumika kama ramani ya kuongoza ufanyaji wa mabadiliko yoyote kwenye mifumo ya TEHAMA na Teknolojia nyengine, hili lina umuhimu mkubwa kwa kuwa mabadiliko ya aina yoyote yanaweza kuleta matokeo yasiyotarajiwa kwenye utendaji kazi wa mifumo kwenye Taasisi na kuondoa ufanisi na tija na wakati mwengine kusababisha hasara hususani pale ambapo mabadiliko husika yasiposimamiwa na kuratibiwa vyema kwa viwango bora kubalifu vya TEHAMA.

Kwa mujibu wa kifungu nambari 2.2.2.3(i), (ii), (iv), (v) na (vi) cha Mwongozo wa Maendeleo, Upataji, Uendeshaji na Utunzaji wa Maombi ya Serikali Mtandao Tanzania hati ya Nambari eGA/EXT/APA/006 ambayo inaitaka Taasisi ya umma inayoanza kupokea usaidizi wa matengenezo inapaswa kuhakikisha kuwa mabadiliko yoyote, kama vile hitilafu na kurekebisha hitilafu, kusanikisha 'patches' na uboreshaji hufanywa kwa mujibu wa mchakato wa usimamizi wa mabadiliko na hunakiliwa ipasavyo.

Ukaguzi umebaini kuwa OCGS haina mpango huo jambo linalopelekea uwepo wa hatari kubwa za kuingia katika matatizo yanayoweza kusababishwa na ufanywaji wa mabadiliko bila ya kuzingatia miongozo ya Serikali.

Kutokuwepo na mpango wa kusimamia mabadiliko yanayofanyika katika mifumo kunaweza kusababisha kujitokeza kwa changamoto nyingi za kiutendaji zitakazopelekea mifumo ya Afisi kutofanya kazi kwa ufanisi kama ilivyokusudiwa jambo ambalo linaweza kusababisha kukosekana usalama wa taarifa, upotevu wa taarifa, kuharibika kwa mifumo na hatimae kuingiza hasara Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa OCGS kusimamia utengenezaji wa mpango wa kufanya mabadiliko kwenye mifumo ya TEHAMA ikiwemo Tovuti ya OCGS kwa kuzingatia miongozo ya Kitaifa na Kimatarifa na vilevile kuhakikisha kwamba mpango huo unazingatiwa kwenye mabadiliko yote yanayofanyika kwenye TEHAMA ikijumuisha kufanya uimarishaji wa mifumo kupitia "updates and upgrades" au kubadilisha "codes", kubadilisha mfumo n.k.

#### 4.1.24.2 Kukosekana kwa Muongozo wa kukabiliana na hali ya dharura (Emergency Responce Procedures and Processes)

Kwa mujibu wa kifungu nambari 2.2(6)(1) cha Muongozo wa Serikali Mtandao Tanzania kinachohusiana na Viwango vya Usanifu wa Usalama na Miongozo ya Kitaalamu wa 2017 *'Security Architecture-Standars and Technical Guidelines:2017'* ambacho kinaitaka Taasisi za Umma kuhakikisha kuwa kuna Muongozo wa kukabiliana na hali ya dharura inayoweza kujitokeza ili kuhakikisha mwitikio unaofaa wa tukio unaweza kuhamasishwa inapohitajika.

Ukaguzi umebaini kwamba OCGS haina muongozo wa kukabiliana na dharura mbali mbali zinazoweza kujitokeza katika mazingira ya kazi jambo ambalo ni kinyume na matakwa ya miongozo ya Tanzania. Hata hivyo wakati wa ukaguzi tuliarifiwa kuwa wafanyakazi wanaripoti tukio kupitia simu au kuhudhuria ofisi ya TEHAMA.

- Wafanyakazi wa kitengo cha TEHAMA wanaweza kupoteza muda kutafuta njia sahihi za kushughulikia dharura au tukio la kimtandao.
- Wafanyakazi wanaweza kuwa hawajui jinsi ya kushughulikia dharura vizuri bila mwongozo wa wazi.

Ukaguzi unaishauri OCGS kusimamia utengenezwaji wa muongozo wa kukabiliana na hali ya dharura ambayo inaweza kutokea katika maeneo mbali mbali ya TEHAMA ili kuwasaidia wafanyakazi kwenye harakati zao za kila siku.

#### 4.1.24.3 Dosari za kiusalama zilizobainika katika Chumba cha Mitambo (Server Room)

Ukaguzi ulitembelea katika chumba cha Mitambo (Server Room) cha OCGS Unguja ambapo chumba hicho vile vile hutumika kusimamia na kuendesha mitambo ya kamera za ulinzi (CCTV Camera) zilizofungwa kwa ajili ya kuweka usalama wa Afisi.

Kwa mujibu wa muongozo wa kimataifa ISO 27002:2013 kifungu nambari 11.1.2 ambacho kinaelezea chumba cha sava kinapaswa kulindwa na udhibiti sahihi wa kuingia ili kuhakikisha kwamba ni wafanyakazi walioidhinishwa tu wanaoruhusiwa kuingia. Wakati wa ukaguzi tumebaini mambo tofauti kama yalivyoainishwa hapo chini:-

i. Kutokuwepo kwa kitabu cha kumbukumbu 'A physical log book' wala vifaa vya biometrikia jambo ambalo limepelekea tarehe na saa ya kuingia na kutoka kwenye chumba cha seva kutorikodiwa. Hii inapelekea udhibiti duni wa kuingia na kutoka kwenye chumba cha Seva.

ii. Kiyoyozi (AC) kilichopo kwenye chumba cha sava kutofanya kazi ipasavyo. Hii hupelekea kiyoyozi (AC) kujizima wenyewe mara kwa mara, na wakati mwingine, inachukua muda mkubwa kuwasha upya, na kusababisha chumba kuwa na joto.

iii. Mlango wa chumba cha seva ulioko sio madhubuti kwa ajili ya kudhibiti ufikiaji usioidhinishwa. Mlango huo wa Seva umetengenezwa kwa mbao pamoja na paneli za kioo, hivyo huruhusu kuonekana ndani ya chumba kutoka nje. Hivyo mtu yoyote akiwa na funguo ya chumba cha sava anaweza kuingia bila kikwazo chochote na kuweza kufanya uhalifu kama uharibifu au wizi.

iv. Kutokuwepo kwa kigunduzi cha moto '*fire detector*' ndani ya chumba cha seva badala yake kigunduzi cha moto kipo nje ya chumba cha seva na vile vile kutokuwepo kwa vitambua unyevu Kiotomatiki '*Automatic moisture detectors*'.

v. Dari la chumba cha seva hufanya unyevu unyevu na kupelekea kila baada ya muda kubadilishwa kwa dari hilo.

vi. Hakuna taratibu zilizoainishwa za wageni na orodha ya watumiaji walioidhinishwa kuingia kwenye chumba cha seva.

vii. Kukosekana kwa mchoro wa miundombinu ya mtandao unaoakisi hali halisi (*Updated Network Diagram*) and *As Built Document.* Kupitia majadiliano tulifahamishwa kuwa aliyejenga jengo na waliofunga mtandao hawakuelewana mwisho wa kazi, ndiyo maana taarifa na nyaraka nyingi hazipo kama vile '*As-Built Infrastructure Document na Wiring 'iliyoidhinishwa* na mchoro wa mpangilio wa mtandao ikiwa ni pamoja na Orodha ya Nodi.

viii. Kutokuwepo kwa daftari la kusajili rasilimali za TEHAMA, kunapelekea uwezekano wa kuondolewa vifaa vya TEHAMA bila ruhusa kutoka kwenye chumba cha seva au ofisi yote kwa ujumla.

Kuwepo kwa dosari hizo kunaweza kusababisha ugumu katika kufuatilia shughuli na kuchunguza matatizo kwenye chumba cha sava, vile vile joto lililoongezeka linaweza kuathiri utendaji na ufanisi wa vifaa vya chumba cha seva, pamoja na kusababisha hatari ya usalama na upotevu wa data.

### 4.1.25 MAHAKAMA YA ZANZIBAR

Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa Mahakama ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 4.1.25.1 Kushindwa kutekeleza Sera ya Haki Mtandao (e-Jusice policy)

Haki Mtandao (e-Justice) ni njia ya utowaji wa huduma za Mahakama kupitia mitandao ya kielektroniki ambapo inamuwezesha Jaji au hakimu kuendesha mashauri na wananchi kupata haki zao mahakamani kupitia mifumo ya TEHAMA.

Ukaguzi umebaini kuwa Mahakama imeshindwa kutekeleza sera ya Haki Mtandao (e-Justice policy) ambapo imeainisha mipango mikakati ya utowaji wa huduma kupitia mifumo ya kielektroniki.

Kuwepo kwa dosari hiyo kunapelekea Mahakama kuonekana kushindwa kufanya mabadiliko ya uendeshaji wa huduma zake kutoka katika hali ya kawaida (manual) kwenda katika mifumo ya kielektroniki kama ilivyoelekezwa kupitia sera ya Haki Mtandao.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mahakama kufanya mapitio ya sera ya Haki Mtandao na kuifanyia maboresho ili kuhakikisha mipango mikakati ya TEHAMA inatekelezwa ipasavyo ili kufikia lengo la upatikanaji wa huduma za Mahakama (Haki) kupitia mitandao ya kielektroniki.

#### 4.1.25.2 Kutokutumika kwa Mfumo wa Usimamizi wa Mashauri (CMS)

Ukaguzi ulifanya mapitio ya mfumo wa CMS na kubaini kuwa Mahakama haijaanza kuutumia mfumo huo na badala yake kazi za usimamizi na uendeshaji wa mashauri zinatekelezwa kwa njia ya kawaida (Manual).

Kuwepo kwa dosari hiyo, kunamaanisha kuwa Mahakama imeshindwa kubadilisha mfumo wa utowaji wa huduma zake kupitia mifumo ya kielektroniki wa CMS kama ilivyoelekezwa katika sera ya Haki Mtandao (e-Justice policy), ili kuharakisha upatikanaji wa haki kwa wakati uliopangwa kwa mujibu wa Waraka Nambari 1 wa Jaji Mkuu wa 2018.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mahakama kufanya mapitio ya mfumo wa CMS na kuufanyia maboresho kwa mujibu wa mahitajio ya Mahakama ili kuwezesha mfumo huo kutumika katika utekelezaji wa sera ya Haki Mtandao (e-Justice) kwa kuwawezesha wananchi kupata haki kwa wakati.

#### 4.1.25.3 Kutokuwepo kwa mgawanyo wa majukumu ndani ya mfumo wa ZanWakili

Ukaguzi umebaini kuwa kila mtumiaji wa ndani ya Mahakama ameunganishwa kuwa Msimamizi wa mfumo (System Admin), hali hiyo inamuwezesha kutekeleza jukumu la kukaguwa nyaraka na kuidhinisha maombi ya kuwa Wakili wa Mahakama ya Zanzibar.

Kuwepo kwa dosari hiyo, kunapelekea mtendaji yoyote aliyesajiliwa katika mfumo huo kutekeleza jukumu la Mrajisi wa Mahakama kwa kuidhinisha maombi ya Uwakili, na Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 19 cha Sheria ya Mawakili Zanzibar ya mwaka 2020, ambapo inaelekeza kwamba Mrajisi wa Mahakama ndiye mwenye mamlaka ya kumsajili na kumuidhinisha mtu kuwa Wakili wa Mahakama ya Zanzibar.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mahakama kuzingatia mgawanyo wa majukumu katika utowaji wa haki za kuufikia mfumo (access right), ili kila mtumiaji aweze kutekeleza majukumu yake ndani ya mfumo kwa mujibu wa nafasi yake.

Hivyo, kwa watumiaji wanaostahiki kupitia nyaraka na kuidhinisha maombi ya uwakili watengezewe na kupewa haki yao (access right), na watumiaji ambao ni wasimamizi wa mfumo wabakie na haki ya kusimamia uendeshaji wa mfumo pekee. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

## Jadweli Nambari 48: Orodha ya watumiaji wa ndani (internal users) ambao wamepewa haki ya kuwa wasimamizi wa mfumo

| UserID | First name | Middle name | Last name | Email | Phone | Prv | Status |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Hafidh | Malik | Ali | hafidhm18@gmail.com | 255719606436 | Admin | Active |
| 2 | Harusi | Sadiq | Rashid | rashidharusi85@gmail.com | 255773526738 | Admin | Active |
| 3 | Mwanaid | Ibrahim | Mahmoud | mahmoudmwanaidibrahim@gmail.com | 255718552434 | Admin | Active |
| 4 | ASIYA | AMOUR | ISSA | asyaamour751@gmail.com | 255714209025 | Admin | Active |
| 5 | ABDILLAHI | MOHAMED | NAIM | ubaydi91@gmail.com | 255713335513 | Admin | Active |
| 6 | Farhat | Yussuf | Mwinyi | farhaty72@gmail.com | 255779029772 | Admin | Active |
| 7 | Salha | Saad | Mbarouk | salinka2@yahoo.com | 255768087252 | Admin | Active |
| 8 | JAMILA | SAID | KASSIM | jamilasaid991@gmail.com | 255778152471 | Admin | Active |
| 9 | Biubwa | Hassan | Fadhil | biubwahasfadhil@gmail.com | 255628985847 | Admin | Active |
| 10 | Mbarouk | Khamis | Omar | mbarouk8@yahoo.com | 255716468502 | Admin | Active |
| 11 | Valentina | A | Katema | registrar@judiciaryzanzibar.go.tz | 255714605557 | Admin | Active |
| 12 | BALU | LADA | BALU | ladanyo007@gmail.com | 255629899459 | Admin | Active |
| 13 | Rahma | Kassim | Sultan | rahma.sultan@judiciaryzanzibar.go.tz | 255774683398 | Admin | Active |
| 14 | Ashura | Ali | Mohamed | ashuramohamed91@gmail.com | 255629227188 | Admin | Active |
| 15 | Mhe. Khamis | Ramadhan | Abdallah | cj@judiciaryzanzibar.go.tz | 255777428094 | Admin | Active |
| 16 | Salum | Hassan | Bakar | salum.bakar@judiciaryzanzibar.go.tz | 255777429290 | Admin | Active |

### 4.1.25.4 Mfumo unashindwa kumtambua mtumiaji aliyeidhinisha ombi la mtu kuandikishwa kuwa Wakili wa Mahakama ya Zanzibar

Katika kupitia udhibiti wa mfumo, tumebaini kuwa mfumo hauwezi kunasa taarifa za mtumiaji aliyeidhinisha maombi ya mtu anayetaka kuandikishwa kuwa wakili wa Mahakama ya Zanzibar.

Kuwepo kwa dosari hiyo, kunapelekea mfumo kushindwa kutoa ushahidi wa kubainisha mtendaji aliyefanya miamala isiyostahiki wakati wa kuchakata maombi ya uwakili ndani ya mfumo kwa ajili ya uwajibikaji (accountability).

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mahakama kuhakikisha kwamba mfumo unazingatia kunasa taarifa za shughuli zinazofanywa na watumiaji (activity logs), ili kuweka kumbukumbu za matukio kwa ajili ya kukagua na kubainisha dosari za kiutendaji pamoja na kutumika kama ushahidi kwa ajili ya uwajibikaji.

#### 4.1.25.5 Mawakili walioorodheshwa, waliandikishwa kwa kutumia nambari za simu na baruapepe za kubuni

Ukaguzi ulifanya uchambuzi wa taarifa za mfumo na kubaini kwamba zaidi ya mawakili 1,100 walioandikishwa walikuwa na anuani ya baruapepe "advocates_system@gmail.com" pamoja na nambari ya simu "255000000000" zinazofanana na zisizo na uhalisia.

Kuwepo kwa dosari hiyo, kunatoa taaswira ya kwamba mfumo hauna udhibiti wa kulinda uadilifu wa taarifa zinazoingizwa (data integrity) na kupelekea mfumo kuzalisha ripoti zisizo sahihi (mislead) kwa watumiaji watakaozihitaji kuzifanyia maamuzi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mahakama kufanya maboresho ya mfumo kwa kuweka udhibiti wa uthibitishaji wa data (data validation control) ili kulinda usahihi na kutokujirudia kwa taarifa zinazoingizwa. Aidha, ukaguzi unashauri kwa zoezi la utakatishaji wa data (data cleaning) kufanyika ili kuziboresha taarifa za mawakili walioandikishwa na hatimae kuwa katika usahihi na uhalisia.

#### 4.1.25.6 Mfumo kushindwa kutengeneza (generate) Nambari ya Utambulisho ya wakili (Roll Number) kiotomatiki

Ukaguzi ulibaini kuwa mfumo wa ZanWakili unashindwa kuzalisha nambari ya utambulisho wa wakili (roll number) na badala yake wakili hupatiwa nambari hiyo nje ya mfumo (manually) kulingana na nambari iliyokuwepo katika daftari la orodha ya mawakili (roll book).

Hali hiyo inapelekea kushindwa kuwatafuta (searching), kuwabainisha (identifying) na kuwathibitisha (verifying) mawakili/vakili halali walioandikishwa na Mahakama kupitia mfumo huo kwa kutumia nambari zao za uwakili endapo itahitajika. Vile vile inaweza kusababisha nambari moja ya utambulisho kupewa zaidi ya Wakili mmoja jambo ambalo litapelekea kushindwa kumtambua wakili husika wakati wa kutafuta taarifa zake ndani ya mfumo huo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mahakama ya Zanzibar, kufanya maboresho ya mfumo wa ZanWakili kwa kujumuisha utowaji wa nambari kiotomatiki kwa wakili aliyeandikishwa ili kuweza kutunza kwa ufanisi orodha ya mawakili / mavakili kama ilivyoelekezwa katika kifungu nambari 21 cha Sheria ya Mawakili Zanzibar ya 2020.

### 4.1.26 MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI ZANZIBAR (ZMA)

Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 4.1.26.1 Udhibiti duni katika chumba cha Seva cha Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar (ZMA)

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa udhibiti duni wa chumba cha Seva ambapo chumba cha Seva hakina udhibiti wa moja kwa moja wa moto (automatic fire suppression system), vile vile kutokuwepo kwa Kamera za ulinzi (CCTV Camera) na mlango wa kuingilia katika chumba cha Seva upo katika hali dhaifu.

Hali hii ni kwenda kinyume na miongozo ya viwango bora kubalifu vya kimataifa. Vile vile hali hii inaweza kuleta athari mbalimbali ikiwemo hatari ya Upotezaji wa Vifaa, kuvuja kwa habari Nyeti, kuharibika na kupotea miundombinu na rasilimali za TEHAMA. Aidha, inaweza kusababisha kuongezeka kwa hatari za kiusalama wa taarifa na usiri.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar (ZMA) kuchukuwa hatua ili kuweza kutatua changamoto hii iliyojitokeza.

#### 4.1.26.2 Udhaifu katika mfumo wa kusajili Meli na Mabaharia (Vessels & Seafarers Registration Systems)

Ukaguzi wetu umebaini uwepo wa udhaifu katika mfumo wa kusajili Meli na Mabaharia (Vessel & Seafarers Registration System) ambapo mapungufu hayo yameorodheshwa kama ifuatavyo:-

- **Kukosekana kwa mpangilio mzuri wa kutoa Ripoti za Vyombo vya Baharini**

Ukaguzi umebaini Ripoti zinayotolewa katika mfumo wa Kusajili meli (Vessel Registration System) hazitenganishi Meli za ndani, Meli za nje na vyombo vidogo vidogo na badala yake hutoa ripoti mchanganyiko.

Hali hii inapelekea changamoto kubwa kwa watendaji pale wanapohitaji ripoti za vyombo mahsusi kutoka kwenye mfumo.

- **Ripoti haziwezi kuchuja (Filtering) meli zilizo Hai (Active) na zilizokwisha muda (Expired)**

Ukaguzi umebaini kuwa Ripoti za ujumla za mfumo wa kusajili meli, haziwezi kuchuja meli zote zilizo Hai (Active) na zilizokwisha muda (Expired), meli zote zinaonekana katika hali mchanganyiko, ripoti hizi zinapatikana katika ripoti mjumuisho (Custom Report).

Changamoto hii inapelekea kushindwa kuweza kuchanganua ripoti hizi na kufatilia kwa hatua meli zilizokwisha muda.

- **Kuruhusu kujirejea kwa majina ya Meli ndani ya mfumo**

Ukaguzi umebaini mfumo wa Usajili wa Meli kuruhusu kusajili Meli zenye majina sawa (Vessel Name Duplication).

Hali hii husababisha ndani ya mfumo kuwa na majina ya meli yaliyojirejea na hivyo kupelekea kwa mtumiaji kufanya makosa wakati wa ujazaji wa taarifa za meli husika au kutoa ripoti zenye makosa.

- **Ripoti za mjumuisho haziwezi kutolewa "export" ndani ya mfumo wa kusajili meli**

Ukaguzi umebaini kuwa mfumo wa kusajili meli, hauwezi kutoa "export" ripoti mjumuisho "custom report" ndani ya mfumo.

Watendaji wanapochuja na kupanga ripoti "Filtering & Sorting" ndani ya mfumo wanashindwa kuzitoa ripoti hizo baada ya kuzichuja.

Hali hii inapelekea watendaji na watumiaji wa mfumo kushindwa kuzitumia ripoti hizo nje ya mfumo kwa kufanya uchambuzi.

- **Mfumo kushindwa kutafuta taarifa za baharia (Searching) kwa kutumia Hati ya kusafiria (Passport)**

Ukaguzi umebaini mfumo wa kusajili Mabaharia (Seafarers Registration System) kutoweza kutafuta taarifa za mabaharia kwa kutumia hati ya kusafiria (Passport).

Hali hii inaweza kuleta changamoto mbalimbali ikiwemo kushindwa kujua ni baharia gani anatumia hati ya kusafiria Fulani. Hii ilileta changamoto wakati tunasajili Baharia kwa kutumia hati ya kusafiria lakini zoezi letu halikufanikiwa kwa sababu nambari ya hati ya kusafiria tuliyoingiza tuliambiwa imetumika na Baharia mwengine. Hata hivyo Hatukuweza kujua namba hiyo hati ya kusafiria kama imetumika na Baharia gani ndani ya mfumo kwa sababu mfumo hauwezi kutafuta (Search) baharia kwa kutumia nambari ya hati ya Kusafiria.

Ukaguzi unaushauri Uongozi wa Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar (ZMA) kuchukuwa hatua ili kuweza kutatua changamoto hizo zilizojitokeza.

### 4.1.26.3 Udhaifu katika mfumo wa Bill Portal kutokuonesha Status za "Control Number" zilizoghairika (Cancelled) na zilizokwisha muda (Expired)

Ukaguzi umebaini mfumo wa Bill Portal unaweza kutoa "Status" za "Control number" katika hali mbili, zisizolipiwa yaani (Outstanding) na zilizolipiwa (Paid) tu. Hali hii inaleta changamoto ya kutoweza kujua control number zote zisizolipiwa yaani "Outstanding" ikiwa zimeghairishwa (cancelled) au zimeisha muda wa matumizi "Expired".

Hali ya kutokuwepo Status ya Control number zilizoghairishwa (Cancelled) au na zilizokwisha muda wa matumizi "Expired" kunaweza kuleta changamoto kwa upande wa Ripoti na kutaka kujua sababu ya kuwa na Control number zisizolipiwa, na ikiwa zimelipiwa controlled number zilizotolewa kimakosa basi zionekane zimeghairishwa ili zisiwemo katika "waiting list" ya Ripoti zisizolipiwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar (ZMA) kuchukuwa hatua ili kuweza kutatua changamoto hii iliyojitokeza.

### 4.1.26.4 Udhaifu katika mfumo wa kutoa Leseni wa Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar (ZMA)

Ukaguzi umebaini kuwa mfumo wa kutoa Leseni wa ZMA umejitokeza mapungufu mbalimbali kama yafuatayo:-

- **Mfumo kuruhusu kupokea Nenosiri (Password) dhaifu**

Ukaguzi umebaini kwamba mfumo unaruhusu kusajili nenosiri (Password) dhaifu wakati wa kufungua "Account".

Hali hii imebainika kwa kufungua "user account" na kuweka nenosiri (Password) isiyofuata mbinu za kiusalama za neno siri lakini kwa bahati mbaya neno siri hili iliruhusiwa na mfumo.

- **Mfumo Hauwezi kutoa Ripoti maalum (Custom Report) kwa baadhi ya taarifa**

Tumebaini mfumo kutoweza kutoa ripoti maalum (Custom Report) kwa baadhi ya taarifa muhimu zinazopatikana ndani ya mfumo huo.

Mfano tulijaribu kutafuta ripoti maalum ya Kampuni kwa kutumia eneo husika "Location" ilipo Kampuni hiyo lakini hatukupata, vilevile tulijaribu kutafuta Kampuni zote zilizokuwa na leseni hai (Active License) lakini hazikuweza kuonekana ndani ya mfumo na badala yake zinatokea ripoti ya leseni za Kampuni mchanganyiko yaani "Active & Expired".

#### 4.1.26.5 Kuweza kusajili jina la Kampuni zaidi ya mara moja

Ukaguzi umebaini kuwa mfumo unaruhusu kusajili jina la Kampuni zaidi ya mara moja "Company Name Duplication". Hali hii inaweza kuwachanganya watendaji/watumiaji wa mfumo pale wanapotaka kufanyia kazi Kampuni ambayo imejitokeza mara mbili, kujua ipi sahihi, vile vile kuna uwezekano mkubwa wa kutolewa Ripoti zisizokuwa na uhalisia baada ya Kampuni zilizochujwa wakati wa kutafuta (Searching) kujitokeza mara mbili.

Ukaguzi unauishauri uongozi wa Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar (ZMA) kuchukuwa hatua ili kuweza kutatua changamoto hii iliyojitokeza.

#### 4.1.26.6 Kutotumika kwa mifumo ya Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar (ZMA) kwa upande wa Pemba

Ukaguzi umebaini Mifumo yote inayopatikana Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar (ZMA) haitumiki kwa upande wa Afisi za Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar (ZMA) Pemba isipokuwa mfumo wa Bill Portal tu. Mteja akihitaji huduma ambayo inapatikana kupitia mifumo ya ZMA, itamlazimu taarifa zake zitumwe Makao Makuu Unguja kwa ajili ya kufanyiwa kazi.

Kuchelewa kutolewa kwa huduma ndani ya taasisi kunaweza kusababisha athari mbali mbali zinazoweza kuathiri sifa ya taasisi, ufanisi wa shughuli zake, na uzoefu wa watumiaji. Baadhi ya athari hizo ni pamoja na kucheleweshwa kukamilika kwa shughuli zinazohusiana na huduma hizo jambo ambalo linaweza kupunguza ufanisi wa kazi na kuathiri mzunguko wa kazi ndani ya taasisi.

Aidha, ikiwa huduma zinahusiana na Taasisi au mapato, kuchelewa kutolewa kwa huduma kunaweza kusababisha hasara ya mapato. Wateja wanaweza kukosa fursa za kuhudumiwa na kupelekea kuhama kwa washindani.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZMA kuhakikisha unazingatia umuhimu wa kutoa huduma kwa wakati na kuhakikisha michakato inaimarishwa ili kukidhi mahitaji ya wateja kwa ufanisi zaidi. Hii inaweza kujumuisha kuimarisha miundombinu, mafunzo ya wafanyakazi, na kutumia Teknolojia ili kuboresha mchakato wa utoaji wa huduma.

## 5.0 HITIMISHO

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 nilifanya ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa kuzingatia mifumo ya udhibiti wa ndani, taratibu za ununuzi, utayarishaji wa nyaraka kwa kuzingatia sheria na kanuni zilizowekwa pamoja na kuzingatia Viwango kubalifu vya Kitaifa na Kimataifa vya Taasisi za juu za hesabu zinazotolewa na Shirika la Kimataifa la Taasisi za Juu za Ukaguzi ambazo zinahusu ukaguzi wa kisekta.

Nilitoa barua za ukaguzi (Management letter) zinazoonyesha dosari kwa kila Taasisi niliyoikagua na pale ambapo dosari hiyo ilikosa majibu na ushahidi sahihi ilichukuliwa na kubainishwa katika kitabu hichi kuwa ni dosari iliyokosa majibu.

Ni matumaini yangu kwamba watumiaji wa taarifa hii watanufaika na kujifunza kwa yale yote yaliyoelezwa na kubainishwa kwa uwazi ikiwemo Wakuu wa Taasisi kuweza kuyafanyia kazi na kufanya maboresho ili dosari hizo zisiweze kuendelea kujitokeza kwa mwaka ujao. Katika suala hili nitashukuru kama nitapokea maoni kutoka kwa watumiaji wa ripoti hii juu ya jinsi ya kuiboresha zaidi au kunipa miongozo ya namna ya kutanua wigo wa kazi zangu katika siku zijazo.

Nichukue fursa hii kwa dhati kumshukuru na kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa jitihada zake anazoendelea kuzichukua kuijengea uwezo Afisi yangu katika utekelezaji wa majukumu yake ikiwemo kuboresha stahiki na maslahi ya watumishi, kunipa nguvu na kuniunga mkono wakati wa uwasilishaji wa taarifa zangu pamoja na kuzitolea maelezo na maelekezo kwa Viongozi mbalimbali wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar juu ya namna ya kufanya maboresho ya dosari zinazobainika katika Taasisi zao.

Aidha, natoa shukurani zangu za dhati kwa viongozi wote wanaotenga muda wao kumshauri Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na kumuunga mkono na kumpa moyo katika harakati za kuliongoza Taifa hili na nia yake njema ya kuliletea maendeleo na mafanikio ikiwemo kuboresha maslahi ya mwananchi mmoja mmoja katika uibuaji wa miradi ya maendeleo yenye lengo la kukuza kipato na uchumi wa Nchi hii.

Mwisho kabisa niwashukuru wale wote waliojitokeza kuniunga mkono kwa namna moja au nyengine na kufanikisha upatikanaji wa taarifa hii bila ya kuwasahau Waandishi wa Habari kwa namna walivyojitoa kuitangaza na kuifikisha taarifa hii kwa kutumia vyombo vyao mbali mbali vya ndani na nje ya Nchi.

# KIAMBATISHO NAMBARI 1

## Kiambatisho Nambari 1: Orodha ya Mifumo ya TEHAMA ya Taasisi za Umma iliyokaguliwa kwa mwaka wa Fedha 2022/2023

| Namba | Jina la Mfumo | Lengo Kuu la Mfumo | Taasisi Husika |
|---|---|---|---|
| 1. | Integrated Regulatory System (ZIRS) | Kuwezesha kazi za Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Kimtandao | ZURA |
| 2. | Complaint Management System (CMS) | Kusajili na kufuatilia malalamiko ya Wananchi kuhusiana na Changamoto za Huduma za Maji na Nishati | |
| 3. | Vessels Registration and Seafarers Registration | Kusajili Meli za kitaifa na kimataifa.Vilevile mfumo huu husajili taarifa za mabaharia. | ZMA |
| 4. | Local Seafarers Registration System | Kutoa vibali kwa Mabaharia wa vyombo vidogo vidogo tu. | |
| 5. | License and permit Management System | Kutoa leseni na vibali kwa Kampuni au watu wanaofanya shughuli zao baharini au pembezoni mwa bahari | |
| 6. | Billing Management System | Kutoa "Control Number" kwa Kampuni au watu wanaotaka kulipia huduma za ZMA | |
| 7. | Voucher Management System | Kutengeneza voucher za malipo kwa upande wa matumizi ya Mamlaka. | |
| 8. | E-PORT | Mfumo wa Bandari Mtandao unaoratibu shughuli zote za Bandari ya Malindi | ZPC (Zanzibar Port Corporations) |
| 9. | Terminal Operating System | Kusimamia na kuratibu upangiliaji wa mizigo mbali mbali kama vile magari na makasha (containers) katika eneo la "yard" ya bandari | |
| 10. | Enterprise Resource Planning | Unasimamia mambo ya Kiutawala ikiwemo masuala ya mapato na matumizi, rasilimali watu, mali za Shirika, manunuzi, mishahara, stoo, pamoja na kuandaa hesabu za kila mwisho wa mwaka ndani ya Shirika | |
| 11. | Fleet Fuel Management System | Mfumo unaosimamia upakiaji wa mafuta katika vyombo vya Bandari | |
| 12. | Vessel Traffic System | Mfumo wa usimamizi wa "traffics" za Meli baharini. | |
| 13. | Case Distribution System | Kuhifadhi Tarifa za Kesi zinazofuatiliwa na kufanyiwa kazi na Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi. | ZAECA |

| Namba | Jina la Mfumo | Lengo Kuu la Mfumo | Taasisi Husika |
|---|---|---|---|
| 14. | ZFDA Portal / IMS | Kufanya usajili wa majengo, bidhaa, ukaguzi wa majengo, ukaguzi wa GMP (Good Manufacturing Practice), kusajili maombi ya Kibali, usajili wa wafamasia na ukusanyaji wa fedha | ZFDA |
| 15. | Laboratory Information Management System (LIMS) | Kusajili sampuli za maabara | |
| 16. | Pharmacovigilance System | Kuripoti athari mbaya za dawa zilizotumiwa na wagonjwa kutoka katika maeneo tofauti kwa lengo la kubaini madhara ya dawa hizo na kudhibiti. | |
| 17. | Clinical Trials System | Unatumiwa kuhifadhi na kuchakata taarifa za majaribio ya sampuli za kliniki | |
| 18. | Zanzibar Investrment Electronic Window (ZIEW) | Kusaidia shughuli za ukuzaji wa uekezaji na shughuli nyengine za taasisi kielektroniki | ZIPA |
| 19. | Human Resource Management Information System | Kusimamia taarifa za rasilimali watu pamoja na mishahara ya wafanyakazi | ZSTC |
| 20. | Statistics Management System | Kuhifadhi taarifa za ZSTC kwa lengo la kupata takwimu kamili | |
| 21. | Financial Information Management System | Kusimamia taarifa za kifedha za ZSTC | |
| 22. | QR Code | Kutoa msimbo wa QR (QR Code) za taarifa za bidhaa na huduma za ZSTC | |
| 23. | IFMIS(EPICOR10) | Kusimamia fedha za Serikali kwa upande wa mapato na matumizi | ORFM |
| 24. | MFUMO WA BAJETI NA MATUMIZI (BAMAS) | Utengenezaji wa Bajeti pamoja na Matumizi yote ya Serikali kupitia taasisi zenye voti | |
| 25. | Electronic Monitoring and Evaluation (M&E) | Kusimamia na kutathmini miradi inayofanyiwa kazi na Tume ya Mipango Zanzibar | |
| 26. | OTRMIS | Kurahisisha ufanisi na usimamizi madhubuti wa mashirika ya uwekezaji ya umma Zanzibar | |

| Namba | Jina la Mfumo | Lengo Kuu la Mfumo | Taasisi Husika |
|---|---|---|---|
| 27. | National Online Business System | Kurahisisha kazi, kuimarisha udhibiti wa utoaji wa leseni, kuongeza uwazi na uwajibikaji na kuboresha utunzaji wa kumbu kumbu za biashara | |
| 28. | ZAA ID | Mfumo wa kutengenezea vitambulisho vya kuingia ndani ya Mamlaka za Viwanja vya Ndege | ZAA |
| 29. | SAS | Mifumo inayosimamia uendeshaji wa shughuli za uwanja wa ndege | |
| 30. | Car sticker system | Mfumo wa kutengezea stika za maegesho ya gari | |
| 31. | BCEG systems | Mifumo inayosimamia uendeshaji wa jengo la terminal 3 | |
| 32. | Parking System | | |
| 33. | POSHO PLUS | Mfumo unaotumika kwa ajili ya rasilimali watu | |
| 34. | Sand Permit Management System (Madini Management System) | Mfumo unaotumika kwaajili kusimamia udhibiti na uchukuaji wa maliasili zisizorejesheka | WMNM |
| 35. | ZanID Registration System | Mfumo unaotumika kwa ajili ya usajili na utoaji wa vitambulisho vya Mzanzibar | ZCSRA |
| 36. | HR- Payroll System | Mfumo unaosimamia taarifa za mishahara na rasilimali watu | OR-KSUUB |
| 37. | LADS | Mfumo unaosimamia na kusajili vituo vya watoa huduma za kisheria | |
| 38. | e-Library System | Mfumo unaosimamia taarifa za kisheria katika sehemu moja ikiwa kama ni kitovu cha kitaifa cha taarifa za kisheria (One Stop Centre) | |
| 39. | FuMiS | Mfumo unaosimamia taarifa za mafao ya pencheni na viinua mgongo | ZSSF |
| 40. | eDMIS | Mfumo unaosimamia mafaili ya nyaraka za viinua mgongo na Pencheni | |
| 41. | ARUTI | Mfumo unaosimamia taarifa za rasilimali watu na mahudhurio | |
| 42. | ZIDRAS | Mfumo Mkuu unaosimamia kodi | ZRA |
| 43. | VFMS | Mfumo unaosimamia makusanyo ya kodi kupitia POS | |
| 44. | Suprima | Mfumo unaosimia malipo ya Umeme kwa njia ya Tukuza | ZECO |

| Namba | Jina la Mfumo | Lengo Kuu la Mfumo | Taasisi Husika |
|---|---|---|---|
| 45. | SAP ERP | Mfumo unaosimamia shughuli za ndani za Afisi | |
| 46. | Equillium | Mfumo unaosimamia malipo ya umeme kwa njia ya post paid | |
| 47. | GLPI Asset Register | Mfumo unaosimamia Taarifa za rasilimali za Afisi | |
| 48. | Core Bank System | Mfumo unaosimamia taarifa za kibenki | PBZ |
| 49. | Vendor Registration System | Mfumo unaosajili na kutoa vyeti vya kufanya biashara ya usambazaji. | ZPPDA |
| 50. | Quck Book | Mfumo unaosimamia taarifa za matumizi na mapato | ZBS |
| 51. | ZAMIS | Mfumo unaosimamia taarifa za mirathi kwa Marehemu | Wakf |
| 52. | Hajj Found System | Mfumo unaosimamia taarifa na shughuli za Mahujaji | |
| 53. | ZanWakili | Mfumo unaosimamia taarifa za Mawakili Zanzibar | Mahakama Zanzibar |
| 54. | Case Management System (CMS) | Mfumo wa usimamizi wa mashauri yaliyofunguliwa katika Mahakama ya Zanzibar. | |
| 55. | Mfumo wa Ukusanyaji wa Taarifa za Mapato (MUTM) | Mfumo wa usimamizi wa taarifa za ukusanyaji wa mapato yanayokusanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. | WN(AR)TMSMIM |

# KIAMBATISHO NAMBARI 2

## Kiambatisho Nambari 2: Baadhi ya Zabuni zilizobainika ambazo hazina Thamani

| Division | RFx Published Date | RFx Closing Date | RFx Award Date | RFQ Value | Number of Invited bidders | Number of Responded | Awarded Supplier | Supplier Awarded |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| ZANZIBAR BURAEU OF STANDARDS (ZBS) | 27/01/2023 13:09 | 24/02/2023 10:00 | 20/07/2023 16:18 | null | 4. | 3. | BUREAU VERITAS TANZANIA LIMITED | 0. |
| ZANZIBAR BURAEU OF STANDARDS (ZBS) | 27/01/2023 13:09 | 24/02/2023 10:00 | 20/07/2023 16:18 | null | 4. | 3. | BUREAU VERITAS TANZANIA LIMITED | 0. |
| ZANZIBAR BURAEU OF STANDARDS (ZBS) | 27/01/2023 13:09 | 24/02/2023 10:00 | 20/07/2023 16:18 | null | 4. | 3. | SGS Geneva | 0. |
| ZANZIBAR BURAEU OF STANDARDS (ZBS) | 27/01/2023 13:09 | 24/02/2023 10:00 | 20/07/2023 16:18 | null | 4. | 3. | SGS Geneva | 0. |
| ZANZIBAR GOVERNMENT PRINTING PRESS | 21/06/2023 09:33 | 27/06/2023 10:00 | 10/07/2023 13:18 | 0. | 1,181. | 3. | KILIMANI COUNTY CLUSTER PARTNERSHIP | 0. |
| DIRECTOR OF PUBLIC PRESECUTION (DOPR) - PEMBA | 16/05/2023 09:31 | 16/05/2023 11:00 | 16/05/2023 12:36 | 780,000. | 1. | 1. | ZANZIBAR GOVERNMENT PRINTING PRESS AGENCY (ZGP) | 0. |
| MINISTRY OF HEALTH (MOH) | 02/06/2023 13:21 | 15/06/2023 12:00 | 21/06/2023 08:56 | 0. | 1,162. | 2. | MUZAMMIL LIM-ITED | 0. |

| Division | RFx Published Date | RFx Closing Date | RFx Award Date | RFQ Value | Number of Invited bidders | Number of Responded | Awarded Supplier | Supplier Awarded |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| FIRST VICE PRESIDENT'S OFFICE (OMKR) | 22/05/2023 11:31 | 08/06/2023 09:00 | 06/07/2023 09:34 | 60,791,875. | 1,147. | 5. | KIN INVESTMENT COMPANY LIMITED | 0. |
| ZANZIBAR AGRICULTURE RESEACH INSTITUTUTE | 06/06/2023 14:14 | 07/06/2023 11:00 | 07/06/2023 12:07 | 0. | 1. | 1. | ZANZIBAR GOVERNMENT PRINTING PRESS AGENCY (ZGP) | 0. |
| MINISTRY OF STATE PRESIDENT'S OFFICE, LABOUR ECONOMIC | 19/04/2023 12:44 | 20/04/2023 10:00 | 25/04/2023 10:08 | 2,600,000. | 4. | 1. | ZMOTION STU-DIOS | 0. |
| ZANZIBAR STATE TRADING CORPORATION (ZSTC) | 24/04/2023 14:26 | 13/06/2023 13:30 | 04/07/2023 12:20 | 0. | 1,159. | 7. | SCENIC CONSTRUCTION AND CONSULTANCY | 0. |
| y | 27/03/2023 13:32 | 11/04/2023 10:00 | 22/05/2023 10:08 | 1. | 995. | 5. | BLUEDOT COMPANY LIMITED | 0. |
| SCHOOL OF LAW (SoL) | 13/03/2023 12:37 | 20/03/2023 15:00 | 21/03/2023 17:55 | 1,000. | 4. | 2. | ZANZIBAR GOVERNMENT PRINTING PRESS AGENCY (ZGP) | 0. |
| FIRST VICE PRESIDENT'S OFFICE (OMKR) | 27/03/2023 13:35 | 11/04/2023 10:00 | 12/06/2023 16:08 | 1. | 6. | 1. | KIN INVESTMENT COMPANY LIMITED | 0. |

| Division | RFx Published Date | RFx Closing Date | RFx Award Date | RFQ Value | Number of Invited bidders | Number of Responded | Awarded Supplier | Supplier Awarded |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| PERSIDENT'S OFFICE CONSTITUTION LEGAL AFFAIRS PUBLIC | 13/03/2023 14:52 | 27/03/2023 13:00 | 27/03/2023 15:27 | 200,000. | 10. | 2. | SHENGO ENTERPRISES | 0. |
| DEPARMENT OF LIVESTOCK DEVELOPMENT (DLD) | 24/03/2023 10:50 | 20/04/2023 09:00 | 05/05/2023 13:59 | 3,000,000. | 1,026. | 1. | GENERAL ELECTRICAL CENTER LIMITED | 0. |
| PRESIDENT'S OFFICE REGIONAL ADMINISTRATION | 30/01/2023 15:04 | 13/04/2023 11:45 | 18/05/2023 07:59 | null | 7. | 3. | LUKOLO COMPANY LIMITED | 0. |
| STATE UNIVERSITY OF ZANZIBAR (SUZA) - MAIN CAMPUS | 15/02/2023 20:44 | 04/03/2023 11:00 | 03/05/2023 21:41 | null | 5. | 3. | NALASA PERFECT COMPANY LIMITED | 0. |
| ZANZIBAR CITY COUNCIL (ZCC) | 31/01/2023 13:31 | 01/02/2023 10:00 | 01/02/2023 12:37 | null | 10. | 4. | Zancatering and Take Away Company Limited | 0. |
| ZANZIBAR SEAWEED COMPANY LIMITED (ZASCO) | 03/02/2023 17:21 | 06/02/2023 08:00 | 06/02/2023 16:12 | 54,848,000. | 805. | 2. | COLORFUL TRAVEL AGENT (SMC - PRIVATE) CO. LTD | 0. |
| ZANZIBAR UTILITIES REGULATORY AUTHORITY (ZURA) | 16/01/2023 09:24 | 25/01/2023 09:00 | 21/04/2023 11:26 | null | 10. | 7. | MODERN BUILDING CONTRACTORS LTD | 0. |

| Division | RFx Published Date | RFx Closing Date | RFx Award Date | RFQ Value | Number of Invited bidders | Number of Responded | Awarded Supplier | Supplier Awarded |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| ZANZIBAR GOVERNMENT PRINTING PRESS | 21/12/2022 14:23 | 24/12/2022 10:00 | 24/12/2022 21:24 | null | 1. | 1. | ZANZIBAR GOVERNMENT PRINTING PRESS AGENCY (ZGP) | 0. |
| PUBLIC PROCUREMENT AND DISPOSAL OF PUBLIC ASSETS | 06/01/2023 16:44 | 13/01/2023 11:00 | 16/01/2023 11:06 | null | 22. | 1. | STONE TOWN TRADERS LTD | 0. |
| HIGH COURT OF ZANZIBAR (HC) | 20/12/2022 13:43 | 22/12/2022 13:00 | 22/12/2022 17:03 | null | 639. | 4. | VEDAS CONSTRUCTION COMPANY LIMITED | 0. |
| WAQF AND TRUST COMMISSION (WATC) | 11/01/2023 12:07 | 07/02/2023 10:00 | 08/02/2023 08:54 | null | 12. | 3. | JUMA ISSA OMAR | 0. |
| ZANZIBAR ROAD FUND (ZRF) | 22/01/2023 14:14 | 22/01/2023 18:35 | 23/01/2023 14:51 | null | 19. | 1. | NEW REFRESHMENTS & FOOD SOLUTION | null |
| STATE UNIVERSITY OF ZANZIBAR (SUZA) - INSTITUTE OF TOURISM | 22/01/2023 12:43 | 16/05/2023 21:20 | 26/05/2023 23:28 | null | 9. | 2. | ZEM ELECTRICAL AND SERVICE WORK CO LTD | null |
| CHIEF GOVERNMENT CHEMIST LABORATORY AGENCY | 19/01/2023 17:31 | 20/01/2023 09:50 | 27/02/2023 14:25 | null | 12. | 4. | SPICY RESTAURANT | null |

| Division | RFx Published Date | RFx Closing Date | RFx Award Date | RFQ Value | Number of Invited bidders | Number of Responded | Awarded Supplier | Supplier Awarded |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| ANTI-SMUGGLING UNIT (KMKM) | 12/01/2023 15:41 | 13/01/2023 07:00 | 23/01/2023 08:48 | null | 3. | 1. | KOMESA CIVIL & ELECTRICAL ENGINIEERING COMPANY LIMITED | 0. |
| OFFICE OF DIRECTOR OF PUBLIC PROCECUTIONAS | 09/01/2023 10:33 | 02/02/2023 10:00 | 02/05/2023 08:24 | null | 7. | 5. | STONE TOWN TRADERS LTD | 0. |
| THE HOUSE OF REPRESENTATIVES (BLW) | 11/01/2023 12:59 | 28/02/2023 10:00 | 06/04/2023 12:32 | 70,000,000. | 1. | 1. | ZANZIBAR GOVERNMENT PRINTING PRESS AGENCY (ZGP) | 0. |
| ZANZIBAR BURAEU OF STANDARDS (ZBS) | 14/12/2022 13:46 | 15/12/2022 14:00 | 19/12/2022 14:46 | 10,000,000. | 618. | 9. | Africom Limited | null |
| MINISTRY OF INFORMATION, YOUTH, CULTURE AND SPORTS | 30/11/2022 11:49 | 05/12/2022 15:00 | 12/12/2022 11:53 | null | 1. | 1. | ZANZIBAR GOVERNMENT PRINTING PRESS AGENCY (ZGP) | 0. |
| HIGH COURT OF ZANZIBAR (HC) | 08/12/2022 16:22 | 16/12/2022 13:30 | 20/12/2022 08:23 | null | 624. | 3. | VEDAS CONSTRUCTION COMPANY LIMITED | 0. |
| INSTITUTE OF PUBLIC ADMINISTRATION (IPA) | 06/12/2022 14:56 | 08/12/2022 11:00 | 13/12/2022 08:59 | null | 604. | 1. | VISTA GENERAL SUPPLIER COMPANY LIMITED | 0. |

| Division | RFx Published Date | RFx Closing Date | RFx Award Date | RFQ Value | Number of Invited bidders | Number of Responded | Awarded Supplier | Supplier Awarded |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| ZANZIBAR AIRPORT AUTHORITY (ZAA) | 20/10/2022 17:13 | 21/10/2022 11:30 | 21/10/2022 16:10 | null | 8. | 5. | DOUBLE PLUS COMPANY LIMITED | 0. |
| WAQF AND TRUST COMMISSION (WATC) | 12/10/2022 12:08 | 24/10/2022 10:30 | 31/10/2022 17:19 | 10,147,225. | 5. | 1. | OSAJU COMPANY LIMITED | 0. |
| ZANZIBAR AIDS COMMISSION (ZAC) | 08/11/2022 12:29 | 18/11/2022 12:30 | 18/11/2022 12:46 | 8,400,000. | 29. | 5. | MUZAMMIL LIMITED | 1. |
| PERSIDENT'S OFFICE CONSTITUTION LEGAL AFFAIRS PUBLIC | 08/11/2022 09:57 | 01/12/2022 15:30 | 06/12/2022 15:19 | 1,500,000. | 5. | 1. | JAWAJA AUTO PARTS | 0. |
| PEOPLE'S BANK OF ZANZIBAR (PBZ) | 11/10/2022 16:40 | 25/10/2022 11:00 | 16/01/2023 10:43 | null | 8. | 5. | ZENITH TOURS AND TRAVEL LIMITED | 0. |
| ZANZIBAR CITY COUNCIL (ZCC) | 19/09/2022 15:41 | 23/09/2022 16:00 | 26/09/2022 13:00 | 7,000,000. | 4. | 2. | BUDDA AUTO PARTS | null |

# KIAMBATISHO NAMBARI 3

## Kiambatisho Nambari 3: Zabuni zisizokuwa na thamani halisi ya fedha kwenye Mfumo

| S/N | RFx Code | RFx Title | Division | RFx Award Date | Awarded Supplier | Supplier Awarded | Audit Remark |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | rfq_15081 | UNUNUZI WA VIFAA VYA KUEZEKEA BANDA LA SKULI - BLM CHAKE | CHAKE CHAKE MUNICIPAL COUNCILS (CCMC) - PEMBA | 22/03/2023 12:46 | MAROO MASTER GENERAL SUPPLIER | 31,034,225,000. | Input data error |
| 2 | rfq_15081 | UNUNUZI WA VIFAA VYA KUEZEKEA BANDA LA SKULI - BLM CHAKE | CHAKE CHAKE MUNICIPAL COUNCILS (CCMC) - PEMBA | 22/03/2023 12:46 | MAROO MASTER GENERAL SUPPLIER | 31,034,225,000. | Input data error |
| 3 | rfq_15081 | UNUNUZI WA VIFAA VYA KUEZEKEA BANDA LA SKULI - BLM CHAKE | CHAKE CHAKE MUNICIPAL COUNCILS (CCMC) - PEMBA | 22/03/2023 12:46 | SULEIMAN NASSOR ALI | 23,762,775,000. | Input data error |
| 4 | rfq_15081 | UNUNUZI WA VIFAA VYA KUEZEKEA BANDA LA SKULI - BLM CHAKE | CHAKE CHAKE MUNICIPAL COUNCILS (CCMC) - PEMBA | 22/03/2023 12:46 | SULEIMAN NASSOR ALI | 23,762,775,000. | Input data error |
| 5 | rfq_14039 | PROVISION FOR DEVELOPMENT OF ICT INFRASTRUCTURE (SMZ/F.123/CS/QCBS/2022- | ZANZIBAR PORTS CORPORATION (ZPC) | 22/06/2023 20:08 | SOFTNET TECHNOLOGY LIMITED | 1,971,268,582. | Officially not awarded due to over budget |
| 6 | rfq_18886 | - UNUNUZI WA VIFAA VYA GARI DHMT MJINI SMZ 374B | MINISTRY OF HEALTH (MOH) | 23/05/2023 23:11 | JAWAJA AUTO PARTS | 10,400,140,000. | |

| S/N | RFx Code | RFx Title | Division | RFx Award Date | Awarded Supplier | Supplier Awarded | Audit Remark |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 7 | rfq_8696 | ZABUNI KWA AJILI YA KUJENGA VIBANDA PUMPING HOUSE PAMOJA NA FENSI (JUMLA | ZANZIBAR WATER AUTHORITY (ZAWA) | 12/05/2023 11:27 | OSAJU COMPANY LIMITED | 1,279,576,434. | Awarded values was 878,860,853 and not yet paid |
| 8 | rfq_23698 | UNUNUZI WA CHAKULA WHVUM | MINISTRY OF INFORMATION, YOUTH, CULTURE AND SPORTS | 04/07/2023 09:05 | MASHALLAH FRESH FOOD | 14,000,000,000. | Input data error |
| 9 | rfq_22969 | UNUNUZI WA VIFAA VYA SERVICES YA GARI SLS 216 A | ZANZIBAR MARITIME AUTHORITY (ZMA) | 26/07/2023 14:43 | G.M TRADERS | 374,000. | Not implimented |
| 10 | rfq_18027 | UNUNUZI WA KOMPYUTA NA PRINTA | ZANZIBAR MARITIME AUTHORITY (ZMA) | 08/05/2023 10:27 | STONE TOWN TRADERS LTD | 14,750,000. | Actual value of 12,717,000 |
| 11 | rfq_19629 | KUFANYIWA SERVICES VIPOZA HEWA VYA MAMLAKA YA USAFIRI BAH | ZANZIBAR MARITIME AUTHORITY (ZMA) | 30/05/2023 12:25 | MAESTRO ENTERPRISES COMPANY LIMITED | 1,465,000. | Actual value of 1,250,000 |
| 12 | rfq_20875 | UCHAPISHAJI WA VITABU VYA TOZO KWA AJILI YA WATALII WANAO SAFIRI KATIKA VYOMBO | ZANZIBAR MARITIME AUTHORITY (ZMA) | 13/06/2023 08:36 | MULTI COLOR PRINTERS LIMITED | 2,650,000. | Actual value of 6,693,000 |
| 13 | rfq_23640 | UNUNUZI WA LIFE JACKET | ZANZIBAR MARITIME AUTHORITY (ZMA) | 09/07/2023 10:54 | KIKI GENERAL SUPPLIER | 4,700,000. | Not implimented |
| 14 | rfq_18685 | UNUNUZI WA CLUTCH PLATE, PRESSURE PLATE NA REISE BEARING | ZANZIBAR MARITIME AUTHORITY (ZMA) | 31/05/2023 13:54 | ADEM STORE | 1,150,000. | Not implimented |
| 15 | rfq_18797 | UNUNUZI WA UPT CABLE , SWITCH 16 POTS NA RJ CONNECTA | ZANZIBAR MARITIME AUTHORITY (ZMA) | 17/05/2023 08:48 | STONE TOWN TRADERS LTD | 1,630,000. | Not implimented |

| S/N | RFx Code | RFx Title | Division | RFx Award Date | Awarded Supplier | Supplier Awarded | Audit Remark |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 16 | rfq_20881 | UNUNUZI WA COMPUTER DESK TOP MOJA NA PRINTE | ZANZIBAR MARITIME AUTHORITY (ZMA) | 15/06/2023 08:30 | Africom Limited | 3,037,000. | Not implimented |
| 17 | rfq_18744 | UNUNUZI WA COMPUTER LAP TOP | ZANZIBAR MARITIME AUTHORITY (ZMA) | 22/05/2023 10:25 | Biggie Electronic's Dealers | 1,900,000. | Not implimented |
| 18 | rfq_19642 | UNUNUZI WA VIFAA KWA AJILI YA SERVICES YA GARI SLS 238 A | ZANZIBAR MARITIME AUTHORITY (ZMA) | 31/05/2023 11:59 | BIN AMIR GENERAL TRADER | 335,000. | Not implimented |
| 19 | rfq_19998 | UNUNUZI WA VIFAA VYA STATIONARIES (ZMA) | ZANZIBAR MARITIME AUTHORITY (ZMA) | 06/06/2023 14:51 | DOUBLE PLUS COMPANY LIMITED | 15,995,700. | Not implimented |
| 20 | rfq_16442 | UNUNUZI WA VIFAA KWA AJILI YA SAVICES YA GARI | ZANZIBAR MARITIME AUTHORITY (ZMA) | 25/04/2023 09:34 | MIEMBENI LUBRICANTS CENTER | 585,000. | Not implimented |
| 21 | rfq_16998 | UNUNUZI WA VIFAA VYA SOLAR POWER | ZANZIBAR MARITIME AUTHORITY (ZMA) | 19/04/2023 14:36 | NAJ GLOBAL PLANET CO.LTD | 3,480,000. | Not implimented |
| 22 | rfq_14082 | UNUNUZI WA VIFAA MBALIMBALI /ZMA | ZANZIBAR MARITIME AUTHORITY (ZMA) | 28/03/2023 12:13 | F & AS EQUIPE AND GENERAL | 4,660,000. | Not implimented |
| 23 | rfq_8600 | UNUNUZI WA VIFAA VYA KUANDIKIA ( STATIONARIES) | ZANZIBAR MARITIME AUTHORITY (ZMA) | 19/01/2023 11:24 | ZANZIBAR GOVERNMENT PRINTING PRESS AGENCY (ZGP) | 2,976,000. | Not implimented |
| 24 | rfq_7497 | UNUNUZI WA VIFAA KWA AJILI YA MATENGENEZO YA AFISI - MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI | ZANZIBAR MARITIME AUTHORITY (ZMA) | 10/01/2023 15:45 | F & AS EQUIPE AND GENERAL | 2,250,000. | Actual value of 2,590,000 |